**14 MEI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 14 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. REGINA H. MIKENZE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Askari ni kundi kubwa muhimu sana katika jamii yetu na kwa mazingira ya kazi yao kuumia kazini ni rahisi sana. Ni kwa nini, sasa Serikali isione haja, na pengine wakati umefika sasa kwa Askari hao kujiunga na Mfuko wa Fidia Kazini *(Workers Compensation Fund – WCF)* ili Askari hawa wanapopata majanga au kuumia kazini mfuko uweze kuwatibia ili na wao wanufaike na mafao yanayotolewa na mfuko huo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa nafasi hii ya kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mchafu amesema kwa aina ya majukumu wanayofanya vijana wetu wa vyombo vya ulinzi na usalama, kuumia kazini ni jambo linalotarajiwa. Kwa sasa, utaratibu unaotumika kuhusu masuala ya fidia kwa vyombo vya ulinzi na usalama uko kisheria na unazingatia sheria na kanuni ambazo zinawataka kwamba masuala ya fidia yafanywe kwa taratibu za kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunapokea wazo la Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafanya tathmini kuona kama tunaweza tukapanua wigo kutoka kwenye mifuko ya *WCF* na kuweza ku-*accommodate* watumishi walioko kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Jambo hilo litakapokuwa limekamilika, tutaweza kulitaarifu Bunge lako Tukufu kupitia taratibu zetu za Kibunge, kama jambo hilo litaweza kutekelezeka kwa utaratibu huo au kuboresha utaratibu unaotumika sasa ndani ya vyombo vya ulinzi na usalama.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Isack Joseph Copriano.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unajua fika mwaka huu nchi yetu imepata mvua nyingi za kutosha na kusababisha barabara nyingi kukatika na kukosa mawasiliano. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka fedha za dharura wakati tukisubiri bajeti ya 2026/2027 kutekelezwa ili kurudisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Isack Joseph almaarufu Kadogoo, kwa swali zuri ambalo linagusa maeneo mengi ya nchi yetu. Ni kweli kumetokea uharibifu katika maeneo mbalimbali ya barabara zetu zote zinazohudumiwa na *TANROADS* na zile zinazohudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua madhara hayo ambayo yamejitokeza kutokana mvua zilizonyesha maeneo mengine zikiwa ni mvua nyingi kuliko ilivyotarajiwa. Hata hivyo, pamoja na tathmini hiyo kufanyika, kama unavyojua, masuala ya kiujenzi huwa yanategemea pia hali ya hewa kwamba huwezi ukafanya ujenzi imara ikiwa mvua zinaendelea. Kwa hiyo, Serikali inachofanya, imechukua hatua za dharura maeneo ambako mafuriko yalisababisha kukosekana kwa mawasiliano, kurejesha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ujenzi wa kurejesha miundombinu katika hali ya kawaida unatarajiwa ufanyike baada

ya mvua kupungua. Kwa utaratibu huo, uwezekano mkubwa wa ujenzi huo utaanza kufanyika tutakapokuwa tumeshaanza kutekeleza bajeti mpya ya Serikali. Katika utekelezaji wa bajeti hiyo mpya ya Serikali Wizara zetu hizi; Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI zinazosimamia *TARURA* na *TANROADS* wana mafungu ya matengenezo ya barabara mpya, pia wana mafungu ya kufanya matengenezo ya kurejesha barabara ambazo zilikuwa zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweka mkazo, na mahitaji ni takribani shilingi bilioni tatu kwa upande wa barabara za *TARURA* na zaidi ya shilingi bilioni nane kwa upande wa barabara zinazohudumiwa na *TANROADS*. Serikali itaweka nguvu kuhakikisha tunarejesha barabara hizo zirejee katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maelekezo ya Mheshimiwa Rais, ambayo ndiyo maelekezo ya Serikali, ni Wizara zetu hizi na taasisi zetu zinazojenga barabara, kuhamia kwenye ujenzi wa kutumia teknolojia ya kisasa na kujenga barabara za kudumu hasa katika maeneo korofi ili kuepusha uwezekano wa kuwa kila mwaka tunapeleka fedha, halafu mvua ikinyesha mara moja au mara mbili, ile fedha yote inazolewa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaelekeza pia kwenye kujenga barabara zinazodumu hasa kwenye maeneo korofi ili kuepusha hasara ambayo inajitokeza ya kila mvua inaponyesha fedha hizo zinakwenda na maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi nchini inayohusisha wananchi na hifadhi za misitu. Migogoro hii inapelekea migongano ya mara kwa mara kati ya *TAWA, TFS* na wananchi, jambo ambalo husababisha vifo vya wananchi na kuchomewa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo ni kwenye Jimbo langu la Katavi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja akatoa maelekezo, lakini maelekezo yale hayajazingatiwa. Hivi tunavyoongea, kuna sintofahamu, wananchi wanachomewa mazao yao na wanazuiwa kuvuna. Nini kauli ya Serikali kwenye jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Thomas Kampala kwa kulileta jambo hili. Ni kweli kumekuwepo na migogoro kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyoitaja, imedumu kwa muda mrefu. Hata katika ziara ukiondoa jambo la migogoro ya ardhi ya mtu na mtu, mtu na taasisi, eneo lingine linalofuatia ni migogoro hii inayohusisha watu pamoja na taasisi zetu za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nchi, ni lazima tukubaliane kwamba kila mtu anatakiwa aheshimu sheria; wananchi pamoja na watekeleza sheria. La pili, imekuwa kukitokea matatizo ya kiusimamizi kwamba watu wanaachwa wanalima kama ni mazao, wanalima. Wakishamaliza kulima ndio unakwenda utekelezaji wa sheria, ikihusisha kuwazuia kuvuna na kufyeka mazao. Hilo jambo siyo la kiungwana na halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nielekeze, maeneo yote ambako hatukuchukua hatua ya kuzuia, hatukuchukua hatua ya kutoa elimu; ikiwa wananchi wameshakamilisha kulima, wako kwenye hatua za kuvuna, tusifanye kazi ya fyeka mazao yao wala tusifanye kazi ya kuvuna kwa niaba yao. Waacheni wavune, lakini tukishamaliza kuvuna maeneo yote yale ambayo tunajua hayapaswi kulimwa, maeneo yote ambayo tunajua hayapaswi kufungwa, hutumia kwa mifugo, tupeleke elimu ya kuwaelezea wakulima wasilime katika msimu wa kilimo utakaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo hilo, zipo tuhuma pia kwamba baadhi ya wasimamia sheria wanaacha makusudi watu walime halafu wao wakachukue yale mazao. Katika baadhi ya maeneo wanaenda kuyafyeka tu ya yule ambaye hajaweza

kuwapa fedha katika baadhi ya maeneo, wanaacha wale ambao wanatoa fedha walime ilhali wale ambao hawajatoa fedha wanawafyekea. Hivyo hivyo na masuala ya kiufugaji, wapo ambao makundi mengine ambao wanaona wameweza kuelewana kwa namna yoyote ile, wanawaacha na wale ambao hawafikii makubaliano, wanawanyang'anya mifugo yao. *Double standard* ya aina hiyo haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie jukwaa hili kuelekeza kwamba maeneo ambayo wakulima walishalima, wasifyekewe mazao yao. Baada ya mavuno, ifanyike kazi ya kuwaelekeza maeneo ambayo hayapaswi kulima, maeneo ambayo hayapaswi kufugia ili tuweze kwenda na kuheshimu sheria na kuweza kuheshimu maeneo yale ambayo tumekubaliana yatumike kwa matumizi maalum.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, hata kunyang'anya vyombo. Nilipita eneo moja nikakuta wamenyang'anya trekta la mtu mmojawapo ilhali wengine mashamba yao yapo. Kwa hiyo, inaonekana tu lengo ilikuwa ni lile trekta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashamba, wapo waliolima, hii na yenyewe haikubaliki. Nilisema matrekta ya aina hiyo yarudishwe kwa wahusika ili tuanzie pale mwanzo, tutoe elimu na tuzuie watu kwenda kufanya shughuli za uzalizaji kwenye maeneo ambayo yamezuiwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Latifa Juwakali.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, unafahamu kwamba ada za wanafunzi wa vyuo vikuu ni muhimu sana kwa kuendesha vyuo vyetu, lakini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya vyuo vikuu kuwazuia wanafunzi ambao hawajamaliza au hawajakamilisha ada kufanya mitihani mwishoni mwa mitihani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ataungana nami kwamba baadhi ya wananchi ambao hawajakamilisha ada hizo ni kwa sababu pengine ni kutokana na

umaskini wa wazazi wao au kukosa ada au kukosa ada ya mikopo ambayo ni matarajio makubwa ya vijana ya nchi hii. Ni ipi kauli ya Serikali ili kuwapa moyo vijana vya nchi hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Latifa Juwakali, kwa kuwasemea vyema vijana wetu wa Kitanzania hasa wanatokea familia za kawaida za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu ambao ni wa pande zote kwamba ada zile zinasaidia hivi vyuo au taasisi ziweze kujiendesha hasa zile ambazo hazipokei ruzuku ya Serikali kwa kiwango cha kuweza kujiendesha. Hata hivyo, upo kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba inatokea katika baadhi ya wanafunzi wanakwama kabisa kutokana na mazingira alikotokea.

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu ambao umekuwa ukitumika miaka mingi hata enzi ambapo hapakuwa na elimu bila ada ilikuwa ni wanafunzi kuruhusiwa kufanya mitihani, lakini watakapotakiwa kuchukua vyeti vyao, watalazimika kulipa kwanza zile ada ambazo hawakuwa wamezilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nielekeze taasisi zetu za elimu kuzingatia utaratibu ule ambao umekuwa ukitumika wa kutokuwazuia wanafunzi kufanya mitihani, kwa sababu mitihani ni jambo la maandalizi. Mwanafunzi anakuwa ameshajiandaa, yuko tayari kwa ajili ya mitihani, na jambo la ada siyo la kwake. Kwa hiyo, anapata adhabu kutokana na hali halisi ya kimaisha ya familia yake. Hili ni jambo ambalo siyo jema.

Mheshimiwa Spika, turejee kwenye ule utaratibu ambao mitihani ikifika, wanafunzi wafanye mitihani, wapimwe, kwa sababu hawapimwi kwa ada, wanapimwa kwa maandalizi ya mafunzo waliyoyapata na utaratibu ule wa kwamba atakapohitaji cheti chake lazima awe amemaliza mahitaji yote ya kimalipo ambayo alitakiwa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, taasisi ziendelee kuwa-*engage* kuongea na wazazi mara kwa mara kuwakumbushia kwamba kuna mahitaji ya kifedha ambayo mwanafunzi wao, ama mtoto wao hajayamalizia ili waweze kuweka utaratibu wa kuyalipa bila kuathiri masomo ya mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anayelipa ada anakuwa mzazi, siyo mwanafunzi. Kwa hiyo, mwanafunzi jukumu lake ni kusoma, na vyuo pamoja na kuzingatia ukweli ule kwamba vinatakiwa kupata fedha ili viweze kujiendesha, utaratibu mzuri zaidi ufanyike ule ambao uliendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fedha kwenye upande wa mikopo ya elimu ya juu na vyuo vya kati ili kuongeza idadi kubwa zaidi ya watoto ambao wananufaika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani, fedha zinazokwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu zimeongezeka kwa takribani mara mbili kutoka shilingi bilioni takribani 400 hadi shilingi bilioni 900 na ziada, jambo ambalo tunaamini limeongeza pia idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai pia kwa wanufaika ambao waliwahi kunufaika na mikopo kuendelea kurejesha ili Serikali iweze kuwapatia wanafunzi wengi zaidi wigo wa kupata mikopo hiyo na kunufaika na elimu ya juu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu ya muda, tumekuwa na wauliza maswali kwa Waziri Mkuu wanne tu. Ahsante sana kwa majibu mazuri. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na pole kwa msukosuko uliojitokeza. Unaweza ukawa na mitambo mizuri, lakini mambo haya yakatokea; na haya ndiyo yaliyowapata Yanga jana. Pole sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumza jambo muhimu sana la teknolojia mpya ya barabara. Teknolojia hizi zimeletwa nchini miaka mingi sana, lakini kuna uzito na utata wa wataalamu wetu kutokutaka kuzitumia, matokeo yake tunatengeneza barabara halafu baada ya miezi mitatu, minne zinakufa.

Kwa hiyo, imekuwa kama ni *habit* au *hobby* ya watu kutengeneza barabara kwa kutumia fedha za umma bila kuzingatia uimara wa barabara zetu. Ninakuomba sana, teknolojia hizi zipo, Serikali ihakikishe inazitumia ziweze kuokoa fedha za umma, na vilevile barabara ziweze kudumu na kukaa kwa muda mrefu katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, leo tumepata changamoto kubwa ya mitambo, na mitambo hii ni mipya kutoka *BOSCH*. Hii ni kampuni kubwa yenye uwezo mkubwa sana, lakini *these things happen*. Inawezekana ni *disruption* na mtikisiko kidogo wa baadhi ya mitambo au umeme umesababisha. Hata hivyo, ninashukuru na kumpongeza Katibu na timu yake, tume-*improvise* na sasa Bunge linaendelea kwenye ukumbi wetu huu, na ratiba ya Bunge itaendelea mpaka hapo ukumbi wetu utakapoimarika.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 123 (3) inasema: *"Mbunge atakayeamua kutumia Kifungu chenye mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala la mahsusi la sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja."*

Waheshimiwa Wabunge, jana kwenye kipindi cha bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, kulitokea hoja ya Mheshimiwa Sanga na nilimkalisha chini kwa sababu hakutumia Kanuni vizuri. Nimepitia *Hansard* yake, nitaisoma kama ifuatavyo:-

***"MHE. FESTO R. SANGA:*** *Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, ninaipongeza Serikali kwa kazi ambayo inaifanya kwenye ujenzi wa viwanja nchini.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu sera ya Serikali ni kuhakikisha kila mkoa unakuwa na uwanja wa ndege, na sisi watu*

*wa Mkoa wa Njombe tumekuwa na uhitaji wa uwanja wa ndege kwa muda mrefu. (Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali za viongozi kwenye ilani, na kwenye majibu hapa ya kuonesha kwamba mnaweza kujenga Uwanja wa Njombe.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majibu ambayo Serikali imekuwa ikitoa ni kwamba kuna majadiliano yanaendelea.*

***MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga.*

***MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninatamani commitment ya Serikali.*

***MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, hoja yako haiendani na sera specific, umetaja eneo lako. Kwa hiyo, kaa chini.*

***MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa sera."*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli Mheshimiwa Sanga alianza kwa sera, lakini alitaja sera bila kuendana na utaratibu wa kuuliza swali kwenye shilingi ya Waziri kwa mujibu wa ilivyotakiwa. Unatakiwa useme: *"Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali ni kujenga viwanja Kigoma, Tabora, Nachingwea, na maeneo ambayo yana mvuto wa kiuchumi kama Njombe. Mheshimiwa Waziri, ninaomba commitment ya Serikali, ni lini sasa viwanja hivi pamoja na cha Njombe kitaingizwa katika mkakati wa Serikali?"*

Waheshimiwa Wabunge, jamani ninaomba sana msome hizi Kanuni. Kanuni zetu, zipo ziko *very clear* na kama hatutafuata Kanuni, na Mheshimiwa Sanga ni mtaalamu sana wa michezo; sisi tukikaa hapa ni ma-*referee* siyo makocha, tunasimamia Kanuni. Kwa hiyo, ninaomba sana tuzingatie kanuni zetu.

Vilevile, Mheshimiwa Aeshi akarudia *the same thing,* kuhusu uwanja wa meli *Lake* Tanganyika. Kwa hiyo, ilibidi tuwakatishe wakae chini kwa sababu hawakufuata utaratibu wa Kikanuni.

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahishwa sana na Wabunge kwenye maswali ya Waziri Mkuu, wote mnalenga kwenye sera. Kwa hiyo, kwenye suala la mshahara, ni hivyo hivyo, twendeni na sera. Unaweza ukazunguka halafu baadaye ukaleta ukaingiza eneo lako na lika-*qualify* kwenye kushika mshahara wa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge ulifanyika uchaguzi wa Wajumbe mbalimbali waliokwenda kuliwakilisha Bunge katika vyombo vingine vya kikanda. Miongoni mwao ni pamoja na Wajumbe watano waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge katika Bunge la Afrika *(Pan-African Parliament)*.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge la Afrika *(Pan-African Parliament)* lilikutana kwenye Kikao chake cha Saba cha Dharura kilichofanyika kuanzia tarehe 26 Aprili hadi tarehe 6 Mei Mjini Midrand Afrika Kusini. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa katika kikao hicho ni pamoja na uchaguzi wa viongozi wa *caucus* mbalimbali pamoja na uteuzi wa Wajumbe katika kamati mbalimbali za Bunge la Afrika.

Waheshimiwa Wabunge, katika uchaguzi huo Tanzania ilifanikiwa kupata nafasi mbili za uongozi (uwakilishi) ndani ya *PAP* kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula alichaguliwa kuwa *Rapporteur* wa *Eastern Africa Caucus* na Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Baraza la Vijana *(PAP Youth Caucus)*. Ninawapongeza sana kwa namna mlivyoweza kuiwakilisha Tanzania na kuweza kuchaguliwa katika Mabunge mengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, na Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Bunge la Afrika kushika nafasi hizo muhimu za uongozi. Ni imani yangu watazitumikia nafasi hizo kwa weledi na uadilifu mkubwa wakiwa wamebeba taswira ya Bunge letu na nchi kwa ujumla katika nyanja za Kimataifa. Ushindi huu umedhihirisha ushawishi na uwezo wa wawakilishi wa Tanzania katika diplomasia ya kikanda na Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho niwatakie majukumu mema Wabunge wenzetu hawa katika kuzitumikia nafasi hizo, na Mungu awasimamie. Sasa ninamwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Paresso aendelee na shughuli zinazofuata.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na maswali na tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Ninamwita Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Kilindi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 337

**Ujenzi wa Madaraja katika Jimbo la Kilindi**

**MHE. SALEHE M. MHANDO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja yaliyoharibika katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kilindi ili kurahisisha usafiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 871.59 unaohudumiwa na

*TARURA*. Aidha, ina jumla ya vivuko 1,066 ambapo madaraja makubwa ni matatu, *box* kalvati 592, *Solid drift* 466, *vented drift* tano. Daraja moja linafanya kazi na yaliyoharibika mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya usanifu na kujenga madaraja ambapo mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mgera lenye upana wa meta 20 kwa awamu ya kwanza na ujenzi umefikia 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Daraja hilo la Mgera. Aidha, Serikali imeshakamilisha usanifu wa Daraja la Negero lenye upana wa meta 80 ambapo ujenzi wake unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na ukarabati wa madaraja yaliyochakaa katika Wilaya ya Kilindi ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 ilikarabati Daraja la Ngeze, Barabara ya Kwekivu - Ngeze kwa gharama ya shilingi milioni 7.8 na kujenga *box* kalvati jipya Barabara ya Mapanga - Mlingotini kwa gharama ya shilingi milioni 24.14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti ili kuendelea na ujenzi wa madaraja mapya na kukarabati madaraja yaliyochakaa kote nchini ikiwemo Jimbo la Kilindi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, maswali ya nyongeza.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya miaka minne sasa tangu madaraja kadhaa katika Jimbo la Kilindi kukatika kabisa ikiwemo Daraja la Negero, Daraja la Vunila, Daraja la Tamota, Daraja la Kwamfyomi, Daraja la Sambu na Daraja la Makelele. Hali hii imeleta changamoto kubwa sana hasa kwa wagonjwa kwa

kipindi chote hicho, lakini zaidi mama zetu wajawazito ambao siwezi kuelezea kwa undani kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni haja ya kuchukua hatua za dharura katika kuhakikisha kwamba inakwenda kuwawezesha *TARURA* kuweza kurejesha huduma za usafirishaji katika maeneo hayo niliyoyataja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kutokana na bajeti ndogo wanayopata *TARURA* Wilaya ya Kilindi, na kwa mazingira magumu ambayo nimeyaeleza, Serikali haioni haja sasa ya kuweza kuweka mpango wa kuiongezea bajeti *TARURA* Wilaya ya Kilindi ili uweze kukabiliana na changamoto kubwa zinazokabili miundombinu ikiwemo madaraja na vivuko katika Jimbo la Kilindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbwana Mhando Salehe, Mbunge wa Kilindi. Ninafahamu kwamba Jimbo la Kilindi ni moja ya majimbo yenye changamoto za barabara pamoja na madaraja, na Mheshimiwa Mbunge mara kwa mara amewasilisha taarifa za kuhitaji matengenezo hayo. Kwa taarifa njema Mheshimiwa Mhando bajeti ya *TARURA* kwa Jimbo la Kilindi imeongezeka kwa zaidi ya mara tatu na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020/2021 bajeti ilikuwa shilingi bilioni moja kwa mwaka, lakini huu mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* Kilindi ni takribani shilingi bilioni 3.94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza Serikali inatambua kwamba tuna uhitaji mkubwa wa kujenga madaraja na barabara ya Kilindi na ndiyo maana bajeti imeongezeka kwa zaidi ya mara tatu. Jambo la muhimu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tumeshafanya tathmini ya madaraja yote yaliyoharibika, na tayari tunaendelea na taratibu za kibajeti kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako madaraja ambayo tunaendelea na ujenzi hivi sasa na pia yako madaraja ambayo tunaendelea kuandaa utaratibu wa fedha kwenda kuhakikisha yanajengwa na kurejesha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo litafanyika na bajeti ya Serikali itaendelea kuongezwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha ili barabara za Kilindi ziweze kupitika vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda, hatutakuwa na maswali ya ziada. Wale wenye maswali ya msingi watauliza swali moja tu la nyongeza na siyo maswali mawili ya nyongeza.

Tunaendelea, na sasa ninamwita Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti, aweze kuuliza swali lake.

Na. 338

**Mapato ya Utalii kwa Halmashauri ya Serengeti**

**MHE. MARY D. SURATI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Halmashauri ya Serengeti inapata *Service Levy* kutokana na shughuli za utalii Wilayani humo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kifungu cha (6), (7), (8) na (9) vimebainisha vyanzo vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ushuru wa huduma ni miongoni mwa vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika Sheria hiyo kinachotozwa kwa kiwango cha 0.25% ya mauzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imekuwa na changamoto ya kukusanya ushuru huo kwa kuwa Kampuni nyingi za utalii zipo katika Halmashauri ya Jiji la Arusha hivyo kupelekea kampuni hizo kulipa ushuru wa huduma katika halmashauri hiyo licha ya utalii wenyewe kufanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa maelekezo ya mgawanyo wa ushuru huo kwa uwiano wa 60% kwa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ambapo shughuli za utalii hufanyika na 40% kwa Halmashauri ya Jiji la Arusha ambapo yapo makao makuu ya kampuni hizo. Hatua hii imepunguza mgongano wa utendaji katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ushuru huo, pia takwimu za makusanyo zinaonesha kuwa mapato hayo yanaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ipo kwenye hatua za mwisho za kuandaa Kanuni za Usimamizi na Ukusanyaji wa Ushuru wa Huduma. Pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zitaainisha namna bora ya kugawana mapato yatokanayo na ushuru wa huduma kati ya halmashauri moja na nyingine pale inapotokea migongano ya kimapato, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Daniel Surati, swali moja dogo la nyongeza.

**MHE. MARY D. SURATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini mchakato huu umeanza takribani miaka 16 iliyopita. Sisi Watu wa Serengeti kwa mchango ambao tunachangia kwa Taifa, inakuwaje mpaka leo hii hatunufaiki moja kwa moja katika mapato haya? Ninaomba

kujua kwa niaba ya wananchi wa Serengeti; ni lini sisi Watu wa Serengeti tutaanza kupata mapato hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimhakishie Mheshimiwa Surati kwamba tayari Serikali imelifanyia kazi. Miaka hiyo iliyopita hatukuwa na mwongozo wa 60% kwa halmashauri ambako shughuli zinafanyika kwa maana ya Serengeti kwa muktadha huu na 40% kwa Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushaweka mwongozo huo na umeanza kufanya kazi. Ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, katika kipindi cha mwaka wa fedha huu 2025/2026 kuanzia Machi mpaka Julai Halmashauri ya Serengeti imepata takribani shilingi bilioni 1.51 kutokana na ushuru huo unaotokana na shughuli za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dalili ni njema. Tunafahamu bado kuna kazi ya kufanya. Nimhakikishie kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba changamoto hii inaondoka na Halmashauri ya Serengeti inanufaika na mapato ya utalii.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapa, aweze kuuliza swali lake.

Na. 339

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Jimbo la Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata za Kimkakati za Chunyu, Berege, Godegode na Mlembule - Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia mwaka 2025/2026 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 1.19 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali, lakini imetoa shilingi bilioni 3.4, ujenzi wa vituo vya afya na shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imewasilisha maombi Hazina ya jumla ya shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati 94 ambapo Kata ya Chunyu imetengewa shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu muhimu katika vituo vya afya 364 kisha kuendelea na ujenzi wa vituo vya kimkakati kadiri vitavyokidhi vigezo. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima, swali moja la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu zuri la Serikali nina swali moja la nyongeza. Tarehe 2/1/2026, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jimbo la Mpwapwa katika Kata ya Gulwe. Alikuwa akikagua uharibifu wa miundombinu ya *SGR* uliosababishwa na mvua nyingi zilizokuwa zinanyesha. Kwa kuzingatia kwamba Kata ya Gulwe ina kituo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, swali.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** ...ina stesheni ya *SGR*. Niliomba kijengwe kituo cha afya ili kukabiliana na matukio ya ajali ambayo yanaweza kutokea. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wataalamu wamefika tumewaonesha eneo la kujenga kituo cha afya. Sasa ninataka kujua, ni lini ujenzi huu utaanza ili watu hawa wa Gulwe na wasafiri wote wawe katika hali nzuri ya usalama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara katika eneo hili, na pia alitoa maelekezo ambayo Serikali inakusudia katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 kuanza ujenzi katika Kituo cha Afya cha Gulwe ambacho kitahudumia wakazi zaidi ya 13,000, pamoja na wale abiria wanaohudumiwa na kituo chetu cha *SGR*. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Ritta Ernespher Kabati, Mbunge wa Kilolo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 340

**Ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Kimara na Idete – Kilolo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Kimara na Idete – Kilolo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Ernespher Kabati, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Idete. Aidha, ujenzi umehusisha jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)*, choo cha nje pamoja na kichomeataka. Ujenzi wa *OPD* umefika hatua ya lenta sawa na 35%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imetenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara katika Kituo cha Afya Ilula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele cha kukamilisha miradi viporo ya vituo vya afya 364 ili viweze kutoa huduma muhimu zikiwemo huduma za dharura za upasuaji kisha itaendelea na ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati zitakazokidhi vigezo. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali moja la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Ninashukuru kwanza kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, sera ya Serikali ni kujenga vituo vya afya kila kata na ujenzi wa zahanati kila kijiji, lakini Wilaya yetu ya Kilolo zaidi ya kata 15 hazina vituo vya afya na vijiji 61 havina zahanati. Miundobinu ni mibovu, wazazi wanapata shida kwenda kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, nini mkakati wa Serikali kutoa kipaumbele kwa maeneo haya ya Kilolo ambayo hayapitiki na hayana barabara, yaweze kujengewa vituo vya afya na zahanati katika vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, wakati ikiwasilisha Randama, kipindi tunapitisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tuliweka bayana kwamba kipaumbele ni kukamilisha maboma ya zahanati zaidi ya 19,000 na kukamilisha vituo vya afya na vile vituo vya afya vya kimkakati ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kabati kwamba Sera ya Serikali ni kujenga zahanati kila kijiji na tayari tumeshajenga zaidi ya zahanati 6,556, na pia tumejenga vituo vya afya 154 na hospitali 194.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa mipango mizuri ya Serikali ya Awamu ya Sita tutaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati, na lile lengo la kufikia kwamba wananchi wetu wapate huduma ndani ya kilometa tano tunaendelea kulifanyia kazi ili wananchi wetu wapate huduma hizi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jafar Seif pamoja na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tunawashukuru kwa majibu yenu kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea, sasa ni Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Ninamwita Mheshimiwa Thomas Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki, aweze kuuliza swali lake.

Na. 341

**Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uwekezaji wa Umma Nchini**

**MHE. THOMAS M. KITIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uwekezaji wa Umma nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Kitima kwa namna anavyowawakilisha wananchi wake. Pia, kwa kuwa, ninajua kwamba Mheshimiwa Kitima ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, ninafahamu jinsi ambavyo amekuwa mahiri kwenye kusimamia shughuli za Kamati ile, na ni shughuli za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yetu, kwa maana ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tayari imepokea maelekezo kutoka Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu Muswada wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma. Kwa sasa, vikao vya kitalaamu vya Serikali vinaendelea kupitia rasimu ya muswada huo. Mara baada ya vikao vya kitaalamu kukamilisha kazi hiyo, ofisi yetu itawasilisha rasimu ya muswada huo Bungeni kwa ajili ya hatua nyingine za kibunge kuelekea kuupitisha kuwa sheria. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Kitima, swali moja la nyongeza.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, ili kuweza kuipa nguvu ya kusimamia mitaji ya umma; kwa mfano, kuitengenezea bodi yake, kuibadilisha jina na kufafanua majukumu yake vizuri, ili iweze kutekeleza majukumu yake kisawasawa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia jibu langu la msingi ni kwamba, kwa sasa wataalamu wanaendelea kupitia rasimu ambayo italetwa Bungeni. Muswada huo utakaoletwa Bungeni baada ya kukamilisha mchakato, unahusisha pia uboreshwaji wa Ofisi ya *TR (Treasurer Registrar)* ili aweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Mheshimiwa Kitima ana lengo la kuhakikisha *TR* anafanya shughuli zake kikamilifu ili sasa mashirika ya umma ambayo anayasimamia yaweze kuleta tija na yasiwe tanuri la fedha za umma, badala yake ziweze kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kusisitiza kwamba, mchakato ule unahusisha maboresho ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa ni Wizara ya Fedha. Ninamwita Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge wa Ilemela, aweze kuuliza swali lake.

Na. 342

**Kuandaa Kanuni za Bima za Lazima**

**MHE. KAFITI W. KAFITI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaandaa Kanuni za Bima za lazima, ili kutekeleza Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 na kuongeza mapato ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya Mwaka 2022, imefanya marekebisho ya Sheria ya Bima, Sura 394, ili kuongeza wigo wa bima za lazima kwa lengo la kuongeza kinga kwa majanga, ambayo yana madhara makubwa kwa wananchi yanapotokea. Utekelezaji wa marekebisho hayo katika Sheria husika unailazimu Serikali kuandaa kanuni, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Kanuni za Bima za Lazima. Kwa sasa, zoezi la ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kuhusu rasimu hiyo, linaendelea. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili, Serikali imedhamiria kukamilisha mchakato huu mapema iwezekanavyo. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, swali moja la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, sekta ya bima nchini ni moja ya taasisi za kifedha zinazoongeza mapato kwenye mfuko wa Serikali, je, nini sasa kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba, kanuni hizi zitakwenda kukamilika? Nini *commitment* ya Serikali katika hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba mchakato huo unaenda kukamilishwa haraka iwezekanavyo, lakini kwa namna ninavyoona ndani ya mwaka huu, siyo mwaka wa fedha, taratibu hizo zitakuwa zimekamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mshamu Ali Mshamu, ahsante kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa ni Wizara ya Kilimo. Ninamwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Devota Minja.

Na. 343

**Viwanda vya Kuongeza Thamani Zao la Chikichi**

**MHE. DEVOTA M. MINJA K.n.y. MHE. KIZA H. MAYEYE** aliuliza: -

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuchochea viwanda vya kuongeza thamani ya zao la chikichi ili kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula nje ya nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kula nchini, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuhamasisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mafuta, hususani zao la chikichi. Katika kutekeleza hilo, uzalishaji wa chikichi umeongezeka kutoka tani 51,834.42 mwaka wa fedha 2023/2024 hadi tani 74,302.65 mwaka wa fedha 2024/2025. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vya kuongeza thamani ya zao la chikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi katika mwaka wa fedha 2026/2027 itazalisha na kusambaza miche ya chikichi 2,000,000 katika maeneo ya uzalishaji na kuendelea kuwezesha uchakataji wa zao la chikichi kwa kutoa mashine 18 za kuongeza thamani zao la chikichi

kwenye vyama 18 vya wakulima wa zao hilo. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la chikichi kwa kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 48,000 kwa ajili ya zao la chikichi katika Mikoa ya Kigoma na Morogoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota Minja, swali moja la nyongeza.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali ina mkakati wa kuhakikisha sasa zao la mchikichi linazalishwa katika Mikoa ya Morogoro na Kigoma. Serikali kwa sasa inatumia gharama kubwa sana kuingiza mafuta nchini kwa sababu, hatuna uwezo wa kuzalisha. Iko mikoa mingine mingi ambayo ina uwezo wa kuwa na mazao ya mchikichi mbali na Kigoma na Morogoro. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha mikoa hiyo na yenyewe inazalisha michikichi, ili tupate mafuta ya kutosheleza nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri kwamba, bado tuna changamoto ya uzalishaji wa mafuta nchini, na ndiyo maana moja ya jitihada kubwa ya Serikali sasa ni kuhakikisha kwamba, tunaongeza uzalishaji nchini, na siyo tu kwenye zao la chikichi peke yake, hata alizeti bado tunaweka msisitizo. Kwa hiyo, Wizara imefanya *mapping* ya kuainisha kila zao linafiti eneo gani. Kwa hiyo, kwa tafiti zilizofanyika sasa, inaonesha chikichi inakubali zaidi katika Mikoa ya Kigoma na Morogoro ambako sasa tunataka tuweke msisitizo mkubwa na maeneo mengine ndiyo tutaweka msisitizo kwenye mazao kama ya alizeti, karanga na ufuta, ambayo yote yanaleta matokeo ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jukumu la Serikali ni kuendelea kufanya tafiti. Tukipata katika hayo maeneo mengine, kama mikoa ambayo anaitaja Mheshimiwa Mbunge, tutafanya hivyo, ili kuhakikisha kwamba chikichi inaenda katika maeneo mengi na uzalishaji unaongezeka. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mbunge wa Kyerwa, aweze kuuliza swali lake.

Na. 344

**Uboreshaji wa Kilimo cha Kahawa, Kyerwa**

**MHE. KHALID M. NSEKELA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha pembejeo, huduma za ugani, bei na masoko ya uhakika ya Kimataifa kwa zao la kahawa katika Jimbo la Kyerwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania inatekeleza mpango wa kuzalisha na kusambaza bure miche bora ya kahawa kwa wakulima, ambapo katika kipindi cha msimu wa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2024/2025 jumla ya miche 9,406,192 ya kahawa imesambazwa bure kwa wakulima wa Kahawa, Wilayani Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeimarisha huduma za ugani kwa Wilaya ya Kyerwa kwa kuwapatia Maafisa Ugani pikipiki 33 na mashine moja ya kupimia afya ya udongo. Aidha, jumla ya wakulima 300 wa zao la kahawa wamepatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora cha zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Tasnia ya Kahawa. Lengo la Mkakati huo ni kuimarisha na kuongeza wigo wa mauzo ya kahawa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, Serikali imeanza kutumia Balozi za Tanzania nje ya nchi kuitangaza kahawa ya Tanzania kupitia mikutano, makongamano na maonesho ya Kimataifa, ikiwemo *Africa Fine Coffee Association*

*Conference and Exhibition,* na maonesho makubwa ya kahawa Japan. Jitihada hizi zinalenga kuongeza mauzo ya kahawa yetu katika masoko mapya katika nchi za Algeria, Morocco, China, Korea ya Kusini, Marekani, Canada, Urusi, China, Misri na Japan.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalid Nsekela, swali moja la nyongeza.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, Wilaya ya Kyerwa inaongoza kwa uzalishaji mkubwa wa zao la kahawa, na ni zao ambalo linaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni, je, Serikali haioni kwamba, ni muda muafaka sasa kuifanya Kyerwa iwe sehemu ya kipaumbele na kimkakati kwa ajili ya uzalishaji wa zao hili la kahawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza kaka yangu Khalid Mussa Nsekela, Mbunge wa Kyerwa, kwa swali lake la msingi. Namthibitishia tu kwamba, Kyerwa ni miongoni mwa halmashauri ambazo sisi Wizara ya Kilimo tunaziangalia kwa jicho la karibu. Ndiyo maana utaona katika miaka hii miwili tu ya fedha, tumepeleka miche mingi, na bado tutaongeza, lakini siyo katika halmashauri yake tu, yaani ni katika ule Mkoa mzima wa Kagera. Ni moja ya mikoa ambayo sasa tunafufua kabisa zao la kahawa kwa sababu, ni zao ambalo linatuletea fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo lipo ndani ya mipango, na tunaendelea kutekeleza kwa kuongeza hizo pembejeo, miche pamoja na Maafisa Ugani katika eneo lake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, na sasa ni Wizara ya Ujenzi. Ninamwita Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, aulize swali lake.

Na. 345

**Ujenzi Wa Barabara ya Njiapanda – Mang'ola – Matala**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Njiapanda – Mang'ola – Matala, ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kipindi cha masika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali moja la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweza kutembelea eneo hilo la Bonde la Eyasi, kutoka Karatu – Njiapanda kwenda Eyasi, pia, Naibu Waziri alikuwepo katika msafara huo na alijionea hali ya barabara hiyo ya kutoka Karatu kwenda Mangolo kilometa 50, je, sasa Serikali ina mkakati gani wa kutafuta fedha ili kuitengeneza kwa kiwango cha lami barabara hiyo yenye kilometa 50, ambayo ni kutoka Njiapanda kwenda Mang'ola?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, moja ni kwamba, barabara hii tumeisanifu yote kutoka Karatu, Mang'ola hadi Matala kwenda Sibiti. Bahati nzuri, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nilikuwepo katika ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali, tunatambua kwamba, eneo hili la Mang'ola ndilo linazalisha zao la kitunguu ninadhani Tanzania na kwa Afrika Mashariki nzima. Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba, hiyo barabara walau tuanze kuijenga kwa awamu kwenda Mang'ola ambako tayari pia kuna skimu kubwa sana ya umwagiliaji. Pamoja na kuanza, hata kama ni kwa awamu, ifike kwenye hospitali ya Wilaya, kilometa tano, ambayo pia ipo katika hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, maelekezo ya Waziri Mkuu yamezingatiwa, na tumeiweka katika mpango wa kuanza kuijenga, endapo tutakuwa tumepitishiwa bajeti yetu ambayo tunategemea kuiwasilisha katika siku zinazofuata, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninakushukuru kwa majibu yako hayo muhimu, tutayafuatilia.

Tunaendelea, na sasa ninamwita Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, aweze kuuliza swali lake.

Na. 346

**Ujenzi wa Barabara ya Nzega hadi Kagongwa**

**MHE. JOHN S. LUHENDE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Nzega – Itobo – Igusule hadi Kagongwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Nzega – Itobo – Igusule hadi Kagongwa, kilometa 65, unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 18.3 kuanzia Kagongwa hadi Igusule zimejengwa mpaka tabaka la tatu la barabara kwa ufadhili wa mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta *(EACOP)*. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kumalizia ujenzi wa tabaka la lami kwa sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu ya barabara hii iliyobaki kuanzia Igusule hadi Nzega, urefu wa kilometa 46.7 itajengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Luhende, swali moja la nyongeza.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Serikali kwa sasa ina ujenzi mkubwa wa *SGR*, wananchi wa Wilaya ya Nzega na Wilaya ya Igunga tunategemea kutumia mradi huo kupitia Barabara hiyo ya Nzega – Itobo hadi Bukene. Je, nini mpango wa Serikali kuhusu ukamilishaji wa barabara hiyo ili tuweze kunufaika na *SGR* wakati itakapokamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Serikali na hasa kwa vituo vyote vya *SGR*, vituo vyote vimeainishwa ambavyo wananchi watakuwa wanavitumia wakati wa *SGR* na vimepangiwa bajeti vijengwe, yaani barabara zijengwe kutoka kwa wananchi hadi kwenda kwenye vituo, kuanzia Dar es Salaam mpaka kote Mwanza na mpaka Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara zote zimeainishwa. Kama hiyo itakuwa ni moja ya barabara, basi iko kwenye mpango wa kuijenga ili kuwaunganisha wananchi kwenye barabara kubwa na vituo vya *SGR* kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa Mheshimiwa Mbunge, kama Bukene ndiyo kituo kikuu ambacho *SGR* itakuwa na kituo, nitaomba tuonane ili tuweze kujiridhisha kama ni moja ya vituo ambavyo vitajengwa barabara ya lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Sasa ninaomba tuwatambue wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo.

Tunaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, ambao ni wageni 21. Hawa ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wameongozwa na Balozi; na Mheshimiwa Balozi Said Juma Mshana ambaye ni Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Balozi Jean Pierre Massala, ambaye ni Balozi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo hapa nchini. Waheshimiwa Mabalozi karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Mheshimiwa Willy Mishiki Buhini, huyu ni Mbunge wa Bunge la Taifa na Kiongozi wa msafara kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo; Mheshimiwa Musongela Horie Yvonne, Mbunge wa Bunge la Taifa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Amin Kabaka Shemu, Mbunge wa Bunge la Taifa; Mheshimiwa Yanik Baruan Lumbala, Mbunge wa Bunge la Taifa; Ndugu Tibutu Katota Albert, Msaidizi kutoka Bunge la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo; Ndugu Mawete Malondika Binevo, Mtaalamu wa Mafuta na Nishati kutoka *DRC*; Ndugu

Gabriel Juakali, Mtaalamu wa Ulinzi na Usalama kutoka *DRC;* naNdugu Prince Kasikuza Ndegesi, Mtaalamu wa Ulinzi na Usalama, kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni Ndugu Bea Mujula Frida, Afisa wa Habari na Mawasiliano kutoka nchini; Ndugu Mondanangulu Tambwe Edmond, Afisa kutoka Ubalozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo hapa nchini; Ndugu Joseph Steven Lizer, Afisa kutoka Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo; na Ndugu Abdallah S. Kirungu, Afisa Mambo ya Nje Mkuu, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Wengine ni Ndugu Mwita Hamis Nyandoto, Afisa Mambo ya Nje kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Ndugu Emilian Kikweku Afisa Mambo ya Nje, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Ndugu Tarik Kasi Chamzimi, Afisa Mambo ya Nje, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Ndugu Rose Shayo, Afisa Habari, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Ndugu Philip Haule, Afisa Mambo ya Nje, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Ndugu Safieli Edmund Manongi, Afisa Mambo ya nje, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, pamoja na wageni wote karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Waziri wa Mifugo, Balozi, Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ali Kakurwa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, iliyochambua na kushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2025/2026, sasa ninaomba kutoa hoja kuwa, Bunge lako Tukufu likubali na kupokea na kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha na mpango wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2026/2027. Ninaomba hotuba yangu yenye kurasa 189 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na pongezi; awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na ukarimu kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Bajeti ikiwa ni mkutano mahsusi wa Bunge wa kufanya uamuzi kuhusu masuala ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, na hivyo kupata imani na ridhaa ya umma ya kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Mbunge na kisha kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ninamwahidi kwamba, nitafanya kazi zangu kwa utii, bidii na uadilifu. Vilevile ninampongeza Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawapongeza Bi. Agnes Kisaka Meena, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu; Dkt. Dkt. Fabian Magawa Madele, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Mifugo; na Prof. Mohammed Ali Sheikh, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi pamoja na Wabunge wenzangu tunayo imani kwamba, Mheshimiwa Zungu ataliongoza Bunge letu kwa misingi ya usawa, umahiri na weledi mkubwa. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, pamoja na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu. Aidha, ninampongeza Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uratibu na ushirikiano wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninawashukuru viongozi, Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi makini wa bajeti yetu. Ushauri wao umewezesha Wizara kufanya maboresho stahiki na ya kimkakati. Hakika, Kamati hii imetusaidia sana na inaendelea kutusaidia. Kwa upande wetu tunaahidi kuendelea kuipatia Kamati hii ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii adhimu, kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge, na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mbunge wa Kundi la Vijana kutoka Mkoa wa Mwanza, kwa umahiri wake mkubwa wa kuchapa kazi, ushauri na ubunifu wake wenye tija uliotusaidia sote katika uongozi na usimamizi wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa ridhaa yako, nitoe taarifa fupi kwamba tarehe 11 Mei, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani alijifungua salama mtoto mrembo wa kike, kwa jina anaitwa Francine Francisco. Kwa hiyo, ninaye Naibu Waziri pamoja na Msaidizi wa Naibu Waziri. Kwa hiyo, nimekamilika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Ndugu Agnes Kisaka Meena, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Fabian Magawa Madele, Naibu Katibu Mkuu Mifugo na Prof. Mohammed Ali Sheikh, Naibu Katibu Mkuu Uvuvi, kwa kuwa viongozi mahiri, wabunifu na wanaojituma katika kuziendeleza sekta za mifugo na uvuvi na kwa kuwasimamia watumishi wa Wizara ninayoiongoza, kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa dhati ya moyo wangu ninawashukuru sana watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu kikamilifu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwashukuru wadau wa sekta za mifugo na uvuvi, wakiwemo wawekezaji na wafanyabiashara wa pembejeo na mazao ya mifugo na uvuvi, wafugaji, wavuvi, wakuzaji viumbe maji, wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi, wahifadhi wa mazingira, ekolojia pamoja na wadau wengine katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Aidha, mchango wao umeendelea kuchangia katika kutoa ajira, kuimarisha Uchumi wa Buluu na usalama wa chakula pamoja na lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kuwashukuru wadau wa maendeleo, taasisi za fedha na mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika juhudi za Serikali za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiendelea na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vifo vya Wabunge wenzetu, ambao ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Wafanyakazi. Tunawaombea Marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya sekta ya mifugo na uvuvi kwa muhtasari. Sekta ya mifugo imeendelea kuwa sekta muhimu katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa Taifa. Kwa mwaka 2024 sekta ya mifugo ilichangia 6.2% ya pato la Taifa na

kukua kwa 5.0. Aidha, zaidi ya kaya milioni 6.5 zinafanya shughuli za ufugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ina mchango mkubwa katika usalama wa chakula, uzalishaji wa malighafi za viwanda, ajira na kuchangia ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni, kupitia mauzo ya mifugo na mazao yake nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa mifugo wa aina mbalimbali nchini, hatua iliyochangia kuongezeka kwa idadi na thamani ya mifugo hiyo. Thamani ya jumla ya mifugo imeongezeka kutoka shilingi trilioni 33.22 mwaka 2024/2025 hadi shilingi trilioni 34.33 mwezi Aprili, 2026 kwa makundi yote ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa idadi ya mifugo katika kipindi cha marejeo. Mathalan, idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 39.24, hadi milioni 40.57, mbuzi kutoka milioni 28.59 hadi milioni 29.60 na kondoo kutoka milioni 9.66 hadi milioni 9.94, kuku kutoka milioni 108.22 hadi milioni 113.36 na nguruwe wameongezeka kutoka milioni 4.13 hadi milioni 4.36. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa tisa hadi wa 10 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo, ambapo uzalishaji wa wanyama umeongezeka kwa asilimia nne nukta nne kutoka tani milioni 1.05 zenye thamani ya shilingi trilioni 10.38, mwaka 2024/2025 hadi tani milioni 1.1 zenye thamani ya shilingi trilioni 10.84, Aprili 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuuza mifugo yao, kutolewa kwa elimu ya uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo, kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa, uboreshaji wa mbari za mifugo na kukuwa kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 11 na 12 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026 uzalishaji wa mayai umeongezeka kwa 10.87% kutoka milioni 7.11 mwaka 2024/2025 hadi milioni 7.88 mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa vituo 28 vya kutotolesha vifaranga vya kuku vilivyopo nchini, mashamba 26 ya kuku wazazi, kuongezeka kwa ufugaji wa kuku wa mayai na hatua mbalimbali ambazo Serikali imezichukua, ikiwemo udhibiti wa magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mbegu za malisho umeongezeka kwa 85.05% kutoka tani 222.54 mwaka 2024/2025 hadi tani 411.25 mwaka 2025/2026 kutoka kwenye mashamba ya Serikali na binafsi. Aidha, uzalishaji wa malisho umeongezeka kwa 128.49% kutoka tani 14,185 mwaka 2024/2025 hadi tani 32,411.31 mwaka 2025/2026. Vilevile, usindikaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani 720,000 mwaka 2024/2025 hadi tani 897,750 mwaka 2025/2026 sawa na 56.11% ya lengo la kusindika tani milioni 1.6. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 13 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuratibu na kutekeleza kampeni kabambe ya chanjo na utambuzi wa mifugo kitaifa, ambapo hadi Aprili, 2026 jumla ya mifugo milioni 50.62 imechanjwa na kutambuliwa ikiwa na sawa na 66.2% ya lengo la kuchanja na kutambua mifugo milioni 76.32 kwa mwaka. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 14 na 15 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi. Sekta hii imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu, ambapo katika mwaka 2024 sekta hii ilichangia 1.6% ya pato la Taifa na kukua kwa asilimia mbili nukta tatu. Aidha, sekta ya uvuvi imeendelea kunufaisha Watanzania wapatao milioni sita katika mnyororo wa thamani, wakiwemo wavuvi 205,556 na wakuzaji viumbe maji 53,992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sekta ya uvuvi ni nguzo muhimu katika kuimarisha usalama wa chakula na lishe na inachangia 30% ya protini inayotokana na wanyama. Hadi Aprili,

2026, uzalishaji wa mazao ya uvuvi nchini umeongezeka kwa 10.02% kufikia tani 659,242.69 zinazojumuisha tani 477,661.93 kutoka uvuvi wa asili na tani 181,580.76 kutoka ukuzaji viumbe maji ikilinganishwa na tani 599,200.33 zinazojumuisha tani 466,956.88 kutoka katika uvuvi wa asili na tani 132,243.45 kutoka ukuzaji viumbemaji zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hadi Aprili, 2026 tani 37,988.30 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 493.16 na samaki wa mapambo 209,772 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.46 waliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa mrabaha wa shilingi bilioni 13.42. Aidha, ulaji wa samaki nchini kwa mtu kwa mwaka umeongezeka kwa 27.8% kutoka kilo 7.9 mwaka 2024/2025 hadi kilo 10.1 mwaka 2025/2026. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 15 hadi 16 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026. Bajeti iliyoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 99 iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 476.65, ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 101.52 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 375.14 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida, katika mwaka 2025/2026 Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 101.52 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 47.26 ni mishahara na shilingi bilioni 54.25 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hadi Aprili, 2026 shilingi bilioni 66.04 zimepokelewa, sawa na 65.05% ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 33.51, sawa na 70.90% ni kwa ajili ya mishahara; na shilingi bilioni 32.53 sawa na 59.95% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 375.14 kwa ajili ya

kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 227.99 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 147.14 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026 jumla ya shilingi bilioni 120.37 sawa na 32.08% ya bajeti ya maendeleo zimepokelewa, ambapo shilingi bilioni 95.30 sawa na 41.80% ni fedha za ndani na shilingi bilioni 25.07 sawa na 17.03% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli ya Serikali katika mwaka 2025/2026 ya Wizara Mifugo na Uvuvi ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 94.11. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 49.90 kilipangwa kukusanywa kupitia sekta ya mifugo na shilingi bilioni 44.20 kupitia sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusanyo ya kila mwezi, sekta ya uvuvi ilitarajiwa kukusanya wastani wa shilingi bilioni 3.68 na sekta ya mifugo ilitarajiwa kukusanya wastani wa shilingi bilioni 4.16. Hadi Aprili 30, 2025 Wizara imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 66.92 sawa na 85.3% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 78.42 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika makusanyo hayo, sekta ya mifugo imekusanya shilingi bilioni 34.13 kati ya shilingi bilioni 41.58 ya lengo la miezi 10, sawa na 82%; na sekta ya uvuvi imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 32.79 kati ya shilingi bilioni 36.84, sawa na 89% ya lengo la miezi 10. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 17 hadi 22 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea na hatua za kuunganisha Bodi ya Nyama Tanzania na Bodi ya Maziwa Tanzania ili kuunda bodi itakayosimamia mazao yote ya Mifugo. Bodi hiyo itakuwa na jukumu la kuratibu, kuendeleza, kuhamasisha na kusimamia uzalishaji, usindikaji, biashara pamoja na mazao yote ya mifugo. Uundaji wa bodi hiyo uko katika hatua za mwisho za maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na mpango wa kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Mamlaka itakayoundwa itawezesha usimamizi endelevu wa rasilimali za

uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Kuongezeka ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya uvuvi, usalama wa chakula ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa. Uundaji wa mamlaka hiyo ya uvuvi upo katika hatua za mwisho za maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za uhimilishaji, katika mwaka 202025/2026 Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji *(Nike)* kimezalisha jumla ya dozi 72,747 za mbegu na kuzisambaza, sawa na 48.50% ya lengo la kuzalisha dozi 150,000. Vilevile Wizara imewajengea uwezo wahimilishaji 60 kutoka katika mamlaka za Serikali za mitaa na kuendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji, ambapo hadi Aprili, 2026 jumla ya ng'ombe 74,345 wamehimilishwa katika mikoa 26 ya Tanzania bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uzalishaji na usambazaji wa mitamba, katika kuboresha mbari za mifugo nchini Serikali inaendelea kuyaimarisha mashamba matano ya kuzalisha Mifugo ya *Sao Hill* lililoko Mufindi, Mabuki lililoko Misungwi, Ngerengere lililoko Morogoro na Ngaramo lililoko Masasi, pamoja na Kitulo lililoko Makete yenye jumla ya ng'ombe 7,355 ikilinganishwa na ng'ombe 6,542 waliokuwepo mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka 2025/2026 mashamba hayo yamezalisha jumla ya mitamba bora 826, sawa na 82.6% ya lengo la kuzalisha mitamba 1,000 ambapo mitamba 177 imesambazwa kwa wafugaji. Pia mashamba ya watu binafsi manane yamezalisha mitamba bora 3,508 na kusambaza mitamba 3021. Serikali itaendelea kuboresha mashamba yake kwa kuyawezesha zaidi kutokana na ongezeko la mahitaji ya wafugaji kuhitaji mitamba bora ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeingiza jumla ya ng'ombe 5,328, mbuzi na kondoo 24,540 na nguruwe 171 wa mbegu kutoka nchi za Kenya, Afrika Kusini, Uganda, Ufaransa na Namibia. Aidha, kwa madhumuni hayo jumla ya dozi 22,567 za mbegu za ng'ombe na jumla ya dozi 40 za mbegu bora za nguruwe ziliagizwa kutoka nchi za *Denmark*, *Brazil*, Ufaransa, Afrika Kusini na Marekani. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 30 hadi 33 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uzalishaji wa kuku wa wanyama na mayai, Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa kuku ikiwemo uanzishwaji wa mashamba ya kuku wazazi na vitotoleshi, ambapo hadi Aprili, 2026 jumla ya mashamba 27 yameanzishwa na kuendelezwa. Hadi Aprili, 2026 jumla ya vifaranga vya kuku milioni 83.93 vimezalishwa, kusambazwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi. Uwekezaji huo umechangia kupungua kwa uingizaji wa vifaranga vya kuku wazazi kutoka milioni 1.16 mwaka 2024/2025 hadi vifaranga milioni 1.03 mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mauzo ya vifaranga kwenda nje ya nchi yameongezeka kutoka vifaranga milioni 1.91 mwaka 2024/2025 hadi vifaranga milioni 5.75 mwaka 2025/2026. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 32 hadi 34 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya mifugo na mazao yake, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia mauzo ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi Aprili 26 jumla ya tani 12,763.77 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 54.65 zimeuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 9,913.61 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 40.37 zilizouzwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la 22.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yamefikiwa kupitia hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayoendelea kuifanya kwa umahiri kupitia diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kusimamia biashara ya maziwa nchini ambapo jumla ya lita za maziwa milioni 101.48 zenye thamani ya shilingi bilioni 152.2 zilisindikwa na kuuzwa katika masoko ya ndani na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vibali vya kuingiza maziwa kutoka nje ya nchi vimepungua kutoka vibali 630 vyenye jumla ya

lita milioni 11.55 zenye thamani ya shilingi bilioni 22.97 mwaka 2024/2025 hadi vibali 609 vyenye jumla ya lita milioni 10.09 zenye thamani ya shilingi bilioni 21.62 kwa mwaka 2025/2026, kutokana na hatua za Serikali za kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuongeza usindikaji ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ngozi imeendelea kuimarika, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya vipande vya ngozi ghafi milioni 2.27 vyenye uzito wa kilo milioni 7.08 na thamani ya shilingi bilioni 8.07 viliuzwa katika nchi za Nigeria, Kenya, Jibuti, Ethiopia, China, Ghana, Togo na Pakistani, ikilinganishwa na vipande vya ngozi milioni 1.65 vyenye uzito wa kilo milioni 6.29 na thamani ya shilingi bilioni 7.95 vilivyouzwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika ngozi, ambapo hadi Aprili, 2026 jumla ya vipande 478,850 vya ngozi ya ng'ombe na 994,000 vya ngozi za mbuzi na kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 37.17 vimesindikwa katika hatua za awali; na vipande 522,898 vimesindikwa hadi hatua ya kati na kuuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi milioni 668.79. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 34 hadi 40 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, ardhi ya malisho na vyakula vya mifugo; Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi imeendelea kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyowezesha kutenga hekta 196,324.25 za maeneo ya malisho mwaka 2025/2026. Mipango hiyo imefanyika katika vijiji 187 vya wilaya 22 katika mikoa 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii imewezesha ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho kufikia jumla ya hekta milioni 3.69 kwa mwaka 2025/2026 kutoka hekta milioni 3.49 mwaka 2024/2025. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2026 hekta milioni 1.35 katika vijiji 365 zimepimwa na kutangazwa. Hekta 216,971.56 katika vijiji 114 zimefanyiwa upembuzi na uhakiki kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mbegu za malisho hapa nchini umeongezeka kwa 85.5% kutoka tani 222.54 mwaka 2024/2025 hadi tani 411.25 mwaka 2025/2026 kwenye mashamba ya Serikali na binafsi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.78. Aidha, uhifadhi wa malisho umeongezeka kwa 128.49 kutoka tani 14,185 mwaka 2025/2025 hadi tani 32,411.31 mwaka 2025/2026 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.03.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya udhibiti wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali imewatambua jumla ya wafugaji 321 katika Halmashauri za Mvomero, Gairo, Kilombero, Kilosa, Malinyi, Ulanga, Mlele, Sikonge, Kaliua, Urambo, Bahi, Kibaha, Mbarali, Magu na Sengerema. Hatua hizo zinalenga kuwapatia wafugaji elimu ya umiliki wa ardhi, matumizi endelevu ya raslimali za malisho na kuhamasisha upangaji wa ardhi ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ushirikishwaji wa wadau katika uendelezaji wa maeneo ya malisho, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Watu na Wanyamapori imewezesha uendelezaji wa hekari 1,285 katika vijiji 26 kwa kuondoa vichaka, mimea vamizi na kudhibiti mmomonyoko wa udongo kwa kufukia makorongo yenye urefu wa kilometa 173 katika kongani za malisho za Leleki, Muliamunyi, Muliatata katika Wilaya za Longido, Sepeko katika Wilaya ya Monduli na Mwada Ngaiti katika Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia programu ya *Sustainable Nature Based Livelihoods* imeuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji, ambapo vijiji 44 vya Wilaya za Simanjiro, Longido na Mbulu vimeandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kutenga maeneo 53 ya malisho yenye jumla ya hekta 790,865.54 ambazo zimepatiwa hatimiliki za kimila kwa lengo la kuimarisha umiliki na usimamizi wa maeneo hayo, hivyo kuchangia kuongezeka kwa upatikanaji wa malisho. Taarifa

zaidi inapatikana katika ukurasa wa 40 hadi 44 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uendelezaji wa raslimali za vyakula vya mifugo, katika mwaka 2025/2026 jumla ya maeneo 949 ya kuzalisha kuuza na kuhifadhi rasilimali za vyakula vya mifugo yamekaguliwa na kupatiwa vibali. Aidha, jumla ya maeneo mapya 57 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Shinyanga, Dodoma, Kagera, Kilimanjaro, Tanga, Rukwa na Mwanza ya kuzalisha vyakula vya mifugo yamesajiliwa. Usajili huu umeongeza maeneo ya kuzalisha vyakula vya mifugo kutoka maeneo 279 mwaka 2024/2025 hadi maeneo 336 mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 uzalishaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka hadi tani 898,750 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.44, ikiwa ni ongezeko la 24.69% ikilinganishwa na tani 720,000 mwaka 2024/2025 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.15. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 45 hadi 46 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti, mafunzo na huduma za ugani: Utafiti wa mifugo na uvuvi. Katika mwaka wa 2025/2026 jumla ya miradi 51 ya utafiti inayohusu uboreshaji wa mbari za mifugo, nyanda za malisho na wingi wa mtawanyiko wa samaki katika eneo la Ziwa Tanganyika na ukanda maalum wa uchumi wa bahari imeratibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile taasisi za *TALIRI* na *TAFIRI* zimesambaza teknolojia 19 zilizoibuliwa kutokana na utafiti uliofanyika kwa lengo la kuwafikia wadau katika mnyororo wa thamani wa sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mafunzo ya mifugo na uvuvi, katika mwaka 2025/2026 Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi *(LITA* na *FETA)* imeongeza udahili kutoka wanafunzi 6013 mwaka 2024/2025 hadi wanafunzi 6,088 mwaka 2025/2026. Aidha, kupitia wakala hizo, Wakala inaendelea na zoezi la kuhuisha mitaala mbalimbali ikiwemo mitaala ya mtawala wa mafunzo ya usimamizi wa bandari za uvuvi na

logistiki na mitaala na mtawala wa teknolojia ya uzalishaji wa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za ugani nchini, Wizara imetoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani wa Mifugo na Uvuvi 1,123 kutoka katika halmashauri 184 kuhusu Usimamizi wa Sheria za Mifugo na Uvuvi; Uanzishwaji wa Mashamba ya Malisho ya Mifugo; Mbinu Bora za Ukuzaji Viumbe Maji; Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Uvuvi; na Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo hayo ni mwendelezo wa kuwapatia mafunzo rejea Maafisa Ugani nchini ambapo jumla ya Maafisa Ugani 2,781 kati ya 5006 waliopo wamepatiwa mafunzo rejea. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 46 hadi 50 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho iliyo Bora *(BBT),* ambapo Serikali imetoa shilingi bilioni saba ili kuwawezesha vijana 308 kuwekeza katika miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba, kilimo cha mwani, ufugaji wa majongoo bahari na unenepeshaji wa kaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, imepokea jumla ya shilingi bilioni 23.69 zilizotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuwawezesha vijana kupata mikopo yenye masharti nafuu ya kuwekeza katika sekta za mifugo na uvuvi. Fedha hizi zilitolewa kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Siku 100 za Uongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026 Wizara imepokea na inaendelea kuchambua jumla ya maombi 3004 ya vijana wanaohitaji kujiajiri katika minyororo ya thamani ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia fedha hizi. Fedha hizi zinasimamiwa na benki yetu ya kilimo ya *TADB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeanza kutekeleza mradi wa *BBT* wa miaka mitano katika kituo chake cha Taasisi ya *TALIRI* - Kongwa. Mradi huu unalenga kuwawezesha vijana na

wanawake kujiajiri kupitia mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo hususan unenepeshaji wa mbuzi kibiashara, uzalishaji wa malisho kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji pamoja na uchakataji wa vyakula vya mifugo kibiashara. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 50 hadi 52 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji na usambazaji wa chanjo za magonjwa 13 ya kipaumbele. Katika kuimarisha upatikanaji wa chanjo za magonjwa yanayoathiri afya ya mifugo na biashara za kikanda na Kimataifa pamoja na magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, upatikanaji wa usambazaji wa chanjo nchini umeongezeka kutoka dozi milioni 728.15 mwaka 2024/2025 hadi dozi milioni 750.33 Aprili, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uzalishaji wa chanjo ndani ya nchi yetu umeongezeka kutoka dozi milioni 153.93 mwaka 2024/2025 hadi dozi milioni 200.92 Aprili 2026. Ongezeko hilo limechangiwa na hatua mbalimbali za kuhamasisha wafugaji kuchanja Mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuiwezesha Tanzania kufikia vigezo vya Kimataifa katika biashara ya mifugo na mazao ya mifugo, katika mwaka 2025/2026 Serikali imeendelea kusimamia kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo Kitaifa iliyozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kampeni hiyo, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya dozi milioni 19.10 za chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe, sokota ya mbuzi, na kondoo dozi milioni 17.22, na mdondo wa kuku dozi milioni 40.00. Pia, kampeni hiyo imewezesha kufunguka kwa soko la nyama na vifaranga vya kuku wa mayai katika nchi za Qatar, Ushelisheli, Sierra Leone, Cote d'Ivoire, na China. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 52 hadi 56 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2025/2026 uzalishaji wa samaki umeongezeka kwa asilimia saba nukta nne kufikia tani 526,763.40 zenye thamani ya shilingi trilioni 4.90 ikilinganishwa na

tani 490,372.83 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.12 zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uzalishaji huu bado haukidhi mahitaji ya samaki ambayo ni wastani wa tani milioni 1.25 kwa mwaka. Serikali inaendelea na hatua mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya samaki nchini zikiwemo kudhibiti uvuvi usiozingatia sheria, kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, kuhamasisha na kuwekeza katika shughuli za viumbe maji pamoja na kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika maji ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kuwa kinara wa uzalishaji wa mwani Barani Afrika ambapo hadi Aprili, 2026, tani 132,479.29 za mwani zenye thamani ya shilingi bilioni 13.91 zimezalishwa ikilinganishwa na tani 88,615.2 zenye thamani ya shilingi bilioni 9.30 zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 49.5%. Ongezeko hili linatokana na hatua za Serikali za kuhamasisha uzalishaji kwa kuwapatia wakulima wa mwani mafunzo, pembejeo, kuhamasisha matumizi ya bidhaa zitokanazo na mwani, na kuimarika kwa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la ndani imeendelea kuimarika ambapo hadi mwezi Aprili, 2026 jumla ya tani 439,673.63 zenye thamani ya shilingi bilioni 4.20 ziliuzwa katika soko la ndani, ikilinganishwa na tani 422,639.10 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.83 zilizouzwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarika kwa biashara ya samaki katika soko la ndani kumetokana na kuimarika kwa miundombinu ya ubaridi ya kuhifadhi mazao ya uvuvi, na miundombinu ya usafirishaji wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa lengo la kudhibiti uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi isiyozingatia sheria, Wizara imefanya doria zenye siku kazi 4,202 sawa na 50.02% ya siku kazi 8,400 zilizopangwa kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya doria hizo yaliwezesha kukamatwa kwa zana mbalimbali zisizoruhusiwa kisheria, ikiwemo nyavu za timba 4,768, nyavu za makila 2,167, nyavu za dagaa 4,075, nyavu za kokoro 9048 ikiwemo kokoro la mita 700 yaani viwanja saba vya Benjamin Mkapa, lililokamatwa katika halmashauri ya Uvinza mkoani Kigoma. Vilevile, watuhumiwa 1,047 waliokuwa wakifanya shughuli za uvuvi kinyume cha sheria walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Kokoro hili lilivutwa kwa masaa sita baada ya wananchi kula ugali wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali kwa kuvipatia boti 10 na pikipiki 40 kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uvuvi. Aidha, Wizara inaendelea kuwezesha upatikanaji wa ndege nyuki mbili, gari tatu, na pikipiki 14 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika maziwa makuu na bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kuimarisha udhibiti na ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya ukaguzi kwenye maeneo ya uzalishaji, masoko, na vituo vya mipakani vya kusafirisha mazao nje ya nchi. Taarifa ya kina inapatikana katika ukurasa wa 64 hadi 66 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2025/2026, jumla ya vibali 245 vimetolewa vikijumuisha vibali 94 vya kuingiza chakula cha samaki kutoka nje ya nchi, vibali 76 vya kusafirisha mwani mkavu nje ya nchi, na vibali 75 vya ukuzaji viumbe maji kibiashara. Aidha, leseni tisa za kusafirisha mwani kwenda nje ya nchi zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026, uzalishaji wa vifaranga vya samaki umeongezeka kwa 63.6% kufikia milioni 202.67 ikilinganishwa na vifaranga milioni 123.88 vilivyozalishwa mwaka 2024/2025. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa idadi ya vitotoleshi kutoka 49 hadi 66. Aidha, matumizi ya chakula bora cha samaki yameongezeka kwa 34.7% kufikia tani 20,510.69 kutoka tani 15,226.67 za mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, jumla ya wananchi 21,910 wamepatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki, ikilinganishwa na wananchi 11,216 kwa mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 95.3%. Pia, wakulima 5,595 wa mwani wamepatiwa mafunzo ikilinganishwa na wakulima 2,565 mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 118.8%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ujenzi wa mabwawa na vizimba umeongezeka, ambapo hadi Aprili, 2026 yamefikia mabwawa 35,720 na vizimba 3,343, ikilinganishwa na mabwawa 34,642 na vizimba 1,636 kwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia tatu nukta moja na 104.3% mtawalia. Hapa niipongeze Serikali kupitia Mheshimiwa Rais kwa mchango wake na fedha alizozitoa kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika ufugaji wa samaki, ambapo hadi Aprili, 2026, jumla ya matanki 353 yanayotumia mifumo ya kurejeleza maji yamesanikishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kupandikiza samaki katika maji ya asili ili kuongeza upatikanaji wa samaki kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kwa wananchi. Hadi Aprili, 2026, Wizara imepandikiza vifaranga 844,000 vya samaki katika ziwa Ikimba lililopo Wilaya ya Bukoba, Bwawa la Haubi lililopo Wilaya ya Kondoa, Dodoma, na Bwawa la Gereza la Kwamngumi lililoko Korogwe, Tanga. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 58 hadi 70 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia taasisi za mifugo za *TALIRI, LITA, NARCO, TMB, TDB, NIC,* na *TVLA,* imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa katika kuimarisha sekta ya mifugo na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Taarifa zaidi kuhusu utendaji na utekelezaji wa taasisi hizi upo katika ukurasa wa 70 hadi 88 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia taasisi za Uvuvi za *TAFIRI, FETA, MPRU, NLQC*, maabara ya Uvuvi, na *DSFA*, pia

zimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa katika kuimarisha sekta ya uvuvi na kuongeza kipato kwa wananchi pamoja na pato la Taifa. Taarifa ya kina ya utekelezaji wa taasisi hizi nilizozitaja upo katika ukurasa wa 88 hadi 100 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania, Wizara kupitia ufadhili wa programu ya kuendeleza uchumi na jamii ya Japan, imekabidhiwa meli ya kisasa, *TAFICO FV.01* ya Uvuvi wa bahari kuu, ambayo ilizinduliwa kwa kishindo na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 25 Aprili, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale waliofuatilia, shughuli haikuwa ndogo. Meli hiyo itaendeshwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP).* Aidha, upatikanaji wa meli hii ni mojawapo ya hatua ya kimkakati katika kuimarisha *TAFICO* na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea kuimarisha *TAFICO* kwa kuipatia vitendea kazi na miundombinu ya kisasa. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 91 hadi 100 wa kitabu cha hotuba. *TAFICO* ilikuwa tayari imelala usingizi fofofo, sasa hivi imezinduka na inaamka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Wizara kupitia mradi wa *ASDP II*, imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko yenye thamani ya shilingi bilioni 280.59 ambapo hadi Aprili, 2026, ujenzi huu umefikia 97% na fedha zote hizi ni fedha za Watanzania, ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa bandari hiyo, kutatoa ajira za moja kwa moja 300, na ajira 3,000 katika mnyororo wa thamani. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa masoko ya samaki sita, na inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za ununuzi wa meli nyingine mbili za uvuvi wa bahari kuu, pamoja na ujenzi wa mialo 30 ya samaki. Taarifa ya kina inapatikana katika ukurasa wa 100 hadi 112 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kuchochea uzalishaji, na kuongeza tija katika sekta za mifugo na uvuvi, Wizara kupitia Dawati la Mitaji na Uwekezaji imewaunganisha wadau wa sekta binafsi na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na benki za *CRDB, Equity Bank, NMB, TADB* na *TCB*, imewezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 698.14. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 417.69 zilitolewa kwa sekta ya uvuvi kwa wanufaika 27,114, na shilingi bilioni 280.45 zilitolewa kwa sekta ya mifugo kwa wanufaika 5,356.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, jinsia, na UKIMWI; katika kuimarisha utawala bora na utoaji wa huduma kwa wananchi, jumla ya watumishi 89 wameajiriwa, 76 wamepandishwa vyeo, 22 wamebadilishwa kada, na wanane wameteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi. Aidha, Wizara imewezesha watumishi 113 kushiriki bonanza la michezo na mashindano ya SHIMIWI ili kuimarisha afya zao na kupunguza magonjwa sugu yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2025/2026 Wizara ilihamasisha jumla ya watumishi 1,041 kujikinga na VVU na UKIMWI na magonjwa mengine sugu yasiyoambukiza kwa kutoa vifaa kinga na kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari, ambapo jumla ya watumishi 107 walihamasishwa na kupima afya zao kwa magonjwa sugu yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya habari na mawasiliano; katika mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha mifumo ya *TEHAMA* ya Wizara inatoa huduma bora kwa wananchi na inasomana na mifumo mingine ndani ya Serikali. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 112 hadi 117 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa bajeti kwa mwaka 2026/2027; mpango wa bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99, kwa mwaka 2026/2027 umeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa maandalizi ya Mpango wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mpango wa

Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano awamu ya nne kwa kipindi cha 2026/2027 hadi 2030/2031, Mpango Kabambe wa Kilimo 2050, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Hotuba ya kuzindua Bunge la Kumi na Tatu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa bajeti wa Wizara pia umezingatia programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili, *(ASDP II)* na Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2022/2023 hadi 2036/2037, na Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi ya Mwaka 2021/2022, 2026/2027. Masuala mengine yaliyozingatiwa katika kuandaa Mpango huo yanahusu Sera za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027, mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo: kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi; kuhamasisha uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi; na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwenye sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,; katika mwaka 2026/2027, Fungu 99 limepangiwa kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 166. Kati ya kiasi hicho, shilingi 94, 494, 998,000 zinatarajiwa kukusanywa kupitia sekta za mifugo, na shilingi bilioni 71,503,002,000 kupitia sekta ya uvuvi. Taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 117 hadi 124 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi na kazi zitakazotekelezwa mwaka 2026/2027:

(i) Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya masoko ya Mifugo na Uvuvi, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa minada, mialo, maghala, pamoja na vituo vya kukusanyia maziwa;

(ii) Kukamilisha usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa Bandari ya pili ya Uvuvi, Bagamoyo;

(iii) Kuendelea kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa pamoja na ng'ombe wa nyama;

(iv) Kuendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo na utambuzi wa mifugo;

(v) Kuendelea kutafuta masoko ya bidhaa za mifugo na uvuvi;

(vi) Kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho pamoja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya malisho;

(vii) Kuendelea kuwezesha vijana kujiajiri katika sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia mikopo yenye riba nafuu;

(viii) Kuendelea kufanya tafiti na kutoa mafunzo kwenye sekta za mifugo na uvuvi;

(ix) Kuendelea na ujenzi wa jengo la maabara ya veterianari, Dodoma;

(x) Kuendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi;

(xi) Kukamilisha ununuzi wa meli mbili mpya za uvuvi wa bahari kuu; na

(xii) Kuendelea kusambaza mbegu bora za mifugo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zaidi inapatikana katika ukurasa wa 125 hadi 158 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha hotuba yangu, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio katika mwaka 2025/2026, ambayo yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi

kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwemo mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa, asasi zisizokuwa za kiserikali, sekta binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zaidi kuhusu wote ambao tunatambua mchango wao inapatikana katika ukurasa wa 159 hadi 163 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaomba kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia, na bahati nzuri watatu ni Wabunge katika Bunge hili la Kumi na Tatu; Mheshimiwa Ndaki, Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Ashatu. Wamejenga msingi imara ambao mimi na wenzangu tunajisikia fahari kuwa sehemu ya mchango wao, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninampongeza na kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na maarifa na ustahimilivu. Ninamshukuru pia kwa maelekezo anayotupatia kama Wizara kuhakikisha rasilimali za mifugo na uvuvi zinachangia katika Uchumi wa Buluu ili kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaomba kutumia jumla ya shilingi 433,379,125,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 98,279,420,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 335,099,705,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo: Fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi 98,279,420,000, matumizi ya mishahara ni shilingi 49,452,723,000, matumizi mengineyo ni shilingi 48,826,697,000. Fedha za matumizi ya maendeleo ni shilingi 335,099,705,000, fedha za ndani ni shilingi 193, 795,218,000, na fedha za nje ni shilingi 141,304,487,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa WaBunge kwa kunisikiliza.

Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.mifugouvuvi.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHE. BALOZI DKT. BASHIRU ALLY KAKURWA (MB.), WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIOYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua na kushauri kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2025/2026, sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2025/2026. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2026/2027.

**Shukrani, Pongezi na Pole**

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na ukarimu, kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Bajeti, ikiwa ni Mkutano mahsusi wa Bunge wa kufanya uamuzi kuhusu masuala ya msingi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Aidha, naomba kwa dhati kabisa nimpongeze **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushindi mkubwa aliopata katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na hivyo kupata ridhaa ya umma ya kuaminiwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita (**6**).

3. ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali; akiwemo **Mheshimiwa Balozi Dkt.**

**Emmanuel John Nchimbi** kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, kwa kuchaguliwa kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba,** Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana.

4. ***Mheshimiwa Spika***, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua tena kuwa Mbunge na kisha kuniteua kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vilevile, ninampongeza **Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Aidha, nawapongeza **Bi. Agnes Kisaka Meena** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu, **Dkt. Fabian Magawa Madele** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) na **Prof. Mohammed Ali Sheikh** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu (Uvuvi).

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukupongeza wewe mwenyewe **Mheshimiwa Musa Hassan Zungu**, Mbunge wa Jimbo la Ilala kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nina imani kwamba utaliongoza Bunge letu kwa umahiri na weledi mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa **Daniel Baran Sillo,** Mbunge wa Babati Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika***, nachukua fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika,** Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri,** Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Vilevile, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninawashukuru viongozi, wajumbe na Sekretarieti ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi

makini wa Bajeti yetu. Ushauri wao umewezesha Wizara kufanya maboresho stahiki na ya kimkakati. Hakika, Mheshimiwa Spika Kamati hii itatusaidia sana. Kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea kuipatia Kamati hii ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

7. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani** (**Mb**) Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa Kundi la Vijana, kutoka Mkoa wa Mwanza kwa umahiri wake mkubwa wa kuchapa kazi, ushauri na ubunifu wake wenye tija uliotusaidia sote katika uongozi na usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

8. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapongeza **Bi. Agnes Kisaka Meena** (Katibu Mkuu-Wizara ya Mifugo na Uvuvi), **Dkt. Fabian Magawa Madele** (Naibu Katibu Mkuu-Mifugo), na **Prof. Mohammed Ali Sheikh** (Naibu Katibu MkuuUvuvi), kwa kuwa viongozi mahiri na wabunifu katika kuziendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuwasimamia watumishi wa Wizara kwa ufanisi. Pia, ninawashukuru watumishi wa Wizara kwa utendaji na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kikamilifu.

9. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwashukuru wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi wakiwemo wawekezaji na wafanyabiashara wa mazao wa mifugo na uvuvi, wafugaji, wavuvi, wakuzaji viumbemaji, wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi, wahifadhi wa mazingira na ikolojia pamoja na wadau wengine katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Aidha, mchango wao umeendelea kuchangia katika kutoa ajira, kuimarisha Uchumi wa Buluu na usalama wa chakula na lishe. Pia, ninapenda kuwashukuru Wadau wa Maendeleo, Taasisi za fedha, na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika juhudi za Serikali za kuendeleza shughuli za Mifugo, Uvuvi na Ukuzaji Viumbemaji.

**Salamu za Pole**

10. ***Mheshimiwa Spika***, wakati tukiendelea na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026, Wizara ilipokea kwa masikitiko

makubwa taarifa za vifo vya Wabunge, ambao ni:- Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Mbunge wa Jimbo la Isimani; Mheshimiwa Jenister Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Tunawaombea marehemu wote Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.

11. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026, na Mpango na Bajeti ya Fungu **99 -** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2026/2027.

## B. HALI HALISI YA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI KWA MUHTASARI

### Sekta ya Mifugo

12. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mifugo imeendelea kuwa Sekta muhimu katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa Taifa. Kwa mwaka 2024, Sekta ya Mifugo ilichangia asilimia **6.2** ya Pato la Taifa na kukua kwa asilimia **5.0.** Aidha, zaidi ya kaya milioni **6.5** zinafanya shughuli za ufugaji hapa nchini. Sekta hii ina mchango mkubwa katika uzalishaji wa malighafi za viwanda, ajira na kuchangia ongezeko la upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo ya mifugo na mazao yake nje ya Nchi.

13. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa mifugo ya aina mbalimbali nchini, hatua iliyochangia kuongezeka kwa thamani ya mifugo kutoka Shilingi **33,216,845,677,000** kwa mwaka 2024/2025 hadi Shilingi **34,328,243,052,500** mwezi Aprili, 2026 kwa makundi yote ya mifugo. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa idadi ya mifugo katika kipindi cha marejeo. Mathalani, idadi ya ng'ombe imeongezeka kwa asilimia **3.4** kutoka ng'ombe **39,241,375** hadi **40,569,621**, mbuzi wameongezeka kwa asilimia **3.5** kutoka mbuzi **28,592,597** hadi **29,598,648**, na kondoo wameongezeka kwa asilimia **3.0** kutoka kondoo **9,658,880** hadi **9,944,352**. Pia, kuku wameongezeka kwa asilimia **4.7** kutoka kuku **108,221,085** hadi **113,361,461**, ambapo

kuku wa asili wameongezeka kutoka **47,391,131** hadi **49,754,408** na kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **55,689,577** hadi **58,466,677**. Vilevile, nguruwe wameongezeka kwa asilimia **5.6** kutoka nguruwe **4,131,962** hadi **4,362,829** (**Kiambatisho Na.1A & 1B**).

14. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia **4.4** kutoka tani **1,054,114.03** zenye thamani ya Shilingi **10,378,706,595,000** Mwaka 2024/2025 hadi tani **1,100,489.85** zenye thamani ya Shilingi **10,835,318,512,861.04** Aprili, 2026**.** Katika kipindi hicho, kiasi cha nyama ya ng'ombe kilichozalishwa ni tani **689,811.46**, nyama ya mbuzi tani **159,465.19**, nyama ya kondoo tani **33,087.56,** nyama ya kuku tani **156,341.21** na nyama ya nguruwe tani **61,784.42** ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani **666,227.02**; mbuzi tani **150,014.29**; kondoo tani **31,647.60**; kuku tani **147,449.98** na nguruwe tani **58,775.14** kwa Mwaka 2024/2025 (**Kiambatisho Na.2**). Aidha, ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao, kuenea kwa elimu ya uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo, kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa, uboreshaji wa mbari za mifugo na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya Nchi.

15. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imeendelea kusimamia Tasnia ya Maziwa nchini kwa lengo la kuinua kipato cha wadau na mchango wa Tasnia hiyo kwenye Pato la Taifa. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia **5.2** na kufikia lita **4,218,529,224** hadi kufikia Aprili, 2026 ikilinganishwa na lita **4,009,985,001** zilizozalishwa mwaka 2024/2025, kati ya hizo, lita **2,826,414,580** sawa na asilimia **67** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **1,392,114,644** sawa na asilimia **33** zilitokana na ng'ombe wa maziwa wafugwao kisasa. Ongezeko la maziwa limechangiwa na kuongezeka kwa ng'ombe bora wa maziwa na utoaji wa elimu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kibiashara. Aidha, lita **101,478,030** za maziwa zilisindikwa ikilinganishwa na lita **90,416,788.5** zilizosindikwa mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la asilimia **12**. Sambamba na hilo, vituo vya kukusanyia maziwa vimeongezeka na kufikia vituo **275** hadi mwezi Aprili, 2026

ambavyo vilikusanya maziwa lita **97,805,035** ikilinganishwa na vituo **269** mwaka 2024/2025 vilivyokusanya lita **95,614,978.76** sawa na ongezeko la asilimia **2.3.** Aidha, ongezeko la vituo vya kukusanyia maziwa na usindikaji wa maziwa lilitokana na viwanda vilivyopo kuongeza uwezo wa usindikaji halisi dhidi ya uwezo uliosimikwa na kuongezeka kwa hamasa ya uwekezaji katika teknolojia za kuongeza thamani ya maziwa.

16. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka 2025/2026, uzalishaji wa mayai umeongezeka kwa asilimia **10.87** kutoka **7,105,907,370** mwaka 2024/2025 hadi **7,878,319,505** mwaka 2025/2026. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa vituo **28** vya kutotolesha vifaranga vya kuku vilivyopo nchini, mashamba **26** ya kuku wazazi, kuongezeka kwa ufugaji wa kuku wa mayai na hatua mbalimbali ambazo zimeendelea kuchukuliwa ikiwemo udhibiti wa magonjwa.

17. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa mbegu za malisho (***nyasi, mikunde na vipando***) umeongezeka kwa asilimia **85.05** kutoka tani **222.54** mwaka 2024/2025 hadi kufikia tani **411.25** mwaka **2025/2026** kutoka kwenye mashamba ya Serikali na binafsi. Aidha, uzalishaji wa malisho (*Saileji* na *hei*) umeongezeka kwa asilimia **128.49** kutoka tani **14,185** mwaka 2024/2025 hadi tani **32,411.31** mwaka 2025/2026. Vilevile, usindikaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani **720,000** mwaka 2024/2025 hadi kufikia tani **897,750** mwaka 2025/2026. Uzalishaji huu ni sawa na asilimia **56.11** ya lengo la kuzalisha tani **1,600,000** (**Kiambatisho Na 3A na 3B**).

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, kufuatia kuzinduliwa kwa Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo wa miaka mitano (5) na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Juni, 2025 Mkoani Simiyu, Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa ya Mifugo kwa kuratibu zoezi la Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ambapo, hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya mifugo **50,621,137** imechanjwa na kutambuliwa ikiwa ni sawa na asilimia **66.2** ya lengo la kuchanja na kutambua mifugo **76,323,300** kwa mwaka**.** Aidha, Serikali inaendelea kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine kwa

kuratibu uogeshaji wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, jumla ya michovyo **1,643,568,297** ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe **798,314,523**, mbuzi **524,931,563**, kondoo **289,526,439** na punda **30,795,772**. Michovyo hii ni sawa na asilimia **71.46** ya lengo la mwaka la michovyo **2,300,000,000**. Vilevile, uogeshaji wa mifugo umesaidia kupunguza matukio ya vifo vya mifugo nchini kwa asilimia **3** kutoka **34,029** mwaka 2024/2025 hadi **30,109** kufikia Aprili, 2026.

**Sekta ya Uvuvi**

19. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Uvuvi imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu ambapo katika mwaka 2024, sekta hii ilichangia asilimia **1.6** ya Pato la Taifa (GDP) na kukua kwa asilimia **2.3**. Aidha, katika kuimarisha Uchumi wa nchi, kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini kwa mtu mmoja mmoja, Sekta ya Uvuvi imeendelea kunufaisha watanzania wapatao milioni **6** katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Uvuvi, wakiwemo wavuvi **205,559** na wakuzaji wa viumbemaji **53,992.** Vilevile, Sekta ya Uvuvi ni nguzo muhimu katika kuimarisha usalama wa chakula na lishe, na inachangia asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2026, uzalishaji wa mazao ya uvuvi nchini umeongezeka kwa asilimia **10.02** kufikia tani **659,242.69** zinazojumuisha tani **477,661.93** kutoka uvuvi wa asili na tani **181,580.76** kutoka ukuzaji viumbemaji ikilinganishwa na tani **599,200.33** zinazojumuisha tani **466,956.88** kutoka katika uvuvi wa asili na tani **132,243.45** kutoka ukuzaji viumbemaji zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha usafirishaji wa mazao nje ya nchi ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, tani 37,988.30 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi **493,159,932,259.50** na samaki wa mapambo **209,772** wenye thamani ya shilingi **2,456,123,765.43** waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa shilingi **13,422,684,227.38.** Aidha, ulaji wa samaki nchini kwa mtu kwa mwaka umeongezeka kwa asilimia **27.8** kutoka kilo saba pointi tisa **(7.9)** mwaka 2024/2025 hadi kilo 10.1 mwaka 2025/2026. (kiambatisho Na.4)

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/2026

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

21. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (**Fungu 99)** iliidhinishiwa Shilingi **476,655,072,000** ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi **101,516,670,000** ni Matumizi ya Kawaida na Shilingi **375,138,402,000** ni Matumizi ya Maendeleo.

### Matumizi ya Kawaida

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara ilitengewa kiasi cha Shilingi **101,516,670,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **47,264,785,000** ni Mishahara na Shilingi **54,251,885,000** ni Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, hadi kufikia Aprili, 2026, Shilingi **66,038,322,366.20** zimepokelewa sawa na asilimia **65.05** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,512,232,929.08** sawa na asilimia **70.90** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **32,526,089,437.12** sawa na asilimia **59.95** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### Miradi ya Maendeleo

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) inaendelea kutekeleza miradi ya Maendeleo kupitia Programu tatu (**3**), ambazo ni Mkopo wa Masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kupitia dirisha la *Extended Credit Facility* (ECF), Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) na Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Katika Mwaka 2025/2026 jumla ya Shilingi **375,138,402,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **227,994,375,000** ni Fedha za Ndani na Shilingi **147,144,027,000** ni Fedha za Nje. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya Shilingi **120,365,341,839.19** sawa na asilimia **32.08** ya Bajeti ya Maendeleo zimepokelewa ambapo Shilingi **95,299,384,538.08** sawa na asilimia **41.80** ni Fedha za Ndani na Shilingi **25,065,957,301.11** sawa na asilimia **17.03** ni Fedha za Nje.

### Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026**,** Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi **94,105,000,000**. Kati ya kiasi hicho, Shilingi **49,900,001,000** kilipangwa kukusanywa kupitia Sekta ya Mifugo na Shilingi **44,204,999,000** kupitia Sekta ya Uvuvi. Kwa makusanyo ya kila Mwezi, Sekta ya Uvuvi ilitarajiwa kukusanya wastani wa Shilingi **3,683,749,916.67** na Sekta ya Mifugo ilitarajiwa kukusanya wastani wa Shilingi **4,158,333,416.67 (Jedwali Na. 1).**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## Jedwali Na. 1: Taarifa ya Mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli Kuanzia Julai 2025 hadi Aprili, 2026

| GFS Code | Chanzo | Bajeti Iliyoidhinishwa 2025/2026 | Makadirio Julai 2025-April, 2026 | Makusanyo Halisi kwa Mwaka Julai 2025-April, 2026 | Ufanisi (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Sekta ya Mifugo** | | | | | |
| 14220379 | Export Fee | 440,000,000 | 366,666,666.67 | 486,955,898 | 133% |
| 14210137 | Recepts from Veterinary Charges | 14,605,000,000 | 12,170,833,333.33 | 13,163,028,980 | 108% |
| 14220218 | Compound Fee | 1,250,001,000 | 1,041,667,500.00 | 391,054,489 | 38% |
| 14220217 | AHMP fees (Local) other than livestock market | 500,000,000 | 416,666,666.67 | 306,801,849 | 74% |
| 14220217 | Livestock Movement permit | 24,105,000,000 | 20,087,500,000.00 | 10,108,672,124 | 50% |
| 14220175 | Livestock market fees | 7,490,000,000 | 6,241,666,666.67 | 8,152,166,781 | 131% |
| 14220190 | Sale of siemen and liquid Nitrogen | 430,000,000 | 358,333,333.33 | 279,636,250 | 78% |
| 14220191 | Receipts from Sale of Heifers | 880,000,000 | 733,333,333.33 | 1,119,474,400 | 153% |
| 14220193 | Receipts from sale of seeds and hey | 200,000,000 | 166,666,666.67 | 123,732,700 | 74% |
| **Jumla Ndogo** | | **49,900,001,000** | **41,583,334,166.67** | **34,131,523,471** | **82%** |
| | | | | | |
| **Sekta ya Uvuvi** | | | | | |
| 14230171 | Fishing & Export License | 1,314,999,000 | 1,095,832,500 | 1,019,798,058 | 93% |
| 14230170 | Export Royalty | 28,096,000,000 | 23,413,333,333 | 13,557,983,379 | 58% |
| 14220222 | Import Royalty | 3,000,000,000 | 2,500,000,000 | 9,251,989,387 | 370% |
| **FS Code** | **Chanzo** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2025/2026** | **Makadirio Julai 2025-April, 2026** | **Makusanyo Halisi kwa Mwaka Julai 2025-April, 2026** | **Ufanisi (%)** |
| 14220218 | Compound Fees | 1,605,000,000 | 1,337,500,000 | 829,493,740 | 62% |
| 14220217 | Movement Permit | 3,760,000,000 | 3,133,333,333 | 5,078,243,763 | 162% |
| 14210149 | Exclusive Economic Zone Fishing License | 3,700,000,000 | 3,083,333,333 | 1,709,790,000 | 55% |
| 14220216 | Receipt from Sale of Laboratory Services | 1,900,000,000 | 1,583,333,333 | 1,115,062,037 | 70% |
| 14220213 | Prawn Fishing License | 62,000,000 | 51,666,667 | 25,143,172 | 49% |
| 14220194 | Receipts from Sale of Fingerlings | 330,000,000 | 275,000,000 | 179,460,904 | 65% |
| 14220161 | Miscellaneous Receipts | 437,000,000 | 364,166,667 | 25,930,153 | 7% |
| **Jumla Ndogo** | | **44,204,999,000** | **36,837,499,167** | **32,792,894,591** | **89%** |
| **Jumla Kuu** | | **94,105,000,000** | **78,420,833,334** | **66,924,418,062** | **85.3%** |

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 30, 2026, Wizara imekusanya kiasi cha Shilingi **66,924,418,062** sawa na asilimia **85.3** ya lengo la kukusanya Shilingi **78,420,833,334** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026. Aidha, katika makusanyo hayo, Sekta ya Mifugo imekusanya Shilingi **34,131,523,471** kati ya Shilingi **41,583,334,166.67** ya engo la miezi 10 sawa na asilimia **82** na Sekta ya Uvuvi

imekusanya kiasi cha Shilingi **32,792,894,591** kati ya Shilingi **36,837,499,167** sawa na asilimia **89** ya lengo la miezi 10.

**Maeneo ya Vipaumbele katika Mwaka 2025/2026** 26. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara imetekeleza maeneo manne (**4**) ya kipaumbele ambapo utekelezaji wake umezingatia matakwa ya Dira (**2025**); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (***FYDP*** III) kwa kipindi cha 2021/2022 – 2025/2026; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025; Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030 (***Sustainable Development Goals–SDGs*, 2030**). Aidha, utekelezaji huo umezingatia Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006; Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024; Mpango Kabambe wa Sekta ya Kilimo 2050 (***Agriculture Master Plan*** - ***AMP***, 2050), Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (***ASDP*** II); Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2021/22–2036/37; na Mpango wa Mabadiliko wa Sekta ya Mifugo wa mwaka 2022/23 – 2026/27. Utekelezaji wa vipaumbele hivi umewezesha Wizara kupata mafanikio na matokeo ambayo yameelezwa katika Hotuba yangu. Aidha, vipaumbele hivyo na mikakati yake ni pamoja na: -

1. Kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi

**Mikakati ya Utekelezaji:**

(i) Kuboresha upatikanaji wa mbari bora za mifugo na viumbemaji ikiwemo madume, mitamba na vifaranga vya samaki;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na samaki, na upatikanaji wa maji kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi;

(iii) Kuongeza thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(iv) Kukuza masoko na biashara ya mazao ya mifugo na uvuvi; na

(v) Kuimarisha afya ya mifugo, viumbemaji na mifumo ya utambuzi wa mifugo.

2. Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi

**Mikakati ya Utekelezaji:**

(i) Kuboresha vituo vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;

(ii) Kutambua na kuanzisha kanzidata ya wafugaji, wavuvi, wakuzaji viumbemaji na wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi; na

(iii) Kuanzisha vyombo maalum vya utendaji kwa ajili ya kusimamia na kulinda rasilimali za mifugo na uvuvi.

3. Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi

**Mikakati ya Utekelezaji:**

(i) Kuimarisha Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ili kuchagiza na kujenga uwezo wa vijana na wanawake kujiajiri katika shughuli za mifugo, uvuvi na ukuzaji viumbemaji;

(ii) Kuimarisha uwezo wa usimamizi, udhibiti na uvuvi katika Bahari Kuu;

(iii) Kuwawezesha wavuvi kupata vifaa vya kisasa vya uvuvi zikiwemo boti na vizimba vya kufugia samaki;

(iv) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuboresha miundombinu na teknolojia za ufugaji na uvuvi wa kisasa;

(v) Kuboresha miundombinu ya mifugo ikiwemo minada, majosho, mabwawa, visima, maghala na vituo vya kukusanyia maziwa;

(vi) Kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo na ujenzi wa masoko na mialo ya kupokelea samaki; na

(vii) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

4. Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi

**Mikakati ya Utekelezaji:**

(i) Kuboresha huduma za utafiti, mafunzo na ugani kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbemaji; na

(ii) Kuimarisha uwezo wa Taasisi za Utafiti na Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi.

**Sera, Sheria na Kanuni za Mifugo na Uvuvi**

27. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 pamoja na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kwa kupitia Sheria na Kanuni mbalimbali katika Sekta hizo. Aidha, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imefanya marekebisho ya Kanuni ya *The Animal Disease* (*Animal and Animal Products Movement Control (Amendment) Regulations*, G.N 32/2026; *The Animal Disease* (*Ante and Post Mortem Inspection* (*Amendment*) Regulations G.N 33/2026; *Fisheries (Amendment) Regulations*, G.N 64/2026 na *Fisheries (Aquaculture)* (*Amendment) Regulations*, G.N 65/2026. Pia, Wizara imetafsiri Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya Uvuvi, 2026 pamoja na kufanya majumuisho ya Marekebisho ya Tozo za Uvuvi kuanzia mwaka 2018 mpaka 2025 itakayoitwa *The Fisheries (Fees) Regulations*, 2026 ambayo kwa sasa ipo katika hatua mbalimbali za maamuzi. Vilevile, Wizara imefanya marekebisho ya *The Animal Disease (Veterinary Pesticides Control) Regulations*, 2025.

28. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na kuandaa Kanuni mpya ili ziendane na mabadiliko ya kisera, kiuchumi na kiteknolojia. Kanuni mpya zinalenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kulinda maeneo muhimu ya mazalia na makuzi ya samaki, kudhibiti mbinu, njia, zana na teknolojia za uvuvi; na kuboresha mazingira ya biashara kwa kulinda usalama na ubora wa mazao ya uvuvi. Aidha, Kanuni mpya zinalenga kuimarisha usimamizi na udhibiti wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na kuzalisha nyavu, maduka ya samaki na kusambaza zana za uvuvi, uzalishaji, matumizi na usambazaji wa barafu. Pia, Kanuni zinalenga kukidhi matakwa, masharti na viwango vya masoko ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuunganisha Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) ili kuunda Bodi moja itakayosimamia mazao yote ya mifugo. Bodi hiyo itakuwa na jukumu la kuratibu, kuendeleza, kuhamasisha na kusimamia uzalishaji, usindikaji, biashara na masoko ya mazao yote ya mifugo. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imeandaa Waraka wa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Mazao ya Mifugo ya mwaka 2026. Waraka huo umeshawasilishwa katika ngazi za maamuzi.

30. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeandaa Waraka kuhusu Mapendekezo ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi. Aidha, Mamlaka itakayoundwa itawezesha na kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya uvuvi, usalama wa chakula, usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbemaji, ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa. Waraka huo upo katika ngazi za maamuzi.

**Uzalishaji, Masoko na Uboreshaji wa Mbari za Mifugo**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa mbari bora za mifugo. Maeneo yaliyopewa uzito ni pamoja na kuimarisha huduma za uhimilishaji; Uzalishaji na

Usambazaji wa Mitamba; Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai pamoja na kuboresha Biashara ya Mifugo na Mazao yake.

**Huduma ya Uhimilishaji**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (*National Artificial Insemination Center (NAIC)*) ni kituo pekee cha Serikali kinachotoa huduma ya uhimilishaji nchini. Kituo hiki ni muhimu kwa utekelezaji wa mikakati ya Serikali ya kuboresha mifugo nchini ili kuongeza tija ya uzalishaji wa nyama na maziwa. Aidha, kituo kina jumla ya madume ya mbegu za ng'ombe wa nyama na maziwa **33** ambayo huzalisha mbegu kwa ajili ya uhimilishaji.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, jumla ya dozi **72,747** za mbegu zimezalishwa sawa na asilimia **48.50** ya lengo la kuzalisha dozi **150,000** na kusambaza dozi **88,997.** Vilevile, kupitia Kituo cha NAIC, Wizara imewajengea uwezo wahimilishaji **60** kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji ambapo hadi Aprili, 2026, jumla ya ng'ombe **74,345** wamehimilishwa katika mikoa **26** ikilinganishwa na ng'ombe **58,235** waliohimilishwa katika kipindi kama hicho Mwaka 2024/2025.

**Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuendelea kuboresha mbari za mifugo nchini, Serikali inaendelea kuyaimarisha mashamba matano (**5**) ya kuzalisha mifugo ya Sao Hill (Mufindi), Mabuki (Misungwi), Ngerengere (Morogoro), Nangaramo (Masasi) na Kitulo (Makete) yenye jumla ya ng'ombe **7,355** ikilinganishwa na ng'ombe **6,542** waliokuwepo mwaka 2024/2025. Aidha, katika Mwaka 2025/2026, mashamba hayo yamezalisha jumla ya mitamba bora **826** sawa na asilimia **82.6** ya lengo la kuzalisha mitamba **1,000** ambapo mitamba **177** imesambazwa kwa wafugaji. Pia, mashamba ya watu binafsi (**8**) yamezalisha mitamba bora **3,508** na kusambaza mitamba **3,021.** Vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mashamba yake kwa kuyawezesha zaidi kutokana na ongezeko la mahitaji ya mitamba bora.

35. ***Mheshimiwa spika***, ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mifugo nchini, Serikali imeboresha mbari za mifugo ambapo katika kipindi cha Mwaka 2025/2026, imeingiza jumla ya ng'ombe **5,328** mbuzi/kondoo **24,540** na nguruwe **171** wa mbegu kutoka nchi za Kenya, Afrika Kusini, Uganda, Ufaransa na Namibia. Aidha, kwa madhumuni hayo, jumla ya dozi **22,567** za mbegu za ng'ombe na jumla ya dozi **40** za mbegu bora za nguruwe ziliagizwa kutoka nchi za Denmark, Brazil, Ufaransa, Afrika Kusini na Marekani. Kati ya hizo, dozi **16,913** hazijatenganishwa kijinsi, dozi **5,654** zimetenganishwa kijinsi na dozi **33** ni za viinitete kwa ajili ya shughuli za kiutafiti zilizoagizwa kutoka Marekani.

**Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai**

36. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi ambapo katika tasnia ya kuku imeendelea kuwa kinara kwa kutoa ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijana na wanawake. Aidha, uwekezaji wa wadau katika mashamba ya kuku wazazi na vitotoleshi umeendelea kukua ikihusisha jumla ya mashamba **27.** Kati ya hayo mashamba **25** ni ya kuku wazazi (*Parent Stock Farms*), mashamba **2** ya kuku wazazi halisi (*Grand Parent Stock farms*) na vitotoleshi 28. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vifaranga vya kuku **83,926,271** vimezalishwa, kusambazwa na kuuzwa ndani na nje ya Nchi. Kati ya hivyo, vifaranga vya kuku wa nyama ni **70,524,913,** kuku chotara ni **10,267,960** na kuku wa mayai ni **3,133,398.**

37. ***Mheshimiwa Spika***, kukua kwa uwekezaji uliofanyika kwenye mashamba ya kuzalishia vifaranga vya kuku nchini kumesababisha kupungua kwa uingizaji wa vifaranga vya kuku wazazi kutoka **1,157,974** mwaka 2024/2025 hadi vifaranga **1,025,642** mwaka 2025/2026. Aidha, mauzo ya vifaranga kwenda nje ya Nchi yameongezeka kutoka vifaranga **1,909,078** mwaka 2024/2025 hadi vifaranga **5,751,584** mwaka 2025/2026. Ongezeko la mauzo ya vifaranga nje ya Nchi limechangiwa na kuimarika kwa uzalishaji, udhibiti wa magonjwa na uanzishwaji wa mashamba makubwa yanayofuga kuku kibiashara.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Kuratibu Tasnia ya Kuku Tanzania

*(TPECC)* imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Taifa wa Tasnia ya Kuku pamoja na kuaandaa makongamano mawili (2) ya kimataifa ambayo ni *Tanzania Poultry Futures Forum na Collaborative Poultry Lab platform* yaliyowaleta pamoja zaidi ya wadau **2,200** kutoka katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na nje ya Afrika.

**Biashara ya Mifugo na Mazao yake**

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Mkakati wa kuongeza mauzo ya mifugo na mazao yake nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza fedha za kigeni, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia mauzo ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya tani **12,763.77** zenye thamani ya Dola za Marekani **54,654,931.61** zimeuzwa katika masoko ya nchi mbalimbali ikilinganishwa na tani **9,913.61** zenye thamani ya Dola za Marekani **40,366,846.3** zilizouzwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **22.3**. Kiasi hicho kinajumuisha tani **8,228.48** za nyama ya mbuzi, tani **3,787.38** za nyama ya kondoo, tani **675.31** za nyama ya ng'ombe, tani **38.60** za nyama ya nguruwe na tani **33.90** za nyama ya kuku.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuendelea kuongezeka kwa mauzo ya nyama nje ya nchi ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongeza ushirikiano na mahusiano ya kidiplomasia yaliyosababisha kufunguka kwa fursa za kibiashara nje ya nchi. Katika kipindi hiki, nyama kutoka Tanzania imeuzwa kwenye masoko ya nchi za Bahrain, Comoro, Hong Kong, Kenya, Kuwait, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Ushelisheli, Umoja wa Falme za Kiarabu na Vietnam.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kusimamia biashara ya maziwa nchini ambapo jumla ya lita za maziwa **101,478,030** zenye thamani ya Shilingi **152,217,045,000** zilisindikwa na kuuzwa katika masoko ya ndani ya Nchi. Aidha, vibali vya kuingiza maziwa kutoka nje ya Nchi vimepungua kutoka **630** vyenye jumla ya lita **11,551,987.87** zenye

thamani ya Shilingi **22,969,085,568.85** mwaka 2024/2025 hadi vibali **609** vyenye jumla ya lita **10,089,768.50** zenye thamani ya Shilingi **21,623,010,316.22** kwa mwaka 2025/2026. Kupungua kwa kiasi cha maziwa yanayoagizwa kutoka nje ya Nchi kunatokana na hatua za Serikali za kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hivyo, kuwezesha ongezeko la usindikaji ndani ya Nchi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarika kwa biashara na masoko ya mazao ya mifugo nchini kwa Mwaka 2025/2026, kumechangia kuongezeka kwa ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka. Kiwango cha unywaji wa maziwa kwa mtu mmoja kwa mwaka uliongezeka kutoka lita 68.7 mwaka 2024/2025 hadi kufikia lita **70.5**, sawa na asilimia **2.6** mwaka 2025/2026, ulaji wa nyama kutoka kilo **17.6** mwaka 2024/2025 hadi kilo **18.4** mwaka 2025/2026 na ulaji wa mayai kutoka mayai **119** mwaka 2024/2025 hadi mayai **132** mwaka 2025/2026 kwa mtu kwa mwaka. Pamoja na ongezeko hilo, ulaji wa mazao hayo bado haujafikia viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ambavyo ni lita 200 za maziwa, kilo 50 za nyama na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa ngozi umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika Mwaka 2025/2026, jumla ya vipande vya ngozi **15,712,174** (ng'ombe **4,905,172**, mbuzi **8,005,927** na kondoo **2,801,075**), vyenye thamani ya Shilingi **35,332,861,735** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande **15,191,500 (**ng'ombe **4,735,000,** mbuzi **7,728,000** na kondoo **2,728,000),** vyenye thamani ya Shilingi **34,125,750,000**, vilivyozalishwa Mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo limechangiwa na wadau kupatiwa mafunzo kuhusu ufugaji wa kisasa ikiambatana na uvuanaji wa mifugo, uchunaji na uhifadhi wa ngozi.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, Biashara ya ngozi imeendelea kuimarika na kuchangia katika Pato la Taifa. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vipande vya ngozi ghafi **2,273,160** vyenye uzito wa kilo **7,081,784** (ng'ombe vipande **1,107,533** mbuzi vipande **815,939** na kondoo vipande **349,688)** vyenye thamani ya Shilingi **8,072,883,156** viliuzwa katika nchi za Nigeria, Kenya, Djibouti, Ethiopia, China, Ghana, Togo na Pakistan ikilinganishwa na vipande vya ngozi **1,651,088** vyenye uzito wa kilo **6,287,881** (ng'ombe vipande

**1,232,833,** mbuzi vipande **298,978** na kondoo vipande **119,277**) vyenye thamani ya Shilingi bilioni 7.95 vilivyouzwa katika nchi za Nigeria, Kenya, Djibouti, Ethiopia, China na Pakistan Mwaka 2024/2025. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameongezeka kutokana na mahitaji ya soko la ngozi isiyosindikwa kuongezeka katika nchi za Nigeria, Kenya na Togo. Pia, Wizara imewawezesha wamiliki wa machinjio za kisasa zilizoko chini ya Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Huru Maalum ya Kiuchumi (*TISEZA*) kwa kuwaondolea kodi ya kusafirisha ngozi nje ya nchi. Hatua hii imeleta mafaniko ya kupata soko la ngozi za mbuzi na kondoo kwa kusafirishwa kwa kiwango kikubwa kwenda nchini Kenya.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Tasnia ya Ngozi imeendelea kusimamia biashara na ubora wa ngozi kwa kusajili na kutoa leseni kwa maghala **51** ya ngozi kwa kampuni zinazosafirisha ngozi kwenda nje ya Nchi. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Sekta Binafsi kwa kuendeleza na kufanya ukaguzi wa maghala ya ngozi katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Dodoma.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika ngozi ambapo hadi Aprili, 2026, jumla ya vipande **478,850** vya ngozi ya ng'ombe na **984,000** vya ngozi za mbuzi na kondoo vyenye thamani ya Shilingi **37,167,366,000** vimesindikwa (***Kiambatisho Na*.5)**. Aidha, Wizara imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa malighafi kwa kuwaunganisha wamiliki wa viwanda vya kusindika ngozi na wazalishaji wa ngozi. Pia, jumla ya vipande **522,898** vya ngozi za kondoo na mbuzi vilivyosindikwa hadi hatua ya kati vimeuzwa katika nchi za Pakistan, China, na Ethiopia kwa thamani ya Shilingi **668,786,542**.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani ya zao la ngozi, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi ambapo katika Mwaka 2025/2026, jumla ya jozi za viatu **3,690,800** zimezalishwa ikilinganishwa na jozi **3,391,200** zilizozalishwa Mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa

uzalishaji wa bidhaa za ngozi kutoka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) wanaotengeneza bidhaa za ngozi pamoja na ongezeko la upatikanaji wa ngozi bora (***Kiambatisho Na***. 6).

**Maji, Ardhi ya Malisho na Vyakula vya Mifugo**

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka 2025/2026 Serikali imeendelea kufuatilia na kuhuisha taarifa za miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo iliyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo jumla ya malambo na mabwawa **223** yametambuliwa katika Halmashauri za Wilaya **14** za Rorya, Mpwapwa, Serengeti, Butiama, Tarime, Manyoni, Musoma, Bahi, Kongwa, Dodoma Jiji, Kilwa, Mkuranga, Bunda na Buchosa. Aidha, miundombinu hii inahudumia takribani mifugo **925,830,** ikijumuisha ng'ombe **668,733**, mbuzi **159,773** na kondoo **97,324.**

**50.** ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imeendelea kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyowezesha kutenga hekta **196,324.25** za maeneo ya malisho mwaka **2025/2026.** Mipango hiyo, imefanyika katika vijiji **187** vya Wilaya **22** katika mikoa ya Tanga, Singida, Katavi, Shinyanga, Rukwa, Tabora, Mtwara, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Pwani, Iringa, Lindi, Manyara, Simiyu, Morogoro, Kagera na Geita. Mipango hii imewezesha ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho kufikia hekta **3,686,026.08** kwa mwaka **2025/2026** kutoka hekta **3,489,701.13** Mwaka **2024/2025**. Aidha, hadi kufikia Aprili 2026 hekta **1,349,486.29** katika vijiji **365** zimepimwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN Na.597 na 718). Pia, hekta **216,971.56** katika vijiji **114** zimefanyiwa upembuzi na uhakiki kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN Na. 248).

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, Uzalishaji wa mbegu za malisho (nyasi, mikundekunde na vipando) hapa nchini umeongezeka kwa asilimia **85.5** kutoka tani **222.54** mwaka 2024/2025 hadi tani **411.25** mwaka 2025/2026 kutoka kwenye mashamba ya Serikali na binafsi yenye thamani ya Shilingi **1,782,555,250**. Aidha, uhifadhi wa malisho (Saileji na Hei) umeongezeka kwa asilimia **128.49** kutoka tani **14,185** mwaka 2024/2025 hadi tani **32,411.31** mwaka 2025/2026 yenye thamani ya Shilingi **8,025,414,000.** Ongezeko la

uzalishaji wa mbegu na malisho limechangiwa na kuimarishwa kwa huduma za ugani.

**Udhibiti wa Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi**

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya udhibiti wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka **2025/2026**, Serikali imewatambua jumla ya wafugaji **3,021** katika Halmashauri za Mvomero, Gairo, Kilombero, Kilosa, Malinyi, Ulanga, Mlele, Sikonge, Kaliua, Urambo, Bahi, Kibaha, Mbarali, Magu na Sengerema. Hatua hizo zinalenga kuwapatia wafugaji elimu ya umiliki wa ardhi, matumizi endelevu ya rasilimali za malisho na kuhamasisha upangaji wa matumizi bora ya ardhi ili kulinda maslahi ya watumiaji wengine wa ardhi.

**Ushirikishwaji wa Wadau katika Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho**

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la Watu na Wanyama Pori, imewezesha uendelezaji wa ekari **12,085** katika vijiji **26** kwa kuondoa vichaka, mimea vamizi na kudhibiti mmomonyoko wa udongo kwa kufukia makorongo yenye urefu wa kilometa 1**73,** katika kongani za malisho za Lelek, Muriamunyi, Muriatata katika Wilaya ya Longido, Sepeko katika Wilaya ya Monduli na Mwada - Ngaiti katika Wilaya ya Babati.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Ujamaa Community Resource Team* (UCRT) kupitia Programu ya *Sustainable Nature Based Livelihoods,* imewezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji ambapo Vijiji **44** vya Wilaya za Simanjiro (**22**), Longido (**13**) na Mbulu (**9**) vimeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kutenga maeneo **53** ya malisho yenye jumla ya hekta **790,865.54** ambazo zimepatiwa Hati Miliki za Kimila kwa lengo la kuimarisha umiliki na usimamizi wa maeneo hayo, hivyo kuchangia kuongezeka kwa upatikanaji wa malisho.

**Uendelezaji wa Rasilimali za Vyakula vya Mifugo**

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha ubora wa vyakula vya mifugo kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama Sura ya **180** na Kanuni zake. Katika mwaka 2025/2026 jumla ya maeneo **949** ya kuzalisha, kuuza na kuhifadhi rasilimali za vyakula vya mifugo yamekaguliwa na kupatiwa vibali. Aidha, jumla ya maeneo mapya **57** (Arusha (**7**), Dar es Salaam (**29**), Pwani (**10**), Mbeya (**1**), Shinyanga (**2**), Dodoma (**2**), Kagera (**1**), Kilimanjaro (**1**), Tanga (**1**), Rukwa (**2**) na Mwanza (**1**) ya kuzalisha vyakula vya Mifugo yamesajiliwa. Usajili huu umeongeza maeneo ya kuzalisha vyakula vya Mifugo kutoka maeneo **279** mwaka **2024/2025** hadi **336** mwaka **2025/2026.**

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kibiashara ya vyakula vya mifugo na uhamasishaji wa uwekezaji kwa Sekta binafsi. Katika mwaka **2025/ 2026** uzalishaji umeongezeka hadi tani **897,750** zenye thamani ya Shilingi **1,436,400,000,000,** ikiwa ni ongezeko la asilimia **24.69** ikilinganishwa na tani **720,000** mwaka **2024/2025** zenye thamani ya Shilingi **1,152,000,000,000**. Kasi hii ya ukuaji imechagizwa na kuongozeka kwa viwanda vidogo na vya kati, unafuu wa kodi kwenye malighafi za virutubisho, upatikanaji wa teknolojia za kisasa za usindikaji, soko la uhakika la vyakula vya mifugo, na kuwepo kwa mafunzo na elimu ya lishe bora ya mifugo kwa wafugaji nchini. Kati ya vyakula vilivyosindikwa, tani **610,470** ni vyakula vya kuku wa nyama na mayai, sawa na asilimia **68**, tani **197,505** ni vyakula vya nguruwe sawa na asilimia **22** na tani **89,775** ni vyakula vya ng'ombe wa maziwa na nyama, sawa na asilimia **10.**

**Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani**

**Utafiti wa Mifugo na Uvuvi**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti wa mifugo na uvuvi nchini katika vituo nane (**8**) vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (*TALIRI*) na vituo vitano (**5**) vya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*). Aidha, jumla ya miradi **51** ya utafiti inayohusu uboreshaji wa mbari za mifugo, nyanda za malisho, na

wingi na mtawanyiko wa samaki katika eneo la Ziwa Tanganyika na Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (EEZ) imeratibiwa.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuboresha utafiti wa mifugo na uvuvi nchini, inaendelea na zoezi la Uhuishaji wa Agenda za Utafiti wa Mifugo na Uvuvi za Mwaka 2020-2025 ili kuakisi Dira ya Taifa ya Maendeleo (Dira 2050) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025. Lengo ni kuwaandaa na kuwahimiza wadau kufanya utafiti unaoendana na mahitaji ya soko na kusambaza matokeo ya utafiti yaliyohifadhiwa katika taasisi za utafiti kwa watumiaji.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi za Utafiti za TALIRI na TAFIRI imesambaza teknolojia **19** zilizoibuliwa kutokana na utafiti uliofanyika kwa lengo la kuwafikia wadau katika mnyororo wa thamani wa mifugo na uvuvi. Teknolojia hizo zinahusu uboreshaji wa mbari za ng'ombe, mbuzi, kuku; udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa kwa dawa; uboreshaji wa nyanda za malisho ya mifugo; vyakula bora vya samaki, mfumo wa kidigitali wa kutambua maeneo yenye samaki baharini na kuuza samaki (*vua, uza, nunua kidigiti);* na uongezaji wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi.

**Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi (***LITA na FETA***) kwa lengo la kuandaa wahitimu mahiri wa fani hizo. Udahili umeongezeka kutoka wanafunzi **6,013** mwaka 2024/2025 hadi **6,088** mwaka 2025/2026. Aidha, Wizara kupitia Wakala hizo, inaendelea na zoezi la kuhuisha mitaala mbalimbali ikiwemo Mtaala wa Mafunzo ya Usimamizi wa Bandari za Uvuvi na Lojistiki na Mtaala wa Teknolojia ya Uzalishaji wa Kuku. Lengo la kuanzisha mitaala hii ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, hasa kwa ajili ya vijana na wanawake na kukidhi soko la wadau la uhitaji wa mabaharia watakaosaidia katika uendeshaji wa meli za uvuvi, uendeshaji wa bandari za uvuvi pamoja na kupata wataalam mahiri katika Tasnia ya kuku nchini kulingana na mahitaji ya sasa.

**Huduma za Ugani**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za ugani nchini, Wizara imetoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani wa mifugo na uvuvi **1,123** kutoka katika Halmashauri **184** nchini. Mafunzo yalitolewa yalihusu Usimamizi wa Sheria za Mifugo na Uvuvi; Uanzishwaji wa mashamba ya malisho ya mifugo; Mbinu bora za ukuzaji viumbemaji; Usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Mafunzo hayo ni mwendelezo wa kuwapatia mafunzo rejea maafisa ugani nchini ambapo jumla ya Maafisa ugani **2,781** kati ya **5,006** waliopo wamepatiwa mafunzo rejea. Aidha, huduma za ugani zimeendelea kutolewa kupitia maonesho mbalimbali kwa wadau **276,314** wa mifugo na uvuvi (Sabasaba, **42,311**; Nanenane **226,786**; na Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani **7,217**).

**Mradi wa BBT Project I (TALIRI – Kongwa)**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imeanza kutekeleza Mradi wa BBT Project I utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano **(5)** katika Kituo cha TALIRI – Kongwa. Mradi huu unalenga kuwawezesha vijana na wanawake kujiajiri kupitia mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo, hususan unenepeshaji wa mbuzi kibiashara, uzalishaji wa malisho kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji, pamoja na uchakataji wa vyakula vya mifugo kibiashara. Aidha, mradi utawezesha vijana kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za uzalishaji.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuingia mikataba ya ununuzi wa mitambo na vifaa vya shamba, vikiwemo magari matatu **(3),** malori mawili **(2)** ya kusafirishia mbuzi, magari mawili **(2)** ya kubebea nyama yenye mfumo wa ubaridi, matrekta na vifaa vyake seti tano **(5),** mitambo ya kuvunia malisho seti tano **(5),** *Backhoe Loader* moja **(1),** pamoja na seti tatu **(3)** za mitambo ya kuvunia na kutengeneza majani vunde (*silage*). Aidha, nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kituo atamizi cha unenepeshaji wa mbuzi na uzalishaji wa malisho zimekamilika. Kupitia mradi huu, miundombinu mbalimbali itajengwa ikiwemo mabanda ishirini na

matatu **(23)** ya mbuzi yenye uwezo wa kuhifadhi mbuzi 23,000 kwa wakati mmoja, maghala matatu **(3)** ya kuhifadhia malisho, kiwanda cha kuchakata vyakula vya mifugo chenye uwezo wa kuchakata tani **40** kwa siku, pamoja na miundombinu ya makazi ya vijana **218** na ukumbi wa mafunzo. Vilevile, Wizara ipo katika hatua za majadiliano (*Negotiation*) ya kuingia mkataba na mzabuni atakayefanya ukarabati wa miundombinu ya Kituo cha TALIRI – Kongwa ili kuwezesha kituo hicho kuanza kudahili vijana mwezi Juni 2026.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ambapo Serikali imetoa Shilingi **7,000,000,000** ili kuwawezesha vijana **308** kuwekeza katika miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba, kilimo cha mwani, ufugaji wa majongoo bahari na unenepeshaji wa kaa nchini. Aidha, Wizara imepokea jumla ya Shilingi **23,685,829,751** zilizotolewa na Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kuwawezesha vijana kupata mikopo yenye masharti nafuu ya kuwekeza katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Hadi Aprili 2026, Wizara imepokea na inaendelea kuchambua jumla ya maombi **3,004** ya vijana wanaohitaji kujishughulisha katika minyororo ya thamani ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia fedha hizi.

**Upatikanaji na Usambazaji wa Chanjo za Magonjwa 13 ya Kipaumbele**

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha udhibiti wa magonjwa ya mifugo nchini unafanyika kwa viwango vya kimataifa, uzalishaji wa chanjo za Wanyama umeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya chanjo nane (**8**) za magonjwa ya kipaumbele zimezalishwa nchini ambazo ni Homa ya mapafu ya Ng'ombe **(CBPP**), Homa ya Mapafu ya Mbuzi **(CCPP),** Sotoka ya Mbuzi na Kondoo **(PPR),** Kimeta (*Anthrax*), Mdondo **(ND),** Ugonjwa wa Kutupa Mimba (**Brucellosis**), Mapele Ngozi **(LSD)** na Gumboro **(IBD)**. Aidha, hatua zaidi zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ili kufanikisha uzalishaji wa chanjo ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo **(FMD),** Mahepe **(Marek's),** Kichaa cha Mbwa (***Rabies),*** Ndigana Kali **(ECF)** na Homa ya Bonde la Ufa **(RVF)**.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa chanjo za magonjwa yanayoathiri afya ya mifugo na biashara za kikanda na kimataifa pamoja na magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, uzalishaji na usambazaji wa chanjo nchini umeongezeka kutoka dozi **728,153,645** mwaka 2024/2025 hadi kufikia dozi **750,331,970** Aprili, 2026. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa chanjo ndani ya nchi umeongezeka kutoka dozi **153,952,375** mwaka 2024/2025 hadi kufikia dozi **200,920,210** Aprili, 2026**.** Kati ya chanjo zilizozalishwa nchini, jumla ya dozi **63,641,885** zimezalishwa na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na dozi **137,278,325** zimezalishwa na Sekta Binafsi. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi mbalimbali za kuhamasisha wafugaji kuchanja mifugo yao ikiwemo; Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ambayo imelenga kuhakikisha asilimia **70** ya Mifugo nchini inachanjwa.

### Utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuiwezesha Tanzania kufikia vigezo vya kimataifa katika biashara ya mifugo na mazao ya mifugo katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kusimamia Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa. Kupitia kampeni hiyo, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya dozi **19,099,100** za chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (**CBPP**), Sotoka ya Mbuzi na Kondoo dozi **17,224,200** na Mdondo wa Kuku (**ND**) dozi **40,000,000**. Aidha, Wizara imeratibu usambazaji wa vifaa vya kutolea chanjo vikiwemo *automatic syringe* (**3,270**), Sindano (**32,700**), buti (**2,180**), *ovaroli* (**2,180**), glovu **1,090,** majokofu **90** na vishikwambi **4,500.** Vilevile, Wizara imenunua na kusambaza pikipiki **700** kwa maafisa mifugo nchini ili kuwezesha utekelezaji wa zoezi la chanjo na utambuzi wa mifugo kitaifa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya ng'ombe **9,115,297** sawa na asilimia **47.37** ya lengo wamechanjwa dhidi ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), mbuzi na kondoo **2,672,237** sawa na asilimia **15.51** dhidi ya ugonjwa wa Sotoka (PPR) na kuku **38,833,603** sawa na asilimia **97.08** wamechanjwa dhidi ya

Mdondo, Ndui na Mafua ya Ndege. Aidha, Jumla ya mifugo **2,566,887** imewekewa hereni za kielektroniki kwa ajili ya utambuzi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa umewezesha kufunguka kwa soko la chanjo za Tanzania kwa nchi za Botswana, Ghana na Mongolia. Aidha, utekelezaji wa Kampeni hiyo umewezesha kufunguka kwa soko la nyama la nchini Qatar na Ushelisheli, na soko la vifaranga vya kuku wa mayai kwa nchi za Siera Leone, Cote *d'Ivoire* na China. Pia, nchi za Congo DRC, Misri na Mauritius zimeonesha nia ya kufungua masoko yao ya nyama kwa Tanzania.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti weledi wa watoa huduma za afya ya mifugo na kuimarisha utoaji wa huduma bora, katika Mwaka 2025/2026 Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, imefanya ukaguzi wa vituo **1,256** vya kutolea huduma za afya ya wanyama katika Halmashauri **59**. Aidha, ili kuhakikisha wahitimu wa fani ya afya ya mifugo wanapata mafunzo ya ujuzi unaostahili, Baraza la Veterinari Tanzania limefanya ukaguzi katika vyuo **12** vya mafunzo ya afya na uzalishaji wa wanyama ambavyo ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (**SUA**), Kampasi za LITA Morogoro, Tengeru (Arusha), Temeke (Dar es Salaam), Madaba (Ruvuma), Mabuki (Mwanza), Kikulula (Kagera) na Chuo cha KARUCO (Kagera), Taasisi ya Kilimo na Mifugo Igabiro (Kagera), Chuo cha Mahinya (Ruvuma), Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (Mbeya) na Chuo cha Sayansi na Teknolojia Chato (Geita). Ukaguzi huo umebainisha umuhimu wa kuimarisha mafunzo kwa vitendo ili wahitimu wawe na weledi wa kutosha.

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania limesajili madaktari **111** wa wanyama na kufanya idadi yao kufikia **1,098**. Kati ya hao wanaume ni **966** na wanawake ni **132**. Aidha, wataalam wasaidizi **565** wa afya ya wanyama wameandikishwa na kuorodheshwa na kufanya idadi yao kufikia **6,880** ambapo kati yao wanaume ni **4,344** na wanawake ni **2,536**. Pia, jumla ya leseni **70** zimetolewa kwa wataalam wa mifugo wakiwemo wakaguzi wa nyama **14,** wahimilishaji **25** na wataalam wa maabara **31** na kufanya

wakaguzi wa nyama kufikia **976**, wahimilishaji **101** na wataalam wa maabara za veterinari **115**. Vilevile, vituo **283** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **3,011**.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Baraza imeendelea kusimamia mafunzo kwa vitendo (*internship*) kwa wahitimu wa Shahada ya Udaktari wa Wanyama. Aidha, jumla ya wahitimu **98** wa udaktari wa wanyama wanaendelea na mafunzo hayo katika vituo **85** vilivyopo katika Mikoa mbalimbali. Pia, mitihani ya kuandikisha wataalam wa stashahada ya afya na uzalishaji wa wanyama imefanyika kwa wahitimu **1,657**.

**Uzalishaji wa Samaki**

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka 2025/2026 uzalishaji wa samaki umefikia tani **526,763.40** (tani **412,821.67** kutoka maziwa makuu, tani **52,229.99** kutoka katika bahari, na tani **12,610.27** kutoka katika mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu na maji mengine madogo na tani **49,101.47** kutoka ufugaji wa samaki (**Kiambatisho Na. 7A na 7B** ) zenye thamani ya Shilingi **4,902,953,248,000.73** ikilinganishwa na tani **490,372.83** za samaki zenye thamani ya Shilingi **3,124,076,643,000.38** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Hivyo, uzalishaji wa samaki nchini kutoka katika maji ya asili na ukuzaji viumbemaji umeongezeka kwa asilimia **7.4.** Hata hivyo, uzalishaji huu bado haukidhi mahitaji ya samaki ambayo ni wastani wa tani **1,254,000** kwa mwaka. Serikali imeendelea na hatua mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya samaki nchini zikiwemo kudhibiti uvuvi usiozingatia sheria, kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, kuhamasisha na kuwekeza katika shughuli za viumbemaji pamoja na kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika maji ya asili.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kuwa kinara wa uzalishaji wa mwani barani Afrika ambapo hadi Aprili, 2026 tani **132,479.29** za mwani zenye thamani ya shilingi **13,910,325,765** zimezalishwa ikilinganishwa na tani **88,615.2** zenye thamani ya shilingi **9,304,596,000** zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la asilimia **49.5.** Ongezeko hili linatokana na hatua za Serikali za kuhamasisha uzalishaji kwa kuwapatia wakulima wa mwani mafunzo, pembejeo,

kuhamasisha matumizi ya bidhaa zitokanazo na mwani na kuimarika kwa soko.

**Biashara ya Mazao ya Uvuvi**

**75. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la ndani imeendelea kuimarika ambapo hadi mwezi Aprili, 2026 jumla ya tani **439,673.63** zenye thamani ya shilingi **4,196,003,304.22** ziliuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na tani **422,639.10** zenye thamani ya shilingi **2,827,577,871.62** zilizouzwa mwaka 2024/2025. Kuimarika kwa biashara ya samaki katika soko la ndani kumetokana na kuimarika kwa miundombinu ya ubaridi ya kuhifadhi mazao ya uvuvi na miundombinu ya usafirishaji wa mazao ya uvuvi.

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

**76. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia, kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi na kuhakikisha zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imeendelea kusimamia Sera ya Taifa ya Uvuvi, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya uvuvi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa kufanya yafuatayo;-

**(a) Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi**

**77. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imehuisha Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi. Lengo la Mwongozo huu ni kuiwezesha Serikali, jamii ya wavuvi, na wadau wengine kushirikiana katika kusimamia, kulinda, kutunza, kuendeleza na kuvuna kwa njia endelevu rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kiuchumi, ajira, bioanuai, uhakika wa chakula kwa Taifa kwa kuzingatia Sera na Sheria za uvuvi zilizopo.

**78. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini ya utendaji kazi wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) vilivyoko katika Halmashauri za Wilaya za Mpwapwa, Chamwino, Iringa, Nkasi, Uvinza, Kilwa, Lindi, Mafia na Mkuranga. Aidha, katika kuziimarisha BMUs, Wizara imevipatia vikundi **34** vya

wavuvi madeli **99** kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Vilevile, Wizara, kwa kushirikiana na Shirika la *International Union for Conservation of Nature (IUCN)*, imeanzisha Jukwaa la Wadau wa Sekta ya Uvuvi katika Mkoa wa Mtwara kwa lengo la kuimarisha usimamizi shirikishi wa maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na maeneo ya uvuvi kwa kuunganisha nguvu miongoni mwa wadau.

**b) Udhibiti na Elimu kuhusu Uvuvi Usiozingatia Sheria na Usimamizi wa Maeneo ya Mazalia ya Samaki**

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa lengo la kudhibiti uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi isiyozingatia sheria na kanuni katika Maziwa Makuu, Bahari na maji madogo, Wizara imefanya doria zenye siku kazi **4,202** sawa na asilimia **50.02** ya siku kazi **8,400** zilizopangwa kwa mwaka 2025/2026. Matokeo ya doria hizo yaliwezesha kukamatwa kwa zana mbalimbali zisizoruhusiwa kisheria ikiwemo Nyavu za timba **4,768**, nyavu za makila **2,167**, nyavu za dagaa **475**, nyavu za kokoro **948** ikiwemo kokoro la mita **700** lililokamatwa katika Halmashauri ya Uvinza, kamba za kokoro mita **99,680,** vyandarua **63**, mitumbwi ya kasia **434**, injini za boti **124**, tanki za mafuta **22** na boti **172**. Pia, samaki wachanga kilo **12,720.81** na kaa hai wachanga kilo **4,312** walikamatwa. Vilevile, jumla ya watuhumiwa **1,047** waliokuwa wakifanya shughuli za uvuvi kinyume cha Sheria, Kanuni za Uvuvi na taratibu walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi za kisheria. Aidha, elimu kwa vitendo ilitolewa kwa jamii za wavuvi katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Kigoma na Simiyu.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** elimu ya madhara ya uvuvi usioendelevu na usiozingatia sheria imetolewa katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu, Katavi, Rukwa na Kigoma ambapo zaidi ya wananchi **20,000** wamefikiwa kupitia mikutano, semina na mafunzo ya muda mfupi kuhusu masuala ya Sheria, Kanuni za Uvuvi, Miongozo pamoja na usalama wa majini na uokozi (*Maritime Safety and Security*).

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali kwa kuvipatia boti **10** na pikipiki **40** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uvuvi. Aidha, Wizara inaendelea kuwezesha upatikanaji wa ndege nyuki mbili (**2**), gari tatu (**3**) na pikipiki **14** kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi.

### (c) Ukaguzi wa Mazao ya Uvuvi Yanayosafirishwa Ndani na Nje ya Nchi

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kuimarisha Uthibiti wa ubora, viwango na masoko ya mazao ya uvuvi kwa kufanya ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo viwanja vya ndege, bandarini, mipakani, masoko ya samaki, viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, maghala, mabucha ya samaki pamoja na mialo yakupokelea samaki. Aidha, ukaguzi ulifanyika katika viwanda **22** vya kuchakata samaki, viwanda **45** vya kuhifadhi na kuchakata samaki hai (kamba kochi, kaa na samaki wa mapambo), mialo iliyosajiliwa **143** ya kupokelea samaki, masoko **6**, maghala pamoja na mabucha yaliyosajiliwa **527**, vituo **293** vya kugandisha samaki, viwanda **18** vya kuchakata mabondo, meli **4** za uvuvi wa kambamiti katika maji ya ndani na vyombo **1,890** vya kusafirisha mazao ya uvuvi. Vilevile, jumla ya vyeti **5,756** vya afya vilitolewa kwa ajili ya uhakiki wa mazao ya uvuvi yaliyosafirishwa kwenda nje ya nchi na sampuli **9,850** zilikusanywa na kuwasilishwa katika Maabara ya Taifa ya Uvuvi kwa ajili ya uchunguzi wa vimelea na unyevu.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2025/2026, jumla ya vibali **245** vimetolewa vikijumuisha vibali **94** vya kuingiza chakula cha samaki kutoka nje ya nchi, vibali **76** vya kusafirisha mwani mkavu nje ya nchi, vibali **75** vya ukuzaji viumbemaji kibiashara. Aidha, leseni **9** za kusafirisha mwani kwenda nchi za China, Afrika Kusini, Hispania, Uingereza, Marekani, Canada, Australia, Kenya, Burundi, Ufaransa, Korea na Denmark zimetolewa (***Kiambatisho Na.8***).

**Maabara ya Uvuvi Tanzania**

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, huduma za uchunguzi wa ubora wa samaki na mazao mengine ya uvuvi yanayouzwa kwenye masoko ya ndani, kikanda na kimataifa zimeendelea kuimarika nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiasi cha sampuli **2,756** za samaki na mazao mengine ya uvuvi, mazingira ya maji asili na ukuzaji viumbemaji zimefanyiwa uchunguzi wa vimelea na kemikali sawa na asilimia **91.80** ya lengo la sampuli **3,000**, ili kukidhi viwango vya ubora na usalama wa samaki na mazao mengine ya uvuvi kitaifa, kikanda na kimataifa kwa ajili ya kulinda afya ya jamii.

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Maabara imeendelea kuhuisha hadhi ya ithibati kupitia ukaguzi wa kina uliofanyika Februari, 2026 na taasisi inayosimamia masuala ya ithibati katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Development Community Accreditation Service - SADCAS*) na kuendelea kukidhi kiwango cha kimataifa cha umahiri wa upimaji wa Maabara cha ISO/IEC17025:2017. Hivyo, Maabara imeendelea kulinda ithibati katika njia za uchunguzi **19** za samaki na mazao mengine ya uvuvi na ubora wa maji.

**Ukuzaji Viumbemaji**

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2026, uzalishaji wa vifaranga vya samaki umefikia **202,657,335** ikilinganishwa na vifaranga **123,877,354** vilivyozalishwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **63.6** (***Kiambatisho Na. 9***). Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa idadi ya vitotoleshi kutoka **49** hadi **66**. Aidha, matumizi ya chakula bora cha samaki yamefikia tani **20,510.69** kutoka tani **15,226.67** za mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **34.7** (***Kiambatisho Na. 10)*** Kiasi hicho kinajumuisha tani **10,073.28** zilizozalishwa nchini na tani **10,437.4** kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na tani **5,879.00** zilizozalishwa nchini na tani **9,347.67** kutoka nje ya nchi kwa mwaka 2024/2025.

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, jumla ya wananchi **21,910** (Wanawake **11,469;** Wanaume **10,441**) wamepatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa ikilinganishwa na wananchi **11,216** (Wanawake **6,000;** Wanaume

**5,216**) kwa mwaka 2024/2025 sawa ongezeko la asilimia **95.3.** Pia, wakulima **5,595** wa mwani wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, uhifadhi na uongezaji thamani zao la mwani ikilinganishwa na wakulima **2,563** mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **118.3**

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa shughuli za ukuzaji viumbemaji zinatekelezwa kwa kuzingatia sheria na kanuni bora, Wizara imefanya ziara za ukaguzi **193** za pembejeo na mazao ya ukuzaji viumbemaji yanayoingia na kutoka nje ya nchi kupitia Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Vilevile, ukaguzi umefanyika katika vitotoleshi **26,** vizimba **711**, mabwawa **345**, matanki **23** na viwanda viwili (**2**) vya kutengeneza chakula cha samaki katika Mikoa tisa (**9**) ya Mwanza, Kigoma, Mara, Kagera, Morogoro, Simiyu, Dodoma, Pwani na Dar es Salaam.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji viumbemaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2026. Pia, idadi ya miundombinu ya uzalishaji wa viumbemaji imeongezeka hadi kufikia mabwawa **35,720** na vizimba **3,343** ikilinganishwa na mabwawa **34,642** na vizimba **1,636** kwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezo la asilimia **3.1** na **104.3** mtawalia. Ongezeko la vizimba limechangiwa na juhudi za Serikali za kutoa mikopo yenye masharti nafuu na kuanisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa vizimba zilizovutia uwekezaji wa sekta binafsi. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika ufugaji wa samaki ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya matanki **353** yanayotumia mifumo wa kurejeleza maji (*Recirculation Aquaculture System – RAS* na *In-Pond Raceways System - IPRS*) yamesanikishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kupandikiza samaki katika maji ya asili ili kuongeza upatikanaji wa samaki kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kwa wananchi. Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imepandikiza vifaranga **844,000** vya samaki katika Ziwa Ikimba (**822,000**) lililopo Wilaya ya Bukoba; Bwawa la Haubi **(12,000**)

lililopo Wilaya ya KondoaDodoma na Bwawa la Gereza la Kwamngumi la Korogwe, Tanga (**10,000**).

**D. TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**
**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TALIRI imeendelea kufanya utafiti katika nyanja za mifugo na malisho ambapo miradi ya utafiti **13** na majaribio **38** inaendelea kutekelezwa. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa miradi hiyo yamechangia katika kusambaza teknolojia bora za ng'ombe chotara wa nyama na maziwa. Jumla ya ng'ombe chotara **286** wa nyama na maziwa walizalishwa, ambapo ng'ombe wa nyama **112** na wa maziwa **56** tayari wamesambazwa kwa wadau. Ng'ombe hao wa nyama walisambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro (Siha na Hai), Dodoma (Bahi, Mpwapwa na Kongwa), Mwanza (Misungwi na Magu), Shinyanga (Kahama), Simiyu (Bariadi), Arusha (Longido na Monduli), Manyara (Babati na Simanjiro) na Morogoro (Morogoro DC). Vilevile, ng'ombe chotara wa maziwa walisambazwa katika Mikoa ya Tanga (Muheza na Tanga Jiji), Mbeya (Mbeya Jiji), Pwani (Mkuranga) na Dodoma (Kongwa, Mpwapwa na Bahi) kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mifugo na tija kwa wananchi.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TALIRI imeendelea kutunza na kuhifadhi Mbari za mifugo zenye sifa mbalimbali ikiwemo ukuaji, uhimilivu wa magonjwa na uzalishaji ambapo jumla ya mifugo **180** ya mbari tofauti za Mbuzi (*Gogo white, Buha, Sukuma, Norwegian, Toggenburg, Newala, Pare white, Sonjo Red, Galla, Malya, Boer*, *Crossbreeds*) na Kondoo wa asili (*Black Head Persian and Red Maasai*) wamezalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro (Siha), Pwani (Kisarawe), Dodoma (Mpwapwa), Dar es Salaam (Ilala), Arusha (Longido na Arumeru) na Shinyanga (Kahama Mji). Vilevile, jumla ya mbuzi na kondoo chotara **480,** mbuzi wa asili waliboreshwa **415** na kondoo wa asili waliboreshwa **47** walizalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro (Siha), Dodoma (Dodoma Jiji, Mpwapwa na Bahi), Pwani (Kisarawe na Mkuranga), Mbeya (Mbeya Jiji), Dar-es-Salaam (Ilala) na Arusha (Longido na Meru).

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti wa Mifugo Naliendele, inaendelea na utafiti wa kuboresha kuku wa asili aina ya Horasi ambaye ana sifa za ukuaji wa haraka, ustahimilivu wa mazingira magumu na uzito mkubwa ukilinganisha na kuku wengine wa asili. Utafiti huu unalenga kuzalisha na kuboresha kizazi cha kuku wa Horasi chenye uwezo wa kufikia wastani wa uzito wa gramu **1**,**500** ndani ya wiki **16** (miezi minne) na kutaga wastani wa mayai **200** kwa mwaka ikilinganishwa na kuku wa asili asiyeboreshwa ambaye hufikia uzito wa gramu kati ya **1**,**200** – **1,500** kwa mwaka na kutaga mayai kati ya **30**-**45** kwa mwaka. Kituo kinazalisha kuku hao kupitia teknolojia ya uhimilishaji (*Artificial Insemination)*, lengo ikiwa ni kuwa na uhakika wa taarifa za kitafiti kwa kila uzao. Kwa sasa Mradi umefikia hatua ya kizazi cha pili cha kuku hao na unatarajiwa kukamilika baada ya kizazi cha sita, huku kila kizazi kikifanyiwa tathmini ya mwaka mmoja.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa malisho ya mifugo kwa wafugaji, Wizara kupitia TALIRI imefanya utafiti wa mbegu za malisho ambapo aina tisa (**9)** za mbegu hizo zimepata ithibati. Kufuatia ithibati hiyo Wizara na Taasisi zake pamoja na Sekta binafsi zimeanza utaratibu wa kuzalisha mbegu hizo kwa lengo la kuwafikia wafugaji wengi na kuepuka kuagiza mbegu nje ya nchi. Aidha, TALIRI imezalisha **kilo 7,354** za mbegu za nyasi za punje na kilo **13,300** za mbegu za nyasi za vipando zimezalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Mbeya, Pwani, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Iringa. Pia, Taasisi imezalisha jumla ya marobota **48,571** ya hei ambapo marobota **36,370** yalisambazwa kwa wadau wa mifugo katika mikoa hiyo kwa lengo la kuhamasisha kilimo cha malisho na faida ya uhifadhi wa malisho. Aidha, TALIRI imetoa mafunzo kwa wahimilishaji 40 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TAFIRI imeendelea kufanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki wa tabaka la juu (*pelagic species*). Kwa awamu ya kwanza, utafiti umefanyika katika eneo la asilimia **10** ya maji ya Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone - EEZ*) ya Tanzania, ambapo imebainika uwepo wa tani **10**,**582** za samaki. Aidha, TAFIRI ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha

utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki wa tabaka la juu katika Ziwa Tanganyika kwa kushirikiana na nchi za Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Jamhuri ya Zambia.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TAFIRI imefanya tathmini ya hali ya uvuvi wa aina tatu za jodari, yaani Jodari-machomakubwa (*Bigeye tuna*), Jodari-mapezinjano (*Yellowfin tuna*), na Sehewa-miraba (*Skipjack tuna*) katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari wa Tanzania. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha uwepo wa kiasi cha tani **385,950** za Jodari machomakubwa, tani **927,723** za Jodari mapezinjano, na tani **103,289** za Sehewamiraba kinachoweza kuvunwa katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari wa Tanzania kwa mwaka. Aidha, matokeo ya utafiti huu yanatoa taarifa muhimu kwa kampuni za uvuvi za TAFICO na ZAFICO katika kuweka mikakati ya uvuvi endelevu katika eneo la ukanda huu.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya Bahari (*Marine spatial planning*), Wizara kupitia TAFIRI imefanya utafiti wa mazingira ya viumbemaji katika sakafu ya Bahari (*Bottom habitat mapping*) ili kutathmini hali ya mazingira, uwepo wa rasilimali za uvuvi na makazi yake. Utafiti unaonesha uwepo wa makazitete (*sensitive habitats*) ikiwemo matumbawe, nyasi bahari na nyanda za sponji (*sponge beds*) katika kina cha maji cha zaidi ya mita **50** ambayo yanahitaji uangalizi maalum. Pia, utafiti umebaini uwepo wa bustani za matumbawe (*coral gardens*) ambazo ni vivutio vya utalii.

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TAFIRI imewajengea uwezo wadau **60** kuhusu ufugaji wa samaki wa asili wa Ziwa Tanganyika kwa njia ya vizimba; watafiti na maafisa uvuvi **50** kuhusu utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi. Aidha, hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya vifaranga **407,709** vya samaki vimezalishwa ambapo vifaranga **70,000** ni aina ya Sato wa Tanganyika (*Oreochromis tanganicae*), vifaranga **325,709** ni aina ya Sato wa Ziwa Victoria (*Oreochromis niloticus*), na **12,000** ni aina ya Sato wa Ziwa Nyasa (*Coptodon rendalii*). Pia, TAFIRI imeanza utafiti wa ukuzaji wa samaki aina ya Kuhe (*The giant cichlid-Boulengerochromis*

*microlepis*) wanaopatikana Ziwa Tanganyika kwa njia ya vizimba ambapo kufanikiwa kwa utafiti huu kunatarajiwa kuongeza uzalishaji wa samaki na kipato kwa wananchi.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba unategemea ubora wa maji katika eneo husika. TAFIRI inaendelea kufanya utafiti kuhusu ubora wa maji kwenye Ziwa Victoria na Tanganyika katika maeneo tisa (**9**) ya ufugaji samaki yakiwemo maeneo matano (**5**) katika ghuba ya Mwanza, matatu (**3**) katika ghuba ya Shirati na eneo moja (**1**) la Katabe katika Ziwa Tanganyika. Aidha, matokeo ya utafiti huo yameonesha ubora wa maji katika maeneo hayo unakidhi viwango vinavyohitajika kuwezesha ukuaji wa samaki na uendelevu wa mazingira ya kufugia.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha ufungaji wa vitimeza katika kumbi saba (**7**) za mihadhara kwenye kampasi za Morogoro (**200**), Madaba (**100**), Temeke (**100**), Buhuri (**200**), Tengeru (**150**), Kikulula (**50**) na Mpwapwa (**100**). Aidha, LITA inaendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara tatu (**3**) katika Kampasi za Songwe, Madaba na Buhuri; hosteli nne (**4**) katika Kampasi za Kikulula, Buhuri, Madaba na Songwe; na jengo moja la utawala katika Kampasi ya Songwe.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, LITA imeweza kudahili wanafunzi **4,996** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **4,928** waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2024/2025. Ongezeko hilo limechangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi zake nane (**8**). Aidha, kupitia Kampasi ya Buhuri mafunzo yametolewa kwa wafugaji na maafisa ugani wa mifugo **1,023** kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupitia mradi wa Maziwa Faida kwa ufadhili wa Serikali ya Ireland. Vilevile, katika kuimarisha umahiri wa wahitimu kwa njia ya mafunzo kwa vitendo, LITA ilipeleka wahitimu tisa (**9**) katika Chuo cha Shandong

nchini China kupitia programu ya kubadilishana wanafunzi kwa muda wa miezi mitatu.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, LITA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imewajengea uwezo wakufunzi **219** katika nyanja mbalimbali, ambapo wakufunzi **174** kutoka Kampasi nane (**8**) za LITA na vyuo binafsi viwili (**2**) wamejengewa uwezo katika mbinu za utoaji mafunzo kwa kutumia mitaala mipya ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu (SAT) na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Aidha, wakufunzi **16** wa LITA wamejengewa uwezo katika teknolojia ya maziwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Warsaw cha Poland; wakufunzi **12** katika teknolojia mpya za ufundishaji wa Moduli za Afya ya Mifugo nchini Hungary kupitia mradi wa EDUVET; wakufunzi nane (**8**) katika teknolojia ya uzalishaji wa kuku kwa kushirikiana na Kampuni ya Silverlands kutoka Iringa na Chuo cha AERES kutoka Uholanzi; na wakufunzi tisa (**9**) katika teknolojia ya uzalishaji wa malisho kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu (SAT) lililopo Morogoro.

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia LITA kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya kuku imefanikiwa kuandaa rasimu ya Mtaala wa Teknolojia ya Uzalishaji wa Kuku ili kukidhi mahitaji ya watalaam mahiri katika Sekta ya Mifugo. Aidha, Mtaala huu utakuwa ni chachu ya kuongeza uzalishaji wa zao la kuku kwa jamii kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali ikiwemo vijana na wanawake wanaojihusisha na shughuli za ufugaji wa kuku pamoja na kupata wataalamu mahiri watakaoweza kujiajiri au kutoa huduma katika mnyororo wa thamani wa Tasnia ya kuku.

**Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Tanzania (FETA)**

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia FETA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuandaa rasilimaliwatu yenye ujuzi, umahiri na ushindani katika Sekta ya Uvuvi. Jumla ya wanafunzi **1,09** amedahiliwa katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Mbegani-Pwani (**539**), Nyegezi-Mwanza (**443**) na Kibirizi- Kigoma

(**110**). Mafunzo haya yanazingatia mfumo wa umahiri (*Competence-Based Education and Training*), yakilenga kuzalisha wahitimu wabunifu, wanaojiajiri na wenye uwezo wa kuongeza tija katika uchumi. Hatua hii inatekeleza malengo ya Dira 2050 ya kujenga uchumi shindani unaotegemea rasilimaliwatu yenye ujuzi, pamoja na kuongeza ajira kwa vijana. Hatua hizi zinalenga kupanua uwekezaji wa kimkakati katika mtajiwatu (*human capital*) ambao ni nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi endelevu.

**105.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji na ushindani wa Sekta, FETA inaendelea kuboresha mitaala mitano (**5**) iliyopo na kuanzisha mitaala mipya kumi na mbili (**12)** inayozingatia mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Mitaala hii inaandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya NACTVET. Hatua hii inalenga kuongeza ubunifu, ujuzi wa kisasa na uwezo wa wahitimu kushiriki kikamilifu katika uchumi wa viwanda na huduma. Miongoni mwa mitaala mipya iliyoanzishwa ni Mtaala wa Usimamizi wa Bandari za Uvuvi na Lojistiki ambao ni muhimu katika kusaidia uwekezaji mkubwa unaoendelea katika miundombinu ya Bandari za Uvuvi (Bandari ya Uvuvi ya Kilwa na ya Bagamoyo). Kupatikana kwa wataalam hawa kutaimarisha ufanisi katika matumizi ya miundombinu hiyo na kuongeza thamani ya uwekezaji wa Serikali katika sekta hii.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala inaendelea kuratibu mafunzo ya Ubaharia yanayokidhi matakwa ya Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F (*International Convention on Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Fishing Vessel Personnel, 1995 STCW-F95)* pamoja na mafunzo ya Uangalizi wa Meli za Uvuvi Baharini (*Sea Observer Course*). Mafunzo haya yanalenga kutoa mabaharia wenye ujuzi na viwango vinavyokubalika kimataifa, kuongeza ubora wa mazao ya uvuvi na kulinda mazingira ya bahari. Kupitia mafunzo haya, vyeti vya mabaharia kutoka Tanzania vitatambulika kimataifa, jambo litakalofungua fursa za ajira si tu ndani ya nchi kupitia meli za TAFICO na ZAFICO zinazovua kwenye Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (EEZ), bali pia nje ya Nchi katika meli za uvuvi za mataifa mengine. Aidha, utekelezaji wa mafunzo haya utachochea ajira kwa vijana na wanawake, kuongeza mapato ya fedha za kigeni, kuimarisha

udhibiti na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, na kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupanua wigo wa fursa za kiuchumi kwa wananchi, washiriki **7,459** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nyanja za uzalishaji, uchakataji, uhifadhi, ujasiriamali na masoko ambayo yalihusisha mbinu bora za ufugaji wa samaki wa kibiashara (**183**); ufugaji wa Majongoo Bahari (**208**); unenepeshaji wa Kaa (**157**); kilimo cha mwani (**293**); mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu (**730**); uchakataji wa mazao ya uvuvi (**1,564**); ufundi stadi wa matengenezo ya majokofu na vipoza hewa (**54**); uendeshaji na usalama wa vyombo vidogo katika maziwa na bahari (**147**); masoko ya bidhaa za uvuvi, ujasiriamali, ubunifu na fedha (**1,009**); usalama kwenye maji, kuogelea na kujiokoa (**209**); mafunzo ya ulinzi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi na uongozi kwa BMUs (**94**); mafunzo ya udhibiti ubora kwa wafanyakazi wa viwandani (**254**); na mafunzo ya lishe na usalama wa chakula kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari (**2,557**).

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA)**

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa uhakika wa chanjo za mifugo, Wizara kupitia TVLA imezalisha na kusambaza jumla ya dozi **63,641,885** za chanjo za aina saba **(7)** za magonjwa ya kipaumbele nchini sawa na asilimia **87.2** ya lengo la kuzalisha dozi **73,000,000.** Uzalishaji ulijumuisha chanjo dhidi ya magonjwa ya Mdondo (TEMEVAC I-2) dozi **59,384,000;** Kimeta dozi **358,000**; Chambavu dozi **74,700**; Homa ya Mapafu ya Ng'ombe dozi **3,500,400**; Kutupa Mimba dozi **3,785**; muunganiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) dozi **186,000;** na Homa ya Mapafu ya Mbuzi dozi **135,000**. Aidha, TVLA imeendelea kufanya tafiti **13** ambazo zinalenga kuibua teknolojia za uzalishaji wa chanjo za mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kuwajengea uwezo watafiti.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026 hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 TVLA kupitia maabara zake kumi (10) imefanya uchunguzi wa magonjwa ya wanyama ambapo jumla ya sampuli **63,440** zilifanyiwa uchunguzi na magonjwa mbalimbali

yalitambuliwa yakiwemo Mdondo na Ndui kwa kuku, Homa ya Nguruwe, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Nagana, Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Ugonjwa wa Midomo na Miguu na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe. Ukilinganisha na mwaka 2024/2025 Wakala ilipima jumla ya sampuli **37,550** ikiwa ni ongezeko la sampuli **25,890**. Vilevile, Wakala imefanya uchunguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo, ambapo jumla ya sampuli **1,873** za vyakula vya mifugo zimefanyiwa uchambuzi na ushauri wa kitaalam umetolewa kwa wazalishaji wa vyakula hivyo pamoja na wafugaji. Aidha, TVLA imeendelea kulinda Ithibati ya ISO/IEC17025:2017 kwa vipimo 10 vya uchunguzi wa magonjwa kimaabara kupitia ukaguzi uliofanywa mwezi Oktoba 2025 na Taasisi inayosimamia masuala ya Ithibati katika nchi za SADC.

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kutafuta na kuibua masoko ya nyama nje ya nchi, TVLA imefanikiwa kupima sampuli **3,810** kutoka kwa wanyama waliokusudiwa kuchinjwa kwa ajili ya kukidhi matakwa ya viwango vya soko la nchi ya Qatar. Sampuli hizo ni sawa na asilimia **30** ya wanyama wote waliokusudiwa kuchinjwa kwa mujibu wa vigezo vya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH).

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu la kusajili na kuhakiki ubora wa viuatilifu kwa ajili ya mifugo, hadi kufikia Aprili, 2026 Wakala imetoa vibali **74** vya kuingiza viuatilifu kwa ajili ya mifugo sawa na asilimia **49.3** ya lengo la kutoa vibali **150**. Vibali hivyo vilihusisha uingizaji wa lita **725,081.34** za viuatilifu vya kimiminika pamoja na kilo **10,000** za viambata vya kutengenezea viuatilifu. Vilevile, Wakala ilitekeleza programu za kutoa elimu kwa wadau wa mifugo kuhusu ubora na matumizi sahihi ya viuatilifu katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Mtwara, Singida, Iringa na Kigoma. Kupitia programu hizo, jumla ya wadau **312** walifikiwa kati ya wadau **400** waliolengwa, sawa na asilimia **78** ya lengo la mwaka 2025/2026.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma za Wakala, TVLA imeendelea kuboresha miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za kimaabara kwa kuanza ujenzi wa jengo jipya la ghorofa nne (**4**) katika Kituo cha Wakala cha Kanda ya Kati

Dodoma. Aidha, Wakala imeendelea na ukarabati wa majengo ya maabara na ununuzi wa vifaa, ambapo hadi Aprili, 2026 umefanyika ukarabati katika jengo la kituo cha Magonjwa Ambukizi na Bioteknolojia pamoja na Kituo cha Wakala Kanda ya Ziwa - Mwanza. Vilevile, Wakala imeendelea kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa chanjo katika Taasisi ya Uzalishaji wa Chanjo (*Tanzania Vaccines Institute -TVI*) iliyopo Kibaha - Pwani.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) imeendelea kusimamia uvuvi katika Ukanda Maalumu wa Uchumi wa Bahari (EEZ) ambapo hadi mwezi Aprili, 2026, Mamlaka imetoa leseni **42** ambapo **leseni 40** ni kwa meli za kigeni na leseni mbili (**2**) kwa meli za Tanzania ikilinganishwa na leseni **30** zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, DSFA imetoa jumla ya vibali **24** vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania, vibali viwili (**2**) vya uwakala wa meli, na vibali saba (**7**) kwa meli saidizi. Kupitia utoaji wa leseni na vibali hivyo, DSFA imekusanya jumla ya Shilingi **7,474,540,000** sawa na asilimia **46.14** ya lengo la kukusanya Shilingi **11,957,328,477** kwa mwaka 2025/2026.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, DSFA imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika EEZ na nje ya mipaka ya Tanzania kwa kutekeleza maazimio ya kikanda na kimataifa yakiwemo ya Kamisheni ya Jodari ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission - IOTC) na Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Commission – SWIOFC). Aidha, DSFA imeendelea kusimamia shughuli za uvuvi kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli (*Vessel Monitoring System - VMS* na *Automatic Identification System – AIS*) na kuweka Waangalizi wa Uvuvi katika meli zinazovua katika EEZ ya Tanzania.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia MPRU imeendelea kusimamia na kuendeleza maeneo **18** yenye

hifadhi za bahari tatu (**3**) (Kisiwa cha Mafia - MIMP, Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma - MBREMP na Silikanti Tanga) na maeneo tengefu (**15**) katika Bahari ya Hindi yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba **2,173**. Maeneo hayo yanahifadhi rasilimali muhimu za kimkakati (*critical strategic assets*) katika kuchochea urejeshwaji wa mifumo ikolojia na kuimarisha utalii endelevu wa bahari na fukwe. Rasilimali hizo ni pamoja na nyasi bahari (*seagrasses*); matumbawe; samaki aina ya Papa potwe, Silikanti, Kasa na Kaa ambao wameripotiwa kutoweka au kuwa katika hatari ya kutoweka.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, MPRU ilifanya jumla ya doria **1,056** zenye jumla ya masaa **7,392** ikilinganishwa na doria **948** zenye jumla ya masaa **6,566** katika mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia **11.4**. Aidha, MPRU imeendelea kushirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za bahari ambapo wanajamii **1,896** walipatiwa mafunzo ya uhifadhi wa rasilimali za bahari (**1,726**) na uzalishaji wa mwani (**170**), na kuanzisha vikundi **35** vya VICOBA na **67** vya usimamizi na uhifadhi (*Village Laison Committee – VLC*) katika Hifadhi ya Kisiwa cha Mafia.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, tathmini ya hali ya matumbawe zimeonesha kuwa kiwango cha matumbawe magumu katika Eneo Tengefu la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Marine Reserves System - DMRS*) kilikuwa asilimia **48.44**, MBREMP asilimia **36.67**, na MIMP asilimia **26.3** ikilinganishwa na kiwango cha asilimia **25** kinachopendekezwa katika eneo la bahari Magharibi mwa Bahari ya Hindi. Ili kurejesha mifumo ikolojia ya bahari, MPRU kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori (*Wildlife Conservation Society - WCS*) iliweka baharini vipande vya matumbawe **7,224** katika eneo la Hifadhi ya Silikanti Tanga (TACMP) na vipande **12,500** katika Eneo Tengefu la Bahari Tanga (*Tanga Marine Reserves System - TMRS*). Vilevile, MPRU kwa kushirikiana na wanajamii ilipanda miche ya mikoko **32,000** katika MBREMP.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania, Wizara kupitia ufadhili wa Programu ya Kuendeleza

Uchumi na Jamii (*Economic and Social Development Program-ESDP*) ya Japan, imekamilisha ununuzi wa meli ya kisasa (TAFICO FV.01) ya uvuvi wa Bahari Kuu yenye urefu wa mita **22** ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 25 Aprili, 2026 na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Meli ya aina hiyo ni ya kwanza kumilikiwa na Serikali kupitia Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na itaendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Aidha, upatikanaji wa meli hii ni hatua ya kimkakati katika kuimarisha Shirika la TAFICO na kutumia fursa za uchumi wa buluu katika kufanya mageuzi kwenda uvuvi wa kisasa na uzalishaji wenye tija ili kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara na kuongeza mchango wa sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026 Wizara kupitia TAFICO chini ya Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agricultural and Fisheries Development Program-AFDP*), imekamilisha ununuzi wa mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani 10 za barafu kwa siku, na usanikishaji wake unaendelea; Ukarabati wa gati lenye urefu wa mita **70** kwa ajili ya kuegesha meli na ununuzi wa magari mawili (**2**) ya ubaridi yenye uwezo wa kubeba uzito wa tani **10** kila moja kwa ajili ya kusafirishia mazao ya uvuvi. Aidha, Upembuzi Yakinifu, Uandaaji wa Michoro na Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) ya mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki (*Fish Feed Mill*) chenye uwezo wa kuzalisha tani **30** kwa siku kinachotarajiwa kujengwa Ilemela–Mwanza, umekamilika; Uandaaji wa michoro na makisio ya gharama za ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya Uvuvi (*Fish Processing Plant*) kinachotarajiwa kujengwa Kilwa Masoko-Lindi umekamilika. Vilevile, mchakato wa ununuzi wa meli mbili (**2**) za uvuvi wa Bahari Kuu na Ujenzi wa ghala la ubaridi lenye uwezo wa kuhifadhi samaki tani **80** hadi **120** kwa siku unaendelea.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2026 NARCO imekusanya jumla ya Shilingi **8,209,281,656.22** ikilinganishwa na kiwango cha Shilingi **5,975,044,928.56** kilichokusanywa kwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia

**27.2**. Mapato haya yanatokana na mauzo ya nyama, ada za vitalu, mauzo ya ng'ombe wazazi, na mazao mengine ya mifugo. Aidha, mwezi Aprili mwaka 2024 NARCO ilikabidhiwa na kuanza rasmi uendeshaji wa Machinjio ya Dodoma ambapo imeongeza mapato kutoka Shilingi **821,407,167** hadi kufikia **1,066,000,000** mwezi Aprili, 2026 ikiwa ni ongezeko la asilimia **23**. Mapato haya yametokana na kukusanya ada ya uchinjaji ng'ombe **28,541** na Mbuzi/Kondoo **70,214**. Pia, NARCO imefanya ukarabati wa Machinjio ya Dodoma awamu ya kwanza hadi kufikia asilimia 80 ili kuongeza ufanisi. Ukarabati huo utasaidia kuboresha huduma za uchinjaji na uchakataji kwa wafanyabiashara binafsi wanaouza nyama nje ya nchi.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NARCO imeendelea kuimarisha Sekta ya Mifugo kwa kushirikisha Sekta Binafsi kwakuwa na wawekezaji wa kimkakati ambapo NARCO imeingia makubaliano na kampuni za Kahama *Fresh Ltd (KFL)*, *Union Meat Co Ltd (UMAL)*, *Liam Ranch Ltd (LRL)* na *Tanzania Game and Livestock Breeders (TGLB)* kwa lengo la kuzalisha kosaafu bora za mifugo kufikia soko la ndani na nje ya nchi kwa kuboresha mnyororo wa thamani. Maeneo yaliohusika ni Ranchi ya Kikulula (Mkoa wa Kagera) na Ruvu (Mkoa wa Pwani), Mzeri Hills (Mkoa wa Tanga) na West Kilimanjaro (Mkoa wa Kilimanjaro) mtawalia. Hadi sasa wawekezaji hao wamewekeza ng'ombe bora wa nyama na maziwa **5,163** na mbuzi na kondoo **7,675.**

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, NARCO imezalisha jumla ya ndama **3,065** (*Friesian* **12**, *Brahman* **86**, *Limosin* **13**, *Simental* **60** na *Boran* **2,894**) sawa na asilimia **64** ya lengo la kuzalisha ndama **4,799**; ukilinganisha na ndama **2,312** waliozaliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Vilevile, NARCO imezalisha na kuuza tani **360.13** za nyama, sawa na asilimia **55** ya lengo la kuzalisha na kuuza tani **653.25** za nyama; ukilinganisha na tani **232.6** zilizozalishwa na kuuzwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2024/2025. Imenenepesha na kuchinja ng'ombe **1,599**, sawa na asilimia **64** ya lengo la kunenepesha na kuchinja ng'ombe **2,500**. Imeuza Mitamba/Madume **125** kwa wafugaji kwa lengo la kuboresha kosaafu za mifugo ikiwa ni sawa na asilimia **14.2** ya lengo la kuuza Mitamba/Madume **733**.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha na kuruhusu ukuaji wa malisho, NARCO imefyeka na kuondoa vichaka ekari **1,866** kwa ajili ya kuboresha na kuruhusu ukuaji wa malisho katika Ranchi za Kongwa (ekari **182**), Ruvu (ekari **220**) na West Kilimanjaro (ekari **232**), Missenyi (ekari **726**), Mzeri Hills (ekari **80**) na Kikulula (ekari **426**), ukilinganisha na ekari **600** zilizofyekwa na kuondoa vichaka katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2024/2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia **68**. Imeanzisha mashamba mapya ya Juncao ambapo ekari **340** zimelimwa na kupandwa katika Ranchi za Kongwa na Ruvu. Aidha, NARCO imezalisha marobota **35,000** ya hei, sawa na asilimia **61** ya lengo la kuzalisha marobota **57,307**; imetoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **237**; na imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **378** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini.

**Bodi ya Nyama Tanzania**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kusimamia shughuli za uzalishaji na biashara ya nyama kwa kufanya ukaguzi katika maeneo ya uzalishaji na biashara ya nyama. Ukaguzi huo unalenga kuhakikisha nyama na bidhaa zake zinakidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 jumla ya wadau **12,538** wamekaguliwa katika mikoa mbalimbali ikilinganishwa na wadau **10,082** waliokaguliwa katika mwaka 2024/2025.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendelea kutekeleza jukumu la kuwatambua na kuwaratibu wadau mbalimbali wanaofanya shughuli za uzalishaji kwenye mnyororo wa Tasnia ya nyama. Hadi mwezi Aprili, 2026 jumla ya wadau **10,569** wametambuliwa na kusajiliwa baada ya kukidhi vigezo. Biashara zilizosajiliwa ni pamoja na viwanda na miundombinu ya kuzalisha nyama, wafanyabiashara wa mifugo na nyama, wasafirishaji wa nyama nje na magari ya kubebea nyama. Aidha, katika kuhakikisha ubora na usalama wa nyama na bidhaa zake, Bodi imetoa mafunzo kwa wasindikaji na wauzaji wa nyama **13,114** katika mikoa ya Arusha (**1,053)**, Dar-es-Salaam (**3,005**), Iringa (**120**), Kagera (**280**), Katavi (**213**), Kigoma (**274**), Manyara (**225**), Dodoma (**773**), Geita (**325**), Kilimanjaro (**453**), Lindi

(**163**), Mara (**338**), Mbeya (**1,220**), Morogoro (**379**), Mwanza (**613**), Pwani (**507**), Ruvuma (**459**), Shinyanga (**487**), Simiyu (**136**), Songwe (**201**), Tanga (**452**), Mtwara (**91**), Morogoro (**379**), Njombe (**348**), Singida (**229**) na Tabora (**712**).

**Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)**

**126. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Bodi ya Maziwa Tanzania imesajili jumla ya wadau **558** wa Tasnia ya Maziwa kati ya **800** waliolengwa sawa na asilimia **69.8**. Wadau waliosajiliwa ni pamoja na wazalishaji **115**; wafanyabiashara **125**; wasindikaji **25**; wakusanyaji **40**; wasafirishaji **95**; waingizaji maziwa nchini **45**; Wauzaji maziwa nje ya nchi **27**, Wasambazaji wa maziwa **31**; na maghala ya kuhifadhia maziwa **55.** Katika zoezi hilo, elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya Maziwa na Kanuni zake ilitolewa. Aidha, ili kuendelea kurasimisha biashara ya maziwa na kupunguza uuzaji holela wa maziwa, Bodi imewezesha uanzishwaji wa sehemu maalumu za kuuzia maziwa (*milk selling points*) **38** katika mikoa ya Dar es Salaam (11), Mbeya (10), Dodoma (3), Arusha (3), Morogoro (3), Iringa (3) Mwanza (2), Kilimanjaro (2) na Geita (1).

**127. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Bodi imeendelea kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Tasnia ya Maziwa ambapo katika mwaka 2025/26, jumla ya wadau **1,051** kati ya **1,200** waliolengwa sawa na asilimia **87.6** walikaguliwa katika Kanda ya Kaskazini (**131**), Kanda ya Kati (**103**), Kanda ya Ziwa (**216**), Kanda ya Mashariki (**458**), na Nyanda za Juu Kusini (**143**). Hatua stahiki zilichukuliwa kwa waliokiuka sheria. Aidha, ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa maziwa, kukuza kipato cha wadau wa Tasnia sambamba na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa, jumla ya wadau **638** kati ya **1,200** waliolengwa sawa na asilimia **53** walipatiwa mafunzo katika maeneo ya ufugaji wa kibiashara wa ng'ombe wa maziwa (**439**) na usindikaji wa maziwa (**199**).

**128. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni (SMP) kwa lengo la kujenga utamaduni wa unywaji wa maziwa na kuboresha afya ya watoto. Hadi kufika Aprili, 2026 shule

zinazoshiriki katika mpango huo ziliongezeka kwa asilimia **56** hadi kufikia shule **218** kutoka shule **140** mwaka 2024/2025. Aidha, idadi ya watoto wanaokunywa maziwa shuleni kupitia Mpango huo imefikia **114,000.**

## E. MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko wenye thamani ya Shilingi **280,585,849,982.73** ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 ujenzi huo umefikia asilimia **97**. Ujenzi umehusisha gati lenye urefu wa mita **315** ambalo limekamilika kwa asilimia **100**; Jengo la utawala asilimia **98**; Jengo la kuzalishia barafu, kuhifadhia, kuandalia samaki pamoja na soko la kuuzia samaki asilimia **96**; Kituo cha kusambazia maji safi asilimia **96**; Kituo cha zimamoto asilimia **80**; Kituo cha kupozea umeme asilimia **97**; Kituo cha kuzalishia gesi ya naitrojeni asilimia **95**; ujenzi wa miundombinu ya kuegesha magari asilimia **96**; Tanki za kuhifadhia mafuta na Karakana ya kutengenezea meli umefikia asilimia **97**.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia ASDP II imeendelea na ujenzi wa masoko sita (**6**) ya samaki ya Tunduma asilimia **35**, Kyamkwikwi (Muleba) asilimia **26**, Masuche (Momba) asilimia **14**, Manda (Ludewa) asilimia **40**, Zingibari (Mkinga) asilimia **65**, Kasanga (Kalambo) asilimia **95** na kukamilisha ujenzi wa Soko la Samaki Mbamba bay (Nyasa). Aidha, ujenzi wa mialo mitatu (**3**) ambapo Chato beach (Chato) umefikia asilimia **97**, Kalungu (Nkasi) asilimia **5** na Ng'ombo (Nyasa) asilimia **48**. Pia, Wizara imeendelea na ujenzi wa vituo viwili (**2**) vya ukuzaji viumbemaji vya Nyengedi asilimia **32** na Ruvula ambapo ujenzi wake umekamilika kwa awamu ya kwanza. Vilevile, Wizara imeendelea na ujenzi wa vituo vya ulinzi na usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ambapo vituo vya Simiyu (Busega) na Nyakalilo (Sengerema) vimekamilika na kituo cha Sota (Rorya) awamu ya pili umefikia asilimia **45**.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia ASDP II imekamilisha ujenzi wa vituo saba (**7**) vya kukusanyia maziwa ambavyo ni Omurushaka (Karagwe), Masama (Hai), Ngaramtoni (Arusha), Mwasonga (Kigamboni), Misufini (Morogoro), Maswa (Simiyu) na Komuge (Rorya). Aidha, ujenzi wa vituo vitatu (**3**) unaendelea Msomera (Handeni) asilimia **85**, Makambako asilimia **70** na Kwemakame (Lushoto) asilimia **70**. Aidha, ujenzi wa minada **23** unaendelea ikiwemo minada **17** ya awali, minne (**4**) ya upili na miwili (**2**) ya mipakani (**Kiambatisho Na.11).** Vilevile, mabwawa matatu (**3**) ya Msomera (Handeni), Kwekikwembe (Kilindi) na Kaiwang (Kiteto) kwa ajili ya kunyweshea mifugo, maghala mawili (**2**) ya Langwira (Mbarali) na Vikuge (Kibaha) pamoja na ujenzi wa mfumo wa umwagiliaji Vikuge unaendelea.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia ASDP II imeendelea na ujenzi pamoja na ukarabati wa miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji ili kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa kituo cha kuendeleza ukuzaji viumbemaji bahari cha Ruvula-Mtwara. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha utendaji wa vituo vitano (**5**) vya kuendeleza ukuzaji viumbemaji vya Machui (Tanga), Ruhila (Ruvuma), Nyengedi (Lindi), Mwamapuli (Tabora) na Kingolwira (Morogoro) kwa kuvipatia vitendea kazi ili kuboresha mazingira ya kazi na kutoa huduma za ugani na uzalishaji vifaranga.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo na kuendelea kukidhi vigezo vya biashara ya mifugo na mazao yake katika masoko ya kikanda na kimataifa, Wizara kupitia ASDP II inaendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kwa kununua na kusambaza chanjo za magonjwa ya kipaumbele. Aidha, jumla ya hereni za kidijitali **36,323,300** zimenunuliwa kwa ajili ya utambuzi wa ng'ombe **19,099,100** pamoja na mbuzi na kondoo **17,224,200** watakaopatiwa chanjo. Mifugo yote itakayochanjwa itatambuliwa kwa hereni hizo na taarifa zake kuingizwa kwenye Mfumo wa Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo. Lengo la utambuzi huu ni kukidhi matakwa ya masoko ya kikanda na kimataifa yanayohitaji utambuzi wa kila mnyama na mazao yake, kurahisisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa, wizi wa mifugo,

pamoja na kuwawezesha wafugaji kupata mikopo na bima. Vilevile, hatua hii itawezesha Serikali na wadau kupanga na kuboresha huduma za mifugo kwa kuzingatia takwimu sahihi za idadi ya mifugo na wafugaji, pamoja na kuwezesha kutambua ubora wa mbegu za mifugo.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Dairy Transformation Project - C-SDTP*) unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka **10** katika mikoa minane (**8**) ya Tanzania Bara, ambapo hadi Aprili, 2026 kaya **469** za wanufaika zilitambuliwa; kilo **1,000** za mbegu za malisho zilisambazwa kupitia mashamba darasa **19** ya wafugaji na ekari **28** zilipandwa malisho. Aidha, mashamba mawili (**2**) ya kuzalisha mitamba ya Kitulo na Sao Hill yalifanyiwa tathmini ili yaweze kutumika kama chanzo cha uhakika cha uzalishaji wa mitamba ya ng'ombe bora wa maziwa; upembuzi yakinifu wa mifumo ya usambazaji maji kwa ajili ya mifugo umefanyika katika Halmashauri za Meru, Arusha, Siha na Moshi; na kufanya maboresho ya mfumo wa taarifa za mifugo wa UTAMBUZI (*National Animal Health and Identification System*). Vilevile, vikundi **162** vya wafugaji vyenye wanachama **9,019** vilitambuliwa ili vishirikishwe kwenye shughuli za mradi; na mikutano ya majukwaa ya wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani wa tasnia ya maziwa iliratibiwa na kufanyika katika Halmashauri **21** zinazotekeleza mradi.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu na malisho kwa kununua vifaa shamba (*drum mowers* **2**, *hay rakes* **2**, *hay bailers* **2** *na forage harvester* **1**) kwa ajili ya mashamba ya Vikuge (Kibaha) na Langwira (Mbarali). Aidha, kazi ya kuondoa vichaka na mimea vamizi katika eneo la malisho hekta **2,000** la Kijiji cha Msomera imekamilika, hivyo kufanya eneo lililoboreshwa katika kijiji hicho kufikia hekta **4,000** ambazo zitachangia kuimarika kwa upatikanaji wa malisho na uwezo wa eneo hilo kuhudumia mifugo mingi.

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Program* - AFDP)**

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi AFDP imekamilisha ujenzi wa vichanja **40** vya kukaushia dagaa katika Halmashauri ya Kilwa (Lindi) na uchimbaji wa kisima kirefu katika Kituo cha Ukuzaji Viumbemaji Kingolwira (Morogoro). Aidha, ujenzi wa Soko la Samaki Kipumbwi (Tanga) umefikia asilimia **45,** ujenzi wa mabwawa **10** na ukarabati wa kitotoleshi katika kituo cha Kingolwira umefikia asilimia **98** na **75** mtawalia. Aidha, ujenzi wa jengo la mafunzo na ofisi – Boma Road (Morogoro) umefikia asilimia **86** na ujenzi wa kituo cha Rubambagwe (Geita) umefikia asilimia **62**. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutapunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa, kuimarisha mazingira ya kibiashara katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa mazao ya uvuvi, huduma za ugani na kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2025/2026 Wizara, kupitia AFDP imetoa mafunzo kwa wanufaika **20,564** ikiwemo wakuzaji viumbemaji **4,333,** wavuvi wadogo **8,917** na wachakataji wadogo **7,314** katika Halmashauri za Wilaya ya Songea, Mbinga, Namtumbo, Tunduru, Nyasa, Igunga, Nzega, Uyui, Bukombe, Chato, Geita, Pangani, Bagamoyo, Mafia na Kilwa. Mafunzo hayo yalilenga kuwapatia stadi za usimamizi bora wa mabwawa ya samaki, kuwajengea uwezo wa kutengeneza chakula cha samaki cha gharama nafuu, kuwawezesha kuzingatia kanuni bora za ukuzaji wa viumbe maji, kuhusu mbinu bora za uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi, mbinu za uvuvi endelevu unaozingatia mabadiliko ya Tabianchi, lishe na jinsia. Pia, jumla ya maafisa ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbemaji **20** wamejengewa uwezo.

**Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (*Extended Credit* Facility– ECF)**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026 Wizara imeendelea na usimamizi na ufuatiliaji wa mradi wa kutoa mikopo ya masharti nafuu ya vizimba na pembejeo za kufugia samaki zenye thamani ya shilingi **7,529,391,121.21** katika mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera, Geita, Katavi, Rukwa, Ruvuma, na Kigoma. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya tani **460.07** za samaki zenye thamani ya Shilingi **3,594,963,147.84** zimevunwa kutoka katika vizimba **301** vya vikundi **73** na kufanya marejesho ya Shilingi **3,033,495,795.97**. Aidha, Wizara inaendelea na usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo hii ili kuhakikisha inatekelezwa kwa tija na kwa maslahi ya jamii.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa ahadi ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa Shilingi **200,000,000,000** kwa vijana ndani ya siku **100** baada ya kuingia madarakani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepokea Shilingi **23,685,829,751.00** kwa ajili ya kukopesha vijana. Kati ya fedha hizo ukopeshaji wa boti za uvuvi pamoja na vifaa vyake ni Shilingi **9,551,151,629,** ufugaji samaki kwa vizimba Shilingi **9,384,678,122** na BBT mifugo Shilingi **4,750,000,000**. Aidha, mikopo hiyo imejikita katika kuwapatia vifaa na pembejeo za ufugaji wa samaki kwa vizimba, boti na zana za uvuvi, ufugaji wa kuku, nguruwe, mbuzi na kondoo na uchakataji wa mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji.

**Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji wa Bahari Tanzania - TASFAM**

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mradi TASFAM imewajengea uwezo jumla ya wakulima wa mwani na wafugaji wa majongoo bahari **1,178** (wanawake **845** na vijana **333**) kuhusu mbinu bora za kilimo cha mwani na uchakataji, na mbinu bora za ufugaji wa majongoo bahari katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha mbinu bora za kilimo cha mwani na uchakataji na ufugaji wa majongoo

bahari. Vilevile, TASFAM inaendelea na upembuzi yakinifu katika maeneo ya ujenzi wa mialo ya samaki katika maeneo ya Miseti, Shuka, Kilwa Kivinje, Kisiju na Mchinga I. Pia TASFAM inaendelea na upanuzi wa soko la samaki la Bagamoyo pamoja na ujenzi wa vituo vya uvuvi na ukuzaji viumbemaji katika maeneo ya Tawalani na Lindi. Hali kadhalika, mradi huo umewezesha ujenzi wa maghala manne (**4**) ya kuhifadhia mwani katika maeneo ya Naumbu, Songosongo, Ndumbani na Kiegeani pamoja na ujenzi wa gati katika kisiwa cha Mbudya.

**F. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIKANDA**

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Programu ya SADC ya Kuhamasisha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi na Ukuzaji viumbe maji endelevu (*PROFISHBLUE*) kikanda imekabidhi vifaa **10** vya usimamizi wa mwenendo wa vyombo vya uvuvi *(vessel monitoring system –VMS*) vilivyosanikishwa kwenye boti za wavuvi katika Ziwa Tanganyika mkoa wa Kigoma, ambavyo vinasaidia usalama na ufuatiliaji wa vyombo vya uvuvi. Aidha, Kupitia mradi huu Wizara imeandaa na kuchapisha Kitabu cha Mapishi ya Samaki na Mazao ya Uvuvi (*A recipe book for fish and fishery products*). Pia, mradi huo umewajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati (*Small and Medium Entreprises - SMEs*) **110** kuhusu taratibu za kupata nembo za ubora na viwango. Vilevile, Mradi umewezesha kufanyika kwa utafiti wa kuangalia wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Tanganyika ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2026.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kupitia Mradi wa Kikanda wa FISH4ACP unaotekelezwa katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika imeimarisha miundombinu ya uvuvi kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa katika Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Uvinza, Tanganyika, Kalambo na Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa kuwezesha usanikishaji na ununuzi wa *Solar Tents* **24**; Majiko banifu **24**; Muyobozi *burner* (vyumba vya kukausha dagaa kwa mkaa wakati wa mvua) **20**; Mtambo wa kuzalisha barafu **1** wenye uwezo wa kuzalisha tani **24** kwa siku na wenye sehemu ya kukaushia dagaa kilo **300** kwa siku; majokofu yanayotumia nishati

ya jua **10**; Mabini (*Ice bin* **20**); pamoja na madeli ya kubebea barafu (*ice box*) **20**.

**MASUALA MTAMBUKA**
**Dawati la Mitaji na Uwekezaji**

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kuchochea uzalishaji na kuongeza tija katika sekta mifugo na uvuvi, Wizara kupitia Dawati la Mitaji na Uwekezaji imewaunganisha wadau wa Sekta Binafsi na taasisi za umma ili kuongeza ajira na mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa. Katika mwaka 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na benki za CRDB, NMB, TADB na TCB imewezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya Shilingi **698,138,626,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **417,690,000,000** zilitolewa kwa Sekta ya Uvuvi (wanufaika **27,214**) kwa ajili ya vizimba, viwanda, boti, ujenzi wa mabwawa ya samaki na wafanyabiashara wa samaki. Aidha, Shilingi **280,448,836,000** zilitolewa kwa Sekta ya Mifugo (wanufaika **5,356**) kwenye Tasnia ya Maziwa, usindikaji wa mazao ya mifugo, unenepeshaji wa mifugo, viwanda vya uzalishaji chakula cha mifugo, kilimo cha malisho, na ufugaji wa kuku.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha uwekezaji, katika mwaka 2025/2026 Wizara imefanikiwa kuhamasisha wadau katika mikoa **14** ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Simiyu, Geita, Kagera, Mara, Njombe, Morogoro, Kigoma, Dar es Salaam, Pwani na Lindi ili kubaini maeneo mapya ya kimkakati ya uwekezaji, hususan katika mnyororo wa thamani ya mazao ya nyama, maziwa, na samaki. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya uandaaji wa maandiko ya kibiashara kwa vyama vya ushirika **12** (Ilemela **2**, Ukerewe **3**, Mafia **2**, Bagamoyo **2**, Nyamagana **3**) na vikundi **28** (Uvinza **2**, Kigoma **4**, Bukoba **6**, Chato **4**, Geita **2**, Nyamagana **4**, Musoma **3**, Rorya **3**) vya wajasiriamali. Pia, zaidi ya wadau **428** wametembelewa na kupewa ushauri wa kitaalam wakiwemo wazalishaji wa chakula cha mifugo; wachakataji wa samaki; wavuvi wadogo na wa kati; wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuku; pamoja na wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa. Ufuatiliaji unaonesha kuwa, kati ya biashara zilizopatiwa ushauri, asilimia **40** kati ya hizo zimeongeza uzalishaji

ndani ya miezi **6–12**, ishara ya matokeo chanya ya huduma za ugani zenye mwelekeo wa kibiashara.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake, inaendelea na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kwa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Bagamoyo inayolenga kubaini na kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza katika mradi. Tathmini ya utekelezaji wa kazi hiyo imefikia asilimia **25**. Aidha, Wizara inaendelea na tathmini kwa miradi mingine **32** ambapo kati ya hiyo, miradi mitano **(5)** ikiwemo ukarabati wa jengo la Mvuvi House, ujenzi wa Kituo cha TAFIRI -Dar – Centre Kunduchi, ujenzi wa national Mariculture resource centre, jengo la utawala (MIMP)-Mafia na majengo ya soko la samaki Bagamoyo tathmini imekamilika.

**Utawala Bora, Jinsia na VVU/UKIMWI**

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utawala bora, Wizara imefanikiwa kuhamasisha watumishi **113** kushiriki bonanza la michezo na mashindano ya SHIMIWI, ili kuimarisha afya ya watumishi na kupunguza Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza. Vilevile, katika kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi jumla ya watumishi **89** wameajiriwa, **77** wamepandishwa vyeo, **22** wamebadilishwa kada na **8** wameteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na wadau wengine imeendeleza mikakati ya kupambana na kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahala pa kazi. Aidha, katika Mwaka 2025/2026 Wizara ilihamasisha jumla ya watumishi **1,041** kujikinga na VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kutoa vifaa kinga na kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari ambapo jumla ya watumishi **107** walihamasishwa na kupima afya kwa Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza ambayo ni shinikizo la juu la damu, uwiano wa uzito na urefu na kiwango cha sukari kwenye damu.

## Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha mifumo ya TEHAMA ya Wizara inatoa huduma bora kwa wananchi na inasomana na mifumo mingine ndani ya Serikali. Mifumo hiyo ni pamoja na *Mifugo Integrated Management Information System* (***MIMIS***) inayotumika kwenye usimamizi na utoaji wa vibali mbalimbali vya kusafirisha mifugo na mazao yake, na Mfumo wa UTAMBUZI unaotumika katika kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo. Mifumo hiyo pia imeunganishwa na mfumo wa TAUSI wa OWM-TAMISEMI unaotumika kukusanya maduhuli ya Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kutumia Mfumo wa Ukusanyaji Maduhuli ya Sekta ya Uvuvi (*Fisheries Revenue Collection Information System* - FiRCIS) pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Uvuvi na Ukuzaji Viumbemaji (*Fisheries and Aquaculture Information Management System* - FAIMS) ambao unasaidia katika ukusanyaji wa takwimu za mavuno ya samaki; Wavuvi kufikia maeneo yanayobashiriwa kuwa na mkusanyiko wa samaki; na Utabiri wa hali ya hewa. Matumizi ya mfumo huo yamesaidia kupunguza gharama za uvuvi wa kubahatisha. Pia, mfumo huo umewezesha wauzaji na wanunuzi wa bidhaa za uvuvi kufanya biashara kupitia jukwaa la soko la Mnada wa Mtandaoni (*Digital Auction*). Vilevile, Wizara inaendelea na zoezi la kukamilisha usanifu na kutengeneza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mifugo na Uvuvi (*Livestock and Fisheries Monitoring and Evaluation System - LFMES*).

## G. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2026/2027

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti wa (Fungu 99) - Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2026/2027 umeandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/2027; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Nne (FYDP IV) kwa kipindi cha 2026/2027 – 2030/2031; Mpango Kabambe wa Kilimo (2050), Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030 (*Sustainable Development Goals – SDGs, 2030*).

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti wa Wizara umezingatia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) na Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo (*Livestock Sector Transformation Plan – LSTP*) kwa Kipindi cha Mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027; Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2022/2023-2036/2037; na Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi ya Mwaka 2021/2022 – 2026/2027. Masuala mengine yaliyozingatiwa wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti hiyo ni pamoja na; Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024 na masuala mtambuka (ikiwemo jinsia, mazingira, usalama wa chakula na lishe, mabadiliko ya Tabianchi, UKIMWI na ajira kwa watoto).

**Vipaumbele vya Mpango**

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Mpango na Bajeti wa Wizara Mifugo na Uvuvi utatekelezwa kupitia vipaumbele vifuatavyo:

1. Kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi

   **Mikakati ya utekelezaji;**

   i) Kuboresha mbari za mifugo na viumbemaji ikiwemo madume, mitamba na vifaranga vya samaki;

   ii) Kuimarisha upatikanaji wa malisho, mbegu za malisho, vyakula vya mifugo na samaki, na upatikanaji wa maji kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi;

   iii) Kuimarisha afya ya mifugo na viumbemaji na huduma bora za maabara na mifumo ya utambuzi wa mifugo;

   iv) Kuimarisha mifumo ya kidigitali katika uzalishaji, masoko na biashara ya mazao ya mifugo na uvuvi;

v) Kuimarisha matumizi ya zana, mitambo na teknolojia za kidigiti katika uzalishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi, ufuatiliaji wa bidhaa na huduma za ugani; na

vi) Kuimarisha ubia na sekta binafsi katika kukuza chapa (*brand*) na uthibitishaji wa bidhaa za mifugo na uvuvi za Tanzania katika masoko ya kimataifa.

2. Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi

**Mikakati ya utekelezaji;**

i) Kufanya mapitio ya sheria, miongozo na kanuni zinazosimamia rasilimali za mifugo na uvuvi;

ii) Kuanzisha vyombo maalum vya utendaji kwa ajili ya kusimamia na kulinda rasilimali za mifugo na uvuvi;

iii) Kuboresha vituo vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi;

iv) Kurasimisha biashara za mazao ya mifugo na uvuvi ili kudhibiti uuzaji holela; na

v) Kutenga maeneo muhimu (*critical habitats*) ya hifadhi na mazingira ya bahari na maji mengine.

3. Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi

**Mikakati ya utekelezaji;**

i) Kuimarisha Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ili kuchagiza na kujenga uwezo wa vijana na wanawake kujiajiri katika shughuli za mifugo, uvuvi na ukuzaji viumbemaji;

ii) Kuimarisha uwezo wa kuvua samaki katika bahari kuu na maji mengine kwa kuwawezesha wavuvi kupata vifaa vya kisasa vya uvuvi na ukuzaji viumbemaji;

iii) Kuimarisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi ili kuboresha utendaji wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO); na kuboresha miundombinu ya mifugo na uvuvi;

iv) Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa mitaji na dhamana kwa ajili ya kuongeza mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika jitihada za kukuza uchumi na kuongeza ajira;

v) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kuongeza uwekezaji na biashara kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi; na

vi) Kutambua na kuhamasisha uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

4. Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani kwenye Sekta za Mifugo na Uvuvi

**Mikakati ya utekelezaji;**

i) Kuboresha huduma za utafiti, mafunzo na ugani kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbemaji;

ii) Kuimarisha uwezo wa miundombinu na rasilimaliwatu katika taasisi za utafiti na mafunzo ya Mifugo na Uvuvi;

iii) Kutoa mafunzo yenye ithibati kwa mabaharia wa meli za uvuvi wa bahari kuu, waendeshaji wa vyombo vya uvuvi, waangalizi na wakaguzi wa uvuvi;

iv) Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi;

v) Kuimarisha uwezo wa taasisi katika kuhaulisha teknolojia za kuongeza uzalishaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na vi) Kuwekeza katika utafiti wa ufanisi wa matumizi ya chakula

cha wanyama, udhibiti wa magonjwa na mifumo ya ufugaji inayostahimili mabadiliko ya Tabianchi.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, **Fungu 99,** limepangiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **166,000,000,000** kati ya kiasi hicho, Shilingi **94,496,998,000** zinatarajiwa kukusanywa kupitia Sekta ya Mifugo na Shilingi **71,503,002,000** kupitia Sekta ya Uvuvi. Aidha, mchanganuo wa makisio ya makusanyo hayo kwa kila kifungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2:**

Jedwali Na.2: Mchanganuo wa Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

| GFS Code | Chanzo | Bajeti Iliyoidhinishwa 2026/2027 |
|---|---|---|
| **Mifugo** | | |
| 14220379 | Export fee | 440,000,000 |
| 14230183 | Receipts from veterinary charges | 46,497,998,000 |
| 14220218 | Compounds fee | 1,300,000,000 |
| 14220217 | Movement Permit Fee other than Livestock Market | 969,000,000 |
| 14220174 | Livestock Movement Permit | 28,210,000,000 |
| 14220175 | Livestock market fee | 7,490,000,000 |
| **GFS Code** | **Chanzo** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2026/2027** |
| 14230194 | Sales of Semens and liquid nitrogen | 430,000,000 |
| 14230206 | Receipts from sales of heifer | 1,760,000,000 |
| 14230207 | Receipts from sales of seeds and hay | 400,000,000 |
| 14220189 | Vaccination fees | 7,000,000,000 |
| **Jumla Mifugo** | | **94,496,998,000** |
| | | |
| **Uvuvi** | | |
| 14230171 | Fishing & Export License | 3,045,000,000 |
| 14230170 | Export Royalty | 30,192,000,000 |
| 14220222 | Import Royalty | 12,050,002,000 |
| 14220217 | Movement Permit | 13,358,000,000 |
| 14230168 | Exclusive Economic Zone Fishing License | 7,400,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 14220216 | Receipt from Sale of Laboratory Services | 3,800,000,000 |
| 14220213 | Prawn Fishing License | 124,000,000 |
| 14230241 | Receipts from Sale of Fingerlings | 660,000,000 |
| 14220161 | Other Administrative Fee | 874,000,000 |
| **Jumla Uvuvi** | | **71,503,002,000** |
| **Jumla Kuu** | | **166,000,000,000** |

## H. MIRADI NA SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA MWAKA 2026/2027 Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo na Uvuvi

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo: Kukamilisha usanifu wa kina na kuanza Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Bagamoyo, kukamilisha ujenzi wa masoko matatu (3) ya uvuvi ya Manda (Ludewa), Zingibari (Mkinga) na Kasanga (Kalambo), kukamilisha ujenzi wa mialo mitatu (3) ya Ng'ombo (Nyasa), Chifunfu (Sengerema), na Igabiro (Bukoba) na kujenga kituo cha kuendeleza ukuzaji viumbemaji cha Mwamapuli na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Ruhila, Kunduchi na Rubambagwe. Aidha, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa kituo kimoja (1) cha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi cha Sota (Rorya).

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa mbegu za malisho kufikia tani **150** kwa kuendelea kuimarisha miundombinu katika mashamba ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya) kwa kujenga mifumo ya umwagiliaji, maghala manne (**4**) ya kuhifadhia mbegu na malisho, ukarabati wa nyumba **10** za watumishi, ofisi tatu (**3**), na ununuzi wa trekta mbili (**2**) zenye vifaa vyake vya kisasa.

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, katika mikakati ya kuongeza mauzo ya nyama nje ya nchi Wizara kupitia NARCO imepanga kuendelea na ukarabati wa machinjio ya Dodoma kwa awamu ya pili. Aidha, Wizara itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vitatu (**3)** vya kukusanyia maziwa katika maeneo ya Msomera, Lushoto na Makambako na ujenzi wa vibanda **10** vya kusanikisha jenereta. Wizara itaendelea kuboresha mbari za mifugo nchini kwa kukiwezesha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kununua vifaa vya kisasa vya maabara pamoja na

madume sita (**6**) ya uzalishaji wa mbegu bora. Sambamba na hilo, Wizara imepanga kuendeleza mashamba ya kuzalisha mitamba ya Ngerengere na Mabuki kwa kuchimba visima viwili (**2**) virefu na kukarabati mabwawa mawili mtawalia. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba (LMUs) kwa lengo la kusambaza mitamba bora kwa wananchi. Katika utekelezaji huo, jumla ya mifugo ya mbegu **120** itanunuliwa pamoja na vitendea kazi stahiki, huku shughuli za uchimbaji wa visima na ukarabati wa mabwawa zikitekelezwa ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji na malisho bora kwa mifugo.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa kwa Kuzingatia Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Dairy Transformation Project - C-SDTP*) kwa kuimarisha uzalishaji, tija na ushindani. Aidha, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:- Kutoa mitamba bora ya ng'ombe wa maziwa yenye mimba kwa kaya **1,600**, zikiwemo zinazomilikiwa na wanawake asilimia **40** na vijana asilimia **30**; Kuweka teknolojia ya uzalishaji wa nishati kwa njia ya biogas katika kaya **4,300**;  na kuwapatia mafunzo wafugaji wa ng'ombe wa maziwa **7,800** kupitia vikundi vya Mashamba Darasa **288** ya Mifugo.

**Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa**

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa Mwaka 2026/2027 imepanga kuendelea na Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Awamu ya Pili nchi nzima kwa kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) dozi **11,000,000** Sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR) dozi **13,000,000,** Kideri, Ndui na Mafua ya kuku dozi **2,000,000,** kuongeza chanjo mpya ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi dozi **3,000,000** na vifaa vitakavyotumika kuvalisha hereni (*ear tag applicators)* **1,840.** Aidha, Wizara itaendelea kuratibu uchanjaji wa magonjwa mengine ya kipaumbele ikiwemo Kichaa cha Mbwa, Kutupa Mimba, Mapele Ngozi, Ndigana Kali, Kimeta na Ugonjwa wa Miguu na Midomo katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani ya Mifugo na Uvuvi**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi tisa (**9)** za LITA na tano (**5)** za FETA. Aidha, Wizara itaratibu na kuwezesha mafunzo kwa Wakufunzi (*Teaching Methodology*) kutoka Kampasi za FETA na LITA na vyuo binafsi vinavyotumia Mitaala ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Pia, Wizara itaendelea kuratibu Vituo nane (**8)** vya TALIRI, vitano (**5)** vya TAFIRI na Taasisi mbalimbali zinazofanya utafiti ili kuhakikisha zinakidhi vigezo na kuzingatia Agenda za Utafiti wa Mifugo na Uvuvi na mahitaji ya kisera.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kuhaulisha maarifa na teknolojia mpya kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbemaji. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kupitia Maonesho ya Sabasaba; Nanenane; Siku ya Ushirika Duniani; Siku ya Chakula Duniani; na Siku ya Mvuvi Duniani. Pia, kuendelea kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa vikundi na vyama vya ushirika vya wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbemaji katika Halmashauri **184** pamoja na kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa ugani **1,000** wa mifugo na uvuvi.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) kwa vijana na wanawake **700** wanaohitaji kujiajiri katika Sekta za mifugo na uvuvi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu. Lengo la programu hii ni kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira na mazao ya mifugo na uvuvi kwa ajili ya lishe na malighafi za viwanda nchini.

**Mradi wa BBT Kongwa– Project I**

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Mradi wa *BBT Kongwa Project I* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) itaongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika mnyororo wa thamani wa mbuzi, kondoo na malisho. Mradi huu utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (**5**) kwa gharama ya Dola za Marekani **32,300,000** sawa na takribani

Shilingi **82,000,000,000** za kitanzania. Aidha, Mradi utawezesha vijana **2,175** kujiajiri katika unenepeshaji wa mbuzi kibiashara, kilimo cha malisho kwa umwagiliaji, na kuchakata vyakula vya mifugo katika Kituo cha TALIRI Kongwa. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Mradi utajenga miundombinu mbalimbali ikiwemo mabanda **23** yenye uwezo wa kufuga mbuzi na kondoo **23**,**000** kwa wakati mmoja, kuchimba visima **12** virefu vya maji, majosho **15**, mabirika **69**, maghala matatu (**3)** ya kuhifadhia malisho, ghala moja **(1)** la vyakula vya mifugo, hostel mbili (**2**) kwa ajili ya vijana wa kike **100** na wakiume **118** kwa wakati mmoja, pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Kituo cha TALIRI Kongwa. Aidha, Wizara itazalisha malisho kibiashara, mradi utahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia teknolojia ya *Centre Pivot*, itakayowezesha kuongeza tija katika uzalishaji wa malisho kutoka marobota **150** hadi **450** ya hei kwa ekari kwa mwaka.

**Sekta ya Uvuvi**

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi itaendelea kutoa huduma ya uchunguzi wa samaki na mazao mengine ya uvuvi, ubora wa maji na udongo katika maeneo ya uzalishaji wa samaki ili kufuatilia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Maabara imepanga kufanya uchunguzi wa sampuli **3,500** za samaki, mazao mengine ya uvuvi, ubora wa maji na udongo na ukuzaji viumbemaji. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha Maabara kwa kununua vifaa vya kisasa vya upimaji wa sampuli; Kukarabati jengo la Maabara ya Dar es Salaam; na Kutoa elimu kwa umma kuhusu ubora na usalama wa samaki na mazao mengine ya uvuvi ili kulinda afya ya jamii.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kusimamia upatikanaji na matumizi sahihi ya takwimu za uvuvi kwa kuwajengea uwezo wakusanyaji takwimu za uvuvi, kuwatambua wavuvi na shughuli zao nchini, kufanya sensa za uvuvi katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa; na maji madogo ili kuandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ya kuleta ufanisi katika usimamizi na uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi, usimamizi, udhibiti na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya doria zenye siku kazi **8,400**, kuweka maboya ya kuonesha mipaka ya maeneo ya mazalia ya samaki katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi shirikishi kwa kufanya tathmini na kujenga uwezo wa vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi (BMUs na CFMAs)**.**

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kusimamia uthibiti wa ubora, viwango na masoko ya mazao ya uvuvi kwa kufanya kaguzi za kawaida **9,200**; Kaguzi za robo mwaka **800**; Kuwajengea uwezo wakaguzi **80** na wadau **1,500**; Kuimarisha Vituo **20** vya Uthibiti wa Ubora na Masoko ya Mazao ya Uvuvi kwa kuvipatia vitendea kazi; na Kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa kwa kuwapatia mafunzo wachakataji **200** wa mazao ya uvuvi na kuhamasisha matumizi ya teknolojia rafiki na kusanikisha mitambo ya kuzalisha barafu na vichanja vya kukaushia Dagaa.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji wa vifaranga na utoaji wa huduma bora za ugani kwa kusimamia na kuendesha vituo nane (**8**) vya Kuendeleza Ukuzaji Viumbemaji (Ruhila – Ruvuma, Kingolwira – Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Machui – Tanga, Nyengedi – Lindi, Ruvula – Mtwara, Dar es Salaam na Rubambagwe - Geita). Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji na usimamizi wa uzalishaji wa pembejeo muhimu za ufugaji samaki ili kuzalisha vifaranga **317,642,400** na tani **53,813.11** za chakula cha samaki. Vilevile, Wizara itapandikiza vifaranga vya samaki **15,000,000** katika maji ya asili ili kuongeza upatikanaji wa samaki. Pia, Wizara inatarajia kutoa huduma za ugani kwa wakuzaji viumbemaji **20,000** ili waweze kuzalisha kwa tija na kufuata sheria, kanuni na mbinu bora. Pia, wakulima **2,500** wa mwani watapatiwa elimu kuhusu uongezaji thamani na matumizi ya bidhaa za mwani na kusanikisha vizimba kumi (**10**) baharini kwa ajili ya majaribio. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa miongozo mbalimbali ya elimu kuhusu mbinu bora za ukuzaji viumbemaji ili kuendana na mahitaji ya sasa.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa shughuli za ukuzaji viumbemaji zinatekelezwa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni, katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi katika mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbemaji na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora katika mikoa sita (6) ya Mwanza, Pwani, Ruvuma, Kigoma, Mara na Tanga. Pia, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uzalishaji na udhibiti wa magonjwa katika maeneo ya ufugaji wa samaki, vitotoleshi na viwanda vya kuchakata chakula cha samaki nchini.

**Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya ASDP II**

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha uendeshaji wa vituo nane **(8)** vya kuendeleza ukuzaji viumbemaji (Ruvula, Machui, Rubambagwe, Ruhila, Nyengedi, Mwamapuli, Kingolwira na Dar es Salaam) kwa kuvipatia vitendea kazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Aidha, Wizara itaandaa mpango na mwongozo wa kusimamia na kuendeleza ufugaji wa samaki kwa vizimba.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Bahari ya Hindi na Maji madogo kwa kununua Ndege Nyuki moja (**1)**, maboya **79**, mizani moja (**1)** inayohamishika. Aidha, Wizara itaboresha mfumo wa usajili na ukusanyaji wa taarifa za wadau wa uvuvi kwa njia ya kielektroniki ili kuwezesha urasimishaji wa Sekta ya Uvuvi.

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)**

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Soko la Samaki Kipumbwi – Pangani; ujenzi wa vyumba viwili vya ubaridi vyenye uwezo wa kuhifadhi tani **40** za samaki (Pangani na Bagamoyo); ujenzi wa vichanja **40** vya kukaushia Dagaa (Mafia na Pangani); na ujenzi wa mahema **11** ya kukaushia mazao ya uvuvi kwa kutumia nishati ya jua *(solar tents)* (Kilwa, Pangani na Mafia).

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na ukarabati na upanuzi wa miundombinu katika vituo

vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mwamapuli (Tabora) na kukamilisha ujenzi wa kituo kipya cha Rubambagwe (Geita). Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa mabwawa, vitotoleshi, majengo, mifumo ya usambazaji maji na ununuzi wa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa vituo.

**Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (*Extended Credit* Facility–ECF)**

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Mikopo ya Masharti Nafuu ya boti za uvuvi, vizimba na unenepeshaji wa mifugo kwa ajili ya vijana na wanawake kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana (OR – MV), Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI), na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

**Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji wa Bahari Tanzania - TASFAM**

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kuanza ujenzi wa mialo mitano (**5**) ya Miseti – Mikindani (Mtwara), Kisiju – Pwani, Shuka, Mtama, Mchinga na Kilwa Masoko – (Lindi); Kujenga kiwanda cha kuchakata dagaa Mkoani Tanga katika mwalo wa Kipumbwi kitakachomilikiwa na TAFICO; Upanuzi wa soko la samaki Bagamoyo – Pwani; Kutoa mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana kwa ajili ya zana za uvuvi na ukuzaji viumbemaji katika Ukanda wa Pwani; Kujenga vituo vya Uvuvi na Ukuzaji Viumbemaji cha Tawalani (Tanga) na Kilwa masoko (Lindi). Aidha, kazi nyingine ni pamoja na kununua Meli ya Mafunzo na Utafiti ya Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) yenye urefu wa mita 30; kujenga Jengo la Mihadhara na kununua vifaa vya maabara katika Kampasi ya FETA Mikindani Mtwara; kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Ukuzaji Viumbemaji (*National Mariculture Resource Centre*) – Kunduchi; Ujenzi wa maghala manne (4) ya kuhifadhia zao la Mwani katika mikoa ya Pwani, Mtwara, Tanga na Lindi; Kukamilisha Jengo la Utawala la Hifadhi ya Bahari Mafia; Ujenzi wa Jengo la Utawala na Makumbusho ya Uvuvi na kununua vifaa vya utafiti kwa ajili ya Maabara katika Kituo cha TAFIRI, Kunduchi Dar es Salaam; Kukarabati na kuweka

vifaa vya Maabara ya Uvuvi (Mvuvi House) Dar es Salaam; Kufanya utafiti wa uwingi na mtawanyiko wa samaki wa baharini; na Kuandaa Mpango wa Upangaji wa Maeneo ya Mavuvi (*marine spatial planning*).

## TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

### Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)

**174.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) itaendelea kufanya utafiti wa mifugo na malisho katika maeneo mbalimbali ya kiupaumbele ambayo ni; uboreshaji na uendelezaji wa mbari za mifugo, uchambuzi na uhifadhi wa kosaafu za mifugo mbalimbali ya asili yenye sifa maalum, uendelezaji wa nyanda za malisho, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho, lishe na ubora wa vyakula vya mifugo. Vilevile, taasisi itaendelea kutekeleza miradi ya utafiti inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza kasi ya usambazaji wa teknolojia bora za mifugo, Aidha, TALIRI itaendelea kuwashirikisha wadau wa Sekta Binafsi kwa kuwapa mafunzo juu ya uzalishaji wa teknolojia hizo kwa viwango sahihi ili kusambaza kwa wahitaji. Pia, taasisi itaendelea kusimamia ujenzi wa jengo la ghorofa tano (5) jijini Dodoma litakalokuwa ofisi za makao makuu ya taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo).

### Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia TAFIRI itaendelea kufanya utafiti katika maeneo ya kipaumbele nane (**8**) kama ifuatavyo; tathmini ya wingi na mtawanyiko wa rasilimali za uvuvi za kipaumbele katika maji ya Kitaifa na Ukanda wa Uchumi wa Bahari; Kuzalisha vyakula bora vya samaki; Kubaini maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwa vizimba katika maziwa na bahari; Ufugaji wa samaki aina ya Kuhe (*Boulengerochromis microlepis*) katika Ziwa Tanganyika; Kilimo cha tija cha Mwani; Mbinu bora za uvuvi wa kambamiti kwa wavuvi wadogo; na Uzalishaji wa vifaranga vya samaki wa baharini; ufuatiliaji wa ongezeko la asidi baharini na athari zake kwa viumbemaji; na Tathmini ya kiasi cha hewa ya ukaa katika

mikoko na nyasi bahari ili Taifa liweze kunufaika. Aidha, TAFIRI inatarajia kuzalisha jumla ya vifaranga vya samaki **1,000,000** vya maji chumvi na baridi.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

**176. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027 LITA itaendelea na ukamilishaji wa miradi ya miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ambayo ni hosteli sita (**6**), kumbi sita (**6**) na jengo la utawala moja katika kampasi za Songwe, Madaba, Tengeru, Kikulula, Mabuki na Buhuri**.** Aidha, LITA itadahili wanafunzi **5,938** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Pia, LITA itaendelea kuwaongezea ujuzi wa kitaalam Wakufunzi ili kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia pamoja na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi ili kubadilishana teknolojia na uzoefu, kuboresha mbinu za utoaji mafunzo na kuanzisha miradi ya pamoja ya mafunzo, utafiti na maendeleo.

**Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

**177. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, FETA itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuendelea kupata wataalam mahiri katika Sekta ya Uvuvi. Wakala itaendelea kuboresha miundombinu ya mafunzo kwa Kampasi zake tano (**5**) ikiwepo ununuzi wa meli ya kisasa ya mafunzo na utafiti. Aidha, itaendelea kudahili na kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi **1,200** na mafunzo ya muda mfupi kwa wadau **8,500**. Vilevile, kuwaongezea ujuzi wa kitaaluma wakufunzi **85** ili kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Pia, Wakala itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu ndani na nje ya nchi ili kubadilishana teknolojia na uzoefu kwa ajili ya kuboresha mbinu za utoaji mafunzo.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

**178. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) itaendelea kusimamia hifadhi za bahari tatu (3) na maeneo tengefu (15), kutekeleza mradi wa uhifadhi na usimamizi wa pamoja maeneo

ya hifadhi yaliyopo katika mpaka wa Tanzania na Kenya katika Wilaya ya Mkinga na Diani-Chale (Kenya) ili kuweza kusimamia kwa pamoja rasilimali zinazopatikana katika eneo hilo. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha miundombinu ya utalii wa kiikolojia (*Ecotourism)* na kutangaza fursa za uwekezaji ikiwemo biashara ya Kaboni ya Buluu na ujenzi wa vivutio vya utalii wa bahari na fukwe.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia MPRU itaendelea kuimarisha usimamizi wa hifadhi za bahari na maeneo tengefu kwa kuendesha doria na kudhibiti uvuvi usiozingatia sheria; kuwekeza katika tafiti na ufuatiliaji wa mifumo ikolojia ya bahari; kuhamasisha na kuwezesha shughuli mbadala za kiuchumi; kuimarisha miundombinu na vitendea kazi, ikiwemo vifaa vya doria na matumizi ya teknolojia za kisasa katika kudhibiti uharibifu wa mifumo ikolojia; kutoa elimu na uhamasishaji kwa umma; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali, wakiwemo taasisi za Umma, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kuliimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania ili liweze kushiriki kikamilifu katika uvunaji wa rasilimali za Bahari Kuu, ikiwa ni sambamba na malengo ya kuimarisha Sera ya Uchumi wa Buluu na kuhakikisha rasilimali hizi zinawanufaisha Watanzania. Hivyo, Wizara itaendelea kuwekeza katika Uvuvi wa Bahari Kuu ambapo uwekezaji huo unaakisi dhamira ya Serikali katika kutekeleza sera na mikakati ya kukuza uchumi wa buluu. Pia, Wizara italiwezesha shirika kununua meli mbili (2) za uvuvi wa Bahari Kuu kati ya nne (4) zilizopo kwenye mpango; ambazo zitaweza kuvua katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (EEZ) ambapo awali haukuweza kufikiwa kutokana na kukosekana kwa meli za aina hiyo. Vilevile, TAFICO itatekeleza mpango fungamanishi utakaojumuisha bandari za uvuvi, mifumo ya ubaridi, viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na masoko ili kuongeza tija katika uvunaji endelevu na matumizi ya rasilimali za uvuvi wa Bahari Kuu.

**181. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) itakamilisha ujenzi wa ghala la ubaridi lenye uwezo wa kuhifadhia samaki tani **100** kwa wakati mmoja; Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki (*Fish Feed Mill*) chenye uwezo wa kuzalisha tani **30** kwa siku; Kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi (*Fish Processing Plant*) Kilwa Masoko-Lindi, chenye uwezo wa kuchakata tani **10** kwa siku kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Program-AFDP*).

**182. *Mheshimiwa Spika,*** TAFICO kupitia Mradi wa TASFAM itajenga kiwanda cha kuchakata Dagaa na samaki katika Mwalo wa Kipumbwi, Pangani-Tanga. Hatua hii itaiwezesha TAFICO kutumia kikamilifu fursa zitokanazo na Uchumi wa Buluu na kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa. Vilevile, Shirika litaimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi katika biashara ya mazao ya uvuvi, pamoja na kukuza ubadilishanaji wa uzoefu na utaalamu katika uvuvi wa Bahari Kuu.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

**183. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Serikali kupitia DSFA inapanga kutoa leseni **81** na vibali **40**, sambamba na kufanya mapitio ya Kanuni za Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Mamlaka. Aidha, DSFA itaendelea kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya Nchi na kusimamia utekelezaji wa makubaliano kati yake na wadau wa uvuvi wa Bahari Kuu.

**184. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, DSFA itaendelea kujitangaza sambamba na kutoa elimu kwa wadau kuhusu vivutio na fursa zinazopatikana katika eneo la Bahari Kuu ikiwa ni pamoja na kuwezesha utumiaji wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko.

**185. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, DSFA itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi katika EEZ kwa kuboresha mifumo ya ufuatiliaji ya mienendo ya meli (*Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification*

*System – AIS*); Kuboresha Programu ya Waangalizi wa Uvuvi (*Fishery Observer Programe*) katika meli; Kufanya ukaguzi wa meli kabla na baada ya kuchukua leseni; na Kufanya doria za anga kwa kutumia Ndege nyuki (*Patrol Drone*) katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Bahari (EEZ) kwa kushirikiana na nchi jirani na Jumuiya za Kikanda.

**Bodi ya Nyama Tanzania (TMB)**

**186. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imepanga kufanya ukaguzi kwa wadau **17,988** wanaojishughulisha na uzalishaji na biashara kwenye mnyororo wa thamani wa nyama. Aidha, Bodi imepanga kufanya utambuzi na usajili wa wadau wa Tasnia ya Nyama **19,336** ili kuhakikisha nyama na bidhaa za nyama zinazozalishwa zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Vilevile, Bodi imepanga kutoa mafunzo ya ufugaji kibiashara kwa wafugaji wapatao **300** kupitia vikundi **10** ili kuboresha upatikanaji wa malighafi bora kwa viwanda vya nyama na kutoa elimu ya uandaaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu zilizopo kwa wahudumu **20,000** wa maduka ya nyama.

**Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB)**

**187. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2026/2027, Bodi ya Maziwa Tanzania **(**TDB) imepanga kutoa mafunzo ya ufugaji bora na matumizi ya teknolojia za kisasa za uzalishaji wa maziwa kwa wadau **1,200** wa Tasnia ya Maziwa; kusajili na kurasimisha biashara kwa wadau **800**; kufanya ukaguzi wa wadau **1,200** katika maeneo ya uzalishaji wa maziwa, vituo vya kukusanyia maziwa, viwanda vya kusindika maziwa, vituo vya biashara ya maziwa, bandari na vituo vya mipakani. Aidha, Bodi imepanga kusajili wadau **800** na kuwawezesha kurasimisha biashara zao. Vilevile, Bodi imepanga kutoa mafunzo kwa wakaguzi **155** wa maziwa kuhusu sheria na utaalam wa kuzingatia katika ukaguzi wa maziwa; kuwezesha uanzishwaji wa vyama vitano (**5**) vya ushirika wa wadau wa Tasnia ya Maziwa; kuimarisha mifumo ya takwimu kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kukuza mawasiliano miongoni mwa wadau wa Tasnia ya Maziwa

na kujenga uwezo wa watumishi wa Bodi kupitia Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko Tabianchi (C-SDTP).

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia NARCO imepanga kuzalisha ndama **4,652**; Kuuza mitamba **657** kwa wafugaji ili kuboresha kosaafu za Mifugo; Kunenepesha na kuchinja ng'ombe **6,012** na kuuza tani **784** za nyama; Aidha, NARCO itaendeleza maeneo ya malisho ya ukubwa wa ekari **1,400** katika Ranchi za Kongwa, Ruvu, Kalambo, Mkata, Mzeri na West Kilimanjaro; Kuzalisha marobota **60,000** ya malisho. Vilevile, Kampuni imepanga kutoa ushauri wa kitaalam kwa wafugaji **450** katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **500** kutoka katika vyuo vya mafunzo ya mifugo nchini.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA)**

**189.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia TVLA itaendelea kutoa huduma za uchunguzi, utambuzi wa magonjwa na uzalishaji wa chanjo kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo nchini. TVLA itazalisha jumla ya dozi **129,130,000** za chanjo zikijumuisha Mdondo (TEMEVAC) dozi **120,000,000**; Homa ya Mapafu ya Ng'ombe dozi **5,500,000**; Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) dozi **1,000,000**; Kimeta dozi **800,000**; Chambavu dozi **600,000**; Kutupa Mimba kwa Ng'ombe dozi **30,000**; Homa ya Mapafu ya Mbuzi dozi **1,200,000**. Aidha, TVLA itafanya uchunguzi wa sampuli **65,000** dhidi ya magonjwa ya mifugo na kushauri namna ya kudhibiti magonjwa hayo. Vilevile, Wakala itafanya uchambuzi na uhakiki wa ubora wa sampuli **6,000** za vyakula vya mifugo kutoka kwa wazalishaji. Pia, Wakala inatarajia kusomesomesha watumishi **28** kwa ngazi ya elimu ya juu, kufadhili miradi mitatu **(3)** ya utafiti na kuwajengea uwezo watumishi **50** katika utafiti wa chanjo na magonjwa ya mifugo.

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha miundombinu ya maabara, Wakala itaendelea na ujenzi wa jengo la maabara Kanda ya Kati Dodoma na maabara ya uzalishaji wa chanjo za virusi TVI – Kibaha; Kununua mashine na vifaa vya uzalishaji wa

chanjo; Kukarabati majengo ya maabara katika Maabara Kuu ya Veterinari iliyopo Temeke; Kuimarisha mbari za mifugo na uzalishaji malisho katika shamba la Mivumoni – Tanga; Kuanza ujenzi wwa maabara Kanda ya Magharibi – Kigoma; Kuboresha vitendea kazi vikiwemo magari na samani za ofisi katika vituo 13; na Kununua vitendanishi vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo katika maabara.

**MASUALA MTAMBUKA**
**Dawati la Mitaji na Uwezeshaji**

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Dawati la Mitaji na Uwekezaji itaendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kuibua maeneo mapya ya uwekezaji, kufanya utafiti wa mnyororo wa thamani na masoko, kuwaunganisha wawekezaji na taasisi za fedha, na kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa uwekezaji nchini. Aidha, Dawati litaendelea kuzihamasisha kampuni za Bima ili ziendelee kuingia katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia, katika kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi litaandaa Mkakati wa ushiriki wa Sekta Binafsi (*Private Sector Engagement Strategy*).

**Utawala Bora, Jinsia na VVU/UKIMWI**

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa na kuelimisha watumishi kuhusu Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya itaendelea kutoa elimu kwa watumishi **1,041** kuhusu udhibiti wa VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi, uzingatiaji wa lishe bora, uzingatiaji wa mazoezi na kuwezesha watumishi **150** kushiriki katika bonanza pamoja na SHIMIWI.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira katika miradi

ya ujenzi wa minada ya mifugo, mialo na masoko ya samaki. Aidha, Wizara imepanga kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi **1,000** katika ukanda wa pwani, kaskazini na nyanda za juu kusini kuhusu utunzaji wa mazingira kwa uvuvi na ufugaji unaostahimili mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, Wizara itaendelea kuandaa Mpango kazi wa Mazingira kwa Sekta ya Uvuvi pamoja na kufanya Tathmini ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Change Vulnerability Assessment*) na kuandaa Mpango wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa ukanda wa Pwani.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027 Wizara itafanya ukaguzi wa mazingira kwa miradi kumi (**10**) ya uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya usimamizi wa mazingira. Pia, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, pamoja na kuanzisha Mtandao wa *Blue Carbon Tanzania* kwa jamii katika ukanda wa Pwani.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, katika kuimarisha uratibu wa masuala ya mazingira katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, Wizara imepanga kuandaa Mpango wa Kwanza wa Mazingira utakaotekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2027/2028 hadi 2032/2033. Mpango huo, utaweka miongozo na mikakati ya kuhakikisha shughuli zote za Sekta hizo zinafanyika kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira, matumizi endelevu ya rasilimali na kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi.

**196.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itafanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii katika miradi ya ujenzi wa masoko mawili (2) ya samaki ya Kalumbu na Kasanga (Rukwa) na mialo miwili (2) ya Ng'ombo (Ruvuma) na Masuche (Songwe) ili kuhakikisha miradi hiyo inazingatia viwango vya Kitaifa vya usimamizi wa mazingira na kulinda ustawi wa jamii zinazozunguka maeneo ya miradi. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya viashiria vya hatari za Mabadiliko ya Tabianchi katika shughuli za uvuvi katika Ukanda wa Pwani kwa lengo la kuandaa mpango wa kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi utakaoimarisha ustahimilivu wa Sekta ya Uvuvi na jamii zinazotegemea rasilimali za bahari.

## Ufuatiliaji na Tathmini

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi na programu mbalimbali zinazotekelezwa kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji. Kazi hii itafanyika kupitia uanzishaji wa mfumo wa kidijiti wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuimarisha ukusanyaji na matumizi sahihi ya takwimu katika uandaaji, utekelezaji wa mipango ya maendeleo na utoaji wa maamuzi.

## Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kukamilisha usanifu na kutengeneza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mifugo na Uvuvi (*Livestock and Fisheries Monitoring and Evaluation System* - LFMES). Aidha, Wizara imepanga kusanifu na kutengeneza mfumo wa dashbodi ya Kisekta ili kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango, ahadi na maagizo ya viongozi na kusaidia kufanya maamuzi yaliyotokana na taarifa na takwimu (*Informed Decision*). Pia, Wizara itaendelea kufanya maboresho kwenye mifumo yake ya TEHAMA na kuifungamanisha na mifumo mingine ndani ya Serikali. Vilevile, Wizara imepanga kuboresha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ili kuongeza ufanisi na kasi ya usimamizi wa rasilimali za Mifugo na Uvuvi.

## Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi za kikanda na kimataifa ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji, masoko na utafiti zinazohusu Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la Dunia la Ukuzaji Viumbemaji kwa mwaka 2026 (*World Aquaculture Conference – WA26T*) litakalofanyika sambamba na Kongamano la Ukuzaji Viumbemaji Afrika (*Aquaculture Africa - AFRAQ26*) kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika tasnia ya ukuzaji viumbemaji. Kauli mbiu ya kongamano ni *"Aquaculture Driving Blue Transformation"* inayoakisi umuhimu wa tasnia ya ukuzaji viumbemaji katika

kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Buluu. Kongamano litasaidia kutangaza fursa za uwekezaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbemaji sanjari na Dira 2050.

## I. HITIMISHO

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapo hitimisha Hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na kwa mafanikio katika Mwaka 2025/2026, ambayo yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikiwemo mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, Asasi Zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Japan, Korea Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ireland, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Oman, Ivory coast, Canada, Ushelisheli, Norway, Marekani, Jumuiya ya Ulaya, Jamhuri ya Watu wa China, Ethiopia, Jordan, Bahrain, Kuwait, Vietnam, Qatar, Comoro na Misri; kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kuzishukuru Taasisi zinazoendelea kushirikiana nasi zikiwemo:- Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority - LTA*), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Commision - SWIOFC), Shirika la Maendeleo la Kiserikali la Nchi za Afrika Mashariki (IGAD), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission - IOTC*), Kamisheni ya Kimataifa ya Usimamizi wa Nyangumi (*International Whaling Commission - IWC*), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission - IOC*), Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria*

*Fisheries Organization - LVFO*), Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association - IORA*), *Western Indian Ocean Marine Science Association* (WIOMSA), na Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness AWARFA*).

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii, kutambua pia mchango wa mashirika mengine tunayoshirikiana nayo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambayo ni: *Heifer International*, *Green Climate Fund, French Development Agency*, Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Kiatomiki (*International Atomic Energy*), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Poland (Polish Aid), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD),Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), OPEC *Fund for International Development*, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya Uholanzi, na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme – ESDP*), na *Overseas Fishery Cooperation Foundation* (OFCF) ya Japan.

**204.** ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru pia taasisi za kifedha na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao hasa, Benki ya Dunia (WB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), *United Nations University* (UNU), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA), Shirika la Misaada la Ireland (*Irish Aid*), na mashirika ya IAEA, UNIDO, CIAT, ASARECA, CCARDESA na GEF kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Gates Foundation, World Wide Fund for Nature* (WWF), *The Nature Conservancy* (TNC), *Wildlife Conservation*

*Society* (WCS), *International Union for Conservation of Nature* (IUCN), *Overseas Fisheries Cooperation Foundation* (OFCF) ya Japan, Vetaid, Care International, OXFARM, *Welcome Trust*, *World Vision*, FARM Africa, *Land O' Lakes, Building Resources Across Communities* (BRAC), *World Society for Protection 143 of Animals* (WSPA), *Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine* (GALVmed), *Institute of Social Studies* (ISS), *International Land Coalition* (ILC), *British Gas International, Sea Sense, SmartFish, Marine Stewardship Council* (MSC), *Gatsby Africa* pamoja na Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**206.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na maarifa pamoja na maelekezo anayotupatia kama Wizara kuhakikisha rasilimali za Mifugo na Uvuvi zinachangia katika Uchumi wa Buluu ili kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu.

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo; Kamati ya Uongozi; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri unaolenga kuboresha na kuimarisha Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, niwashukuru wadau mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wavuvi. Ninapenda kuwaahidi kwamba Wizara itaendelea kusimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi.

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani (Mb), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ushirikiano wake katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, natoa pia shukrani zangu kwa Bi. Agnes Kisaka Meena, Katibu Mkuu, Dkt. Fabian Magawa Madele, Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) na Prof.

Mohammed Ali Sheikh, Naibu Katibu Mkuu (Uvuvi), Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazozifanya.

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027**

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/2027, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaomba kutumia jumla ya Shilingi **433,379,125,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **98,279,420,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **335,099,705,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida: Shilingi **98,279,420,000**
- Matumizi ya Mishahara: (PE) Shilingi **49,452,723,000**
- Matumizi Mengineyo: (OC) Shilingi **48,826,697,000**

(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo: Shilingi 335,099,705,000
- Fedha za Ndani Shilingi **193,795,218,000**
- Fedha za Nje Shilingi 141,304,487,000

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wako na hoja imeungwa mkono. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ninaomba kuwasilisha

Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 Kifungu cha 9 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba taarifa yote iliowekwa Mezani iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *(Hansard)*. Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inahusu muundo wa taarifa yoyote na Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni Utangulizi, Maelezo kamili kuhusu uchambuzi na sehemu ya mwisho inayohusu Maoni, Ushauri na Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni masharti ya Kanuni za Bunge. Kwa masharti hayo, Kamati ilichambua hoja inayojadiliwa na kuandaa taarifa inayowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii ni matokeo ya kuzingatia masharti ya kanuni ya 120 Kifungu cha pili ya Kanuni za Bunge na kuchambua mambo yafuatayo: Moja, hali ya ujumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; pili, uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati; tatu, tathmini ya ukusanyaji maduhuli; na nne, upatikanaji wa fedha kutoka hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya uchambuzi wa Kamati hii ni kujenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 na 28 Machi, 2026 Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika maelezo hayo, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiaji wa ushauri wa Kamati. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia uzingatiaji wa ushauri unaotolewa Bungeni, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati. Kwa mfano, ushauri wa Kamati ulilenga ujenzi wa mabirika na majosho kwa ajili ya mifugo. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilionesha kuwa Serikali imeendelea kujenga majosho na kuhamasisha Sekta Binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye idadi kubwa ya mifugo kuwa na miundombinu ya majosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, upo ushauri ambao utekelezaji wake haujakamilika. Kwa mfano, Kamati iliishauri Serikali ifanye mapitio ya tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambazo ni nyingi kiasi cha kukwamisha ukuaji na maendeleo ya sekta hizo nchini. Kamati ilijulishwa kwamba Serikali inaendelea kufanya mapitio ya tozo mbalimbali jambo linaloonesha kuwa zoezi hilo halijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili yaani Dar es Salaam na Morogoro ili kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi. Ufafanuzi wa kina umebainishwa katika Taarifa ya Kamati Iliyowekwa Mezani mapema asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni hatua muhimu ya Kibunge katika kushughulikia bajeti. Muhtasari wa matokeo ya uchambuzi huo unaonekana katika vielelezo viwili ambavyo ni kielezo cha kwanza na kielezo cha pili. Vielelezo hivyo vinaonesha yafuatayo:-

(i) Mchango wa fedha za ndani umeongezeka kutoka 60.8% ilivyoidhinishwa hadi kufikia 81% ya fedha zilizopatikana;

(ii) Mchango wa fedha za nje umepungua kutoka 39.2% ilivyokadiriwa hadi kufika 18% ya fedha zilizopatikana. Upatikanaji wa fedha za ndani ulikuwa 39.4% dhidi ya 66.6% ya kipindi cha utekelezaji. Upatikanaji wa fedha za nje ulifikia 14.2% dhidi ya 66.6% ya kipindi cha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtiririko huu, siyo rahisi Sekta ya Mifugo na Uvuvi kukamilisha miradi kwa ratiba yake. Mkwamo mkubwa umejitokeza kwenye fedha za nje. Jambo hili kwa maoni ya Kamati, linaitaka Serikali ijipange kutekeleza miradi kwa njia ya kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea Taarifa ya Makusanyo ya Maduhuli na kufanya uchambuzi. Muhtasari wa uchambuzi unaonekana katika kielelezo namba tatu kinachohusu Sekta ya Mifugo na kielezo namba nne kuhusu Sekta ya Uvuvi. Kielezo namba tatu kuhusu Sekta ya Mifugo kinaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Vyanzo viwili vya mapato havikuwezesha ufanisi wa makusanyo. Vyanzo hivyo ni vibali vya kuhamisha mifugo yaani *Livestock Movement Permit* vilivyokuwa na ufanisi chini ya 50% yaani 49% na vibali vya ada mchanganyiko vilivyokuwa na ufanisi wa 37%. Ufanisi wa chanzo cha mapato kinachohusu uuzaji wa mitamba, yaani *Heifer Export Fee, Livestock Market Fee* na *receipts from the veterinary charges* ulizidi 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Ufanisi wa Vyanzo vya Mapato kwa Sekta ya Uvuvi unaonesha kama ifuatavyo:- Chanzo cha mapato kutokana na *Prones Fishing License* hakikufanikisha mapato yoyote. Chanzo cha ada nyinginezo za mambo ya kiutawala kilikuwa na ufanisi wa 8% tu, na chanzo cha mapato kutokana na *Export Loyalty* kilikuwa ufanisi kwa 54%. Ufanisi wa vyanzo viwili vya mapato ambavyo ni *Import Loyalty* na *Movement Permit* ulizidi 100%. Vyanzo vya mapato vya *Fishing and Export License Receipts from sales of fingerings and receipts from sales of laboratory services* vilikuwa na ufanisi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kila sekta katika ukusanyaji wa mapato ya Wizara unaonekana katika kielelezo namba tano na taswira halisi inajitokeza katika kielelezo namba sita. Vielelezo hivyo vinaonesha yafuatayo:-

(i) Mchango wa Sekta ya Uvuvi ulipungua kutoka 47% ilivyoidhinishwa hadi 44.7%. Lakini mchango wa Sekta ya Mifugo uliongezeka kutoka 53% hadi 55%. Sekta ya Mifugo imefikia 54% ya lengo dhidi ya 66.6% ya kipindi cha utekelezaji ikiwa nyuma kwa 12.7%. Sekta ya Uvuvi imefikia 59% ya lengo katika kipindi cha utekelezaji cha 66.6% ikiwa nyuma kwa asilimia saba nukta sita. Kwa wastani, sekta zote mbili ziko nyuma ya lengo la makusanyo kwa 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchanganuo huo, Wizara inaweza kushindwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni tisa nukta nne zilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia Taarifa ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Lengo ni kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti. Muhtasari wa uchambuzi umebainishwa katika kielelezo namba saba ambacho kinaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni 33.9% ya jumla ya fedha zote ikilinganishwa na 21.3% ilivyopangwa kwenye bajeti;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zimepatikana kwa 56% ndani ya kipindi cha utekelezaji ambacho ni 66.6%;

(iii) Fedha za uendeshaji zilizopokelewa zimefikia kiwango cha 50%;

(iv) Upatikanaji wa fedha za ndani na fedha za nje umekuwa pungufu kwa 50%. Fedha za ndani zimepatikana kwa 39.47% na fedha za nje zimepatikana kwa 14.3%. Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mifugo na uvuvi kwa ujumla umekuwa pungufu kwa 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, upo umuhimu kwa Serikali kuziangalia upya Sekta za Mifugo na Uvuvi ili kuendana na misingi ya Dira ya 2050. Aya ya pili kifungu cha pili ya shabaha namba mbili inahusu kutokomeza umaskini uliokithiri makundi yote. Wafugaji na wavuvi ni miongoni mwa makundi yanayoweza kuwa na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ilieleza kipaumbele kwa Sekta ya Mifugo. Ninaomba kunukuu, *"Chama kitaendelea kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Mifugo ili kuimarisha na hivyo kuleta mabadiliko makubwa kwa kuhamasisha kuwezesha uwekezaji katika ufugaji wa kisasa na wa kibiashara pamoja na kuchakata bidhaa za mifugo."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 uchambuzi wa vipaumbele vya Mpango wa Wizara umelenga kubaini iwapo vinazingatia mwelekeo wa Dira 2050 na Ilani ya Uchaguzi 2025. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;

(ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi;

(iii) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na

(iv) Kuimarisha ulinzi, usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha yafuatayo:-

(i) Kipaumbele cha kuongeza uzalishaji masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi kinalenga kuiwezesha sekta kuingia kwenye sekta za mageuzi kupitia kuongeza thamani ya bidhaa sambamba na kutekeleza Ilani ya CCM ya Mwaka 2025 kwa kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo;

(ii) Kipaumbele cha kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kinalenga kuongeza uzalishaji, ajira na mchango wa sekta nyingine za uchumi. Kwa mchanganuo huo, sekta hizo zinaweza kupata vigezo vya sekta za mageuzi vilivyobainishwa kwenye Dira ya 2050;

(iii) Kipaumbele cha kuimarisha utafiti, mafunzo, huduma za ugani kinalenga kuongeza ukuaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na kutekeleza Ilani ya CCM kuhusu kuboresha huduma za ugani, kinga na tiba ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufanisi huo, vipaumbele vya Wizara vinaendana na mwelekeo wa maendeleo uliowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Aidha, vipaumbele hivyo vinazingatia Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadiro ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Katika uchambuzi wa Kamati, ilizingatia maeneo makuu mawili ya rasilimali fedha. Maeneo hayo ni Makadiro ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadiro ya Mapato ulifanyika kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi huo unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Sekta ya Mifugo imeanzisha chanzo kipya cha ada ya chanjo chenye makadirio ya shilingi bilioni saba, huku Sekta ya Uvuvi ikiondoa chanzo cha *compounding fees* kilichokuwepo mwaka uliopita.

(ii) Chanzo kimoja cha mapato katika Sekta ya Mifugo kilichoshindwa kuchangia mapato kwa mwaka 2025/2026 kimejumuishwa katika makadirio;

(iii) Vyanzo viwili vya mapato ya Sekta ya Mifugo vilivyokuwa na ufanisi mkubwa mwaka 2025/2026 vimewekwa katika makadirio ya chini;

(iv) Baadhi ya vyanzo vya mapato kwenye ufanisi mdogo ikiwemo *Compounding Fees Livestock Movement Permit* na chanzo kimoja cha uvuvi vimeongezwa makadirio ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa Wizara ina kazi kubwa ya kufanya ili kuwezesha lengo la mapato yanayokadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa kuzingatia mambo muhimu katika sekta hii. Muhtasari wa uchambuzi huo unaonekana katika kielelezo namba tisa ambacho kinaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya Matumizi Mengineyo *(OC)* yamepungua kwa 9.99% ikilinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha uliokuwa nyuma kwa 16.6% hadi Februari, 2026; na

(ii) Makadirio ya Mishahara yameongezeka kwa 4.62% huku uzoefu wa upatikanaji wa fedha ukiwa nyuma kwa asilimia nne;

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya jumla ya fedha za matumizi ya kawaida yamepungua kwa 3.18% wakati uzoefu wa upatikanaji wa fedha ulikuwa nyuma kwa 10.6%. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 hali hiyo inaonesha uhalisia wa uwezekano wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ulizingatia methodolojia ya ulinganisho kati ya kiwango cha fedha kilichopatikana na makadirio. Muhtasari wa uchambuzi unaonekana katika namba 10 ambacho kinaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za ndani zimeshuka kwa 38.43% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaokwisha;

(ii) Fedha za nje zimepungua kwa 1.08% ikilinganishwa na mwaka 2025. Hali hii inamaanisha kushuka kwa

utegemezi wa vyanzo vya nje kwenye bajeti ya maendeleo kwa asilimia nne; na

(iii) Kwa ujumla bajeti ya miradi imepungua kwa 10.67% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati, maoni ya jumla, ninaomba kubainisha kwa muhtasari majumuisho ya maoni yafuatayo: -

(i) Upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa kiasi kidogo unaweza kuchelewesha utekelezaji wa miradi na kusababisha kuongezeka kwa madeni ya wazabuni ya wakandarasi;

(ii) Uhaba wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo na uvuvi unapunguza mchango wa sekta hizo katika uchumi;

(iii) Changamoto za ubora wa bidhaa na vikwazo vya masoko vinaendelea kuathiri upatikanaji wa masoko ya nje kwa mazao ya mifugo na uvuvi;

(iv) Ili Sera na Sheria za sekta ya mifugo na uvuvi ziendane na wakati zinahitajika kufanyiwa mapitio;

(v) Maabara na sekta za mifugo na uvuvi zinahitaji maboresho na vifaa vya kisasa ili kuongeza ufanisi;

(vi) Upungufu wa Maafisa Ugani na changamoto za dawa za mifugo unaweza kuathiri maendeleo ya sekta hizo;

(vii) Migogoro kati ya wafugaji na wakulima inahitaji ufumbuzi wa kudumu kwa maendeleo ya uchumi; na

(viii) Kukosekana kwa mamlaka za usimamizi wa miradi kunapunguza ufanisi wa sekta.

Mheshimwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya mifugo. Katika sekta ya mifugo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali itatue changamoto ya uhaba wa ufanisi mdogo wa viwanda vya kuchakata maziwa nchini ikiwemo changamoto ya kodi na tozo;

(ii) Serikali iajiri Maafisa Ugani wa kutosha pamoja na kusambaza dawa za mifugo hususan katika maeneo yenye idadi kubwa ya mifugo hapa nchini;

(iii) Ili kupunguza magonjwa na vifo vya mifugo nchini, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa chanjo na kuwezesha uhakika wa upatikanaji wa chanjo katika maeneo yote yenye mifugo hususan maeneo ya pembezoni;

(iv) Serikali ikamilishe utekelezaji wa Sheria iliyotungwa na Bunge kuhusu utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo;

(v) Serikali iandae mpango wa kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata nyama na kupunguza usafirishaji wa mifugo hai kwenda nje ya nchi;

(vi) Ili kuwezesha sekta ya mifugo kuchangia katika mapato nchini, Serikali ihakikishe kuwa inaweka mikakati ya kudhibiti utoroshaji wa mifugo sambamba na kufanya mapitio ya ushuru na tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye sekta ya mifugo;

(vii) Kwa kutumia bajeti ya sekta ya mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ifanye mapitio ya Sera na Sheria zilizopitwa na wakati kama vile Sheria ya Mifugo ya Mwaka 2003 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006;

(viii) Serikali iendelee na juhudi za kuzuia, kudhibiti na kumaliza kabisa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kuimarisha usimamizi na uratibu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na

(ix) Serikali ilipe madai ya wakandarasi na wazabuni yaliyowasilishwa Hazina yenye jumla ya shilingi bilioni 48.6 ili kuendelea kutekeleza kampeni ya chanjo, utambuzi wa mifugo na ujenzi wa miundombinu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya uvuvi. Katika sekta ya uvuvi, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu madhara ya uvuvi haramu ambao unaathiri mazalia ya samaki na kuchangia uhaba wa samaki hapa nchini. Aidha, Serikali isimamie uvuvi endelevu na uzingatiaji wa sheria zinazosimamia shughuli zote za uvuvi na uhifadhi wa mazingira;

(ii) Serikali ikamilishe ununuzi wa meli mbili zitakayowezesha uvuvi eneo la Bahari Kuu kama ilivyotekelezwa kwenye Ilani ya CCM ya Mwaka 2025.

(iii) Serikali iendeleze mpango wa ujenzi wa mashamba darasa ya ukuzaji wa viumbe maji katika Halmashauri za Wilaya ili kusogeza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wananchi;

(iv) Serikali ianzishe programu maalumu ya kupandikiza na kujazilia samaki walio katika hatari ya kutoweka kwa lengo la kuendeleza zao la samaki kama nyenzo ya uchumi na lishe;

(v) Serikali iwezeshe upatikanaji wa mitaji, mikopo na vifaa kwa wavuvi, wakuzaji viumbe maji, vyama vya ushirika na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za kifedha ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa njia ya kisasa na kibiashara;

(vi) Serikali iwajengee wavuvi wazalendo uwezo wa kufanya uvuvi wa kisasa kwa kuwapatia mafunzo na nyenzo;

(vii) Serikali ihamasishe sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ikiwemo uzalishaji wa vifaranga bora vya

samaki na chakula ili kupunguza gharama za uzalishaji; na

(viii) Serikali ipunguze au kuondoa tozo kwa bidhaa za uvuvi zinazoingizwa nchini ili kuwawezesha wavuvi wadogo kumudu gharama za ununuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili dira ya Wizara ambayo ni kuwa na sekta ya mifugo na uvuvi iliyoendelea na yenye hadhi ya Kimataifa ambayo ni uendelevu kiuchumi, kijamii na kimazingira iwe na uhalisia. Kamati inashauri kwamba Serikali izingatie ipasavyo ushauri wote uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linategemewa kutoa ushauri stahiki kwa Serikali. Aidha, bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu inatarajiwa kutekelezwa kwa namna inavyokusudiwa na Bunge lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imefanya kazi ya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato ya Wizara hii kwa lengo la kulisaidia Bunge kufanya uamuzi kwa maslahi ya umma. Uchambuzi uliofanywa, maoni na ushauri uliotolewa unastahili kuzingatiwa wakati wa mjadala kuhusu hoja inayojadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wao, ninatamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda. Ninaomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Bashiru Kakurwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani, kwa ushirikiano

mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Agnes Kisaka Meena kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa Shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2025 (Kanuni za Bunge), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026,

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Msingi wa Uchambuzi, Muundo wa taarifa na njia zilizotumika kushughulikia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii;

(ii) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri kutokana na uchambuzi pamoja na kuhitimisha maudhui ya Taarifa hii.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Taarifa Hii

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 121 (4) kikisomwa kwa pamoja na vifungu vya 7(1)(a), 6(1)(c) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2025, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti yaliyoitaka Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge, yaliitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka fedha 2025/2026. Lengo la masharti hayo ni kuiwezesha Kamati kulinganisha hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka Kamati za Kisekta kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati imetimiza masharti ya Kanuni hiyo kwa kufanya uchambuzi yakinifu na taarifa hii kuletwa mbele ya Bunge kujadiliwa.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Mawanda ya Uchambuzi yanagusa maeneo yafuatayo: -

(i) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(ii) Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(iv) Tathmini ya Ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Upatikanaji wa fedha kutoka hazina.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo hayo yanatokana na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge ambayo inaelekeza kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027. Kwa kufanya hivyo Bunge lako Tukufu linaweza kupata masuala ya kuzingatia kutoka katika taarifa hii kuhusu wasilisho la Mtoa Hoja linalojadiliwa leo.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inahusu matokeo ya uchambuzi na tathmini iliyofanywa na Kamati. Madhumuni yake ni kujenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi aliyoiwasilisha mapema kabla yangu. Masuala yanayochambuliwa na kufanyiwa tathmini ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 na 28 Machi, 2026, Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika maelezo hayo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Mambo hayo yalifanyiwa tathmini kutokana na uchambuzi ili kupata maoni na ushauri wa Kamati.

#### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 Mei, 2025 wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilishauri mambo mbalimbali. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia uzingatiaji wa ushauri huo naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliozingatiwa na Kamati ni kuhusu ujenzi wa mabirika na majosho kwa ajili ya kunyweshea na kuogeshea mifugo. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa Serikali imeendelea kujenga majosho na kuhamasisha Sekta Binafsi na

Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye idadi kubwa ya mifugo kuwa na miundombinu ya majosho.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu kubwa, ipo sehemu ya ushauri ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Mfano wa ushauri huo ni kuhusu mapitio ya tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambazo ni nyingi kiasi cha kukwamisha ukuaji na maendeleo ya Sekta hizo nchini. Maelezo ya Mtoa Hoja yalionesha kuwa Serikali inaendelea kufanya mapitio ya tozo mbalimbali ikiwa na maana kwamba kwa kipindi chote cha takribani mwaka mzima mapitio hayajakamilika. Hali hiyo ni dalili kwamba utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 haujafanikiwa kutatua changamoto ya wingi wa tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi hali inayosababisha maisha ya Wafugaji na Wavuvi kuendelea kuwa duni.

**Mheshimiwa Spika,** juhudi za Serikali za kujenga majosho kwa mikakati iliyowekwa zinastahili pongezi, hali hiyo inahitaji kuendelezwa. Hata hivyo, kusuasua katika utatuzi wa changamoto ya wingi wa tozo kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni jambo linalohitaji kupewa kipaumbele.

**2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa miwili (2) ya Dar es Salaam na Morogoro ili kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Miradi hiyo ni: -

(i) Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO (**Mradi Na. 4486);**

(ii) Ununuzi wa meli 2 za Uvuvi (**Mradi Na. 4429**); na

(iii) Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, Mvomero Vijijini (**Mradi Na. 4486**);

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa miradi hiyo ulizingatia umuhimu wake katika kuimarisha, kufuatilia utekelezaji wa Programu na miradi mbalimbali ndani ya Wizara kama ifuatavyo:-

(i) Ufufuaji wa TAFICO utachochea uongezaji wa thamani katika Sekta ya Uvuvi.

(ii) Ununuzi wa meli mbili za uvuvi utaongeza uwezo wa nchi kushiriki moja kwa moja katika uvuvi wa bahari kuu na kupunguza utegemezi wa wavuvi wa kigeni.

(iii) Mradi wa chanjo ya mifugo utachangia uimarishaji wa afya ya mifugo, kupunguza magonjwa ya mlipuko, kuongeza tija ya uzalishaji wa nyama na maziwa na kuboresha kipato cha wafugaji na kuleta ustawi wa Sekta ya Mifugo.

**(a) Utekelezaji wa Mradi wa Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO (Mradi Na. 4486);**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania – TAFICO ni sehemu ya juhudi za kukuza uvuvi wa kibiashara nchini. Mradi huu una thamani ya Shilingi 20,039,825,089.35 na unatarajiwa kuleta manufaa katika Uchumi wa Taifa. Mradi huu utakapokamilika, utaongeza mapato ya Serikali, utakuza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa na utachangia kupatikana kwa fedha za kigeni. Vile vile kukamilika kwa mradi huu kutawezesha maendeleo ya ajira na ujuzi kupitia nafasi za ajira, ujuzi wa kitaalam ulioboreshwa na uwezo wa wafanyakazi ulioimarishwa katika Sekta ya uvuvi. Zaidi ya hivyo mradi utawezesha ufanisi wa rasilimali za bahari na shughuli za uvuvi kwa namna endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** katika Ziara hiyo Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoukabili mradi huu. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Deni la kiasi cha Shilingi Bilioni 1.25 wanazopaswa kulipwa wakandarasi, watumishi, wazabuni na watoa huduma ni changamoto inayoathiri ufanisi.

(ii) Ukosefu wa bodi ya Wakurugenzi, hali inayoathiri masuala ya utawala bora ambayo ni sehemu muhimu kufikia adhma iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inamaoni kuwa adhma ya Serikali kukuza uvuvi wa kibiashara nchini kupitia ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania ni jambo linalostahili kuungwa mkono na Bunge, wananchi na watu wote wenye nia njema na Taifa hili. Hata hivyo, changamoto zilizobainishwa zinaweza kuathiri tija iliyokusudiwa katika mradi huu. Hivyo basi, kuna umuhimu wa kujipanga ipasavyo kuzitatua changamoto hizo.

**(b) Mradi wa ununuzi wa meli 2 za Uvuvi (Mradi Na. 4429).**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ununuzi wa meli mbili za uvuvi ni hatua ya kimkakati katika Sekta ya Uvuvi. Madhumuni yake ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa Samaki, kupunguza uvuvi haramu na kuongeza ajira. Manufaa ya mradi huu ni kufanikisha adhma ya TAFICO katika Uchumi wa Taifa. Gharama za mradi huu ni shilingi 10,498,589,329 ikiwa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya utekelezaji wa Mradi huu ilionesha kuwa utekelezaji wake unasuasua. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 hakukuwa na meli hata moja iliyonunuliwa. Hata hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzindua Meli moja itakayotumika katika uvuvi wa bahari kuu, hiyo ni ishara nzuri ya katika Sekta ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ufafanuzi huo Kamati ina maoni kwamba utekelezaji wa mradi huu ni jambo linalohitaji usimamizi wa karibu kwa kuwa ni kiini cha dhamira ya Serikali ya kuwezesha Sekta ya Uvuvi nchini kuchangia ipasavyo katika Uchumi wa Taifa. Kwa ujumla mradi huu unatarajiwa kuwa na manufaa zaidi kwa kutegemea usimamizi bora, miundombinu imara na ushirikishwaji wa wadau.

(c) **Mradi wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, Mvomero Vijijini (Mradi Na. 4486);**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kufanikisha utambuzi wa mifugo na kulinda afya ya mifugo kupitia chanjo. Gharama yake ni shilingi 444,827,407.4.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla mradi huu ukikamilika utaweza kusaidia kuleta ufugaji wa kisasa, usimamizi bora wa mifugo, na maendeleo ya kiuchumi kwa wafugaji wa Mvomero Vijijini. Mafanikio hayo ni manufaa makubwa katika Sekta ya Mifugo, Uchumi wa Jamii na Usimamizi wa Rasilimali. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya mkakati wa kuiwezesha Tanzania kukidhi masharti ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH) na kuongeza soko la mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** hali halisi ya utekelezaji inaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Mradi ulikuwa umefikia asilimia 42.8. Kwa hatua hiyo hakuna dalili za mradi huu kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2026. Kwa sababu hiyo adhma ya Serikali kupunguza matumizi ya dawa na kuzuia Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa (UVIDA) kwa Wanyama itashindwa kutimia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo Kamati inamaoni kwamba, upo umuhimu wa Serikali kutafuta vyanzo vya ndani kwa ajili ya mradi huu. Msingi wa maoni haya unatokana na ukweli kwamba gharama za utekelezaji wa mradi huu zinategemea fedha za nje kwa asilimia 100.

### 2.2.3 Mwenendo na Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni hatua muhimu ya kibunge katika kushughulikia bajeti. Hatua hii inaliwezesha Bunge kufatilia utekelezaji wa Bajeti inayoidhinishwa ili kuweka msukumo katika maeneo yanayoongeza ufanisi wa miradi ya maendeleo. Aidha, uchambuzi huu utaliwezesha Bunge kutathmini uwezo wa Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha

zilizotolewa na kutumia uzoefu huo ili kufanya uamuzi sahihi kuhusu makadirio ya bajeti kwa mwaka unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** katika muktadha huo, Kamati ilifanya ulinganisho wa makadirio ya bajeti ya maendeleo, hali halisi ya upatikanaji wa fedha na hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa miradi. Vile vile Kamati ililinganisha kiwango cha upatikanaji wa fedha za ndani na kiwango cha upatikanaji wa fedha za nje ili kupima athari ya upatikana wa bajeti katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuzingatia matokeo hayo katika uchambuzi wa bajeti ya 2026/2027.



**Mheshimiwa Spika,** kwa urahisi katika kuchanganua mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo unaonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Mwenendo na Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| **CHANZO CHA FEDHA** | **FEDHA ILIYOTENGWA** | **% JUMLA** | **FEDHA ILIYOPATIKANA** | **% JUMLA** | **% LENGO** |
|---|---|---|---|---|---|
| Fedha za Ndani | 227,994,375,000 | 60.77606925 | 89,981,163,488 | 81.10635638 | 39.4663963 |
| Fedha za Nje | 147,144,027,000 | ***39.22393075*** | 20,961,020,958 | ***18.89364362*** | 14.2452408 |
| **Jumla** | **375,138,402,000** | | **110,942,184,446** | | |

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali hilo linaonesha uwiano kati ya fedha za nje na fedha za ndani wakati wa kupitisha bajeti, pamoja na hali ya upatikanaji wa fedha. Taswira ya uwiano huo inaonekana katika **Kielelezo namba 2.**

**Kielelezo Na. 2: Fedha iliyotengwa na Fedha iliyopatikana**

| Fedha iliyotengwa | Fedha iliyopatikana |
|---|---|
|  |  |





**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa tarakimu (figures) kutoka kwenye jedwali na kielelezo unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara hii tarehe 23 Mei, 2025 lilikubali mchango wa asilimia 60.8 wa fedha za ndani lakini katika upatikanaji wa fedha mchango wa fedha za ndani umechukua sehemu kubwa hadi kufikia asilimia 81;

(ii) Mchango wa fedha za nje kwenye bajeti ya miradi wakati wa kupitisha bajeti ulikuwa ni asilimia 39.2 lakini hali halisi wakati wa upatikanaji wa fedha imeonesha kuwa mchango wa fedha za nje ni asilimia 18.

(iii) Upatikanaji wa fedha za ndani hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ulifikia asilimia 39.4 ilhali kipindi cha utekelezaji ni asilimia 66.6.


(iv) Upatikanaji wa fedha za nje ulifikia asilimia 14.2 licha ya kuwa kipindi cha utekelezaji kilifikia asilimia 66.6;

(v) Kwa wastani mtiririko wa upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hauoneshi kama kuna uwezekano wa kupatikana kwa fedha zote za kutekeleza miradi ya maendeleo. Mkwamo mkubwa unaonekana kujitokeza kwenye fedha za nje. Yote hayo ni ishara kwa Serikali na nchi kwa ujumla kujipanga kutekeleza miradi ya maendeleo kwa njia ya kujitegemea. Aidha, inaonesha kwamba fedha za ndani zinazohitajika zinategemea usimamizi wa jumla wa Serikali kuhusu vyanzo mbalimbali vya bajeti ya Serikali.

### 2.2.4 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya makusanyo ya maduhuli na kufanya uchambuzi. Njia iliyotumika kuchambua inajumuisha kuweka takwimu za ukusanyaji kwenye grafu kama inavyoonekana kwenye **kielelezo namba 3** kinachohusu makusanyo ya Sekta ya Mifugo na **kielelezo namba 4** Sekta ya Uvuvi.


Kielelezo Na. 3: Makusanyo Sekta ya Mifugo




**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa makusanyo. Vyanzo hivyo ni vibali vya kuhamisha mifugo (lifestock movement permit) vilivyokuwa na ufanisi chini ya asilimia 50 yaani asilimia 49 na vibali vya ada mchanganyiko vilivyokuwa na ufanisi wa asilimia 37. Chanzo cha mapato kinachohusu uuzaji wa heifer, ada ya kuuza nje yaani export fee, lifestock market fee, na receipts from verternary charges zilikuwa na ufanisi uliozidi asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, uchambuzi wa vyanzo vya mapato unaonekana katika kielelezo namba 4.

**Kielelezo Na. 4: Makusanyo Sekta ya Uvuvi**




**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa ufanisi wa vyanzo vya mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Chanzo cha mapato kutokana na prowns fishing licence hakikufanikisha mapato yoyote. Chanzo cha ada nyinginezo za mambo ya kiutawala kilikuwa na ufanisi wa asilimia 8 tu na chanzo cha mapato kutokana na export royalty kilikuwa na ufanisi kwa asilimia 54.

(ii) Vyanzo viwili vya mapato yaani import royalty na movement permit vilikuwa na ufanisi uliozidi asilimia 100.

(iii) Vyanzo vya mapato vya fishing and export licence, receipts from sales of fingerings na receipts from sales of laboratory services vilikuwa na ufanisi wa kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa matokeo hayo uzoefu huu unapaswa kufanyiwa kazi. Kamati inamaoni kwamba kutozingatia matokeo ya uchambuzi huu kunaweza kusababisha makadirio ya mapato kukosa uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa maduhuli ulifanyika kwa lengo la kubaini mchango wa kila Sekta ikilinganishwa na uwiano wa mchango wakati wa makadirio kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5**.



**Kielelezo Na. 5: Uchanganuzi wa Makusanyo ya Maduhuli hadi Februari, 2026**

| CHANZO CHA MADUHULI | LENGO WAKATI WA KUPANGA | % JUMLA | KIASI KILICHOKUSANYWA | % JUMLA | % LENGO |
|---|---|---|---|---|---|
| Sekta ya Uvuvi | 44,204,999,000 | 47 | 23,859,722,211 | 44.7 | 53.9 |
| Sekta ya Mifugo | 49,900,001,000 | 53 | 29,469,999,333 | 55.3 | 59.1 |
| **Jumla** | **94,105,000,000** | | **53,329,721,544** | | |

**Chanzo: Randama Fungu 99**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha lengo na kiasi kilichokusanywa pamoja na mchango wa Sekta uliokusudiwa ikilinganishwa na mchango wa Sekta uliofikiwa. Katika kufanya hivyo taswira halisi inajitokeza katika **Kielelezo Na.6.**

**Kielelezo Na. 6: Lengo wakati wa kupanga na kiasi kilichokusanywa**

| **LENGO WAKATI WA KUPANGA** | **KIASI KILICHOKUSANYWA** |
|---|---|
|  |  |





**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishwa kuwa Sekta ya Uvuvi ichangie

makusanyo ya Wizara kwa **asilimia 47** lakini mchango wake umepungua hadi **asilimia 44.7.** Mchango wa Sekta ya Mifugo ulikadiriwa kuwa **asilimia 53** lakini katika utekelezaji Sekta ya Mifugo imeongeza mchango wake katika makusanyo hadi kufikia asilimia 55;

(ii) Sekta ya Mifugo katika makusanyo imefikia **asilimia 54** ya lengo katika kipindi cha utekelezaji ambacho ni **asilimia 66.6**, hali hiyo inaonesha kuwa Sekta ya Mifugo iko nyuma kwa **asilimia 12.7**;

(iii) Sekta ya Uvuvi imefikia lengo la ukusanyaji kwa asilimia 59 katika kipindi cha utekelezaji cha **asilimia 66.6**. Hali hiyo inaonesha kuwa Sekta ya Mifugo iko nyuma ya lengo la makusanyo kwa **asilimia 7.6**;

(iv) Kwa wastani Sekta mbili chini ya Wizara hii ziko nyuma kwa **asilimia 10**;

**Mheshimiwa Spika,** kwa mchanganuo huo ni wazo kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2026 Wizara hii inaweza kushindwa kukusanya jumla ya **shilingi 9,410,500,000**, hali ambayo itaathiri kiasi cha bajeti kilichoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Aidha ufanisi wa Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi kwa wastani si mzuri katika ukusanyaji. Sekta ya Uvuvi inaufanisi duni zaidi ya Sekta ya Mifugo katika makusanyo ya maduhuli. Hayo yote yanamaanisha kuwa huenda lengo la makusanyo lililopangwa halikuwa na uhalisia au mikakati na juhudi za makusanyo zilihitaji msukumo maalum. Sababu nyingine inaweza kuwa mabadiliko mbalimbali katika shughuli za mifugo na shughuli za uvuvi.

### 2.2.5 Upatikanaji wa fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge inavyostahili, Kamati ilihitaji kufanya tathmini ya upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Hatua hiyo ililenga kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti inayokwisha na kupima iwapo fedha

zilizotolewa na kutumika zinaendana na mpango uliokusudiwa. Uchambuzi huu unaweza kulisaidia Bunge kupima uhalisia wa makadirio mapya ya bajeti, kuhakikisha uwajibikaji wa Serikali katika matumizi ya fedha za umma na kufanya uamuzi wenye msingi wa ushahidi kuhusu mahitaji ya fedha kwa mwaka 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya uchambuzi wa kina Kamati ilichanganua fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya Mishahara, Uendeshaji na Miradi ya Maendeleo. Uchanganuzi huo unaonekana katika **Kielelezo Na. 7**.

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2026**

| UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO FUNGU (99) HADI FEBRUARI, 2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maelezo** | | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2025/2026** | **Fedha Iliyopokelewa hadi kufikia Februari, 2026** | **Asilimia ya fedha zilizopokelewa** |
| **Matumizi ya Kawaida** | Mishahara | 47,264,785,000 | 29,703,590,334.91 | 62.85 |
| | (OC) | 54,251,885,000 | 27,109,619,082.47 | 49.97 |
| ***Jumla Ndogo*** | | **101,516,670,000.00** | **56,813,209,417.38** | **55.96** |
| **Maendel eo** | Fedha za ndani | 227,994,375,000.00 | 89,981,163,488.26 | 39.47 |
| | Fedha za nje | 147,144,027,000.00 | 20,961,020,958.00 | 14.25 |
| **Jumla Ndogo** | | **375,138,402,000.00** | **110,942,184,446.26** | **29.57** |
| **JUMLA KUU** | | **476,655,072,000.00** | **167,755,393,863.6 4** | **35.19** |

**Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Fungu 99**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026:-

(i) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni asilimia 33.9 ya jumla ya fedha iliyopokelewa. Kiwango hicho kinatofautiana na kiwango cha bajeti iliyopangwa kwa uwiano wa asilimia 21.3 ya bajeti yote. Tafsiri yake ni kwamba uwiano wa matumizi ya kawaida uliokuwa umewekwa kwenye bajeti umebadilika wakati wa utekelezaji na kuathiri bajeti ya maendeleo.

(ii) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida imepatikana kwa asilimia 56 katika kipindi cha asilimia 66.6 cha utekelezaji. Hali hii inaweza kusababisha kutokamilika kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2026.

(iii) Fedha za uendeshaji zilizopokelewa zimefikia kiwango cha asilimia 50. Kiwango hicho ni nusu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ilhali kipindi cha utekelezaji ni asilimia 66.6, hali hiyo ni dalili kwamba uendeshaji wa Sekta ya Mifugo unaweza usifikie malengo yaliyokusudiwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2026.

(iv) Upatikanaji wa fedha za ndani na fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo umekuwa pungufu ya asilimia 50. Fedha za ndani zimepatikana kwa asilimia 39.47 na fedha za nje zimepatikana kwa asilimia 14.3.

(v) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mifugo na uvuvi kwa ujumla umekuwa pungufu ya asilimia 40. Hali hii inaleta mashaka katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali hiyo upo umuhimu kwa Serikali kuziangalia upya Sekta za Mifugo na Uvuvi. Sekta hizi zinahitaji kuboreshwa ili kuendana na misingi ya Dira 2050, Shabaha namba 2 katika aya 2.2 inahusu kutokomeza umaskini uliokithiri kwa makundi yote.1 Wafugaji na Wavuvi ni miongoni mwa makundi yanayoweza kuwa na umaskini uliokithiri. Hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge unapaswa kuendana na dhamira hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, ilielekeza kipaumbele kwa Sekta ya Mifugo kama inavyosomeka katika aya ya 18 kipengele 2.1.3.2:

**NANUKUU**

"......Chama kitaendelea kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Mifugo ili kuiimarisha na hivyo kuleta mabadiliko makubwa kwa kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika ufugaji wa kisasa na wa kibiashara pamoja na kuchakata bidhaa za mifugo..."

**MWISHO WA KUNUKUU**[2]

**2.3 Vipaumbele vya Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida vipaumbele vya mpango wa Wizara ndivyo vinavyoelekeza matumizi ya fedha, Kamati ilitambua uhusiano huo kati ya Mpango, makadirio ya matumizi na kuzingatia mpango unaeleza kinachokusudiwa na Wizara kufanyika kwa mwaka wa fedha unaohusika. Makadirio ya bajeti yanaeleza kiasi cha fedha kitakachotumika kuwezesha Wizara kutekeleza mipango yake. Katika uchambuzi wake Kamati ilitaka kujiridhisha iwapo vipaumbele vya Mpango wa Wizara vinazingatia mwelekeo wa Dira 2050 na ahadi iliyotolewa kwa wananchi kupitia Ilani ya uchaguzi ya CCM 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo makuu ya Vipaumbele vya Wizara yanayostahili uchambuzi ni:-

(i) Kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi;
(ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi;
(iii) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi; na
(iv) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa maeneo hayo ya vipaumbele, Kamati ilitaka kupata majibu ya maswali makuu

mawili kwanza, ni kwa namna gani vipaumbele hivi vinaendana na mwelekeo wa Dira 2050. Pili, kuna uhusiano gani kati ya vipaumbele hivyo na Ahadi ya Serikali kupitia Ilani ya CCM.

Tathmini ya Kamati kuhusu maswali hayo inaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Kipaumbele cha kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi kinajielekeza kuiwezesha Sekta ya Mifugo na Uvuvi kuingia katika Sekta za Mageuzi. Kigezo kimojawapo cha Sekta za Mageuzi kilichoainishwa kwenye Dira 2050 ni uwezo wa kuongeza thamani kwa kutoa fursa kwa malighafi na bidhaa kuongezwa thamani kabla ya kumfikia mtumiaji. Aidha, kwa upande wa Ilani ya Uchaguzi kipaumbele hicho kinatekeleza ahadi iliyotolewa na Serikali ya CCM kupitia Ilani ya Uchaguzi ambayo inaahidi kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi kutoka tani 14,000 mwaka 2025 hadi tani 50,000 mwaka 2030.[4]

(ii) Kipaumbele cha kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kinalenga kuziwezesha Sekta hizo kuwa na uwezo wa kuzalisha na kuchochea ajira kwa Sekta nyingine kama vile Sekta ya viwanda na uzalishaji. Kwa msingi huo iwapo Wizara itajielekeza ipasavyo kwenye kipaumbele hicho itafanikiwa kuwa na kigezo cha kuchaguliwa kwenye

(iii) Kipaumbele cha kuimarisha Utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta za mifugo na uvuvi kitaziwezesha Sekta hizi kukua zenyewe na kuchochea ukuaji au uzalishaji wa Sekta nyingine, Sekta hii itakidhi vigezo vya kuingia kwenye Sekta ya mageuzi.6 Aidha, kipaumbele hicho kinalenga kutimiza ahadi iliyotolewa wakati wa uchaguzi, ahadi hiyo ni kuimarisha huduma za ugani, kinga na tiba ya mifugo ili kuwezesha wafugaji kukabiliana na magonjwa na vifo vya mifugo, hivyo kuongeza uzalishaji na mapato.7

3 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2025) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 uk.109 kigezo namba 4

4 Ilani ya Uchaguzi, k.h.a uk.15 hatua namba (v)

Sekta za Mageuzi kama ilivyobainishwa kwenye Dira 2050 kigezo namba 1.[5]

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ufafanuzi huo, Kamati imejiridhisha kuwa, vipaumbele vya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 vinaendana na mwelekeo wa maendeleo uliowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Vipaumbele hivyo vinaonesha adhma ya Serikali kutimiza ahadi yake kwa wananchi. Ulinganifu huo umejitokeza katika maeneo ya kimkakati yanayolenga kukuza uchumi, kuboresha huduma, kuongeza ajira na kuongeza ushindani wa Taifa katika Sekta mbalimbali. Ni maoni ya Kamati kwamba, utekelezaji wa vipaumbele hivyo, unachangia kufikia malengo ya Taifa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa maendeleo. Kwa msingi huo rasilimali fedha, usimamizi madhubuti na ufuatiliaji wa utekelezaji vinapaswa kuzingatiwa ipasavyo.

## 2.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilizingatia kuwa utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa na Wizara unategemea makadirio ya mapato na matumizi. Baada ya uchambuzi wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilijielekeza kwenye uchambuzi wa rasilimali fedha. Katika kufanya hivyo, maeneo makuu mawili ya rasilimali fedha yalizingatiwa. Maeneo hayo ni makadirio ya mapato na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Hayo yote yalifanyika kwa kufanya ulinganisho na yaliyojitokeza katika taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026

### 2.4.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na uwezo wa Wizara kuchangia inavyostahili katika mapato ya jumla ya Serikali Kamati ilichambua makadirio ya mapato. Uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ulitumika katika uchambuzi. Sababu ya kufanya hivyo ni kubaini iwapo makadirio hayo yanaendana na uhalisia, yanazingatia uwezekano wa lengo la makusanyo kufikiwa na yametambua vyanzo halisi vya mapato.

5 Dira 2050, k.h.a uk.108
6 Dira 2050 k.h.a uk. 109 kigezo namba 3.
7 Ilani ya Uchaguzi k.h.a uk 15 hatua namba (iii)

**Mheshimniwa Spika,** makadirio ya mapato yaliyowasilishwa na mtoa hoja mapema leo hii, yamezingatia vyanzo 10 vya mapato katika Sekta ya Mifugo na vyanzo 9 vya mapato katika Sekta ya Uvuvi. Vyanzo hivyo, vinaonekana katika kielelezo Na. 8.

**Kielelezo Na. 8: Mchanganuo wa Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027**

| NA. | CHANZO | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2026/2027 | UFANISI % |
|---|---|---|---|
| | **MIFUGO** | | |
| 1. | Export fee | 440,000,000 | 130 |
| 2. | Receipts from veterinary charges | 46,497,998,000 | 106 |
| 3. | Compounds fee | 1,300,000,000 | 37 |
| 4. | Movement Permit Fee other than Livestock Market | 969,000,000 | 72 |
| 5. | Livestock Movement Permit | 28,210,000,000 | 49 |
| 6. | Livestock market fee | 7,490,000,000 | 128 |
| 7. | Sales of Semens and liquid nitrogen | 430,000,000 | 81 |
| 8. | Receipts from sales of heifer | 1,760,000,000 | 163 |
| 9. | Receipts from sales of seeds and hay | 400,000,000 | 69 |
| 10. | Vaccination fees | 7,000,000,000 | |
| | **JUMLA MIFUGO** | **94,496,998,000** | |
| | **UVUVI** | | |
| 1. | Fishing & Export License | 3,045,000,000 | 90 |
| 2. | Export Royalty | 30,192,000,000 | 54 |
| 3. | Import Royalty | 12,050,002,000 | 347 |
| 4. | Movement Permit | 13,358,000,000 | 158 |
| 5. | Exclusive Economic Zone Fishing License | 7,400,000,000 | 27 |
| 6. | Receipt from Sale of Laboratory Services | 3,800,000,000 | 69 |
| 7. | Prawn Fishing License | 124,000,000 | 0 |
| 8. | Receipts from Sale of Fingerlings | 660,000,000 | 70 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Other Administrative Fee | 874,000,000 | 8 |
| **JUMLA UVUVI** | | **71,503,002,000** | |
| **JUMLA KUU** | | **166,000,000,000** | **81** |

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa vyanzo vya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Kwenye Sekta ya Mifugo kuna chanzo kipya cha ada ya chanjo ambazo ni shilingi bilioni 7. Lakini katika Sekta ya Uvuvi kuna chanzo kimoja cha compound fees kilichokuwepo mwaka wa fedha uliokwisha kimeachwa;

(ii) Katika Sekta ya Mifugo kuna chanzo kilichoshindwa kuchangia mapato mwaka wa fedha 2025/2026 lakini kimejumuishwa katika makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(iii) Katika Sekta ya Mifugo kuna vyanzo viwili vilivyokuwa na ufanisi mkubwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 lakini katika mwaka wa fedha 2026/2027 vimewekewa lengo kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na lengo la mwaka wa fedha uliopita;

(iv) Baadhi ya vyanzo vya mapato vilivyokuwa na ufanisi mdogo vimeongezewa makadirio ya mapato. Katika Sekta ya Mifugo compound fee iliyokuwa na ufanisi wa asilimia 37 na lifestock movement permint iliyokuwa na ufanisi wa asilimia 49 vimeongezewa makadirio ya mapato na kwa upande wa mifugo chanzo kimoja kilichokuwa na ufanisi wa asilimia 27 kimeongezewa makadirio ya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa Wizara ina kazi kubwa ya kufanya ili kuwezesha lengo la mapato yanayokadiriwa. Vinginevyo makadirio haya yanaweza kukosa uhalisia.

### 2.4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya Matumizi ya kawaida yaliyowasilishwa na Mtoa Hoja kwa kuzingatia mambo muhimu katika Sekta hii. Mambo hayo ni mahitaji halisi ya

uendeshaji wa Wizara, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kisheria, utimizaji wa ahadi za Serikali kwa Wananchi katika Sekta inayohusika, mchango wa Sekta katika maendeleo ya Taifa kwa mujibu wa Dira 2050 na uzoefu uliopatikana kuhusu upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika uchambuzi huo Kamati ilitathmini ufanisi na uwiano wa matumizi yanayopendekezwa ili kuhakikisha kwamba bajeti inayoidhinishwa inawezesha utoaji endelevu wa huduma kwa wananchi bila kuathiri nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida yanahusu gharama za uendeshaji wa shughuli za kawaida kwa kujumuisha mishahara (PE) na uendeshaji wa kila siku (OC). Ili kupata uhalisia wa Makadirio haya Kamati ilifanya ulinganisho na upatikanaji wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2025/2026 kama inavyoonekana katika **kielelezo Na.9.**

**Kielelezo Na. 9: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na 2026 na 2027**

| **BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | **BAJETI ILIYOPATIKANA** | **ASILIMIA %** |
| OC | 54,251,885,000 | 27,109,619,082.5 | 49.97 |
| MISHAHARA | 47,264,785,000 | 29,703,590,334.9 | 62.85 |
| **JUMLA** | **101,516,670,000** | **56,813,209,417.40** | **55.96** |
| **MAKADIRIO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** | | | |
| **AINA YA MATUMIZI** | **ILIYOIDHINISHWA** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA %** |
| OC | 48,826,697,000 | (-5,425,188,000) | 9.99 |
| MISHAHARA | 49,452,723,000 | 2,187,1938,000 | 4.62 |
| **JUMLA** | **98,279,420,000** | (-3,237,250,000) | 3.18 |

**Mheshimiwa Spika,** uchanganuzi kwenye jedwali unaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya Matumizi Mengineyo (OC) yamepungua kwa **asilimia 9.99** na uzoefu wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 uliuonesha upungufu kwa asilimia 16.6. kiwango hiki kimepungua ikilinganishwa na uzoefu.

(ii) Makadirio ya Mishahara yameongezeka kwa asilimia 4.62 na uzoefu wa upatikanaji wa fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 ulionesha kuwa nyuma kwa **asilimia 4**.

(iii) Makadirio ya jumla ya fedha za matumizi ya kawaida yamepungua kwa asilimia 3.18 na uzoefu unaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 upatikanaji wa fedha ulikuwa nyuma kwa **asilimia 10.6**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla makadirio ya matumizi ya kawaida yamepungua ikilinganishwa na uzoefu uliopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2026. Hali hiyo inaonesha kuwa kwa kiasi makadirio yanauhalisia, hata hivyo, kwa uzoefu wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 baada ya Bunge kuidhinisha Bajeti hii, Serikali itapaswa kutilia mkazo upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

### 2.4.3 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Kamati ilizingatia dhima kubwa ya bajeti ya maendeleo. Kama unavyofahamu bajeti ya kugharamia miradi ya maendeleo inalenga uwekezaji wa muda mrefu na kuongeza uwezo wa uchumi na huduma za jamii katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Bajeti hiyo ndiyo inayohusika na kuacha alama ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa kupitia Ilani ya Uchaguzi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linapaswa kuwa na jicho katika makadiro ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hayo Kamati ilichambua kwa umakini mapendekezo yaliyowasilishwa na Mtoa Hoja. Vigezo vya uchambuzi vilivyotumika ni uzoefu uliopatikana katika mwaka wa fedha 2025/2026. Methodolojia (Methodology) ya Kamati ni kufanya ulinganisho kati ya kiwango cha fedha kilichopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2026 kwa njia ya asilimia na ukokotozi wa ongezeko au punguzo la bajeti inayoombwa. Uchanganuzi wa makadirio unaonekana katika **Kielelezo Na.10**.

Kielelezo Na. 10: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/027

| MAELEZO | | 2025/2026 | 2026/2027 | Ongezeko / Pungufu % |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi ya Maendeleo | Fedha za ndani | 227,994,375,000.00 | 193,795,218,000 | (38.43) |
| | Fedha za nje | 147,144,027,000.00 | 141,304,487,000 | (1.08) |
| **Jumla** | | **375,138,402,000.00** | **335,099,705,000** | **(10.67)** |

**Mheshimiwa Spika,** kwa matokeo hayo imebainika kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zimeshuka kwa asilimia 38.43; ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaokwisha.

(ii) Fedha za nje zimepungua kwa asilimia 1.08 ikilinganishwa na mwaka 2025/2026. Hali hii inamaainisha kushuka kwa utegemezi wa vyanzo vya nje kwenye bajeti ya maendeleo kwa asilimia 4.

(iii) Kwa ujumla bajeti ya miradi imepungua kwa asilimia 10.67 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa bajeti kwa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji cha asilimia 66, Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa asilimia 29.57 tu ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanaendana na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa Serikali kuzuia athari za kushuka kwa bajeti ya maendeleo katika utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Uvuvi na Mifugo. Kwa kufanya hivyo, mkakati wa Wizara unaolenga kuchagiza na kujenga uwezo wa vijana na wanawake kujiajiri

katika shughuli za mifugo, uvuvi, na ukuzaji wa viumbe maji utatekelezeka.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 145(c) sehemu hii ni sehemu ya mwisho katika taarifa na inajumuisha maoni ya jumla na ushauri kutokana na uchambuzi uliofanyika. Lengo ni kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili makadirio ya mapato ya Wizara hii kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa kufanya hivyo, Bunge lako likumbuke kuwa Dira 2050 inazijumuisha Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwenye mhimili wa uchumi wa Tanzania.[8]

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii pia inazingatia kwamba, kupitia Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 Ibara ya 24 CCM iliahidi kwamba itaielekeza Serikali kuwezesha upatikanaji wa mitaji, mikopo, vifaa kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji, vyama vya ushirika na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za kifedha. Lengo ni kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Maelezo hayo yanaunda muktadha wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi naomba kubainisha kwa muhtasari majumuisho ya maoni kabla ya kutoa ushauri kisekta. Maoni hayo ni:-

(i) Upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge unaweza kukwamisha utekelezaji wa baadhi ya miradi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, na kupelekea kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi wanaodai fedha kiasi cha **Shilingi 48,678,511,274.44.**

8 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2025) k.h.a

(ii) Kukosekana kwa viwanda vya uhakika vya mazao ya mifugo pamoja na uvuvi nchini ikiwemo maziwa, ngozi, kwato, pembe pamoja na mazao ya baharini kunaathiri mchango wa Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwenye uchumi.

(iii) Vikwazo vinavyosababisha mazao ya mifugo na uvuvi yanayozalishwa nchini kukosa masoko nje ya nchi ikiwemo ubora wa bidhaa, vinahitaji kufanyiwa kazi.

(iv) Sera na Sheria za Sekta ya Mifugo na Uvuvi zilizopitwa, zinahitaji kufanyiwa mapitio na kuandikwa kwa lugha inayoeleweka kwa wafugaji na wavuvi pamoja na wadau wengine.

(v) Maabara muhimu kwa ajili ya Sekta za Mifugo na Uvuvi zinaupungufu wa vifaa vya kisasa na zisipowezeshwa kiteknolojia zinaweza kukosa ufanisi na tija katika maendeleo ya Sekta hizo.

(vi) Upungufu wa Maafisa Ugani katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, uhaba na ubora wa dawa za kudhibiti magonjwa kunaweza kusababisha mchango duni wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika uchumi wa Taifa.

(vii) Migogoro kati ya wafugaji na wakulima isipopatiwa ufumbuzi wa kudumu itaathiri mchango wa Sekta za Mifugo na kilimo katika uchumi, amani, maendeleo na ustawi wa jamii.

(viii) Kukosekana kwa Mamlaka za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni jambo linalochangia kuzorota kwa ufanisi wa Sekta hizo. Hali hiyo inapunguza mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika Pato la Taifa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** maoni hayo yanajenga msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

### 3.3 Ushauri wa Kamati kwa kila Kisekta

**Mheshimiwa Spika,** ili kubainisha hatua stahiki kwa Serikali, Kamati inatoa ushauri mahsusi kwa kila Sekta kama ifuatavyo:-

#### 3.3.1 Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mambo ya kuzingatiwa katika Sekta hii wakati wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2026/2027 Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali itatue changamoto ya uhaba na ufanisi mdogo wa viwanda vya kuchakata maziwa nchini ikiwemo changamoto ya kodi na tozo.

(ii) Serikali iajiri Maafisa Ugani wa kutosha pamoja na kusambaza madawa ya mifugo hasa maeneo yenye idadi kubwa ya mifugo nchini. Hatua hii itatatua changamoto ya wafugaji wengi kukosa elimu sahihi ya ufugaji wa kisasa na uhaba wenda za kudhibiti magonjwa ya mifugo.

(iii) Ili kupunguza magonjwa na vifo vya mifugo nchini, Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa chanjo na kuwezesha uhakika wa upatikanaji wa chanjo katika maeneo yote yenye mifugo nchini yakiwemo maeneo ya pembezoni.

(iv) Serikali ikamilishe utekelezaji wa Sheria iliyotungwa na Bunge Sura ya 184 kuhusu utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo. Hatua hii itadhibiti magonjwa, wizi na migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

(v) Serikali iandae mpango wa kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kuchakata wenda a kupunguza usafirishaji wa mifugo hai wenda nje ya nchi.

(vi) Ili kuwezesha Sekta ya Mifugo kuchangia katika mapato nchini, Serikali ihakikishe kuwa inaweka

mikakati ya kudhibiti utoroshaji wa mifugo sambamba na kufanya mapitio ya ushuru na tozo mbalimbali zinazotozwa kwa mifugo.

(vii) Kwa kutumia bajeti ya Sekta ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ifanye mapitio ya Sera na Sheria zilizopitwa na wakati kama vile Sheria ya Mifugo ya Mwaka 2003 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006

(viii) Serikali iendelee na juhudi za kuzuia, kudhibiti na kumaliza kabisa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kuimarisha usimamizi na uratibu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

(ix) Serikali ilipe madai ya wakandarasi na wazabuni yaliyowasilishwa Hazina yenye jumla ya Shilingi 48,678,511,274.44 ili kuendelea kutekeleza kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo na ujenzi wa miundombinu ya mifugo.

### 3.3.2 Sekta ya Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa Sekta ya Uvuvi katika uchumi wa nchi, Serikali itakapotekeleza Bajeti ya Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 izingatie ushauri ufuatao:-

(i) Serikali itoe elimu kwa wavuvi kuhusu madhara ya uvuvi haramu ambao unaathiri mazalia ya samaki na kuchangia uhaba wa samaki nchini. Aidha, Serikali isimamie uvuvi endelevu na uzingatiaji wa sheria zinazosimamia shughuli zote za uvuvi na uhifadhi wa mazingira.

(ii) Serikali ikamilishe ununuzi wa meli mbili zitakayowezesha kuvua eneo la Bahari Kuu kama ilivyoelekezwa na ilani ya CCM ya mwaka 2025. Hatua hii itaongeza upatikanaji wa mazao yatokanayo na uvuvi kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi pamoja na kuongeza mauzo nje ya nchi.

(iii) Serikali iendeleze mpango wa ujenzi wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji katika Halmashauri za Wilaya ili kusogeza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wananchi katika maeneo hayo;

(iv) Serikali ianzishe programu maalumu ya kupandikiza na kujazilia samaki walio katika hatari ya kutoweka kwa lengo la kuendeleza zao la samaki kama nyenzo ya uchumi na lishe.

(v) Serikali iwezeshe upatikanaji wa mitaji, mikopo na vifaa kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji, vyama vya ushirika na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za kifedha ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa njia ya kisasa na kibiashara;

(vi) Serikali iwajengee wavuvi wazalendo uwezo wa kufanya uvuvi wa kisasa kwa kuwapatia mafunzo na nyenzo;

(vii) Serikali ihamasishe sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ikiwemo uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki na chakula ili kupunguza gharama za uzalishaji; na

(viii) Serikali ipunguze au kuondoa tozo kwa bidhaa za uvuvi zinazoingizwa nchini ili kuwawezesha wavuvi wadodo wadogo kumudu gharama za ununuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanyie kazi na kutekeleza ushauri wote uliotolewa. Dira ya Wizara kuwa na Sekta ya Mifugo na Uvuvi iliyoendelea na yenye hadhi ya Kimataifa, ambayo ni endelevu kiuchumi, kijamii na kimazingira itakuwa na uhalisia. Aidha, Wizara itaweza kukuza, kuwezesha na kudhibiti maendeleo ya kisasa ya mifugo, uvuvi, ukuzaji viumbe maji na mazao yake kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linategemewa kutoa ushauri stahiki kwa Serikali. Aidha, bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu inatarajiwa kutekelezwa kwa namna inavyokusudiwa na Bunge lenyewe. Kamati hii imefanya kazi ya uchambuzi wa makadirio ya mapato ya Wizara hii kwa lengo la kulisaidia Bunge kufanya uamuzi kwa maslahi ya umma. Uchambuzi uliofanywa, maoni na ushauri uliotolewa unastahili kuzingatiwa wakati wa mjadala kuhusu hoja inayojadiliwa.

### 4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao, natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika – Mwenyekiti
2. Mhe. Mariamu Ditopile Mzuzuri - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete
4. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi
5. Mhe. Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo
6. Mhe. Khadija Hassani Aboud
7. Mhe. Tauhida Galos Cassian
8. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani
9. Mhe. Omar Marcus Msigwa
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo
12. Mhe. Rita Enespher Kabati
13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel

15. Mhe. Abubakar Alli Omari
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, ndc
17. Mhe. Khalfan Issa Mohamed
18. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi
19. Mhe. Khamis Hamad Yussuf
20. Mhe. Amour Seif Abdalla
21. Mhe. Khalid Mussa Nsekela
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete
23. Mhe. Salum Khamis Salum

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Dkt. Bashiru Kakurwa (Mb) na Naibu Waziri - Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani (Mb), kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Katibu Mkuu - Ndugu Agnes Kisaka Meena, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha **2026/2027,** kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**Deodatus Phillip Mwanyika, Mb**
**MWENYEKITI WAKAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
**14 Mei, 2026**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa uwasilishaji wa taarifa hiyo ya Kamati…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Kiti, hapa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sawa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwatambue wageni waliopo Bungeni ambao ni Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Yupo Mheshimiwa Dkt. Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula; yupo Ndugu Agnes Kisaka, Katibu Mkuu; Ndugu Fabian Magawa, Naibu Katibu Mkuu - Mifugo; Profesa Mohamed Sheikh, Naibu Mkuu - Uvuvi; Ndugu Mark Tsoxo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo; Prof. Lughano Kusiluka, Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari Tanzania; Prof. Amandus Muhairwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Mahabara ya Veterinari Tanzania; Dkt. Blandina Lugendo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi; Dkt. Boniventure Baya, Mwenyekiti wa Bodi ya Hifadhi ya Bandari na Maeneo Tengefu. *(Makofi)*

Vilevile, yupo Dkt. Florens Turuka, Katibu Mtendaji Ofisi ya Rais, Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Ndugu Geodfrey Kirenga, Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Ndugu Andrew Massawe, Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Dkt. Jackline Mkindi, Mjumbe wa Sekretarieti wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Dkt. Mwatima Juma, Mjumbe wa Sekretarieti wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Ndugu Essau Mbegete, Mjumbe wa Sekretarieti wa Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo. *(Makofi)*

Pia, Ndugu Stephano Mgani, Meneja Mshauri wa Kiufundi Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Chakula na Kilimo; Dkt. Charles Tizeba, Waziri Mstaafu wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu Mstaafu Wizara ya Mifugo na Uvuvi na

Mjumbe wa Shirika la *Action for Ocean;* Mheshimiwa Meck Sadick, Mkuu wa Mkoa Mstaafu na Mkurugenzi Mkuu wa Sameki *Limited*; Ndugu William Sarakikya, Mjumbe Mstaafu wa Halmashauri Mkuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa; Ndugu Mathayo Mgusa, Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania; Prof. Raphael Chibunda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine. *(Makofi)*

Vilevile, yupo Prof. Anthony Sangeda, Mkuu wa Idara ya Sayansi za Wanyama, Ufugani Viumbe Maji na Malishi, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine; Prof. Ismail Selemani, Mwenyekiti wa Chama cha Nyanda za Malisho Tanzania; Meja Lutengano Hezron, Kaimu Mkuu Kikosi cha Chita JKT; Ndugu Faud Jaffer, Mkurugenzi Mkuu *ASAS Diaries Limited*; Ndugu Frank Nyabudege, Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Kilimo Tanzania; Nsolo Mlozi, Mkuu wa Kitengo cha Kilimo, Biashara Benki ya *NMB;* na Ndugu Godfrey Ng'urah, Mkurugenzi Mkuu Benki ya Ushirika, karibuni sana Wageni wetu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, ninaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa maonyesho kuhusu Shughuli za Uhifadhi na Utalii zinazotekelezwa na Idara na Taasisi zake.

Waheshimiwa Wabunge, maonyesho haya yatafanyika kuanzia tarehe 15 hadi 18 Mei, 2026 katika viwanja vya maonyesho karibu na Zahanati ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kutembelea maonyesho hayo ili muwe Mabalozi wa Hifadhi Endelevu na Utangazi wa Utalii Nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Musukuma, nilikuona.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba mwongozo wako kuhusiana na jambo lilitokea leo asubuhi. Bunge ni chombo kinachoangaliwa na Watanzania wengi, na ni chombo muhimu sana kwenye Taifa

letu, lakini tumekuwa na matatizo mara kwa mara toka Bunge hili tumeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge Awamu ya Tatu toka tumeingia Bungeni kumekuwa na matatizo mengi sana kuhusiana na visemeo. Kila siku tukiwa hata na Wageni kutoka nchi za nje kwenye michango, kwenye Bajeti kama hii mara inagoma kwa Mwenyekiti, inagoma Spika, inagoma kwa Mjumbe tunasubiri na Watanzania wanaona sisi ndio watu tunaoweza kusimamia viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na haya matatizo, na wewe ni shahidi na hata jana tu umeona kumetokea matatizo, tumepigiwa *alarm*. Sasa tuna taharuki hata kuingia ukumbini sasa tunaogopa. Nilitaka kupata mwongozo kama visemeo hivi vina matatizo, kwa nini tusivirudishe vile vya zamani ili tuendelee na Bunge letu la viwango, kuliko kila siku watu wanaangalia Kimataifa mara *mic* inazima, mara inawaka? Nilikuwa nataka kupata mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia mitandaoni tumekuja ukumbi wa zamani kabisa, hata Mzee Pinda nimesikia yupo humu na yeye hakukaa kwenye ukumbi huu, aliukuta. Sasa nilitaka kupata mwongozo wako ni lini ukumbi wetu utasimama kwa viwango vile tulivyovizoea sisi Wabunge wa zamani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mwongozo wako. Mheshimiwa Musukuma pamoja na Waheshimiwa Wabunge suala hili lilishatolewa ufafanuzi wa kina na Mheshimiwa Spika asubuhi, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wachangiaji wa siku hii ya leo na hapa tuna wachangiaji wengi na muda wetu siyo rafiki, tutatumia dakika sita. Tunao wachangiaji takribani 30, hivyo baadaye pia tutaongeza muda kidogo kwa ajili ya kupunguza idadi hii ya wachangiaji kabla hatujaendelea jioni. Nitamtaja Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, ajiandae Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa. *(Makofi)*

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii nikiwa wa kwanza kabisa. Kwanza kabisa, ninaomba nimpomngeze Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake na jitihada za makusudi za kuweza kuinua sekta hii ya mifugo na uvuvi kwa sababu tumeshuhudia tarehe 25 Aprili akizindua Meli ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki ni historia kwa Tanzania, lakini inaonesha kabisa kwamba ni jinsi gani Mheshimiwa Rais ana maono na maslahi mapana katika Uchumi wa Buluu. Kwa kuwa tumezoea kumiliki Bahari, lakini sasa ni dhahiri kwamba tunamiliki Bahari, na pia tunamiliki na uchumi wa bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika jitihada za makusudi kuweza kuona tunapata mabadiliko makubwa na chanya katika uvuvi na ufugaji, lakini tunatambua kwamba, wafugaji na wavuvi ni jamii kubwa sana ambayo imepiga kura za kutosha kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na kazi kubwa inayofanyika, bado tunaona kuna changamoto nyingi sana zinawakumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hoja nzuri, lakini sijasikia kitu cha kumtambua mfugaji kama mwekezaji. Wameonesha jitihada za kutambua mifugo, jitihada za kampeni za kufanya chanjo, lakini hoja yangu sijaisikia, ya kumtambua mfugaji kama mwekezaji. Hapa ninataka kusema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, ni muda muafaka sasa mfugaji atambulike kama mwekezaji katika nchi yake kwa sababu, tunajua ufugaji unagusa zaidi ya 33% ya ajira za Watanzania. Tunajua kuna wafugaji wakubwa sana ambao wana uwezo, wana vitalu, wana leseni, lakini wafugaji hao hawawezi kufika hata taasisi za kibenki kupata mikopo kwa kutumia vile vibali vyao au leseni kama *collateral* ya kupata mikopo. Kwa hiyo, ni muda muafaka, kama Wizara kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema kwamba, Wizara zina haja ya kushirikiana. Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi wakae na Wizara ya Viwanda na Biashara waone jinsi gani ya kushirikiana na taasisi za kifedha kumtambua huyu mfugaji kwamba, sasa kwa sababu ana leseni na kibali cha miaka 20 na ana kitalu kina ng'ombe wa kutosha, itumike ile kama dhamana ya yeye kukopa na kujiendeleza kwenye ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni changamoto ambayo wanakutana nayo wafugaji. Wafugaji kwa sasa kuna hili jambo la wachimba madini, wanaingia kwenye sehemu za ufugaji kwa sababu, wameambiwa kuna madini. Wanachimba kwa ajili ya kupata madini, wanaacha mashimo makubwa. Sisi Kyerwa tuna ng'ombe takribani 80,000 lakini kwa sasa hivi tumeingiliwa na watu wa kuchimba madini aina ya *tin*. Wanaacha mashimo makubwa, kitu ambacho kinaanza kusababisha ng'ombe wengi kufariki, hii ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, ninatoa rai kwa Wizara kwamba, wakae washirikiane na Wizara hii ya Nishati kuona ni jinsi gani wataweza kuokoa hili janga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninaenda kwenye uvuvi kwa sababu ya muda, hatuwezi kuongea vingi sana, lakini uvuvi tumeona jitihada zimefanyika. Mheshimiwa Rais anafanya jitihada kubwa sana. Ninachoweza kusema kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba, ni wakati muafaka sasa kuwekeza fedha nyingi za Serikali kwenye kupanua na kuendeleza hii Sekta ya Uvuvi. Kuna haja sasa Wizara iweke nguvu nyingi sana katika kupambana na changamoto ya uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni janga kubwa sana kwa uvuvi. Tunatambua bado wapo watu wanavua kwa kutumia baruti, bado wapo wavuvi wanatumia sumu, bado wapo wengine wanatumia nyavu zile ndogo kwa kuvua samaki wachanga. Hili ni janga kubwa. Wakati Serikali inaweka nguvu kubwa kuendeleza hii sekta, huku tunaingiziwa watu wanaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara kwa kuongozwa na Mheshimiwa Waziri, na ninampongeza kwa hilo, kokoro ambalo nimelikamata kwenye Ziwa Tanganyika, bado katika

vyanzo vyote vya wavuvi kuna haja ya kufanya kazi kubwa kuweza kuona huu uvuvi haramu unakabiliwa na unazuiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Kamati imetoa maelekezo; wakati tumetembelea *TAFICO* tumekuta pale kuna magari matatu ya *cold chain* kwa ajili ya kusafirisha samaki. Magari hayo yamekaa muda mrefu sana. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati anamaliza atuelezee kama magari hayo tayari yameanza kufanya kazi, kwa sababu, zile ni fedha za Serikali zimewekwa pale. Magari yanavyozidi kukaa pale chini, maana yake yanaanza kuharibika. Kwa hiyo, tunaomba, magari hayo yamenunuliwa, na ni fedha ya Serikali, yaanze kufanya kazi, tuone tija katika hilo suala la uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa kutambua umuhimu mkubwa wa wavuvi na ufugaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kengele itakuwa inagongwa mara moja peke yake. Ninaomba sana tuzingatie muda kwa sababu ya idadi ya wachangiaji tulionao.

Sasa namwita Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia, lakini vilevile ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa wafugaji. Mnajua katika kampeni ufugaji ilikuwa ni ajenda moja kubwa sana, ambayo ameizungumzia kwa upana, lakini hata kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, kwa miaka mitano inayokuja inasema kwamba, wataongeza malisho

kutoka ekari milioni 3.4 mpaka milioni sit ana vilevile, itakuwa imetoa ruzuku kwenye chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sisi watu wa Bariadi huko tumebahatika kuwa katika ufunguzi wa chanjo, ulifanyikia Bariadi. Kwa hiyo, kuna juhudi kubwa sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hali ya kutengeneza miundobinu ya wafugaji kwetu, kwa Bariadi vijijini kuna ujenzi wa mabwawa kule na kuna majosho. Kwa hiyo, unaweza ukaona juhudi na mtazamo wa Serikali kuona kwamba, wafugaji kuna *transformation* kubwa. Nina-*declare interest,* vilevile mimi ni mfugaji wa Samaki. Kwa hiyo, ni *area* ambayo kidogo ninaweza nikaizungumzia kwa ufasaha kwa sababu, nimo ndani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wanafanya kazi nzuri sana kwa kweli, mara nyingi unakuta hawakai. *Set up* ya Wizara hii kwa kweli, Mheshimiwa Dkt. Bashiru tukimwona amekaa tutakuwa na mashaka sana kwa sababu, ni Wizara ya kutembea. Pia, ninamshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa nzuri sana aliyoitoa. Ninaamini imetuongezea maeneo ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sekta ya Mifugo ni muhimu sana katika Taifa letu. Ukiangalia dira yetu katika ukurasa wa 58, nitasoma kidogo, zimetajwa sekta zenye fursa ya mageuzi kuelekea 2050. Inasema, *"Sekta ya Mifugo itaboresha kwa kuwekeza,"* ni muhimu sana ku-*underline* neno *"kuwekeza katika uzalishaji wa kisasa"* neno *"kisasa"; "...wa bidhaa zinazotokana na mifugo kwa kuongeza tija na thamani, ili kukidhi mahitaji ya masoko ya ndani na nje. Sekta ya Uvuvi itaimarishwa kwa kuendeleza uvuvi na ufugaji wa Samaki"*, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *obvious* kwamba, Sekta ya Mifugo na Uvuvi imewekwa chini ya Sekta ya Kilimo, lakini ni muhimu sana tunapofikiria kwamba, baada ya miaka 25 tuwe na huo uchumi wa *one trillion*, Sekta ya Mifugo ina *contribution* kubwa sana. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, pamoja na kazi kubwa ambayo mnaifanya sasa hivi ya kuleta mageuzi, tunahitaji *transformation* kubwa sana kwenye Sekta ya Mifugo. Unapozungumzia mifugo na uvuvi, maana yake ni kwamba unazungumzia ardhi kwa sababu, lazima utafuga kwenye ardhi. Unazungumzia malisho, unazungumzia maji, kwa hiyo, *transformation* kubwa pamoja na *technology;* ina-*revolve* katika hivyo vitu ambavyo tunavitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *mindset* ambalo tunazungumzia kwa kufanya *transformation* kutoka kwenye ufugaji ambao tunao sasa hivi kwenda huko tunakokutaka. Sasa, *mindset* siyo kitu ambacho ni kirahisi na kwa Wizara. Ushauri wangu ni kwamba, wajiwekee muda. Ni muhimu sana wanapokuwa wana-*deal* na hili jambo wawe na mashamba darasa, kama Mheshimiwa Waziri ulivyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba darasa haya hatuwezi kuwa wafugaji wote, kuwepo na *focus*. Mnaweza kuwepo na maeneo ambayo pengine yanastahili sana kwa ufugaji wa ng'ombe wa nyama au kuna sehemu nyingine wanaweza wakastahili, kwa ajili ya maziwa. Isiwe kila sehemu tunafanya hicho hicho. Kuwepo na *focus* na *persistence* kwa sababu, hili jambo linahitaji muda kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nigusie kwenye uvuvi. Kwa sababu ya muda wenyewe ni mdogo, lakini katika uvuvi kitu ambacho ninakiona ni suala la utafiti, kuwa na mbegu bora; na hili ni hata kwenye mifugo. Suala la utafiti ninafikiri bado tunahitaji uwekezaji mkubwa katika upatikanaji wa mbegu. Leo hii mtu anayetaka kufuga samaki kwenye *cages* zile, ukitaka tuseme labda vifaranga 200,000, Mzee Sariki yuko hapa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa zamani; huwezi ukapata lazima uende nchi ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninajua muda hautoshi, lakini ninaunga mkono hoja. Mengine bahati nzuri *Doktor* tunazungumza na ni *schoolmate* Wangu, nitazungumzanaye *face by face*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, ajiandae Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kwa sababu, muda ni mfupi ninachukua fursa hii kuipongeza Wizara na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Sekta au Wizara ya Uvuvi, Mifugo na Kilimo ni kati ya sekta ambazo tunapoongea uchumi jumuishi ndiyo zinajumuisha vijana wengi, akinamama wengi na Watanzania wengi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali yangu kwa juhudi ambazo imezifanya, hasa ununuzi wa meli kubwa ya uvuvi. Ninadhani hapa tunakwenda kwenye uchumi ambao tumeukosa kwa muda mrefu. Nilikuwa ninaangalia takwimu hapa, ambazo zimetoka kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wanasema Tanzania tunazalisha *almost* tani 500,000 za samaki kutoka baharini. Kwenye maziwa, tuna *almost* tani 400,000; bahari kuu na kwenye mabwawa. Nimeangalia mahitaji ya samaki Tanzania, tunahitaji zaidi ya tani milioni moja. Kwa hiyo, tuna upungufu wa kitoweo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Dkt. Bashiru, ameanza vizuri kazi. Alipoanza alitutembelea Kagera, alikuja pale tukakaa na wavuvi tukasikiliza matatizo yao; amekaa na wafugaji akasikiliza matatizo yao. Ninadhani kilio cha wavuvi alikisikia Mheshimiwa Waziri, hasa tunapoongelea Wilaya ya Muleba. Wilaya ya Muleba ina ukubwa wa *square metre* 10,000, lakini 7,000 ni maji. Kwa hiyo, tunaishi kwenye maji sisi. Wilaya ya Muleba mapato yetu makubwa yanatokana na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri wakati anasoma hotuba yake ameongelea uanzishwaji wa mamlaka ya uvuvi. Ninadhani Mheshimiwa Waziri akilitekeleza hili, kwanza mazao na mapato uvuvi yatapanda na tutapunguza tatizo tulilonalo la vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema, kama nilivyoanza, kwamba hizi ni sekta zinazoakisi uchumi jumuishi ambao

unahusisha watu wengi na vijana wengi. Kwa hili ninaomba tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri, tuanzishe hii mamlaka ya uvuvi ikadhibiti tatizo kubwa la uvuvi haramu linaloendelea katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuishi karibu na ziwa, samaki ni tatizo. Ni tatizo, siyo kwamba watu hawavui, siyo kwamba watu hawana mitaji, mitaji wanayo na wanaingia ziwani, lakini hakuna samaki. Ninaomba tukadhibiti hili, ili tuokoe maziwa yetu kwa vizazi vingine. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, vijana wa Muleba wamenituma, wameniambia jana, na leo wanashukuru. Wamewapatiwa vizimba na wanaendelea kuzalisha na kufuga samaki pale, lakini tatizo kubwa walilonalo Wilaya ya Muleba, vijana hawana chakula cha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapaswa kufuata chakula kutoka Mwanza. Vile vifaranga walivyowapatia tunashukuru, lakini vingine vinaanza kupotea na kufa kwa sababu, ya kukosa chakula. Ninaomba hili sasa tuliangalie na kwenye mipango yetu tujenge kiwanda cha chakula cha samaki Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, Mheshimiwa Waziri, alipokuja Muleba, watu walitoa kilio chao na akawapatia mwezi mmoja kutoa suluhu ya kilio chao. Ninatumaini atakuwa amelifanyia kazi. Ameongea kwamba Ziwa Ikimba wataanza kuvua Samaki. Tatizo tulilonalo Ziwa Burigi, tulipoongelea sera, dira, *Mkumbi II*, 2025 – 2050, tuliongelea Sekta Binafsi. Mialo ya Ziwa Burigi, ninasisitiza kwa umakini mkubwa zaidi, mialo iliyokuwa pale ilifungwa na Serikali. Tunaomba kama ziwa kazi yake ni kuvua samaki, sasa tunafunga mialo tunategemea kufanya nini na hilo ziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wananchi ambao wanazunguka Ziwa Burigi wapatiwe fursa ya kuendelea kuvua samaki na kuchochea maendeleo ya familia zao, kukuza uchumi wao na uchumi wa Taifa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kumalizia hotuba yake atuambie nini hatima ya mialo ya Ziwa Burigi iliyofungwa, na tunakwenda kuifungua lini, ili ziwa liwe na maana? Ni maji pamoja na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ufugaji, Kagera tuna vitalu zaidi. *Ranch* za Taifa ni zaidi ya nusu, lakini Mheshimiwa Waziri alikutana na wafugaji. Ninaiomba Serikali iwekeze zaidi, ndugu yangu, Mheshimiwa Nsekela amesema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja mkono. Nitaomba maelezo jinsi ya ufunguaji wa mialo ya Ziwa Burigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel. Ajiandae Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nimesikiliza hotuba yake kwa makini nimeona kwamba, ana mwelekeo mzuri sana ambao ataufanya na utaleta matumaini makubwa sana kwa wafugaji wetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ameanza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dunia ijayo maeneo ambayo yatakuwa na biashara kubwa, namba moja ni eneo la *IT*, namba mbili ni eneo la chakula, na namba tatu ni eneo la tiba. Wizara hii inaenda kuangukia kwenye eneo la chakula. Kama inakwenda kuangukia kwenye eneo la chakula, ni eneo ambalo linatakiwa pia Serikali ijiwekeze vizuri na iwe makini sana inapokuwa inatunza yale maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu mifano michache. Nimemtazama juzi Waziri wetu, kaka yetu, Mheshimiwa Dkt. Bashiru wakati Mheshimiwa Mchengerwa anawasilisha bajeti yake na akisisitiza kuhusu ujenzi wa Muhimbili, wakati anasisitiza kuhusu ujenzi wa Muhimbili, anasema sisi ni wajamaa. Niliposikia lile neno

wajamaa, nikamwona Waziri Mheshimiwa Dkt. Bashiru akipiga makofi na kufurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, Muhimbili yake ni mashamba makubwa ya mifugo kwenye nchi hii. Muhimbili yake ni *NARCO*, Muhimbili yake ni Mashamba ya *TALIRI*, Muhimbili yake ni kila eneo ambalo kuna ardhi kubwa, ambayo ina uwezo wa kuzalisha mifugo na mambo mengine. Ni maeneo ambayo anatakiwa aende kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TALIRI*. Watu wa Siha wamenituma, wameniambia *"ukitusemea, sema Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI amekuwa ni mtu mzuri sana kwa wafugaji wa Wilaya ya Siha na Wilaya ya Longido. Ni mtu ambaye amekuwa anamaliza migogoro vizuri na kuwatengenezea wafugaji wetu mazingira mazuri."* Ninaomba mumpigie makofi ya kutosha mkurugenzi huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu kuna Shamba la *NARCO*. Ninaishukuru Wizara ya Mifugo, huko nyuma iliona lile eneo ambalo halitumiki na *NARCO* na *TALIRI* wawekezewe wafugaji wetu wadogo. Tulifanya hivyo, ikaondoa moja kwa moja migogoro ya wafugaji na wakulima, lakini imekuja hapa karibuni anatakiwa kuwekezewa mfugaji mmoja kule *NARCO,* anayeitwa Akram. Ushauri Wangu kwa Mheshimiwa Waziri, hatumpingi, mfugaji yule anayetaka kuwekeza, ni wa kwetu, lakini wafugaji hao wadogo ni wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri, asipewe *NARCO* yote kwa sababu, kwa Kilimanjaro ambayo ardhi ni ndogo sana na hakuna maeneo ya wazi, ukimpa tu *NARCO* yote ukaondoa lile eneo ambalo Serikali ilikuwa imewapa wafugaji wetu, ina maana ume-*deny* wafugaji zaidi ya 3,000 wasifuge, wauze ng'ombe wakae nyumbani na hawatakuwa tena na mifugo kwa sababu, wewe kazi yako ni kuwaangalia wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu, naomba na Mheshimiwa Waziri amesema anakuja, aje Siha, aende Longido, awasikilize wafugaji, tukae tuangalie tuone busara ya pamoja bila

kumuumiza mwekezaji anayetakiwa kuwekeza pale, lakini bila kuwaumiza na hawa wafugaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine, hili ni eneo la hela. Nirudi tu pale kwenye afya. Ukiangalia madaktari wetu wanafurahi sana kufanya zile kazi. Ukienda Muhimbili na *investment* kwenye hospitali zetu za mikoa, asilimia kubwa uwekezaji unaofanyika ndani ya hospitali wanazalisha wenyewe madaktari wetu na wanajipa *incentive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwenye haya mashamba makubwa na kwenye hizi ardhi zetu kubwa tuwekeze ndani yake kwa njia namba moja. Kwa mfano, *TALIRI* ambao kazi yao ni utafiti, ni kwa nini tusifanye kazi kubwa ya kuongea na vyuo vikuu vikubwa na taasisi kubwa za vyuo vikuu, ndani ya zile taasisi pakawekwa *research* kubwa ya kufanya mifugo na wakashirikiana kufanya utafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, moja, itatusaidia kujua mambo mengi. Itaboresha mifungo yetu, na pia itaongeza *incentive* kwa wataalam wetu ambao wapo sasa. Nikiwaangalia ninaona, ukiondoa mshahara, hakuna namna nyingine wanayopata kama *incentive*. Kwa hiyo, tukitengeneze namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pale kwetu Siha kuna shamba la *TALIRI* na shamba la *NARCO*. Tukisema pale *TALIRI* wanafanya utafiti halafu *NARCO* wanazalisha ng'ombe bora, halafu ndani ya *NARCO* wanatengeneza kiwanda, na kile kiwanda kinakuwa kinauza nje; na ukienda pale kwenye shamba la *TALIRI* mpaka kuna *stripe* ya kushuka ndege ndogo, maana yake ukiweka kiwanda pale, na vitu vingine wanaweza wakazalisha na faida inayopatikana, itaendelea kuboresha vituo vyetu vya mifugo, na kuongeza *incentive* kwa wataalam wetu Maprofesa ambao wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inauma sana ukimwona Profesa na mazingira yake anapofanyia kazi, haiendani na ukubwa wa elimu aliyonayo. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, moja ya kazi ambayo anataka afanye, na ninataka tu kukambia kwamba

Serikali imefanya kazi kubwa sana, lakini mfano mzuri ni upande huu wa afya ambayo imefanyika. Serikali haijaongeza hela yoyote ya *incentive*. Imetengeneza mazingira ya wataalam kuzalisha wenyewe humo humo, fedha hizo zikasaidia Serikali na fedha hizo zikasaidia wataalam kufanya vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri Siha, na ninaomba tukafanye vizuri kwa maana ya uzalendo na ujamaa tukauone kwa wakulima wetu. Twende tuwasimamie wawekezaji, lakini pamoja na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja mkuu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, ajiandae Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, ajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri Ally.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza nimpongeze sana Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa namna ambavyo Wizara hii ameibeba kama agenda binafsi katika kuleta mabadiliko makubwa. Kwa ufanisi huo ambao tunauona na namna ambavyo ameweka jitihada kubwa, inaleta matumaini kwamba Wizara hii inaenda kupata mabadiliko makubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nollo, ninaomba ujaribu kipaza sauti kingine cha pembeni yako.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuchangia masuala matatu. Moja ni suala la kuchanja mifugo; pili, ni suala la kuweka hereni kwenye mifugo yetu; na tatu, ni suala zima la malisho kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kuweka herein, jambo hili ni muhimu sana, kwanza linatupa utambuzi wa kujua tunayo mifugo kiasi gani? Pili, lina faida muhimu sana kwamba

tutaweza kuwa na takwimu ya kila mfugo. Nchi ya Botswana wamefanikiwa katika suala la utambuzi wa mifugo yao. Kwa hiyo, mfugo anapozaliwa anapewa ile *electronic tag*, taarifa zake zinakuwa kwenye ile *tag,* lakini katika masoko ndani ya nchi yao *local market* huwezi ukauza kama ule mfugo hauna ile *ear tag*. Vilevile, inawapa wafugaji utajiri, kwamba wanakuwa wanajua miliki waliyonayo ya mifugo kama *inventory*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili anaweza akakopesheka benki, na anaweza akaweka *insurance* ya mifugo yake. Vilevile nchi ya Botswana wamefika mbali kwa sababu ya utambuzi wa mifugo na pamoja na kuchanja mifugo yao, sasa wana uwezo wa kuuza. Kwa mfano, wanauza sana nchi ya Ujerumani kwa sababu *traceability* ya mifugo yao inaonekana katika hali nzima ya kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo wameweka jitihada kubwa katika suala zima la chanjo ya mifugo. Sasa nguvu ifanyike kulipa zile shilingi bilioni 8.6 kwa wale wakandarasi wanaodai. Jambo hili ni zuri na Serikali ifanye na ripoti ya Waziri inaonesha kwamba kiwango cha uuzaji wa nyama nje ya nchi umeongezeka kwa sababu ya utambuzi wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine huwezi ukawauzia nyama ya mifugo ambayo haina *address*. Kwa hiyo, lazima muwe mna-*address*, lazima huo mfugo ujulikane matunzo yake na mambo mengine ikiwepo katika hali nzima ya kuchanja mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni suala la malisho. Bado mifugo yetu na wafugaji wetu tunafuga kwa kubahatisha. Nchi nyingi kwa mfano Zimbabwe, ulimaji wa malisho ya mifugo imekuwa ni utamaduni, na siyo jambo la Serikali kuwekeza kulima malisho ya mifugo. Hili tulibadilishe, iwe ni *culture* kwa ajili ya wafugaji wetu. Uwe ni utamaduni wa nchi hii, tulime malisho kwa ajili ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kuchunga, kwamba unatoka Shinyanga unapeleka ng'ombe mpaka Lindi, wanachunga njiani mpaka unashangaa umefika Lindi, hii ni enzi nyingine kabisa. Kwa

hiyo, nilikuwa ninaomba sana suala la malisho Serikali ifanye kampeni ya kutosha ili tuweze kulima nyasi kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la majosho kwa maana ya miundombinu, tunahitaji miundombinu ya majosho, na miundombinu ya mabwawa kwa ajili ya kunywesha mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la *abattoir* (machinjio) kwa ajili ya mifugo. Kwa mfano, machijio ya hapa Dodoma, hatuwezi kusafirisha katika nchi karibu zote za Uarabuni, kwa sababu ya hali ya machinjio yale ilivyo. Ninaishukuru sana Serikali, Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri, ametoa maelekezo kwamba machinjio yale ya Kizota yaanze kufanyiwa ukarabati ili tuweze kupeleka nyama nje ya nchi. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tunaweza kuleta mapinduzi makubwa kwa wafugaji na sekta ya mifugo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, tujikite zaidi kuangalia uwekezaji. Mfugaji awe ni mwekezaji badala ya kuwa ni mtu ambaye umaskini wake na kiasi alichonacho cha ng'ombe haviendani kwa maisha anayoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 36(2) nitaongeza muda kidogo. Nilimtaja Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, ajiandae Mheshimiwa Sara Msafiri Ally.

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Lindi, hususan wakina mama, ninapenda kuipongeza Serikali

kwa uwekezaji mkubwa ambao umefanywa katika ujenzi wa bandari ya uvuvi, bandari ya Kilwa. Serikali ya Awamu ya Sita sasa hivi katika Mkoa wetu wa Lindi katika Wilaya ya Kilwa imejenga mradi wa bandari ambayo inahusiana na uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 280. Mradi huu hadi sasa umefikia 98% ya utekelezaji wake, na muda wowote Mheshimiwa Rais anatarajiwa kwenda kuuzindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Lindi tunashukuru sana na tunaiomba Serikali kupitia mradi huu, kuna miradi mingine midogo midogo ambayo inaenda kutekelezwa inayoambatana na mradi huu wa bandari ya uvuvi. Miradi hiyo ni pamoja na kiwanda cha kuchakata samaki, soko la kisasa la samaki, karakana za matengenezo kwa ajili ya miundombinu hii ambayo itatumika kwenye uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, mradi huu pia unahusiana na ujenzi wa ghala kwa ajili ya zao la mwani. Tunafahamu kwamba zao la mwani nchi hii lilikuwa lipo nyuma kidogo na wakulima ambao wanahusiana na zao la mwani mara nyingi wamekuwa wakikumbana na changamoto ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili linajumuisha wanawake wengi katika maandalizi yake, lakini pia wanawake wengi ndio wanajihusisha katika sekta ya uzalishaji wa zao la mwani. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kitendo cha kuleta hili ghala ambalo tunaenda kupeleka zao la mwani katika mfumo wa soko la Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kulipeleka hili zao katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani unaenda kuwahakikishia wakulima moja kwa moja uhakika wa soko na kuuza mazao yao hali ambayo inaenda kuinua kipato chao cha uchumi. Bandari hii pia tunatarajia kutoa ajira za moja kwa moja za vijana, wananchi 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Lindi, tunatarajia kunufaika na huu utekelezaji wa huu mradi moja kwa moja ambapo wananchi ambao wanahusika na zoezi la uvuvi wanatarajiwa kwenda kuwezesha kwenda kuvua katika bandari

kuu ambapo hapo awali kabla ya utekelezaji wa mradi huu haujatekelezwa wananchi walikuwa wanashindwa kufika kwenye yale maji makubwa, hivyo kushindwa kupata samaki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi huu wa bandari ya uvuvi tunakwenda kuboresha kipato cha Mtanzania moja kwa moja, kwa Mtanzania mmoja mmoja, pia kuinua zile familia ambazo zinahusika na shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Lindi wanaendelea na maandalizi ya kuhakikisha kwamba wananufaika na uwepo wa bandari hii na hawaishii tu kuwa watazamaji. Katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Lindi wananufaika, tarehe 12 mwezi wa Tano, Wilaya ya Kilwa imefanya kongamano kubwa la kuhamasisha wananchi kuwa tayari kutumia fursa ya uwekezaji katika bandari hii pale itakapoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, kwa sababu mradi huu unavipengele vingi, tuiombe Serikali kwamba muda utakapofika miradi hii itekelezwe kwa wakati, pia ikamilike ili kusudi zile gharama kubwa, hii shilingi bilioni 280 ambayo imeshatolewa na Serikali iende kuleta tija ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mifugo. Kwa asili wananchi wa Mkoa wa Lindi sisi siyo wafugaji, lakini Serikali kati ya mwaka 2015/2020 ilikuja na mpango wa kuwahamasisha wafugaji kutoka sehemu mbalimbali za nchi kuhamia Mkoa wa Lindi kwa sababu Mkoa wa Lindi ulikuwa na eneo kubwa ambalo lipo wazi kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wafugaji wale waliitikia wito na wamekuja kwa wingi. Hata hivyo, licha ya kwamba wafugaji wale wamekuja na kutuletea baraka ya uwepo wa chakula kama nyama na maziwa, tumekutana na changamoto ambayo sasa imeanza kuibuka, ya uwepo wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa baadhi ya maeneo, *almost* Wilaya zote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *almost* wilaya zote wananchi wanapambana. Hivyo ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja, atueleze mpango wa Serikali kuhakikisha wanapambana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, ajiandae Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliotangulia kwanza kutoa pongezi nyingi kupitia Wizara yetu hasa kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Menejimenti yote. Ninampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, walifanya ziara ndani ya Jimbo la Mvomero mara tu walivyoapishwa wakatembelea shughuli za ufugaji, tukaenda kwenye mashamba, tunashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mvomero hasa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka nguvu nyingi sana kwenye sekta hii hasa ya mifugo. Tunajua kwamba wananchi wa Jimbo la Mvomero, wakulima na wafugaji tulikuwa hatuwezi tukaelewana kabisa, migogoro hii ilikuwa mikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia historia kabla Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, tulikuwa tumejenga mpaka na mitaro mikubwa kwamba wakulima wakae huku, wafugaji wakae huku, tusichangamane lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,

aliona ipo haja ya kutumia falsafa yake ya *4R* tuweze kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzisha programu ya "Tutunzane" ambayo mlezi wetu mkubwa ni Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kwa kweli wananchi wa Mvomero tumejifunza mengi kutokea kwa Mheshimiwa Rais, kwamba siyo kila migogoro inatatuliwa kitaalamu tu. Mheshimiwa Dkt. Samia ametuonesha jinsi ya kukaa na viongozi wa dini, wazee wa kimila, machifu na mpaka sasa Programu ya Tutunzane imeleta matokeo makubwa hasa Jimbo la Mvomero. Wakulima na wafugaji kila mtu anafanya shughuli zake vizuri na kwa kuelewana. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni Chifu Hangaya. Ule usemi wa Chifu Hangaya tumeuona Mvomero. Ninaomba sana, Wizara tunajua imewekeza sana kwenye mifugo na tunaona kama nchi tunaongoza kwa Afrika, sisi tunayo mifugo mingi, ni namba mbili, lakini kipekee niipongeze Wizara kwamba sasa tupo kwenye *top ten* kwa wauzaji wa nyama kwa nchi zinazouza nyama hasa nje ya nchi. Sisi Tanzania ni *top ten* hasa kwa nchi za Saudi Arabia, Kuwait na nchi nyingine za Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kuona matokeo mazuri, na uwekezaji huu kimsingi tumeanza kupata matokeo kuanzia mwaka 2023 mpaka sasa. Kwa hiyo, hayo ni matokeo makubwa ya Mheshimiwa Rais na juhudi za Wizara katika kuinua sekta ya mifugo hasa kwenye ubora na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaomba nipongeze kwenye suala la chanjo ya Taifa ya mifugo na utambuzi wa mifugo. Kwa kweli hili limetusaidia sana hasa wafugaji. Wafugaji wamekuwa wakitumia madawa mengi yenye *chemical* nyingi kutibu mifugo, matokeo yake nyama inakosa ladha, gharama za matibabu ni kubwa na zinapunguza thamani ya mifugo, lakini kupitia chanjo hii ya mifugo na utambuzi wa mifugo, sasa hivi imepelekea sasa nyama inauzwa nje ya nchi na gharama zile za kutunza mifugo imepungua kwa sababu chanjo ile ina kinga magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze sana Wizara na nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa chanjo hii, na kwa Jimbo la Mvomero tumefanya vizuri. Haya ni matokeo mazuri sana katika kuongeza ubora wa nyama na uhakika wa masoko na wafugaji wamepunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililokuwa ninaomba ni upatikanaji wa mbegu za madume ya mifugo. Bado tunayo changamoto hiyo, na Wizara itusaidie. Sasa hivi ukitaka mbegu bora ya madume ni lazima ukanunue *South Africa* au uende Kenya. Tunaomba Wizara itengeneze utaratibu, ili hiyo mbegu bora ya mifugo ipatikane hapa nchini, ipunguze gharama. Unajua dume moja linafikia mpaka shilingi milioni 15, milioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile tunayo mifumo hii ya uwekezaji wa pamoja au ya *PPP* na tunayo maeneo makubwa ya *NARCO,* basi tuwatafute hao wanaoweza kutengeneza hizo mbegu bora wapewe nafasi waje wawekeze hapa ili mfugaji; na kuna vikundi mpaka vya wakina mama wanafuga, lakini hawana madume; kwa hiyo, kukiwa na sehemu ambapo upatikanaji wa madume haya yanapatikana kirahisi, basi tutaweza kuongeza tija katika ufugaji kwa wananchi wetu na kuongeza pato la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, itasaidia kuondoa ng'ombe wa kienyeji. Sasa hawa ng'ombe wa kienyeji hakuna aina ya ng'ombe wa kienyeji. Aina bora za ng'ombe majina yake yanafahamika na yanakuwa na historia yake, lakini sasa wafugaji wanachofanya, anaenda kwenye zizi la mwenzake akiona dume kubwa la ng'ombe yeye anafikiria hii ndiyo mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukifanya hivyo, ninaamini kabisa hii sekta ya mifugo itachangia pato la nchi na tutaweza kukomboa wananchi wetu kutoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mnada pale wa Mikongeni, uko pale Dakawa, ni mnada wa mifugo. Nimeona *presentation* nzuri sana, tuna bandari ya samaki, tunasema Kilwa *Fishing Harbour;* basi niwaombe lile Soko au Mnada wa Mikongeni uwe wa kimataifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako…

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba tutamalizia na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kwanza, kabisa ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejalia mchana huu tumekutana hapa Bungeni kwa ajili ya kuwakilisha wananchi ambao wametutuma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kuzifanya kwa kusimamia sekta hii ya mifugo kwa kuhakikisha inakuwa bora hapa nchini. Tatu, ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kuendelea kusimamia sekta hii ya mifugo na uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2025 idadi ya ng'ombe nchini kwetu ilikuwa ni 35,300,000; mbuzi ilikuwa 25,600,000; kondoo walikuwa 8,800,000; kuku walikuwa milioni 92,800,000; nguruwe walikuwa 3,800,000. Hii inaonyesha nini? Inaonesha kuwa Tanzania ina utajiri mkubwa wa mifugo Barani Afrika. Sekta hii ya mifugo na uvuvi inachangia pato la nchi yetu kwa asilimia 8.8. Asilimia saba inachangiwa na mifugo na asilimia 1.7 inachangiwa na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuchangia huku sekta hii imekuwa ikiongeza mapato na kuajiri mamilioni ya Watanzania mijini na vijijini. Ninatokea Wilaya ya Uyui, ambayo humo humo kunapatikana jimbo langu la Igalula, ambamo mimi pamoja na

wananchi wangu wa jimbo la Igalula tunaishi. Tuna idadi ya mifugo na tuna ng'ombe 400,000, tuna mbuzi 150,000. Japokuwa tuna mifugo hii bado tunakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo la Igalula bado tunakabiliwa na changamoto ya malisho ya mifugo. Wananchi wetu wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata malisho ya mifugo yao. Vilevile imekuwa ikisababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Ninaiomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine iendelee kutenga na kuongeza malisho kwa ajili ya mifugo yetu ndani ya Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakabiliwa pia na changamoto ya majosho, malambo, mabwawa na visima vya kunyweshea mifugo yetu. Wafugaji wetu wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata vyanzo vya maji. Hivyo, tunaiomba Wizara iwekeze kwenye mabwawa na visima virefu kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji wetu ili waweze kunywesha mifugo yao kwenye maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jimbo la Igalula kuna kata 11 na vijiji 58, lakini majosho hayazidi saba tu. Ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Mifugo itusaidie kutujengea majosho walau 20 ili kuweza kuwasaidia wafugaji wetu waweze kuchanja mifugo yao dhidi ya magonjwa ya kupe na magonjwa mbalimbali, ambayo yanapelekea wafugaji wetu kupata hasara kutokana na magonjwa haya, mifugo mingi inapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa sana ya watumishi. Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ina kata 30 lakini watumishi waliopo pale ni watumishi 10 tu. Tunafahamu kwamba sekta hii ili iweze kwenda inatakiwa elimu kwa wafugaji wetu na inatakiwa zifanyike tafiti mbalimbali kwa ajili ya hawa wafugaji wetu. Sisi tuna watumishi 10 tu ndani ya kata 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ituongezee watumishi ndani ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Uyui, kusudi sasa hawa watumishi watakapokuja kwenye halmashauri zetu waweze kutoa elimu ya

namna ya ufugaji bora kwa wafugaji wetu na namna bora ya kutumia ardhi kwa ajili ya kulisha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa sana ya mikopo kati ya wafugaji na wavuvi. Masharti yaliyowekwa kwenye mikopo wafugaji wengi na wavuvi wengi wanashindwa kunufaika na masharti haya. Mfugaji anaambiwa ili aweze kukopesheka anaambiwa awe na nyumba ya *block*, mvuvi naye anaambiwa awe na nyumba ya *block*. Sisi sote tunawafahamu wafugaji wetu, kwamba wengi wanaishi kwenye nyumba za tope na wanaishi kwenye nyumba za nyasi. Kwa hiyo wanashindwa kuifikia fursa hii ambayo Mheshimiwa Rais ameiweka kusudi wafugaji wengi waendelee kunufaika na fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi waweze kupunguza masharti ili wafugaji wetu na wavuvi wetu waweze kunufaika na mikopo hii. Tunawaona wavuvi wangu wa Kata ya Loya na Kata ya Miswaki, wamekuwa wakishindwa kukopesheka kwa sababu ya kukosa vigezo vya kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri kwa Wizara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti nyingi zimefanyika. Kwa nchi ambazo zilizoendelea zimewekeza kwenye matumizi bora ya ardhi, kwenye teknolojia na kwenye kutumia ranchi za kisasa. Kwa mfano, tunaona nchi kama Brazil wameendelea kwa kutumia vitu hivi vitatu. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Kilimo na Mifugo nasi twende tukawekeze kwenye *angle* hii kwa ajili ya kuwakomboa wafugaji wetu na wavuvi wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, pamoja na changamoto hizi wananchi wa Jimbo la Igalula bado wanampenda…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JUMA M KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya, hasa ya kuziongezea thamani sekta hizi za mifugo na uvuvi. Sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi tumetengenezewa historia kubwa sana, tumebadilishiwa historia kubwa sana kwa kuletewa bandari ya uvuvi, bandari ya kwanza ya uvuvi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari hii ina thamani ya shilingi 280,000,000,000. Tunatarajia kwamba, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, itakuwa na ajira rasmi 300 pamoja na ajira zisizokuwa rasmi, kwa maana ule mnyororo wa thamani, ziko 3,000. Pia ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na mkakati mwingine wa kujenga Bandari ya Uvuvi katika Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa shuhuda wa hizi bandari zote mbili kwa sababu nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo wakati tunapanga mipango ya kuijenga bandari ile na pia nikaenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilwa ambapo nimeshiriki moja kwa moja kwenye zile hatua za awali za kupatikana kwa bandari hii ya uvuvi ya Kilwa. Kwa hiyo ninaweza kusema

kwamba kwa kweli nimeshuhudia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiahidi anatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni shuhuda mkubwa wa bandari hii ya uvuvi ninawiwa kusema kwamba, ikimpendeza Mheshimiwa Waziri amfikishie salaam Mheshimiwa Rais. Tunatamani sana Bandari ya Uvuvi ya Kilwa ipewe jina la Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukanda huu wa Pwani ambako kuna ukubwa wa maelfu ya kilomita na kuna fukwe nzuri za bahari ilikuwa ni sahihi sana kwa Mheshimiwa Rais kutujengea hizi bandari mbili za uvuvi; kwa maana ya Kilwa na upande wa Bagamoyo. Hii inakwenda kuchochea kukuza uchumi wa *blue*. Bandari hii ni *component*, haiishii tu kuwa bandari peke yake, ni lazima kuwe na umeme wa uhakika kwenye bandari ili tuweze sasa kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi, pia ni lazima kuwe na barabara nzuri. Hili la barabara nitakwenda kulichangia wakati utakapofika kuchangia Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hii ya bandari ya uvuvi katika Wilaya ya Kilwa itachochea pia utalii wa kufanya *deep sea fishing* kwenye bahari. Pia itasaidia kuondokana na uvuvi haramu, pamoja na kupata samaki ambao watakuwa wamenona. Tunatarajia kuondokana na kuvua kwenye maeneo yenye maji machache kwenda sasa kwenye kina kirefu. Ninaiomba Wizara itusaidie kuwasaidia jamii za wafugaji waliopo katika Wilaya hii ya Kilwa waweze kupewa mafunzo ya kuvua kwenye kina kirefu, lakini wapatiwe zana za kuvua kwenye hicho kina kirefu, zana za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kilwa hakuna chuo cha uvuvi. Ninaomba ikiwapendeza; ninajua kuwa kule Mbegani Bagamoyo kuna chuo cha uvuvi, ikiwapendeza watusogezee pia kama ni *branch* ama ni Tawi la Mbegani lije pale Kilwa ili kurahisisha angalau kupunguza gharama za kutoka pale Kilwa kwenda kule kwenye wilaya nyingine ama kwenye mkoa mwingine kwa ajili ya kupata mafunzo haya ya uvuvi na mafunzo mengine ya kufanya uvuvi wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kwenye sekta ya mifugo. Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na mifugo mingi Barani Afrika. Ninaona namna ambavyo mifugo yetu imezagaa, ninaweza kusema imezagaa kwa kutokuwa na utekelezaji wa mipango sahihi ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano; tuna eneo letu pale linaitwa ninafikiri ni *NARCO,* ipo Ruvu; lilitengwa kwa ajili ya wafugaji kwenda kufuga mifugo yao pale wakiwa wanakodishwa; lakini mpaka sasa wafugaji wengi wanahama wanatoka kwenye maeneo hayo wanakuja kwenye maeneo ya kusini ambapo sisi wananchi wa Lindi na Mtwara na kwingineko hatujajiandaa kupokea mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na lindi la mifugo, sijui ni lindi au ni limbi…*(Kicheko)*

…sisemi wingi, lindi la mifugo katika wilaya zetu hizi za Mkoa wa Lindi wakati huo huo hatuna malisho ya uhakika kwa mifugo hiyo; na kwa bahati mbaya sana mifugo hiyo sasa inakimbilia kwenye maeneo ya wakulima. Tukumbuke hii mikoa yetu huku sisi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, malizia.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi niombe, kwamba tuje na mipango mahususi ya kuwaweka wafugaji kwenye maeneo sahihi na salama ili tuepuke migogoro ya wakulima na wafugaji. Kwa kuwa shughuli zetu nyingi ni za kulima zaidi kuliko kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa shughuli zetu kwa mchana wa leo na watakaoanza kuchangia jioni ni Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo,

Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na sasa ninamwita Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, wajiandae Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Awali kabisa niwapongeze viongozi wote wa Wizara, (Waziri, Naibu na Makatibu Wakuu wa Wizara hiyo), lakini pia zaidi Mheshimiwa Rais kwa maono yake na usimamizi wake katika sekta hii ambayo kwa kweli inawaajiri Watanzania wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kama mnavyojua na kama walivyochangia wengine hii sekta ya ufugaji na nitachangia zaidi kuhusu ufugaji wa ng'ombe. Hii sekta ya ufugaji pamoja na kwamba ni mila za watu wengi sana za jamii nyingi sana hapa Tanzania, lakini ni sehemu kubwa ya uchumi na ajira yao na ambayo kwa kweli bado mikakati mikubwa inatakiwa ili kuiboresha sekta hii, ili iweze kuchangia kipato cha familia na kaya pamoja na pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii wilaya ambayo ninatoka ya Ngorongoro ambayo 98% ya wakazi wa wilaya ile ni wafugaji, wangefurahi zaidi kupata matokeo makubwa sana ya ufugaji wao. Kama Waziri anavyofahamu wilaya ile iko mpakani, sisi tunastahili sasa hivi kupata viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (nyama na maziwa) kwa sababu wanaonufaika zaidi sana sana na mazao yetu ni nchi jirani ambayo ndiyo inatoa hayo masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunayo changamoto moja kubwa sana kama hiyo ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa za mifugo na mifugo yenyewe. Kwa kweli ningefurahi sana kama Wizara hii ingeshugulikia changamoto nyingine kubwa ya upatikanaji wa malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malisho ya mifugo pamoja na kwamba imebainishwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025 - 2030 kwamba itaongezeka kutoka hekta 3,000,000 hadi 6,000,000. Hilo jambo lingeharakishwa sana, upatikanaji wa malisho, kwa sababu kadri tunavyoendelea kutofikia lengo hilo la upatikanaji wa hekta 6,000,000 ndivyo wafugaji wataendelea kupoteza mifugo yao wakati wa ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo mingi inakufa kwa sababu inakosa majani, inakosa malisho wakati wa kiangazi na mingi sana pamoja na kwamba inakufa kwa kukosa malisho bado Serikali inatakiwa iweke msisitizo zaidi, iende mbio sana kuhakikisha kwamba malisho ya mifugo yanapatikana na kuhakikisha kwamba inazuia mifugo kufa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo mingi sana inakufa wakati wa kiangazi na mifugo inapokufa ndivyo umaskini unavyoongezeka kwa wafugaji. Tusipodhibiti vifo vya mifugo wakati wa kiangazi hatutadhibiti umaskini unaoongezeka kwa kaya na familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kuweka ruzuku ya upatikanaji wa chanjo. Chanjo inapatikana kwa bei nafuu na kwa wingi, lakini inatakiwa kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani wa Mifugo wanasambazwa karibu kila kata au kila kijiji, ili watoe elimu na hamasa ya ufugaji wa kisasa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu maeneo mengi sana ya wafugaji yanakaa karibu na mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa na mara nyingi sana mifugo inapokosea ikaingia maeneo yaliyohifadhiwa, mifugo ile hutaifishwa. Wito ni kukomesha utaifishwaji wa mifugo ambayo ina wenyewe. Tuache kabisa kutaifisha mifugo ya wananchi kwa sababu siyo sahihi na siyo haki kuchukua mifugo ambayo ndiyo uchumi na ndiyo chakula cha familia hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wito wangu kuhakikisha kwamba kunajengwa aina fulani ya mahusiano kati ya maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi na ikiwezekana kabisa hiyo sheria tuipige marufuku kwa sababu kufilisi ni vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekwishaeleza, bahati mbaya sana sisi tuko mpakani na upatikanaji wa masoko ni mgumu sana kwa sababu hatuna aina nyingine yoyote ya masoko tunayoitegemea isipokuwa Kenya. Hii siyo sahihi kwa sababu mifugo mingi inauzwa Kenya, halafu inaenda kuchakatwa nyama ya mifugo huko na maziwa, tunauziwa kupitia Namanga, Arusha na wakati sisi wenyewe tungeweza kunufaika na rasilimali hizo za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wito wangu kwa Wizara na Serikali kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira mazuri kwa wafugaji, ili waweze kupata masoko kwa urahisi na kwa uhakika wakati wakitaka kuuza mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ajiandae Mheshimiwa Joseph Kamonga.

Waheshimiwa dakika zetu ni sita tu.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya na uhai kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninapenda kuipongeza sana Wizara yetu hii, Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha wavuvi na wafugaji wetu wanafikia malengo na kupata maendeleo katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuwekea Waziri mahiri na makini wa Wizara hii ambaye ni mfuatiliaji wa kila siku wa moja kwa moja. Pia, ni Waziri ambaye hana urasimu katika kutekeleza majukumu yake, anapatikana wakati wote na anawahudumia wananchi kwa wakati wote. Haki yake mtu apewe akiwa bado yupo hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu ninaendelea kuishauri Serikali kwa tozo zile mbalimbali za sekta ya uvuvi na sekta ya ufugaji ziendelee kutazamwa ili zitoe unafuu kwa wafugaji wetu na wavuvi wetu, ikiwemo vile vifaa na zana za ufugaji na uvuvi zifikiriwe tena namna ya kodi na tozo mbalimbali ili wavuvi waweze kuzimudu na kutumia katika kazi zao za kila siku. Pia, zipitiwe upya sheria zilizopitwa na wakati ambazo hazimsaidii sasa hivi mvuvi na mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo ninaendelea kuishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mamlaka zile za uvuvi na ufugaji kwa sababu tuna Shirika letu la *TAFICO* tumelifufua.

Ninaipongeza Serikali kwa juhudi hiyo ya kufufua Shirika la *TAFICO* ambapo tunasubiri hiyo mamlaka, ili liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu ninaipongeza sana Serikali. Tumeanza kupata meli ya uvuvi ya kuvua katika bahari kuu. Kwa kweli ni jambo la mfano na ninaendelea kuishauri Serikali, mchakato ule wa kuongeza meli nyingine mbili za uvuvi uendelee ili sasa tuweze kuingia kwenye uvuvi wa bahari kuu rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uzinduzi rasmi wa bandari yetu ya uvuvi kule Kilwa; ninaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha hii bandari ya uvuvi itakuwa ni mkombozi kwa wavuvi, lakini itaongeza uchumi wa nchi. Pia, itaongeza ajira kwa vijana na wanawake na wajasiriamali mbalimbali, hasa katika maeneo ya kule Kilwa ambako bandari hii ndipo ilipo. Ninaipongeza sana Serikali na hatua nyingine ambazo inafanya za kujenga bandari nyingine katika maeneo mengine ya Pwani yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara hii inafanya kazi kubwa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaona na kuwajali wafugaji na wavuvi wa nchi hii kwa kuwapelekea vitendea kazi na zana za kisasa ili waweze kuingia kwenye uvuvi wa faida, uvuvi wenye tija, uvuvi utakaoleta kipato katika nchi na juhudi hizo ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia Serikali kwa kuanzisha ile chanjo ya mifugo. Sasa wafugaji waendelee kuipokea ile chanjo wafuge mifugo yao ili waweze kuingia kwenye soko la kimataifa kwa sababu tunakosa soko la kimataifa kutokana na mifugo yetu kutopatiwa ithibati kutokana na chanjo zile. Tunakosa soko kubwa, wafugaji sasa walishike hili soko la kimataifa ili kuongeza kipato chao, kuongeza ajira, lakini na Serikali nayo itapata mapato makubwa sana tutakapouza mifugo yetu nje ya nchi kwa sababu tayari ina ithibati kubwa ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninapenda kuchukua fursa hii kuwatia nguvu na kuwatia moyo watendaji na viongozi wote wa Wizara hii, lakini pia kumtia moyo na kumtia nguvu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa anayofanya kuhakikisha sekta hizi kwenye uvuvi na ufugaji zinapewa kipaumbele. Tumeona sasa ile kuongeza bajeti katika sekta za uzalishaji, tumeona mafanikio makubwa kwenye sekta hizi, ikiwemo hayo niliyoyasema, bandari ya uvuvi, meli za uvuvi, maboti na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha vilevile kufufua au kuongeza ufanisi katika sekta zetu za utafiti ambazo sekta hizi zitasaidia kwenye chakula cha wanyama, chakula cha samaki na kuanzisha miradi mingine ya kutengeneza chakula na samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe na Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote, ninapenda kuipongeza sana Serikali na kuishukuru kwa kutoa kiasi cha shilingi 800,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Samaki Ludewa ambalo linajengwa pale Kata ya Manda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumamosi nilikuwa huko, nimeona ujenzi unaendelea vizuri. Nimshukuru pia Waziri, Mheshimiwa Dkt. Bashiru, kwa sababu kuna muda kulikuwa na mkwamo. Tuliweza kuwasiliana naye aliweza kutatua tatizo na sasa ujenzi wa soko unaendelea. Mimi mwenyewe nimeshuhudia nikiwa na Mwenyekiti wa Chama, Mzee Stanley Kolimba na Katibu wa Chama. Kwa hiyo, ninaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Wizara ya Vijana imeweza kutoa kiasi cha shilingi milioni 520

kwa ajili ya mikopo ya vijana kupitia Benki ya *CRDB* waweze kufanya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, nishukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, Serikali sasa inakwenda kutengeneza ajira za moja kwa moja kwa vijana zaidi ya 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliweza kufanya ziara. Baada ya mimi kuwasiliana naye aliweza kufanya ziara kata kwa kata kwenda kuunda vikundi hivyo na kusimamia kuhakikisha kwamba jambo hili la Serikali lenye nia njema kwa vijana wa nchi hii linakwenda kutimia. Kwa hiyo, wameshaunda vikundi kwenye kata nne, kwa hiyo sasa Ziwa Nyasa linaenda kuwa na uvuvi wa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nishukuru pia watu wa *TAFIRI* kwa ushirikiano na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Ludewa ambaye alilipia gharama, Baraza la Madiwani liliidhinisha, Mkurugenzi akalipa, watu wa *TAFIRI* walikuja kwenda kufanya utafiti maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba Ludewa. Hii ni kwa sababu kwa muda mrefu Ziwa Nyasa lilikuwa linaaminika kama haiwezekani kwa sababu ya upepo mkali na mawimbi na kina kirefu cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu hawa waliweza kupata eneo la Uhonjo ambalo lipo Kata ya Iwela na tayari tulishawahi kufanya jaribio la kufuga samaki na matokeo yalikuwa mazuri sana. Baada ya hapo sasa, Baraza la Madiwani wakaidhinisha fedha zile za vikundi ili ziweze kukopeshwa kwa vijana kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niipongeze halmashauri, Baraza la Madiwani kwa kuidhinisha fedha zile. Kwa hiyo, kuna vikundi vitano tayari ninavyozungumza vilipewa mkopo na waliweka tayari vizimba Ziwa Nyasa sehemu ya Uhonjo iliyopo Kata ya Lupingu. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana kupata kutokea kwenye Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unavyozungumzia shilingi milioni 520 maana yake hapo, vizimba zaidi ya 100 vitakwenda kuwekwa kwenye ziwa na vijana zaidi ya 100 pia watakwenda kunufaika na

mapato kutokana na mauzo ya samaki. Sasa, hili litapelekea hitaji kubwa sana la vifaranga kwa ajili ya kwenda kuweka kwenye hivyo vizimba zaidi ya 20 ambavyo vinaenda kuanza, ukichanganya na vilivyopo vya halmashauri vitakuwa vingi sana. Kwa hiyo, utafiti tulioufanya kule tuliona watu wa Ruhila walituongoza kwa kushirikiana na Wizara kwamba, vifaranga wanapatikana upande wa wenzetu Malawi ambao wanakubalika kutokana na ikolojia ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Malawi kina kitengo hicho na wanazalisha vifaranga. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri alielekeza wale watu wa Ruhila waweze kuanzisha na *hatchery* yao. Sisi pia tumetafuta wadau mbalimbali, ambao watakwenda kwa Mheshimiwa Waziri kuomba vibali vya kwenda kuchukua samaki wazazi ili waje waanzishe *hatchery* Ziwa Nyasa kuzalisha vifaranga wengi zaidi. Hii itaweza kutatua tatizo la upande wa Kyela na upande wa Nyasa. Kwa hiyo, tutaomba hiyo hoja ya vibali kwa ajili ya kwenda kuchukua wazazi na vifaranga wa kuanzia tuweze kupewa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo naiona tukiachana na hii ya vifaranga ambayo tayari angalau tumejua wapi wanapatikana na huwa nina kawaida ya kuwasiliana na watu wa Ruhila kuweza kupata vibali tukachukue kule, ili tusiharibu ikolojia ya Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, changamoto inayokuja nyingine ni ya chakula cha samaki *(fish feed)* wanaita. Kwa hiyo, chakula cha samaki kwa sasa kwa kiwango kikubwa bado tunategemea kuagiza nje ya nchi. Kwa hiyo, kile chakula kinakuwa ni cha gharama sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kutengeneza chakula cha samaki siyo sawa na mtu anayesomea wanaita *(rocket science)*. Ninafikiri tunaweza tukatengeneza wenyewe chakula cha samaki. Kwa hiyo, ninaomba tutatue hii changamoto ya chakula cha samaki ili Ziwa Nyasa tuweze kufuga samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninaona umeniwashia taa sijui dakika zimeisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nimwombe Mheshimiwa Waziri aje kututembelea, aone tunayofanya Ziwa Nyasa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe; wajiandae Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni na Mheshimiwa Morris Joseph Makoi.

Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi, lakini kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumwamini Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally kwa kumpa nafasi ya kuwa msimamizi wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Pia, niwashukuru sana watendaji wake wote ambao wanampa ushirikiano kutimiza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na machache, kwanza kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kutujali katika maeneo ya Ziwa Tanganyika. Tumepokea pia boti kwa ajili ya doria na tumeendelea kupokea mikopo kwa ajili ya wavuvi; hiyo yote tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wavuvi wa Ziwa Tanganyika na maeneo mengine hali ya Ziwa Tanganyika ni mbaya sana. Hali ya Ziwa Tanganyika ni mbaya sana, mazingira ya uvuvi ni mabaya; kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira, kadhalika ninafikiri hata Ziwa Victoria, hali ni mbaya kwa sababu uvuvi haramu bado upo na umeshamiri sana, samaki wameadimika hawapatikani. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kuendelea kusimamia sheria na miongozo waliyonayo kuhakikisha

kwamba wananusuru Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pia Ziwa Tanganyika tunapakana na nchi nne; Tanzania tunamiliki 41%, Kongo 45%, Burundi asilimia nane na Zambia asilimia nne. Hili eneo lina wakazi wanaotegemea uvuvi karibu katika Ziwa Tanganyika wanaozunguka hili eneo ni karibu 10,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa heshima kubwa kwa kuwa ninaamini kabisa utendaji wako wa kazi siyo wa mashaka mashaka; kuongeza nguvu katika kudhibiti uvuvi haramu. Uvuvi haramu umeshamiri sana, pia kumekuwa na doria ambazo wamekuwa wanafanya *operation* kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu wanaoathirika ni wavuvi wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali wadhibiti kwanza wale wanaosambaza, kwa sababu wavuvi hawa shida yao ni kujikimu; kwa hiyo, hawawezi kuacha kutumia nyavu haramu, lakini nyavu haramu zinapatikana wapi? Zinapatikana kwenye maeneo yetu, siyo kwamba Serikali haiwajui wanaosambaza hizi nyavu haramu. Kwa hiyo, kuliko kwenda kumbuguzi mvuvi ni bora wakadhibiti uvuvi haramu na wale wanaosambaza ili kukomesha kabisa, kwa sababu mbona zinapatikana? Kama zinapita mpaka zinaenda kufika kwa wavuvi kule na wakati wanafanya doria wanakwenda kuwakamata. Lakini wavuvi wameendelea kuathirika sana katika doria wanazozifanya ikiwa ni pamoja na kuwakamata, kuwapiga faini, kuwafunga, lakini kuwafilisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nishauri tena kuhakikisha kwamba wanadhibiti hawa watu wanaochukua hizo nyavu au vifaa hivyo haramu ili kuhakikisha kwamba wanakomesha kabisa. Hata hivyo, wamekuwa wakifanya doria, sioni sehemu ambayo kwa maeneo yetu kama Ziwa Tanganyika kutoka Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa, wanateketeza hizo nyavu baada ya kukamatwa. Kwa maana hiyo, zikishakamatwa, zinarudi tena kwenda kufanya uhalifu. Sasa ni shughuli ambazo unaweza ukakuta kuna watu wamejiwekeza huko kwa ajili ya kujipatia kipato haramu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kudhibiti uvuvi haramu ili kuweza kunusuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya wavuvi katika Ziwa Tanganyika ni mbaya sana, ni mbaya sana kwa maana wanavua hawapati samaki kutokana na uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kumekuwa na mpango wa kupumzisha hili Ziwa Tanganyika, lakini hili ziwa kutokana na jinsi ambavyo tunaligawa katika nchi nne, kuna maeneo wanafunga na maeneo mengine hawafungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa heshima kubwa, katika mwaka huu, wakati wanaendelea kufanya tathmini katika vipindi ambavyo huwa wanafunga kwa miezi mitatu, wawaachie wananchi wasifunge hili ziwa kwa mwaka huu. Kwa sababu hata katika miaka hii miwili, mitatu hali ya uvuvi Ziwa Tanganyika ni mbaya, kwa hiyo, hata wakiendelea kufunga lile ziwa linajifunga na kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi ninaloweza kushauri ni kudhibiti uvuvi haramu ili tuwe na uvuvi endelevu. Kuna nyavu wanazotumia na Mheshimiwa Waziri anajua, ambazo zikikatika ndani ya maji zinaoza baada ya miaka 100 kwa tathmini ambavyo wataalam wamesema. Sasa tukiacha uvuvi haramu ikiendelea ndani ya miaka hiyo 50 au miaka 20 tutabaki na maji matupu hatutakuwa na samaki tena. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ziwa lisifungwe, watoe elimu. Nimshauri pia aunde makundi katika maeneo ya kata na vijiji, ukanda wa maziwa kwa kuanzia Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Walinzi wa Ziwa Tanganyika wawe wavuvi wenyewe, wataalam wanakuja baadhi ya watumishi ambao ni Sekta ya Uvuvi siyo waaminifu wana mtandao mkubwa. Bila shaka Mheshimiwa Waziri anajua kwamba, kuna mtandao mkubwa kuanzia ngazi ya kata kwa watumishi, siyo wote lakini baadhi wana mtandao ambao wanashirikiana na hawa ambao wanafanya shughuli za uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, upande wa wafugaji, katika Jimbo lilotoka la Kalambo, Mkoa wa Rukwa tumeendelea kupokea ndugu zetu hawa wafugaji kutoka kanda ya ziwa na

maeneo mengine. Hawa ni wawekezaji kama wawekezaji wengine tunawapokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, hawa ndugu zetu kumekuwa na changamoto kati ya wafugaji na wakulima; niombe elimu iendelee kutolewa kwa sababu maziwa tunahitaji na nyama tunahitaji, kwa hiyo, mahusiano yawe ni kipaumbele. Hawa wafugaji wanapokuja kuna muda wanatumia nguvu kubwa sana kwa wenyeji ambao ndiyo wamewapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna uwezekano Wizara hizi za Kisekta kama Ardhi, kuwe na utaratibu kwa sababu migogoro mingi inaanzishwa na baadhi ya viongozi wa vijiji kwa kuuza maeneo kwa hawa wageni bila kufuata taratibu mwishoni inakuwa ni migogoro mikubwa. Ili kama kuna uwezekano tuangalie Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji mwisho wake wa kuuza ardhi ni kiasi gani? Sasa Mwenyekiti wa Ardhi anaenda kusaini mkataba wa hekari 1,000, anakuwa sheria hazijui na baadaye inaleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadhibiti pia leseni ambazo zinatoka Wizara ya Uvuvi, zinafanya *export* nje, ambazo zimeendelea kukodishwa bila kufuata taratibu na mwisho kuharibu soko la samaki katikati ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, wajiandae Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi inafanya majukumu yake. Pia

nimshukuru Mheshimiwa Waziri wetu, Naibu Waziri na wale wote ambao wanamsaidia katika kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Bajeti ya Mifugo na Uvuvi, ninaona kama imezingatia mambo mengi mazuri. Hata hivyo, nina ushauri, nimeona hapa Wizara wamesema kwamba wataanzisha ng'ombe wa mtambo wa maziwa na ambao watapeleka katika familia 1,600. Sasa sijajua *specific* kwamba hawa ng'ombe wanapelekwa upande gani. Ninamwomba Waziri, kule Moshi Vijijini tunahitaji ng'ombe hawa sana kutokana na umuhimu wa kubadilisha mbegu ya ng'ombe wa maziwa kule. Kwa hiyo, kama ataweza kutuzingatia walau kwa uchache basi tunamwomba atuzingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia elimu hii ya ufugaji ingetolewa kwa vijana, lakini ilenge vijana ambao tunaanzia shuleni. Kwa mfano tukiweza kutoa elimu hii kwa vijana wetu ambao wako kwenye shule za kata na hata msingi kuanzia darasa la sita na la saba ingeweza ikasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana wengi ambao tunawakuta mtaani sasa hivi wanapatikana au wanazalishwa kutoka kwenye shule za msingi na shule za kata. Kwa hiyo, wakiwa na elimu ile mapema inaweza ikasaidia kuwa na uzoefu na wakati wanaporudi baada ya kumaliza shule wanaweza wakaendelea kujiunga au kuendelea na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwenye eneo hilo hilo kuanzishwa kwa ufugaji wa kuku wa kienyeji kwa wale vijana wa vijijini hasa Jimbo la Moshi Vijijini ambako inaonekana kwamba soko la mauzo kwa ajili ya kuku hao ni kubwa na hata mayai. Kwa hiyo, Wizara kama itakuwa na mpango ikileta Moshi Vijijini tuko tayari kupokea na mahitaji ni makubwa. Tunaamini kwamba hawatatumia gharama kubwa sana kwa sababu tumeshaanza elimu kule na utaratibu unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia Wizara ya Mifugo kama wanaweza wakaunganisha nguvu na Wizara ya Maliasili kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa mbegu za vipando kwa ajili ya nyasi za kulishia mifugo. Kwa sababu wafugaji wetu ambao

wanapatikana katika vijiji 40 vinavyozunguka Mlima wa Kilimanjaro wamekuwa na migogoro na watu wa *KINAPA* na *TANAPA* kwa sababu ya kutafuta malisho kwenye maeneo ya jirani na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, magomvi yamekuwa ni mengi kule kwa sababu ya kutafuta malisho. Kwa hiyo, kama Wizara ya Mifugo wakishirikiana na Maliasili wakasambaza mbegu za majani haya ya vipando ya ng'ombe, mbuzi na kadhalika, wananchi wale wanaweza wakazalisha majani na wakalisha mifugo yao na hiyo ikapunguza yale mambo ya kuingilia kwenye mamlaka zile na kupunguza migogoro ambayo haina lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu mwingine ninashauri Wizara ya Mifugo waanzishe Wakala wa Ugani wa Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu Wizara ya Kilimo ninaona wameanzisha Wagani na inasemekana kwamba wanaweza wakafanya kazi kwa ukaribu na wananchi na watakuwa wameondokana na ule mnyororo wa Wakurugenzi kuwapa majukumu mengine ambayo yanawafanya wanashindwa kufanya wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa sasa hivi kwa mfano Wagani wa Mifugo na Uvuvi hawapatikani katika maeneo ya vijijini kufanya majukumu yao kikamilifu, kwa sababu muda mrefu wanakuwa wameelekezwa na Wakurugenzi kukusanya maduhuli na hata wakati mwingine kukaimu Utendaji Vijiji kwenye vijiji ambavyo havina watendaji. Matokeo yake ni kwamba wakati wafugaji wanawahitaji hawapati kwa muda. Kwa hiyo, wamekuwa ni bidhaa adimu kule vijijini, kama wakianzisha wakala huenda hawa wakafanya kazi kwa bidii, lakini vilevile watawekeza nguvu zao kwenye jukumu hilo na hivyo kuweza kuleta tija zaidi kuliko hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia kuhusiana na vizimba vya samaki. Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanaleta miradi ya uvuvi kwenye maeneo, lakini hawashauriani wala kutoa taarifa kwa Wabunge. Kwa hiyo, matokeo yake fedha zinafika kule kwenye halmashauri ama zinafikia kwenye kata au vijiji na Wabunge hawana taarifa. Matokeo yake, ile miradi haipati

uangalizi mzuri na hata ile hamasa ya vijana ili waweze kufuatilia na kuelekezwa namna ya kufanya inakuwa kidogo ina changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wakati wanaleta miradi ya namna ile Wizara ya Mifugo ijitahidi kuhakikisha kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu ili wahusishe Madiwani na wale watu wa ngazi ya chini ili kuwezesha hilo jambo liweze kuwa na tija ambayo inakusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri vilevile, kwamba katika kuhakikisha kwamba mifugo inaimarika ni vizuri sana tukahakikisha kwamba, hawa vijana ambao tulikuwa tunawapa mikopo ya 10% tungeweza tukaelekeza kwenye mbuzi wa maziwa. Mbuzi wa maziwa katika maeneo yetu ya vijijini kama wangekuwa ni sehemu ya mikopo ya 10% ingeweza kuleta matokeo mazuri kuliko zile fedha taslimu wanazopokea. Kwa kuwa zile fedha kila mtu anachukua akitaka kufanya jambo analolifanya ambalo halina uhakika badala yake matatizo yanakuja kuanzia pale kwenye kurudisha ile mkopo, matokeo yake, yale ambayo yamekusudiwa hayaonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamshauri Waziri kama itampendeza, basi wajaribu kuelekeza nguvu ile ya mikopo ya 10% ambayo imepelekwa kwenye Wizara ya Mifugo katika ile 200,000,000,000 kwenye ukopeshaji wa mbuzi wa maziwa kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ajiandae Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo anaifanya hasa ile ya *operation* kwenye eneo la

Ziwa Tanganyika. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri juhudi ambazo amezianzisha zisiwe za zimamoto. Twende moja kwa moja kudhibiti uvuvi haramu ambao unachangia sana kuua Sekta ya Uvuvi hasa kwenye eneo la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni miongoni mwa watu ambao siafikiani na mpango wa Serikali wa kulifunga Ziwa Tanganyika. Ninafahamu chanzo cha Ziwa Tanganyika kufungwa ni sababu ya uvuvi haramu ambao upo kwenye eneo la Ziwa Tanganyika. Nyavu zinazoletwa kutoka nje ya nchi zimekuwa ni tishio kwa mazalia ya samaki na viumbe hai ndani ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mchangiaji aliyepita alivyosema, zile nyavu ikikatika inaendelea kuua kizazi hadi kizazi kwa kipindi kirefu sana na matokeo yake asilimia kubwa ya uvuvi ndani ya Ziwa Tanganyika unaenda kutoweka. Ili kudhibiti suala hilo ni lazima sasa Serikali ijielekeze kufanya doria ambazo zitasaidia kuondoa kabisa tatizo la uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofanya uvuvi haramu ni jirani zetu, wavuvi kutoka Nchi za Burundi na *DRC* (Congo) ndiyo wanaokuja na hizo nyavu. Lakini bahati mbaya iliyopo hata wale maafisa wetu, Maafisa Samaki ambao wapo kwenye maeneo hayo wanadiriki kushirikiana na hao ambao wanafanya kadhia hiyo mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, lazima tuwe na mpango kazi ikiwa ni pamoja na hao watumishi. Mtumishi wa idara hiyo ya samaki anapokaa kwenye eneo kwa muda mrefu anajenga mazingira ambayo kiukweli yanakuwa na mnyororo mrefu ambao unashirikiana na wavuvi haramu. Kwa hiyo, ninashauri watumishi wawe wanahamishwa mara kwa mara ili kuweza kuondoa hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninashauri kwenye maeneo haya, Serikali itenge maeneo ya mazalia ya samaki. Tunao mfano kwenye maeneo yanayomilikiwa na Jeshi (JKT), kwenye maeneo ambayo yapo kwenye Ziwa Tanganyika,

mazalia ya samaki yapo na samaki wanapatikana. Kwenye eneo la hifadhi, mfano kule Mahale samaki ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungetenga kila eneo tukawa na mazalia ya samaki, tungetenga hayo kama hifadhi tungekuwa na maeneo makubwa ambayo kwa kuwa Ziwa Tanganyika ni refu, kila eneo tungetenga Mkoa wa Kigoma kuwepo na eneo la mazalia karibu hata vituo vitano, Katavi, Rukwa. Tungesaidia sana kutatua tatizo la uvuvi haramu na kusaidia mazalia ya samaki katika ziwa letu ili kuwe na uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vizimba. Mikoa yetu Mkoa wa Katavi, Rukwa tumepata idadi ndogo sana ya vizimba. Mheshimiwa Waziri niombe sana, tuache kuwa na mpango wa kupeleka vizimba kwenye maeneo ya ziwa moja tu. Ukichukua takwimu Ziwa Victoria ndilo ambalo limepata vizimba vingi. Ninajua Mheshimiwa Waziri hatakuja na mfumo kama ule uliokuwepo huko nyuma, aende akavisambaze vizimba. Kwangu Mkoa wa Katavi eneo pekee ambalo linapakana na ziwa ni jimbo langu. Tunahitaji tupate vizimba na maombi walishaleta, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hatujakuwa na vizimba vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo. Kwenye eneo la mifugo Mkoa wa Katavi una idadi ya mifugo mingi sana. Kwa bahati mbaya sana hatuna maeneo ya malisho. Niombe Serikali kwa kushirikiana na halmashauri na halmashauri zishirikiane na Serikali za vijiji, kuhakikisha wanatenga maeneo ya malisho ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo ni tatizo kubwa sana katika maeneo hayo. Wakitusaidia hayo, tutakuwa tumeondoa kabisa tatizo la migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wafugaji wamekuwa wanafanya shughuli ya kufuga mifugo kwa kutangatanga? Ni kwa sababu kwanza hawana malambo, majosho. Sasa ninaomba na kuishauri Serikali hayo maeneo wayasaidie kwa kuchimba majosho na malambo ili tuweze kusaidia jamii ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye; wajiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa Kangi Lugola, wajiandae.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nianze na kumshukuru Mungu kwa kunipa kibali kilichoniwezesha kusimama siku ya leo katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninatambua kazi ambayo Mheshimiwa Waziri, baba yangu Mheshimiwa Kakurwa anaifanya, hongera kwa kazi ambayo anafanya kwa ajili ya Watanzania. Sitakuwa na mengi kwa sababu wenzangu wa Ziwa Tanganyika wamezungumza mengi, lakini ninataka kukazia katika suala la kufunga Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezaliwa Kigoma, nimekulia Kigoma; asilimia kubwa ya watu wa Kigoma wanategemea Ziwa Tanganyika hasa katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, kwangu, lakini na Jimbo la Kigoma Mjini kwa kaka yangu Revocatus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la samaki kuongezeka na kupungua katika Ziwa Tanganyika liko *automatic* toka tunakua, enzi za mababu na mabibi. Kuna wakati samaki wenyewe ziwa linajifunga, linajifungua, samaki wanakuwa wengi, samaki wanakuwa wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, mkakati wa kufunga ziwa kwa Wanakigoma ama Ziwa Tanganyika kwa ujumla, sisi kama wananchi hatukubaliani nalo. Kiukweli tunaona kabisa ni kama hawataki kutusikiliza wananchi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atenge muda akazungumze na wananchi, yawezekana akaletewa ripoti kutoka kwa watu wake wa chini, wakamwambia tumefunga ziwa, tulivyofungua samaki walikuwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kama kuna kipindi watu wa Kigoma walikula sana dagaa wa Mwanza, ni wakati tumefunga Ziwa Tanganyika na likafunguliwa, lakini watu walikosa mboga zilikuwa hazipatikani. Wananchi wa Kigoma hali zetu tunazijua, tukifunga ziwa kuna watu nyama hawaioni ndani ya mwezi au *Eid* mpaka *Eid* ndiyo wanakula nyama. Maana yake, tunapowafungia ziwa watu wanakosa mboga, lakini siyo kukosa mboga tu; kwa mfano, Kigoma Kaskazini, wengi wanategemea uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile ndiyo duka lao, waingie ziwani wakavue, wapate pesa, wasomeshe watoto. Unapomfungia mtu ziwa miezi mitatu tafsiri yake ni kwamba, unamrudisha mtaani akakae bila kazi. Kipindi tumefungiwa ziwa ni kipindi ambacho hata wizi uliongezeka. Watu walikuwa wananyang'anywa mizigo pale Kigoma, wizi ulikuwa mkubwa kwa sababu watu walikosa kazi za kufanya. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri busara iwaongoze watu wa Wizara ya Uvuvi. Wawasikilize wananchi, tukae tutafute namna gani ya kuweza kusaidia samaki zisipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema Waheshimiwa na iko wazi samaki wanapotea kwa sababu ya uvuvi haramu. Watu wanatumia nyavu haramu, lakini hizi nyavu zinaingizwa kutoka nje, zinauzwa. Wavuvi wanakwenda wanazinunua madukani, maana yake wanalipa kodi pia kwa Serikali. Sasa kama Serikali inachukua pesa, watu wananunua nyavu, lakini nyavu hizohizo zikifika kwa mvuvi Ziwa Tanganyika zinaitwa nyavu haramu, hatuwatendei haki wavuvi. Kama ni nyavu haramu, Serikali izuie kuingiza nyavu hizi, ili hawa wananchi wanyonge wasiweze kuzipata hizo nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka nizungumze, ni suala zima la leseni kwa wavuvi. Leo ukikata leseni ya gari kama umekata tarehe 14 ya mwezi Mei, maana yake itakwenda kwisha ndani ya mwaka mmoja, tarehe 14 ya mwezi Mei, 2027, lakini wavuvi leo akikata leseni tarehe 14 mwezi Mei, 2026, ikifika Disemba leseni yake ime-*expire*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba u-*take note* hii, wasaidieni wavuvi, wakate leseni kwa mwaka. Akikata mwezi Mei, mwaka huu,

arudie mwezi Mei mwakani na siyo ikifika Disemba akate tena. Hali ya maisha kwa Watanzania ni ngumu, watu hawana pesa kwenye mifuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumzie suala la vizimba. Wenzangu wamesema, ni kweli ukitazama vizimba vilivyopo katika Ziwa Tanganyika, huwezi kulinganisha na idadi ya vizimba katika Ziwa Victoria. Tunataka Ziwa Tanganyika na sisi tuongezewe vizimba, viwe vya kutosha na visiwe kwa watu wachache ama watu *specific*. Tuwachukue hata wale wavuvi wadogo wadogo na wao waweze kupewa vizimba, waweze kumiliki vizimba na tuweze kupata samaki kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ninataka kuzungumza, ndani ya Ziwa Tanganyika kumekuwa na matukio ya wavuvi kuibiwa mashine, wavuvi kupigwa na majambazi kuwateka. Tunaomba tuwe na ulinzi wa kutosha katika Ziwa Tanganyika, kuwasaidia wavuvi wasiweze kuibiwa mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo kwa wavuvi. Ni kweli tunashukuru Serikali, inatoa mikopo kwa wavuvi, lakini bado si wavuvi wote. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, wavuvi hawa hata wale wadogo kabisa waweze kuaminiwa, waweze kupata mikopo, waweze kufanya kazi zao vizuri bila changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua unataka kuniambia muda…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo muda wako umekwisha.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba dakika moja. Ninataka nigusie suala zima la migogoro ya ardhi, kwa maana ya wafugaji na wakulima. Hili tulichukulie *very serious*. Ukifika huko kwenye majimbo yetu vijijini, wakulima na wafugaji wanakatana mapanga, wanauana, hali ya kuwa sote ni Watanzania. Tutafute namna ya kuondoa hii changamoto. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi na kwa sababu ya muda nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi ambayo wanajaribu kufanya. Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru, sisi tuna imani kubwa sana na wewe. Unajua Katibu Mkuu wa CCM Mstaafu, Balozi, Profesa chuo kikuu huko, maana yake ni mtu ambaye anaifahamu hii nchi sana. Matamanio yetu ni utujengee misingi hiyo ya ujamaa; hii nchi ni ya ujamaa, Watanzania ni wajamaa, ni lazima tuendeshe Wizara hii kijamaa jamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bajeti kuongezeka, lakini sisi bado tunaona bado tungetamani sana Wizara hii ipate bajeti, kwa sababu mahitaji ya Watanzania ni mengi sana. Mabwawa, majosho na maeneo ya malisho, hiyo yote inataka pesa. Kwa hiyo, tungetamani na wito wetu kwa Serikali iendelee kuongeza pesa nyingi sana. Hata kwenye uvuvi huko, mahitaji ya Watanzania kwa masuala ya uvuvi ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli kwa nchi ya kijamaa, tungetamani sana kuona bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwe kubwa sana. Mheshimiwa Dkt. Bashiru, tuna imani kwamba, huko mbele utajenga hoja vizuri, ieleweke zaidi ili Wizara hii iendelee kupatiwa bajeti kubwa zaidi, kwa sababu mahitaji ya Watanzania ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kiteto lina ng'ombe zaidi ya 500,000 na mahitaji ya majosho leo, kwa sababu Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasema kila kijiji chenye ng'ombe, inastahili kuwa na josho. Tunahitaji majosho zaidi ya 40, pamoja na kazi kubwa iliyofanyika, mabwawa zaidi ya 45, Mabwawa kama ya Dosidosi, Ndedo, Bwawani, Sunya na Kijungu**.** Kwa sababu, tunazungumza habari ya dira inayotaka kuwapeleka Watanzania miaka 25 ijayo, ya kuongeza kipato kwa Watanzania, hatutaweza kufika huko kama pesa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wasipopata maeneo ya kutosha ya malisho, tukapata maji ya kutosha kwenye mabwawa, lakini mifugo ikapata dawa kwa wepesi na kwa wakati, tukapata na majosho, huko hatutaweza kufika. Kwa hiyo ni lazima, *formula* pekee hapa ni kuwa na pesa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kweli tunatamani sana Serikali iibebe sekta hii vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti iliyopita kwa sababu Kiteto ina minada mikubwa sana na mapato yanayotokana na mifugo tunapata kupitia minada. Mnada wa Dosidosi, Kibaya na Sunya, sisi tulishaahidiwa hapa kwamba tungepata pesa kwa ajili ya kuboresha minada. Kwa hiyo, matamanio ya Wanakiteto ni kuendelea kuwaambia Serikali watuletee pesa hizi kwa ajili ya minada hii mikubwa, lakini watupatie pesa kwa ajili ya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Ndido, Wizara ilishapeleka karibu 200,000,000, na ni bwawa la 500,000,000. Sasa kwa sababu nimemsikia mara kadhaa akisema, miradi ambayo tumeshaanza tumalize, hebu alichukue hili la Ndido sasa tumalize, halafu tupambane na haya mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitamani sana tujenge mazingira mazuri kwa ajili ya wafugaji. Ninadhani, maeneo haya ya Serikali, ya *NARCO* na Ranchi za Taifa, nchi ya kijamaa kama hii, ningetamani sera yetu iwe maeneo haya tuwape wafugaji wadogo kwa 60% na 40% watumie kwa ajili ya wafanyabiashara wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya kijamaa lazima ionekane kwenye *percent* kwamba *focus* yake iko wapi. Kwa hiyo, tuangalie pamoja na kwamba wanapitia hizo, lakini 60% ya Ranchi za Taifa ziende kwa wafugaji wadogo, ziende kwa vijana, kwa sababu tunataka vijana wetu wapate ajira. Kwa hiyo, tungetamani sana kuwe na maelekezo maalum kwamba, ranchi zetu tuelekeze nguvu huko. Mheshimiwa Waziri, mambo ya jumla mengine, nimezungumza sana habari ya wakulima na wafugaji, vurugu hizi. Nchi ya kijamaa, kwa kweli lazima tujenge misingi na Mheshimiwa Rais tumpongeze hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizungumza Mbunge wa Morogoro hapa, ile Programu ya Tutunzane, ambayo Mheshimiwa Rais ameshaonesha nia. Sisi kazi yetu ni kuendelea kuboresha zaidi, ili tujenge mahusiano ya wakulima na wafugaji. Nchi hii hakuna kijiji hata kimoja, utakuta kina wakulima peke yake ama wafugaji peke yake. Dawa ya hii ni kutengeneza pesa, mipango bora ya ardhi tutenge; anayefuga ajue anafuga wapi, anayelima ajue analima wapi. Hili wazee na viongozi, tuzungumze lugha hapa bila kuonesha kugawa hawa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hii ndiyo kengele ya mwisho, basi ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mifugo. Kwanza ninampongeza sana mtendaji wa Wizara hii, kwa kasi aliyoanza nayo, sisi tunaendelea kumwombea. Aendelee kupambana, mtu mzalendo, mjamaa, anayefikika na ambaye amekubali kuwasogelea wavuvi na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza ni juu ya Bajeti ya Wizara hii. Fedha zinazotengwa na zinazotolewa. Hii ni Wizara nyeti kabisa kwa Watanzania, ni nyeti kwa sababu ni Wizara inayohusu usalama wa chakula katika nchi yetu, lakini ni Wizara tunayoitegemea kwa lishe. Tunajua tuna changamoto nyingi sana za lishe katika nchi yetu. Kuna utapiamlo, kuna udumavu, zaidi ya 30% ya watoto wetu wana udumavu na wao ndiyo Taifa la kesho, kwamba tuseme Watanzania watakuwa na udumavu. Sehemu pekee ambayo viini lishe muhimu kwa binadamu, kwa ajili ya lishe, tunavipata katika vyanzo vya mifugo kuliko ukilinganisha hata kwenye vyanzo vya mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana utaona takwimu za kitaifa za *FAO* au *WHO*, sisi ulaji wetu wa vyakula hivi huko chini, kama ni nyama wenyewe *recommended* ni kama kilo 25 kwa mwaka, sisi bado tuko 15; tunatakiwa tule mayai 300 kwa mwaka

kwa mtu, lakini sisi bado tunakula 106. Maziwa tunatakiwa tunywe zaidi ya lita 200, sisi bado tuko kwenye lita 62, ni kwa sababu upatikanaji ni mdogo. Upatikanaji ni mdogo kama tusipoendelea kuwekeza katika sekta hii, ina maana matokeo yake ni mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii iliyopita, fedha za maendeleo ilitengwa shilingi bilioni 375.138, lakini hadi Februari fedha zilizotolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 110.942. Ina maana bajeti ilitekelezwa kwa 29% au 30%, hebu ona sasa ilivyo hatari. Niiombe Serikali iko hapa, hata kama fedha hizi zimevuka mwaka, hawa watu wapewe fedha wakatekeleze miradi muhimu kwa ajili ya maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha ambayo Waziri ameomba mwaka huu, ukienda kwenye bajeti ya maendeleo, bado fedha zimepungua. Bajeti inayoendelea kutekelezwa ndiyo hii ya shilingi bilioni 375.138, sasa hivi ameomba shilingi bilioni 335.099, imepungua kwa karibu 10% na pointi. Tunaomba hata kwenye majumuisho ya mwisho, itakavyosomwa bajeti ya nchi hii, hii Wizara nyeti iweze kuongezewa fedha ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye nyanda za mifugo. Sisi tumebarikiwa, tuna rasilimali ya ardhi zaidi ya hekta 94,000,000, ambapo 50,000,000 zingefaa kwa nyanda za mifugo, hiyo 44,000,000 ndiyo ingekuwa ya kilimo. Ijapokuwa kinachotumika ni shilingi milioni 9.3 kwenye malisho ya mifugo, sisi tumeweza kupima kiasi cha hekta milioni 3,489,701, lakini bado ni maeneo ambayo kila mtu anaona ni maeneo wazi, yasiyomilikiwa na mtu, yasiyo na sheria, kwa hiyo, kila mtu anavamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari yake ndiyo hii kuhangaika na mifugo, wanazunguka Tanzania nzima hata nje ya Tanzania wakitafuta malisho. Tufike mahali sasa, nyanda za malisho zipimwe, zipewe sheria ili kusaidia mifugo hii isihangaike ikawa na afya bora, lakini ikawa inasambaza magonjwa na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni suala la maji kwa mifugo, ndiyo inayofanya mifugo izurure kote nchini. Kwenye

mifugo tunataka malambo madogo madogo, yanaitwa *charco dams*. Hizi *charco dams* zinawezekana kwenye kila kitongoji cha wafugaji. Kama Wizara ya Maji imeweza kununua mitambo yao wenyewe ya kuchimba maji na visima. Tunaomba basi, hata Wizara ya Mifugo iwe na mitambo yake iwe na ma-*excavator,* ili katika maeneo madogo madogo, hata wafugaji watakuwa tayari kuchangia mafuta, iweze kuwachimbia malambo haya madogo madogo kwenye maeneo yote ya wafugaji, kusaidia mifugo hii isizurure na ikawa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye suala la chanjo na utambuzi wa mifugo. Ninaipongeza Serikali, imezindua hii chanjo, mifugo imechanjwa na bado utambuzi wa hereni unaendelea kuwepo. Hii imetusaidia sana, angalau mifugo sasa hivi masoko yanafunguka, kama hivi sasa hivi tumeshaanza kupata soko la Uarabuni. Ninaomba mpango huu, ni kweli tumeanza kuchanja magonjwa kama *CCPP* (Homa ya Mapafu), lakini bado tuna magonjwa mengi. Tuna *foot and mouth disease, tuna anthrax,* tuna magonjwa mengine. Tunaomba tuwe na kalenda ipelekwe kule halmashauri, watumishi wa halmashauri ndiyo waendelee kuchanja mifugo, kila siku sehemu ya uchanjaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona umeniwashia, kwa hiyo ninashukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kangi Lugola, ajiandae Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga na Mheshimiwa Isack Joseph Copriano.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na mtu anaitwa ratiba. Huyu ratiba huyu, hivi kweli Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kupangiwa siku moja, Mbunge kuongea dakika sita, wakati ng'ombe duniani, Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 ambazo zinahusika na ng'ombe. Katika Afrika, Tanzania ni ya pili nyuma ya Ethiopia, tuna ng'ombe milioni 39. Ratiba huyu basi tu. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri anafanya kazi sana, Wizara imechangamka. Kwenye hotuba yake amezungumzia suala la *BBT*, lakini akaja na ile kauli mbiu ile ya kujenga kesho iliyo bora na hasa kwa kupitia ufugaji wa samaki kwa vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye vizimba kwa sababu ya muda. Tulilenga kwamba tukifuga kwa vizimba, kwanza tutaongeza ajira, lakini pia tutaongeza pato la Taifa kupitia uvuvi. Pia, tutapambana na umaskini ambao umekithiri miongoni mwa watu wa chini, hasa kwenye Ziwa Victoria ambako mimi ninatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie kwa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, sijui kama anazijua changamoto au matishio dhidi ya ufugaji wa samaki kwa vizimba katika Ziwa Victoria? Ninaomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini. Sasa hivi kuna matishio makubwa yameanza kule Ziwa Victoria, hususan kwenye ufugaji wa samaki kwa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wazawa sasa hivi hawako kwenye ushindani ulio sawa, kwa sababu wawekezaji wa kigeni wamekwishatamalaki kwenye Ziwa Victoria. Wengine wamepewa mialo kilometa zaidi ya tano, wakiwemo Wachina na Wazambia. Sasa Waziri akumbuke kule kwao China, kwa mfano wakichukua mikopo, wanachukua kwenye benki kwa asilimia mbili lakini wazawa sisi hapa wakienda kwenye benki ili wawekeze kwenye vizimba, watapigwa mikopo kuanzia asilimia nane mpaka 24%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa wawekezaji wa kigeni watakuwa ma-*giant,* watakuwa na uwezo wa kuzalisha samaki kwa wingi, watatawala masoko na teknolojia. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, wafugaji wazawa watatelekeza vizimba, kwa sababu hata uwezo wa kushindana hawatakuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuhakikisha kwenye mazingira kama haya hawa wafugaji wa vizimba wa kigeni waweze kupata leseni ambazo zina mazingira tofauti. Kwa sababu nimejaribu kufuatilia, mazingira ambayo yanaondoa kabisa ushindani ulio sawa, leseni zao na za wazawa hazina utofauti. Sasa tishio hili Waziri asipolifanyia kazi wafugaji wazawa watatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kumeanza pia, kuwa na wawekezaji wa mitaji ya *briefcase*. Wanatoka kule hawana hela, wanakuja humu wanazungukazunguka, wanapata mikopo

kwenye benki halafu wanaenda kuwekeza kwenye vizimba. Ninamwomba Waziri ajaribu kuhakikisha kwenye eneo la samaki ahakikishe kwamba, zile *inputs* zote ambazo ni sehemu ya mtaji waweze kuwalinda wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje tunakuwa na sera za kulinda viwanda vyetu vya ndani, halafu tushindwe kuwalinda wafugaji wa vizimba ambao ni wazawa, ili kweli waweze kujenga kesho iliyo bora! Hivi kweli, *Tyson* unaweza ukampambanisha na Kiduku au Mwakinyo? Si ni kumuua tu yule!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye suala la uvuvi haramu pale Ziwa Victoria, maeneo ya Jimbo la Mwibara. Mheshimiwa Waziri hii sasa hapana, kuna wavuvi hao wamekuja na teknolojia, ninadhani unaifahamu au umeisikia, inaitwa *manyamu* au *machoteni*. Wanatoka Wilaya ya Busega wanasogea pale Sozia mpaka Kisoria, wana marungu, wana mapanga, wana mawe, wanakatakata nyavu za wavuvi wengine, halafu wanavua kiharamu kwa kutumia hayo *manyamu*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Uvuvi wapo wanawaona na hata wakienda kufanya doria wanawafanya kama mtaji sasa wa kujipatia fedha. Pambana na uvuvi haramu. Nimesikia hapa kwamba, kuna utaratibu wa kufunga Ziwa Tanganyika. Sisi ambao tuko kwenye Ziwa Victoria ni kweli kwenye dagaa tumejaribu, kuna kitu kinaitwa *mtegeruko*, watu *wanategeruka* wanaacha ziwa linapumua halafu wanapata dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo wakifunga Ziwa Tanganyika kwa sababu ya huu uvuvi mwingine na wakaona kwamba, kufunga Ziwa Tanganyika hakutoshi! Sisi Ziwa Victoria tuna wasiwasi kwa sababu, tunajua sasa sisi ndiyo tunafuata. Ninaomba Serikali isije ikajaribu kufanya kitu kama hicho, waimarishe doria. Doria ndizo zitanusuru haya maziwa. Wakifunga maziwa haya na watu wengine wana mikopo, Wasifikiri tu hawa vijana tuliowakopesha ndiyo wana mikopo, kuna wafanyabiashara ambao pia wana mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye sekta hii muhimu ya uvuvi, ingawa mimi siyo mvuvi wala siyo mfugaji sana, lakini nimeshawishika sana kuchangia sekta hii kwa sababu ya mambo makubwa ambayo nimeona yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa niliyokuwa ninaisoma ya kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Bashiru, nimeona mafanikio makubwa kwenye sekta hii ya uvuvi. Hivyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kukuza sekta zote nchini bila kuchagua, ikiwa ni pamoja na hii ya uvuvi na mifugo. Tumeona, hapa inaonesha kazi kubwa zilizofanywa; kwa mfano, nilikuwa Mjumbe wa Kamati hii mwanzoni na tulikuwa tunazungumza habari ya kuwa na meli ya uvuvi. Hapa leo nimeona katika taarifa kaka yangu, Mheshimiwa Bashiru amesoma kwamba, sasa meli ya uvuvi imekwishanunuliwa kwa njia ya ubia. Sisi tunaendelea kupongeza mpango huo wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapo bandari ya uvuvi pia, tumeizungumza, Kilwa Masoko na imefikia 97%. Yote haya ni mafanikio, lakini tukiangalia kwenye upande wa uzalishaji wa mazao ya uvuvi karibu tani 659,000 zimepatikana, ambayo ni ongezeko kama la 10%, lakini pia jumla ya maboti 219 pamoja na vizimba 509 vimetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yote ni mafanikio katika sekta ya uvuvi. Programu ya mafunzo kwa vitendo, kupitia programu za *BBT,* ambapo zaidi ya shilingi 30,000,000,000 zinaendelea kutolewa kwa vijana kuhakikisha kwamba, tunaongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo wakati tumeanza ilikuwa ni kelele, lakini ninafahamu tu ma-*curtail* walioko humu, wanasiasa pamoja na watu wa Serikali walileta shida. Waligoma ile chanzo cha kuweka hereni, lakini nikachangia, mnakumbuka, nikasema jamani wanasiasa waiache Serikali ifanye kazi maana wakati mwingine mambo huwa yanakwama kwa sababu, sisi tunahusika, kwa hiyo, tuipe nafasi Serikali ifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Bashiru, ninamjua amekuwa mjumbe wangu, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira. Mjumbe mwaminifu aliyenitumikia mimi, kama Mwenyekiti, kwa uaminifu sana. Nilivyosikia amepewa Uwaziri wa Uvuvi nilifurahi sana na ninamfahamu pia, Katibu Agnes Meena, ni watu wazalendo. *Sasa ndugu yangu Bashiru umeingia mahali pana wahuni wengi na mahali pagumu, tukiwemo sisi wanasiasa na wafanyabiashara wengine walioko Serikalini.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua sasa mijadala mingi inaendelea hapa kufunga au kutokufunga mabwawa na maziwa. Ninamshauri Waziri kwa uaminifu kabisa, mimi kama mzalendo kwamba, kutakuwa na manung'uniko mengi, lakini aongozwe na sayansi, aongozwe na utafiti, huo ndiyo msingi wake. Maana kila mtu atalalamika, hata mimi ninaweza kuja kulalamika kwa lolote, wewe kwa sababu, huwezi kumdhulumu mtu, ninamjua uzalendo wake, hawezi kumwonea mtu, ahakikishe anaongozwa na sayansi…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** ...na aongozwe na utafiti, hakuna lingine. Yaani hakuna lingine...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, kuna Taarifa.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anachangiaje vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere kwanza sijakuruhusu.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** aah!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mchangaji anachangiaje vizuri, lakini ninaomba tu kwamba na yeye ana mamlaka makubwa sana hapa Bungeni, kusema hii Wizara ina wahuni wengi na wanaochangia ni wahuni! Ninaomba afute hiyo kauli, siyo nzuri sana kwa mamlaka yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere hiyo ni Taarifa au?

Kwa sababu, kwa mujibu wa kanuni na hicho ambacho unakisema, hiyo haiwezi kuwa Taarifa, *unless* ulete kwa utaratibu mwingine. Kama nimemsikia Mheshimiwa hakumaanisha hicho.

Tuendelee, Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaamini kaka yangu alikuwa amesinzia kidogo, ninajua huu ni mchana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Sasa mambo ambayo ninataka kushauri, kwanza tuhakikishe…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Wewe usinipotezee muda. Tuhakikishe mamlaka... *(Kicheko)*

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kangi Lugola.

**TAARIFA**

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Jackson Kiswaga anaanza kuchangia alijipambanua kwamba, yeye hatoki kwenye ziwa lolote hapa nchini. Ninaomba nimpe Taarifa kwamba, kuna msemo au methali inayosema, uchungu wa mwana aujuaye mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nimpe hiyo Taarifa kwamba, sisi tulioko kwenye maziwa ndiyo tunajua matatizo tunayoyapata, kama maziwa yatafungwa. Nimeona nimpe Taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nipokee Taarifa tu. Ni kweli sitoki huko, lakini ninazo taarifa nyingi zinazohusu mambo ya uvuvi na mifugo, kwa hiyo, nimeipokea Taarifa kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaloomba kushauri, nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Uvuvi, Mifugo, Kilimo na Maji tulishauri mamlaka ianzishwe, ili kusaidia kuisimamia sekta ya uvuvi ambayo ina wadau wapatao kama 6,000,000 ambao wanahusika na hii sekta. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na chombo ambacho kinaweza kuwasaidia kudhibiti kwa sababu, tunataka tuwe na uvuvi endelevu, uvuvi utakaoishi. Hatutaki uvuvi utakaokwisha leo, tunataka vizazi vya sasa na vya baadaye viendelee. Ndiyo maana suala la udhibiti halina mbadala wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye mipango ya matumizi bora ya ardhi ni muhimu sana kuendelea kufanya hivyo kwa sababu, migogoro kati ya wafugaji na wakulima imeendelea kuwa mingi kwa hiyo, suala la matumizi bora ya ardhi, Serikali iendelee kujipanga polepole. Ni nchi yetu, wavuvi wanazidi kuongezeka, wafugaji wanazidi kuongezeka, kwa hiyo, tuendelee kuona namna gani tunagawanya maeneo vizuri, ili tuweze kuimaliza migogoro, lakini ninaona ndiyo namna bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba washirikiane sana na sekta ya maji kwa sababu, sekta ya maji tulianza, ninamalizia tu hii kwa sababu, tulianza ule mpango kabambe wa matumizi ya maji, ambapo ndani yake tumesema kuwe na maji, kwa ajili ya wanyama, binadamu na kilimo. Washirikiane vizuri, ili watu wa mifugo wapate mabwawa kutoka kwenye sekta ya maji, wakishirikiana mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, yako mengi tutayaandika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Isack Joseph Copriano; wajiandae Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga na Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo na Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo. Nina-*declare interest,* mimi ni mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri, tunaona ni jinsi gani kila anapotua kuna jambo linaonekana kwamba, Mheshimiwa Bashiru amefika hapo.

Kwa kuwa, dakika sita ni chache, ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mambo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaiomba Wizara hii, kumekuwa kukizungumzwa sana mambo ya migongano kati ya wakulima na wafugaji, halafu tunapata muda mchache wa kujadili jambo hili. Ninasema tu kwamba, jambo hili la wakulima na wafugaji ni jambo ambalo limejadiliwa Bungeni kwa muda mrefu, sasa *solution* ni kutafuta nafasi ya Waheshimiwa Wabunge kuzungumza namna bora ya kutatua changamoto hii kati ya wakulima na wafugaji, ili isiendelee kuwa ni jambo ambalo linajadiliwa Bungeni kila mara. Hilo litakuwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Tarehe 14/11/2025, alisema maneno mazuri ambayo ninatamani sana Mheshimiwa Waziri atembee kwenye eneo hilo. Alisema ataongeza maeneo ya malisho kutoka 3,000,000 mpaka 6,000,000. Sasa ikoje? Iko hivi, lazima tuyaainishe haya maeneo ambayo tunafikiri tunatamani sana yawe ni maeneo ya malisho. Je, ni kwenye vijiji tunakwenda kutathmini maeneo tuliyonayo? Je, ni kuongeza kwenye maeneo ya ranchi? Je, ni kupunguza kwenye maeneo hata ya hifadhi zetu? Je, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* Wizara yake atuambie mikakati gani wanayo ya kwenda kutafsiri Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya kuleta matumaini makubwa au tabasamu kwa Watanzania, hususani wafugaji. Ninaomba sana kwa sababu, hivi tunavyozungumza ranchi zetu nazo sasa hivi zimekuwa kama ni taasisi, hata wakikamata ng'ombe, wanapiga faini kubwa. Hivi kuna maeneo sasa hivi tunavyozungumza, na ninaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo jambo; kuna wananchi huko Morogoro ng'ombe wameshikwa zaidi ya siku mbili, wamefungiwa ndani mpaka sasa hivi. Ni vyema wakaona jinsi ya kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza zaidi jinsi ya kufanya kupata malisho. Mfano, tutengeneze taasisi na taasisi, tuna maeneo mengi ambayo tunaweza kuvuna majani, hata kwenye hifadhi zetu kuliko kuchoma tuvune majani, tuweke kwa kanda,

tuwauzie wafugaji. Punde wanapopata matatizo haya wanakwenda kununua kwenye Taasisi kama *NFRA,* sasa hivi ina chakula kwenye kanda zote. Lazima watengeneze nafasi ya kuvuna majani kwa kipindi hiki tumepata mvua za kutosha, wangetengeneza maeneo ya kuvuna majani, ili kuwauzia wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni lazima tuhakikishe tunajenga mabwawa. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, tunalo bwawa kule Monduli Juu lililojengwa na Hayati Edward Moringe Sokoine miaka ya 1980, limedumu mpaka mwaka 2005. Sasa limekufa lile bwawa na ndiyo lililokuwa linabeba zaidi ya vijiji 30 kwenye Wilaya ya Munduli. Ninamwomba na ninatamani kusikia kama bwawa hilo na lenyewe lipo kwenye mikakati ya kulifufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Wizara sasa ije na mpango kazi na tafiti juu ya kuwapa wafugaji elimu ya kufuga mifugo yenye faida kwa sababu, tukiwa na mifugo mingi ambayo haina faida, haina maana. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ijipambanue vizuri kutengeneza nafasi na kutoa wataalam wazuri wa kwenda kutoa elimu juu ya ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti; ili waeleweke kabisa, siyo kila mahali mifugo inaweza ikastawi. Kuna mifugo kwenye Kanda ya Kaskazini inaweza ikakubali, kama bohemia, kuna mahali pengine hawakubali. Lazima tafiti zifanyike kuhakikisha kwamba, wananchi wanapewa elimu, ili wawe na elimu nzuri ya kufuga mifugo michache yenye tija tuondokane na kufuga mifugo mingi isiyokuwa na tija. Lazima Mheshimiwa Waziri ajipange vizuri kutengeneza wataalam ambao watakwenda kuhakikisha wanatufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, chanjo. Wanajua fika na Mheshimiwa Waziri nilipata muda wa kuzungumza naye, lazima tuwe tunawa-*promote* wawekezaji wanaotengeneza chanjo nchini, ili waweze kuzisambaza na kuhakikisha kwamba, wanazuia za nje zisiingie, ili za nchini zifanye vizuri na wananchi wetu waendelee kupata kipato. Ni lazima wasimame kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo ni lazima wajenge majosho. Wanajua kabisa kwamba, majosho nchini ni uhitaji mkubwa wa wafugaji, watengeneze majosho ya kutosha. Sijui kama kwenye hotuba yake ameyataja, lakini ninatamani sana Mheshimiwa Waziri majosho mengi yajengwe. Ranchi hizi za Taifa ni vyema, kama wenzangu walivyosema, kama tunataka kubinafsisha na kuwapa wawekezaji tuangalie *percentage*, lakini tusimpe mtu li-*ranch* lote akalihodhi mwenyewe pale, ndipo Watanzania wa kawaida wanawakamata wanawatesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima wafanye *research* kwenye *ranch* zetu tulizonazo. Je, zote zinafanya vizuri? Au zimekaa tu zime-*hang*? Nyingine zimekuwa mapori, zimekuwa misitu; je, tuna mikakati gani, kama Wizara, kwenda kusimama na kutengeneza *ranch* zile na kuzifufua, ili kuhakikisha tunakwenda vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri, ni lazima huu mgongano uliopo na ninashukuru kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu anapopita anasema sisi wafugaji ni ndugu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** ... na wakulima kwa hiyo, ninaomba sana tuweke mikakati mizuri ya kutatua hizi changamoto, ili wananchi wetu waweze kuwa na ufugaji bora na sio ufugaji wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2026/2027. Ninaanza mwanzo kabisa kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, lakini pia, kwa msaidizi wake,

Naibu Waziri, kwa kipindi chote toka ameteuliwa tunaona kazi kubwa, ambayo anaifanya ya kumsaidia Waziri na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote walioko katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Baada ya kusema hayo, ninatoa salamu za kipekee kabisa za wananchi wa Hanang kwa moyo wao wa shukrani, hasa wafugaji, kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusababisha sasa angalau wameanza kupata mikopo katika Benki ya *CRDB*. Hili tunamshukuru sana na ninaomba salamu hizi zimfikie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wafugaji wanampenda na wanamshukuru sana kwa hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni ambayo inaweza kuisaidia sana nchi yetu katika kupata fedha za kigeni na fedha za ndani. Wizara hii bila kuwa na miundombinu bado tutaendelea kuona kwamba, hii sio Wizara ya kimkakati ya kuleta fedha kwa kiasi kikubwa, fedha za kigeni pamoja na fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii lazima ijiwekeze katika majosho. Kama tunahitaji kuwa na mifugo ya kisasa, yenye tija, ninaamini tutatoka kuwa wa pili katika Afrika tutakuwa, kama kuna namba nyingine zaidi ya moja, basi tunaweza tukawa namba nyingine zaidi ya moja. Kwamba, tukawa tumefanya kwa ukubwa wake na tukazalisha siyo tu kuwa wa 10 kidunia, tukawa wa pili, watatu au wa kwanza huko kidunia na Afrika tukawa wa kwanza kwa sababu, ya miundombinu na uwekezaji mzuri katika kuhakikisha mifugo yetu inapata malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya majosho inaenda sambamba kabisa na mabwawa. Ni lazima tuhakikishe kwamba, tunapata mabwawa na mabwawa haya yanaweza kutoa fursa kubwa, siyo tu kwenye mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika, lakini pia, kwenye mabwawa tunaweza kupandikiza na kuwekeza samaki na vijana wengine wakaweza kupata ajira. Mbali zaidi tunaweza pia, kutumia mabwawa haya, yakiwa makubwa, basi yakaweza kusaidia kwa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la watumishi katika Wizara hii, mimi ninatolea mfano wilaya yangu, wilaya yangu ina uhitaji wa watumishi 129, lakini waliopo ni watumishi 25. Nina upungufu wa watumishi 104, hii unaona kabisa ufanisi hauwezi kuwa na malengo ya Dira 2050 kwa sababu watumishi ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ruzuku ya madawa, lakini madawa au elimu inayohusiana na masuala ya Mifugo, Wizara hii imejitahidi kwa sasa hivi mnaona mpaka wanauza mbegu za majani, lakini ni nani ambaye anapeleka taarifa kwa mwananchi kule Gidahababieg, kwa mwananchi kule Bassotu, kwa mwananchi kule wa Bassodesh ili waweze kupata taarifa sahihi? Ni lazima tujiwekeze katika kuajiri watumishi katika Wizara hii na hususani kwenye kata zetu na vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bila kuwa na watumishi ni lazima wananchi wetu waendelee kuonewa. Wataonewa katika huduma za madawa zinazotolewa. Huduma za madawa nani anadhibiti? Nani anachoma sindano kule chini kabisa kwenye vijiji vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nina wataalam 25, nina upungufu wa wataalam 104, maana yake ni kwamba hatutakuwa na uwezo wa kuzalisha ng'ombe bora, tutakuwa na uwezo wa kuzalisha ng'ombe ambao tunakimbizana nao mnadani na wanatusaidia tu hapa ndani kwa kula kinyonge na kiubishi hivyo hivyo. Ni lazima tujiwekeze kabisa katika wataalam ili pia tuweze kudhibiti bei na wananchi wetu hususani wafugaji waweze kuendana na Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la minada. Ninatolea mfano na hapa ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, nina minada mikubwa minne ya ng'ombe. Mnada wa Endagaw, mnada wa Bassotu, mnada wa Bassodesh, mnada wa Katesh. Fedha hizi ambazo wanachukua mapato kupitia uuzaji wa ng'ombe, tunaomba sana Wizara ijitahidi kurejesha ili kuweza kuboresha miundombinu baada ya wao kuchukua zile fedha ambazo wanaziokota kule kwenye minada baada ya mauzo yetu ya ng'ombe, basi zirudi ili zitengeneze miundombinu mizuri na

tuweze kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema kwamba, Wizara hii lazima iwekeze kwa watu wake ambao ni wafugaji. Wafugaji hawaeleweki katika ardhi yao ya Tanzania. Mfugaji anakutana na *TFS*, mfugaji kwenye kijiji anakutana na mkulima, mfugaji amekuwa ni sehemu ya kuhamahama, hajui kesho asubuhi ataamkia wapi. Bahati mbaya sana, mfugaji akikamatiwa ng'ombe, amenusurika sana amepigwa faini, lakini wakati mwingine wafugaji ng'ombe zao zinataifishwa na hili halifanyiki huku juu, linafanyika na watendaji wa chini ambao siyo waaminifu lakini wanaumiza kwa kiwango kikubwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wana imani kubwa na Serikali yao ya Chama Cha Mapinduzi, wana imani kubwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo ni lazima Wizara hii ione namna ya kuwalinda wafugaji huko chini katika kuonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, katika suala la Uvuvi, tuhakikishe kwamba tuna maziwa mengi makubwa, lakini hata yale maziwa madogo madogo tuweze kuleta samaki na nchi hii karibu kila Wilaya ina bwawa, ina ziwa, ambalo linaweza kuzalisha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni lazima tuangalie, mifugo yetu, mbegu zetu zinastawi wapi ili ujue Kanda ya Kaskazini utapeleka mbegu gani na Kanda zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaunga mkono hoja, lakini Wizara hii ni lazima Wizara ya Fedha iongezee bajeti ili iweze kutufikisha katika Dira ya Mwaka 2050. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, sasa ninamwita Mheshimiwa Mwatumu Mzamilu Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Kwanza kabisa ninaomba nirekebishe kidogo jina langu, Mwantumu Mzamilu Zodo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kutaka kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja na sisi tumekuwa tukishuhudia, lakini ninaomba niwapongeze Wizara pamoja na Waziri na watendaji wote kwa Wizara hii. Nimeipitia bajeti yote na nimeisoma kwa umakini sana, nimeona mikakati yao, mikakati ni mizuri kama itatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu, kabla sijaenda kwenye mchango ni bajeti. Mimi kama alivyoongea msemaji wa mwisho kabla yangu, ninaomba Serikali ijaribu kuiangalia Wizara hii kwa jicho lingine tena kwa sababu bado hatujapitisha ile bajeti kuu. Nimeshtuka sana kuona zile fedha kwa ajili ya maendeleo, badala ya kuongezeka zinapungua na hapa kila Mbunge akisimama anaomba majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Mbunge mmoja tu hapa alisimama peke yake tu akaomba majosho 20. Bado wengine na wengine hawajasimama. Sasa kwa bajeti hii, ninapata wasiwasi kidogo, kwa hiyo niiombe sana Serikali yangu sikivu ijaribu kuiangalia tena kwa mara ya pili, Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunayo changamoto kubwa ya ajira. Tukitoa watu walioajiriwa Serikalini na sekta binafsi, sekta ambazo zinatoa ajira ni sekta ya kilimo, uvuvi pamoja na mifugo, kwa hiyo hii ni moja ya sekta ambazo zinatoa ajira, kwa wananchi wetu, kwa vijana, wazee, akina mama. Kwa hiyo ni Sekta muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizipongeze jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mfano, kama sisi Tanga mwaka jana alileta zile boti za uvuvi, tulipata boti 38, Sisi tuna wilaya nane, lakini Wilaya nane kati ya Wilaya nane, Wilaya nne zote zimepitiwa na bahari na wananchi wetu shughuli zao kubwa kule ni uvuvi, lakini changamoto kubwa walikuwa wanavua kwa kutumia zile kokoro ambazo sasa hivi hazitakiwi kabisa na zinapigwa vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakishaachana na zile nyavu ambazo hazitakiwi, wanakuwa hawawezi kwenda kwenye

shughuli zao za uvuvi, kwa sababu hawana hivi vifaa vya kisasa ni gharama kubwa na Wizara peke yao hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana hawa wadau wa taasisi za kifedha kama *CRDB, NMB* na Benki yetu ya Kilimo, hawa wamekuwa ni msaada mkubwa sana. Sasa kwa mfano kama mwaka jana, zile boti 38, katika Wilaya ile moja tu ya Tanga, maana yake tuna Wilaya nne pale za Uvuvi. Wilaya ya Tanga tulipata boti 15 tu na kati ya hizo boti 15, walioomba, ilikuwa ni vikundi 47. Kwa hiyo sasa hapo unaweza ukaona, vikundi 32 vyote bado havikupata boti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vikundi vina watu kumi kumi na wale hawawezi kwenda kuvua kwa sababu wana zile nyavu za bei rahisi. Ile boti ikija inakuja na *package* yote na zile nyavu za kisasa ambazo zinatakiwa. Hii boti moja ni 135,000,000 mpaka 160,000,000. Mwananchi wa kawaida, wa kipato cha kawaida, hawezi kumudu kununua hii boti bila ya aidha kupata msaada wa Serikali au kupata mkopo kupitia kwenye hizo taasisi za kifedha ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa unaweza ukaona kama vikundi 32 vilibaki, vyenye watu kumi kumi, ina maana kuna watu zaidi ya 300, ambao wana familia, hawawezi kwenda kutafuta kile kipato chao cha kila siku. Mwaka huu tuna maombi ya vikundi 35, mwaka jana vimebaki 32, lakini bado tuna maombi ya vikundi 35. Kwa hiyo unaweza ukapata hiyo picha na hawa watu ni wale wanaotegemea uvuvi, ili walipe ada wanategemea Uvuvi, ili walipe kodi wanategemea uvuvi na sasa hivi hawawezi kwenda kuvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana Wizara, wajaribu kukaa chini, lakini washirikiane na hizi taasisi za kifedha ili kuokoa maisha ya hawa wananchi, sasa hivi hali zao ni duni kimapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda wangu umekwisha, ninaunga mkono hoja, mengine nitaandika kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko. Mheshimiwa Kinjekitile Ngombale Mwiru atajiandaa, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kupongeza jitihada za Serikali chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anatoa kipaumbele katika sekta hii ya mifugo na uvuvi. Tumeona, dhamira yake ya dhati kabisa kuleta mageuzi katika sekta ya mifugo na uvuvi. Niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati baada tu ya kuapa, kupata ziara ya Mheshimiwa Waziri pia Naibu Makatibu Wakuu nao walikuja, kipindi hicho wakiwa bado hawajakuwa kwenye nafasi hizo ninashukuru sana nimeona kwamba wana nia ya dhati kabisa kuleta mageuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Waziri na nimefurahishwa sana na mikakati ya Serikali, hasa katika kufanya ufugaji wa kimkakati pamoja na uvuvi wa kimkakati. Nimeona dhamira ya dhati ya Serikali katika kuwekeza au kuvutia uwekezaji katika ufugaji wa mifugo hasa kwa kuongea mikataba na wale wafugaji wakubwa wanne, kuwekeza zaidi katika kile kituo chetu cha umahirishaji wa mifugo cha *NAIC* cha Arusha, lakini pia katika kuendeleza mashamba ya mitamba ya mifugo na kuweza kuvutia uwekezaji zaidi katika vitalu vya *NARCO*. Imani yangu ni kwamba kupitia vitalu vya *NARCO* tutapata wawekezaji zaidi wakubwa ambao watafuga kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa pia na nia ya dhati ya Serikali pamoja na Wizara kuona kwamba tunaimarisha ulinzi wa rasilimali za maji, yaani rasilimali za uvuvi, pamoja na kuziendeleza. Ninategemea kwamba katika upande huu basi wa

Uvuvi, basi uvuvi utakuwa unazingatia sheria, lakini pamoja na kuendeleza yale mazao ya maziwa yetu pamoja na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchache wa muda nitaongea machache. Jambo la kwanza nitaanza katika sekta ya uvuvi na kwenye sekta ya uvuvi nitajikita zaidi katika Wilaya yetu ya Muleba, hasa katika Jimbo la Muleba Kaskazini ambalo mimi pia ni mwakilishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tuna changamoto kubwa ya raia wa kigeni kuingia katika ziwa letu la Victoria. Sisi tulitarajia kwamba, kwa vile Serikali imewekeza zaidi katika masoko ya mazao ya uvuvi, basi wale raia wa kigeni watakuwa wanaenda kule kununua aidha dagaa au samaki katika yale masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ambacho tunakiona ni kwamba, hawa raia wa kigeni wanaingia na kwenda kwenye visiwa na kununua samaki na dagaa. Ninaamini kabisa, nia ya dhati ya Serikali ilikuwa ni kwamba kuwawezesha wananchi waweze kwamba, wao ndiyo wavue, lakini pamoja na kuja kuleta kwenye masoko kwa ajili ya kuuza, lakini tunapoona raia wa kigeni wanafika na kuingia kwenye ziwa na kuvua, hasa kwenye Visiwa vyetu vya Kelebe na Goziba, hii inatayarisha kabisa ustawi wa jamii pamoja na uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hivyo ni kwamba tuna changamoto nyingine ya uvamizi kwenye Ziwa Victoria, hasa upande wa Muleba kuna raia wa kigeni, wanakuja wanavamia wale wavuvi na kuwajeruhi pia kuwapora dagaa na samaki wao. Kwa hiyo, ninadhani ni kwamba Serikali inapaswa ijipange sasa katika eneo hili kuona kwamba tunakuwa na ulinzi au kufanya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kimetoa ahadi kwamba kitanunua boti tatu za doria katika upande wa ziwa, upande wa Wilaya ya Muleba. Ninaamini kabisa tukinunua hizi tupate hizi boti tatu, pamoja tukiimarisha na ulinzi wa doria katika ziwa letu tutaweza kukabiliana na hawa raia wa kigeni ambao wanaingia na kuvamia wavuvi wetu pamoja na kuwapora dagaa au samaki wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la msingi ambalo ninaomba pia Serikali ione na nimeona hapo kwenye bajeti wamelisisitiza ni kwamba, Serikali imejipanga kuona kwamba inajenga na kuendeleza Soko la Mazao ya Uvuvi la Kyamkwikwi lililopo Kata ya Izigo. Ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri alishafika pale akaliona, lile soko limefikia 26%, ninaamini kwamba Serikali itawekeza zaidi ili kuona soko hili linakamilika ili wananchi waweze kupata thamani ya uvuvi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kumalizia ni kwamba kwenye Wilaya ya Muleba tuna changamoto ya uhaba wa chanjo ya ugonjwa wa miguu na midomo ya mifugo yetu, ninaomba sana Wizara iliangalie hili ili kuona kwamba tunapata chanjo hii kwa kupitia ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba pia tuna uhaba na changamoto ya wataalam wa mifugo. Tunao wachache, Wilaya ya Muleba ina Kata 43, lakini tunao wataalam 21, tunaomba sana Serikali iliangalie hili pamoja na kuwawezesha pia pikipiki. Kwa upande wa majosho pia tuna uhaba wa dawa za kuogeshea mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishie hapo na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, sasa ninamwita Mheshimiwa Kinjekitile Ngombale Mwiru.

**MHE. KINJEKITILE N. MWIRU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii. Kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili, ningependa sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa, pia ningependa kukishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuongoza wananchi wa Kilwa. Shukrani za dhati na za kipekee, ninapenda kumshukuru Mwenyekiti wa Chama Changu Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na mwisho ningependa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini pamoja na familia yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeifuatilia hotuba ya Waziri, ninapenda kumpongeza kwa hotuba nzuri aliyowasilisha leo Bungeni. Ninaomba nichangie hoja zangu, kwanza kabisa ninapenda nimshukuru tena Rais wangu Dkt. Samia Suluhu kwa kutujengea bandari kubwa ya uvuvi ya kisasa katika Wilaya yetu ya Kilwa Kaskazini, Mkoa wa Lindi, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielekeze mchango wangu kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni migogoro ya wafugaji na wakulima. Ninatokea katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ambalo asili yetu ni uvuvi na ukulima, lakini hivi karibuni shughuli za mifugo zimeongezeka sana ambazo zimekuwa zikituletea matatizo mengi sana kati ya wananchi na wafugaji, ambayo yametusababishia madhara mengi sana na kuhatarisha usalama wa wananchi, kusababisha vifo, majeruhi na kupoteza mali. Hivyo tunaiomba Serikali kulichukulia jambo hili kwa uzito wa kipekee kukomesha kabisa matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na la mwisho ni shughuli za uvuvi. Wilaya yetu ya Kilwa ina fukwe za takribani kilomita 170 ambazo wananchi wanashughulika na shughuli za uvuvi, ninaomba Mheshimiwa Waziri atuangalie kipekee katika mgao wako wa maboti sisi wananchi wa Jimbo la Kilwa, kwa sababu uvuvi ndiyo uti wa mgongo wa wakazi wa Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, wajiandae Mheshimiwa Dickson Lutevele na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Ndugu yetu Bashiru kuwa Waziri katika Wizara hii, ni mtu muhimu sana katika maisha yetu, ninamshukuru sana Naibu wake,

ninamshukuru sana Katibu Mkuu na viongozi wote na watendaji wote wa Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kakurwa ujamaa tuliokuwa tunauona enzi hizo siyo ujamaa uliopo sasa hivi. Ujamaa wa zamani viongozi walikuwa wanakaa wanajadiliana wanatenda, saa hizi mnaweza mkajadiliana halafu ukigeuza kisogo hakuna kinachotendeka. Sasa ninamwomba achanganye ujamaa na ubepari kidogo ili mambo yaende saa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri. Pale Bunda tuliahidiwa na Naibu Waziri aliyekuwepo na bahati nzuri sasa amekuja mwingine...

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa, kwa kifupi.

**TAARIFA**

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa mujibu wa Katiba ni nchi ya ujamaa na kujitegemea, ninataka nimpe taarifa mzungumzaji, sijui kama anaongea kwa utani au *serious*, neno ubepari kwamba uchanganywe na ujamaa anafanya makosa makubwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniface Getere unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea ni mtazamo wake, mimi nimemwambia Mheshimiwa Waziri kwamba awe mkali, sijasema akatae ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri tafadhali, alikuja Naibu Waziri pale Bunda tulikuwa na kaya 200 ambazo ziliomba ng'ombe wa maziwa na bahati nzuri sasa tuna kiwanda, tuna *industrial park* ya maziwa kutoka Jambo lakini ng'ombe tuliowapata madume ni 20 tu kati ya 200. Waziri alikuwa ametuahidi kwamba atatupatia ng'ombe 40 tena ili watu wetu

sasa wabadilike kwenda kuchunga kule porini, wakawe na maziwa kwa sababu tayari tuna viwanda sasa hivi ninamwomba sana, kwa sababu tunayo mashamba ya Serikali na tuna mashamba ya *NARCO* na sera ya Serikali huko nyuma mashamba ya Serikali yalikuwa ni kupatia watu mitamba, sheria sasa hivi ninaona kama haipo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tuombe mashamba ya Serikali yatusaidie kupata mitamba, yatusaidie kupata madume na *NARCO,* Mheshimiwa Waziri ndiyo maana ninasema kwamba sasa aone, tusipoangalia haya mashamba ya *NARCO* yatakuwa ya wafanyabiashara wakubwa tu. Wanakaa, wamepanga mikataba! Mikataba! Mikataba! Akija Waziri mwingine mpya anamwambiwa bwana tayari mashamba yote yana mikataba. Wanasubiri uchaguzi unakaribia tukishaenda kwenye uchaguzi wanaanza mikataba, akija Waziri mpya kuna mikataba! Tusipoangalia hakuna madaraka yoyote atakayofanya kwa *NARCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* nenda pale Missenyi, maeneo yote yaliyopakana na Uganda wanachunga watu upande wa kule tu. Mashamba makubwa makubwa yapo, mtu anapewa shamba zima ana ng'ombe 100, ana ng'ombe 300, halafu anakodisha. Ninaomba mashamba ya *NARCO* yaangaliwe mara mbili mbili.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, Taarifa. Niko hapa.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa, itakuwa Taarifa ya mwisho hiyo.

**TAARIFA**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa Taarifa Mheshimiwa Getere kwa mchango wake mzuri. Katika Wilaya ya Misenye tuna vitalu vingi vya mifugo, lakini vitalu hivyo hakuna hata kimoja ambacho kina mwananchi kutoka nje ya Tanzania. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia imeweka Depo ya

Jeshi wanalinda mipaka yetu vizuri na wananchi wa Wilaya ya Misenyi wanaendelea kufaidi matunda ya Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea. Sasa nisipokee ninafanyaje wakati tunawatetea watu wetu na watu wa kule, ni jamaa zetu sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tafadhali, tulikuwa na mnada wa ng'ombe pale Mikomaliro. Mnada ule mnada wakautoa. Hivi kuna vigezo gani vya kuondoa watu wanataka *study* yao? Sisi vijijini minada ni *study tour*, sasa watu wameanzisha mnada wao umekaa pale miezi 12 halafu unauondoa, wala hakuna mapato, watu wanalia kila siku. Nitakwenda ofisini kwa Waziri tuangalie namna gani ya kurudisha ule mnada ili watu wa kule waweze ku-*enjoy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Bashiru, hivi kweli; unajua katika Bunge hili ndiyo maana kuna Waheshimiwa Wabunge fulani tunaungana pamoja, kisha tunakuwa ma-*group*. Hivi ni nani alipanga ratiba ya siku moja kwa hii Wizara? Ni nani na ni kwa namna gani? Hivi kweli wizara hii ambayo inalisha watu nchi nzima? Ukitaka maziwa ni ng'ombe, ukitaka ngozi ni ng'ombe, ukitaka nini ng'ombe, leo wanakula balenge humu ndani, kwato, balenge, ng'ombe, kila kitu ng'ombe, inapangwa siku moja! Haiwezekani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, hoja ya ratiba siyo sehemu ya mjadala, kwa hiyo jielekeze kwenye mjadala ulioko Mezani…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wangu ni kwamba, nimwombe Mheshimiwa Waziri, baada ya bajeti hii kupita, tunaomba tukae sisi wafugaji na wakulima pamoja tutoe matatizo yetu. Tupate nafasi ya kukaa na Mheshimiwa Waziri. Matatizo ya ng'ombe ni mengi. Kwa hiyo akimaliza hii hoja ya bajeti yake, tukae pamoja. Suala la kuhusu

utaratibu asizingatie, atuite tu twende, hatutamhoji chochote, tunampelekea hoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana, ninaomba kwa kweli siku nyingine wanaopanga ratiba wasiweke hivyo, wanatuumiza. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia afya. Pili ninawapongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende moja kwa moja kwenye hoja kulingana na muda tulionao. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumzia suala zima la migogoro ya ardhi. Suala la migogoro ya ardhi nchini limekuwa ni donda sugu. Suala la migogoro hii sielewi, nilisikia Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa kwenye ziara zake akasema hataki kuona wataalam ama watumishi wa Serikali wakizoea shida za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninashangaa, shida za Watanzania ni pamoja na suala la migogoro baina ya wafugaji na watu wa hifadhi na vilevile baina ya wafugaji na wakulima wetu. Ni nini shida? Nini changamoto? Ni tatizo gani ambalo linasababisha Serikali kutokuitatua migogoro hii, ili kila mmoja wetu ndani ya nchi hii aweze kuishi kwa amani na utulivu na kwa haki anayostahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ikija, ituambie, changamoto ni nini kwenye suala la kuwapatia wafugaji maeneo yao mahususi ambayo wanastahili kuweka mifugo yao kwa ustaarabu na kupewa huduma nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo, kaka yangu Mheshimiwa Getere ametoka kusema hapa; suala la nyama humu ndani tukiulizana leo nani ambaye hajala nyama, nani ambaye hajanywa maziwa hayupo. Lakini ng'ombe hawa tumekuwa tukiwaona ni adhabu, ng'ombe hawa tumekuwa tukiona ni laana, kitu ambacho si sahihi; na sisi kama Taifa pia hatujitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji huyu leo ndiye anayesomesha watoto wake kwa kutumia fedha ya mifugo yake, bila Serikali kumpelekea josho, bila Serikali kumpelekea bwawa, bila Serikali kufanya chochote. Anahangaika mwenyewe kwa jitihada zake. Anasomesha watoto wake, analisha familia yake na mambo mengine. Wakati wengine tumekuwa tukiwatumia wafugaji hawa kwenye shughuli zetu mbalimbali; hata za Kiserikali. Tuna mwenge, tunawafuata wafugaji watupe ng'ombe ili tupate kitoweo. Kwa nini hatutaki kuwathamini wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, suala la migogoro ya ardhi kwa wafugaji, twende tukatatue tatizo hili ili tuwaache hao wafugaji waweze kuishi maisha yenye amani na utulivu ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ambalo ninatamani kulisema ni kuhusu mikopo kwa wafugaji. Mfugaji wetu kitu pekee anachoweza kuweka dhamana ni ng'ombe, kwa sababu ndiyo biashara anayofanya. Leseni yake kubwa ni mifugo yake; lakini leo wafugaji hawawakopeshi wanawaambia kwamba ng'ombe hawezi kuwa dhamana. Kwa nini, eti kwa sababu hana uhai, anaweza akafa, anaweza akaugua, anaweza akafanya nini. Hivi haya maduka yanayoungua Kariakoo na kwingine yanakochomwa moto huko? Kwa nini hawa wafanyabiashara wengine hatuwanyimi mikopo? Kwa nini mfugaji ananyimwa mkopo eti kwa sababu ng'ombe wake anaweza akapata madhara akafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia, kwenye suala la mikopo twende tukatumie mifugo ya wafugaji kama dhamana na sehemu ya kupatiwa mikopo ili waweze kuboresha

miundobinu yao pamoja na kuboresha mifugo yao ili tuweze kujikwamua kiuchumi katika maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la majosho limesemwa; Wilaya ya Chemba ninaomba majosho; Wilaya ya Chemba ninaomba malambo; tuna hali mbaya, hali ni tete. Kwa hiyo suala la majosho na malambo Wilaya ya Chemba ninamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuna mnada wetu mkubwa sana wa soya, ambapo mnada huu hata Mheshimiwa Rais alivyokuja kuwaomba kura alituahidi kwenda kujenga mnada huu. Lakini kwa kuwa tumekuwa tukisafirisha ng'ombe wetu kwa kuwaswaga lakini na kupakia kwenye magari; tunawaswaga ng'ombe, tunaharibu miundobinu ya barabara; tunawapakia ng'ombe kwenye malori, tunawatoa Kagera hadi Dar es Salaam, foleni ng'ombe wanakufa barabarani wanapata ajali, wakulima wetu wanaendelea kupata hasara. Mheshimiwa Rais alituahidi kutujengea pia kiwanda kwa ajili ya uchakataji wa mifugo yetu ambayo inatokana ndani ya Wilaya yetu ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani kusikia neno na Wanachemba na wafugaji wa Chemba wanatamani kusikia neno juu ya suala la kiwanda cha kuchakata mifugo inayotoka Wilaya ya Chemba na kwenda kunusuru uharibifu mkubwa unaofanyika kwenye suala la uharibifu wa barabara. Pili, kuokoa maisha ya ng'ombe na hasara zinazomkuta mfugaji kwa kumsafirisha kwa muda mrefu na ng'ombe yule kufariki ama kupata ajali njiani. Tatu, walaji wetu wa nyama kwenda kupata nyama iliyo bora badala ya kwenda kupata manati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa muda wako na Mungu akubariki sana, uishi maisha marefu kwa hii nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninamwita Mheshimiwa Fadhili Liwaka, ajiandae Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaungana na Waheshimiwa

Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Balozi Kakurwa kwa kazi kubwa na namna ambavyo anahuisha shughuli za sekta hii ya uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu nijielekeze kwanza kwenye kupongeza namna ambavyo hotuba hii imechagiza na imetoa mwelekeo kwenye vipaumbele vya msingi ambavyo sisi kama Taifa tunatamani kupiga hatua kwenye eneo hili la mifugo na uvuvi. Mimi ninatoka Jimbo la Nachingwea na ninaanza kabisa kwa kuleta ombi kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba, ninakuomba sana, moja ya maeneo ambayo ninatamani afike, aje kutembea, lakini pia kuona kazi kubwa ya kilimo na shughuli hizi za mifugo, basi ni Nachingwea na ninazo sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania ni wamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi kwamba tumeshaweka msingi wa Kitaifa kwamba Mtanzania yeyote atafanya shughuli yoyote mahali popote. Mimi binafsi ni muumini kabisa wa kupokea shughuli zote zinazofanywa na Watanzania. Moja kati ya shughuli ambazo nazithamini na kuziheshimu ni shughuli ya ufugaji, lakini lazima niweke rekodi yangu sawasawa. Mimi ni mtoto wa mkulima na nilishawahi kuwaambia baadhi ya watu kwamba pia ni mwindaji; lakini kwa sababu jamii ya Wanachingwea ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Nachingwea imezaliwa, tangu wakoloni wameondoka kwenye mashamba, kuanzia shamba namba moja hadi shamba namba 19, hakuna wakati ambao wamewahi kupigana vita ya kugombea ardhi wala kugombea chakula. Katika siku za hivi karibuni kumeibuka tatizo kidogo na hapa ninaomba nieleweke, kwamba ufugaji tunaupenda na mimi ni mdau namba moja wa wafugaji. Hata hivyo, kilimo pia ndiyo maisha ambayo yametukuza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba, baadhi ya maeneo ikiwemo Nachingwea, suala la mifugo limegeuka kuwa changamoto na ni changamoto

ambayo kila kunapokucha inaibua matatizo na mnyukano baina ya jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati wa kampeni nikiwa ninaomba ridhaa ya wananchi, 75% ya jimbo langu nililoomba kura wananchi walilalamikia juu ya mgogoro wa mifugo kwenda kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wafugaji wamegawanyika; wako wafugaji ambao wanaijua taaluma ya ufugaji kwa kufuata misingi na taratibu zilizowekwa. Hawa tunawafahamu vizuri kabisa na wako hapa, lakini wako wafugaji wamejificha kwenye kivuli cha kutokujua sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti ninataka kuwaomba sana, kundi lolote la wafugaji ambalo linajificha kwenye kivuli cha kutokujua sheria ni makusudi ya kuvunja sheria. Wataalam wa sheria watanikubalia kwamba kutokujua sheria hakuwezi kukupa nafasi ya kufanya makosa. Kwa hiyo kule kwangu ninapata shida sana, na majimbo mengine ya Kanda za Kusini, kwa sababu kumekuwa na tabia ya makusudi kabisa ya wafugaji kuchukua mifugo kwa makusudi kutoka kwenye maeneo waliyopangiwa, kwenda kulisha kwenye mbaazi. Mbaazi Nachingwea ni biashara, tunasomesha, tunajenga na tunakuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha msimu wa mahindi, ninataka kumwambia Waziri, pale mahindi yatakapoanza kuvunwa, moja ya changamoto tutakayokutana nayo ni pamoja na wafugaji kupeleka mifugo yao mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimewaambia ninawapenda sana wafugaji na kule Nachingwea nimewaruhusu. Sasa tufanye vikao na Mheshimiwa Waziri anisaidie, nimpate kiongozi wa wafugaji ili tuongozane. Kwenye jimbo langu sitaki wapigane, ninataka tufanye vizuri, tuwe na sherehe kabisa siku ya wafugaji na wakulima kuondoa haya matatizo. Wafugaji watoe ng'ombe, watoe mbuzi tuchinje na wakulima wenzetu watoe mahindi, watoe mpunga na mtama tupike wali tucheze ngoma. Watu waoane; wafugaji na wakulima wa Nachingwea, tuzaliane tujue ufugaji ni biashara, kilimo ni biashara na kuishi pamoja ni maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninayasema haya? Ninasema kwa uchungu mkubwa kwa sababu rekodi zangu hapa zinanionesha, katika kipindi cha miaka mitatu, moja ya athari tulizozipata, jumla ya ekari zilizoharibiwa za mazao ya chakula ni ekari 115, lakini mazao ya biashara ekari 165 zimeharibiwa. Nachingwea peke yake watu waliopoteza maisha ni watu saba kwa kupigwa mishale. Ninataka kukwambia, siyo kwa kuchekesha, mfugaji unayemsikia na analenga mshale hakuna mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alishapigwa mwalimu wangu mshale jichoni umetokea upande wa pili; *this is not just a story,* kwamba ninachekesha, ni kitu ambacho kimetokea kabisa, watu saba. Watu 23 Nachingwea wamejeruhiwa na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matukio haya huwezi kukuta mkulima amempiga mfugaji. Unajua ni kwa nini? Sababu ni moja tu, mkulima wa Nachingwea, mkulima wa Ruvuma, mkulima wa Kilwa, mkulima wa Liwale, hajui kurusha mshale, hajui kurusha jembe, hajui kurusha shoka wala rungu. Anajua kutumia jembe kwa kulima shambani, anajua kutumia upanga kwa kukata mafukutu ili aweze kufanya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie mtoto wake na kijana wake, aniangalie hapo kwenye *screen* kwa jicho la huruma. Moja ya jambo ambalo nimeji-*commit* kwa wananchi wa Nachingwea ni kwenda kuhakikisha kwamba tuna-*harmonize situation* ya mgogoro huu ili uwe salama. Baba yeye atanisaidia, ninamwomba sana twende Nachingwea tukakae na wakulima, tutafute viongozi wa kimila wanaohusiana na jamii hizi ili tuweze kuzungumza lugha moja tufanye maisha ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dickson Lutevele Villa, ajiandae Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake. Kimsingi tumeona kazi kubwa ambayo wanaifanya na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kumpa moyo Mheshimiwa Waziri. Yako maeneo mawili ninaomba kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumesikiliza na kuangalia michango mingi sana kwenye Ufugaji na Uvuvi, unaona watu wanaoinuka ni wale walioko kwenye Kanda za Maziwa au kule ambako kuna wafugaji wengi. Sasa ninaomba nitoe ushauri. Ushauri wangu ni kwamba, sasa hivi kufuga siyo tena *issue* ya kanda, sasa hivi kufuga ni biashara, kufuga ni fursa. Tumeona soko kubwa la maziwa sasa hivi hapa nchini kwetu. Wafanyabiashara wanajenga viwanda vya maziwa. Tumeona, ili uweze kula samaki, kwa mfano sisi tunaotoka Nyanda za Juu Kusini, ama awe ametoka Mwanza au awe ametoka Mtera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo unaona kwamba, soko kubwa la samaki lipo, lakini kama Wizara haijaja na mikakati mahususi ya kuhakikisha kwamba kila sehemu kunakuwa na fursa za mtindo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaenda kwa mfano kwenye Uvuvi. Ninaomba kuishauri Wizara, iweke mpango yakinifu. Hapa tumekuwa tukizungumza sana kuhusu ajira za vijana, lakini ajira kubwa sana ya vijana tungeweza kuiweka pia kwenye uanzishwaji na uendelezaji wa mabwawa ya samaki; iwe ni ajenda ya Wizara. Leo hii tunasimama hapa watu wa maziwa walioko kandokando ya ziwa, wanavuta vizimba. Wako watu wanalalamika ufungwaji wa Ziwa Tanganyika; lakini kumbe tungekuwa na mbadala hata hawa wasingekuwa wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba kuishauri Wizara, ianze kuangalia namna bora; wakati tunafunga ziwa, kuwe kuna vijana au kuna wafugaji wa samaki ambao

hawategemei ziwa. Tuanze kujifunza kutazama namna gani tunaachana na yale mazoea, kwamba samaki lazima atoke ziwani, kumbe samaki anaweza kutoka kwenye bwawa. Huo ni mfumo ambao mataifa mengi wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mawazo yangu pia kwenye mifugo. Sasa hivi soko la nyama limekuwa kubwa sana, soko la maziwa limekuwa kubwa sana. Tunaomba tuuone mpango wa wizara. Wizara iache kutembea kwenye mipango ya zamani ije na mpango mpya wa namna gani watu wa Nyanda za Juu Kusini wanashiriki kwenye kufuga ng'ombe wa nyama na kushiriki kwenye kuzalisha maziwa ili viwanda vilivyopo Tanzania vianze kupata maziwa kutoka humu humu ndani. Ni fedheha sana kwa Taifa letu kuagiza maziwa kutoka nje wakati ndani wapo watu wanalalamika hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tunategemea ubunifu na umahiri wa Mheshimiwa Waziri tuuone kwenye kuendeleza maeneo haya ambayo hayana historia ya ufugaji wa samaki, wala hayana historia ya ufugaji wa ng'ombe wa nyama na wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, ninaomba kushukuru na ninaunga mkono hoja. Hata hivyo, sisi tunasubiri tuone mapinduzi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kwa kuhakikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapata fedha za kutosha na kuwawezesha kusambaza vifaa muhimu katika maziwa yetu yote. Nimpongeze pia Waziri, Mheshimiwa Bashiru Kakurwa na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri kufanyike utafiti kwa nini kuna uvuvi haramu kwa wakati huu kitu ambacho kwa miongo ya nyuma haukuwepo, kudhibiti nyavu zisizofaa ili

kuondoa kiini cha tatizo ulinzi uongezwe kutumia vifaa vya kisasa vya kidijitali kubaini wavuvi haramu, niombe kutoa ushauri kwa Mkoa wa Arusha. Tunaomba Serikali ije na mkakati thabiti wa kujenga mabwawa ya maji ya kunyweshea ng'ombe na mifugo mengine, katika maeneo ya Wilaya ya Monduli, Longido, Ngorongoro yanakuwa na hali mbaya sana wakati wa kipindi cha ukame (kuvuna maji mengi tunayoyapata wakazi wa mvua za masika)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ije na mpango mkakati wa kuanzisha ufugaji wa samaki katika ukanda huu na hii kupitia vikundi vya akina mama na vijana wapate ujuzi kupitia wataalam kutoka wizarani, hii itatusaidia kuongeza ajira, kukuza uchumi wa mkoa wetu. Tuanze kwa haraka uzalishaji wa majani kwa ajili ya malisho ya mifugo kuunda idara itakayoshughulikia na kupanua masoko ya mifugo na ngozi ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote katika Wizara wa Mifugo na Uvuvi. Ninaunga hoja mkono kwa kesho iliyo bora.

**MHE. ENG. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa maandishi. Kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassani. Kwa mapenzi makubwa na kwa niaba ya Wanabumbuli ninaipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi; hasa Mheshimiwa Waziri Balozi Dkt. Bashiru Ali Kakurwa pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Ng''wansi Kamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote walio chini yao. Pongezi hizi kwa Wizara ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti yenye dira, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini na kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wa Jumla (Kitaifa); kuhusu Maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi; Sekta ya mifugo na uvuvi nchini Tanzania zina mchango mkubwa katika ajira, usalama wa chakula, pato la Taifa, biashara na maendeleo ya viwanda. Licha ya kuwa na mifugo mingi, maziwa makubwa, mito, bahari na mazingira mazuri ya ufugaji na uvuvi, bado sekta hizi zinakabiliwa na changamoto nyingi kama:-

(i) Ufugaji wa kienyeji usio na tija;
(ii) Magonjwa ya mifugo;
(iii) Uhaba wa malisho;
(iv) Uvuvi haramu;
(v) Miundombinu hafifu;
(vi) Teknolojia duni; na
(vii) Ukosefu wa viwanda vya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Kimkakati kwa Tanzania. Tanzania inapaswa kuelekea kwenye:

(i) Ufugaji wa kisasa;
(ii) Uvuvi wa kisasa;
(iii) Uchumi wa buluu *(blue economy);*
(iv) Viwanda vya kuongeza thamani;
(v) Matumizi ya teknolojia; na
(vi) Uwekezaji katika masoko na Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo Muhimu ya Kitaifa; kwanza; kuboresha ufugaji; kuanzisha ranchi za kisasa; kuboresha mifugo; kuongeza huduma za chanjo; na kuanzisha benki za malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kukuza uvuvi wa kisasa kwa kudhibiti uvuvi haramu; kujenga bandari za kisasa za uvuvi; kuanzisha *fish farms*; na kuongeza vifaa vya kisasa vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuongeza viwanda; viwanda vya nyama, maziwa, ngozi, samaki na chakula cha mifugo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuimarisha Miundombinu na Masoko; barabara za vijijini; *cold storage*; masoko ya kisasa; na mifumo ya kidigitali ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Vijana na Wanawake, kuwapa mikopo na mafunzo kwa vikundi vya uzalishaji, ubunifu wa kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yanayotarajiwa ikiwa mapendekezo haya yatafanyiwa kazi: Uzalishaji utaongezeka, ajira zitapanuka, mapato ya wananchi yataongezeka, Tanzania itakuwa kitovu cha biashara ya mifugo na samaki Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mahususi kwa Jimbo la Bumbuli kuhusu Maendeleo ya Mifugo; Uvuvi na Uchumi wa Kijamii. Jimbo la Bumbuli lina uwezo mkubwa wa kuwa kitovu cha ufugaji wa kisasa; kilimo cha bustani; ufugaji wa samaki; nyuki na utalii wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo lina Hali nzuri ya hewa, yenye rutuba, maji ya kutosha, mazingira mazuri ya milimani, nguvu kazi ya vijana. Changamoto kubwa za Bumbuli ni Barabara duni vijijini, ukosefu wa masoko ya uhakika, mitaji midogo kwa vijana, teknolojia duni za uzalishaji, ukosefu wa viwanda vya kuongeza thamani, huduma chache za mifugo na uvuvi. Mwelekeo wa Maendeleo ya Jimbo, Jimbo linapaswa kuelekeza nguvu kwenye; maziwa, kuku, mbuzi, ufugaji wa samaki, matunda, mboga, asali na viwanda vidogo vya usindikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo muhimu ya kukuza uchumi katika Jimbo:-

(1) Milingano; ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama; kuku wa kisasa; kiwanda cha nyama; *fish ponds*; mnada wa kimkakati wa mifugo na majosho ya kisasa.

(2) Mahenzanguu; ufugaji mchanganyiko Mashamba ya mazao ya mifugo na kiwanda cha nyama.

(3) Soni; Kiwanda kikubwa cha kukusanya maziwa maeneo yote kwa kuwa ndio lango kuu la Halmashari ya Bumbuli na pia karibu na barabara kuu Machinjio ya viwango vya kuweza kukusanya mazao ya nyama kutoka maeneo ya Jimbo la Lushoto na Mlalo.

(4) Baga; ufugaji wa mbuzi, nyuki, matunda. Maboresho ya mnada na Majosho yaliyopo.

(5) Kwemkomole *Fish ponds, Poultry projects na* ufugaji wa mbuzi wa kisasa.

(6) Nkongoi; kilimo cha mboga, maziwa, umwagiliaji kwa ajili ya mazao ya mifugo.

(7) Bumbuli na Dule B; *fish ponds,* ufugaji wa maziwa na kiwanda cha maziwa.

(8) Mayo na Kisiwani; utalii, trout farming na kilimo cha matunda.

(9) Usambara; *Eco-tourism* na *Organic farming*.

(10) Vuga; Mafunzo, viwanda vya chakula vya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Jumla kwa Bumbuli ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuboresha barabara za vijijini;
(ii) Kujenga masoko ya kisasa;
(iii) Kuanzisha *cold rooms;*
(iv) Kuwezesha vijana na wanawake;
(v) Kuimarisha vyama vya ushirika,
(vi) Kuanzisha viwanda vidogo vya maziwa; Asali; Nyama na matunda;
(vii) Kutumia teknolojia za kisasa za uzalishaji; na
(viii) masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa uwekezaji mzuri na mipango ya kimkakati, Bumbuli inaweza kuwa Kitovu cha kilimo

cha milimani; Mfano wa ufugaji wa kisasa; Eneo la utalii wa mazingira; na Chanzo kikubwa cha ajira kwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jimbo yatategemea; Miundombinu bora; Elimu na mafunzo; Ushirikiano wa wananchi; na Uwekezaji wa muda mrefu katika sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN S. LUHENDE** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kuhusu umuhimu wa kuboresha sekta ya ufugaji katika Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kueleza kuwa sekta ya ufugaji ni uti wa mgongo wa uchumi wa wananchi wengi wa Jimbo la Bukene. Maelfu ya wananchi wetu wanategemea ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku pamoja na shughuli nyingine za mifugo kwa ajili ya chakula, kipato na maendeleo ya familia zao. Pamoja na umuhimu huo, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazozuia kufikia tija inayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni upungufu wa huduma za mifugo. Katika maeneo mengi ya Jimbo la Bukene, wananchi wanakosa huduma za wataalamu wa mifugo, chanjo pamoja na dawa muhimu za kutibu na kuzuia magonjwa. Hali hii husababisha wafugaji kupata hasara kubwa kutokana na vifo vya mifugo na uzalishaji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kuongeza idadi ya maafisa ugani wa mifugo, kujenga vituo vya huduma za mifugo na kuhakikisha dawa pamoja na chanjo zinapatikana kwa wakati katika kata zote za Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni uhaba wa maji kwa ajili ya mifugo. Wafugaji wetu mara nyingi hulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji, hasa kipindi cha ukame. Hali hii husababisha migogoro kati ya wafugaji na wakulima na

kupunguza uzalishaji. Ninaiomba Serikali kujenga mabwawa ya maji, visima na miundombinu ya kuvuna maji katika maeneo ya wafugaji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni ukosefu wa maeneo rasmi ya malisho. Ongezeko la watu na matumizi mengine ya ardhi limeongeza migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Muhimu Serikali iharakishe upangaji bora wa matumizi ya ardhi, kutenga maeneo ya malisho na kuyapima ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongeza thamani ya mazao ya mifugo ni muhimu pia. Wafugaji wetu bado huuza mifugo yao ikiwa hai kwa bei ndogo badala ya kupata thamani kupitia usindikaji wa nyama, maziwa, ngozi na bidhaa nyingine. Ninaiomba Serikali kuvutia uwekezaji wa viwanda vya kuchakata bidhaa za mifugo karibu na maeneo ya uzalishaji ili kuongeza ajira na mapato ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni wakati sasa wa kuwawezesha wafugaji kupata mikopo nafuu, mafunzo ya ufugaji wa kisasa, pamoja na masoko ya uhakika. Bila mtaji na elimu ya kisasa, ni vigumu kwa sekta hii kukua kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihitimisha, Jimbo la Bukene lina uwezo mkubwa wa kuwa kitovu cha uzalishaji wa mifugo endapo Serikali itawekeza katika huduma za mifugo, maji, malisho, elimu na masoko. Kuboresha sekta hii siyo tu kutainua maisha ya wafugaji, bali pia kutachangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono jitihada za Serikali.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu imechangia takribani asilimia sita ya pato la Taifa *(GDP)*, lakini pia ni chanzo kikuu cha kipato, usalama wa chakula na lishe bora. Kupitia uzalishaji wa mazao kama nyama, maziwa,ngozi na samaki sekta hii imeendelea kuimarisha viwanda vya ndani na

kuongeza mauzo ya nje na kuweza kuongeza fedha za kigeni zinazo chochea ukuaji thabiti wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi na Usindikaji wa Mazao; ninapenda kuipongeza sana Serikali kwa dhamira yake ya dhati kwa wananchi na kuthibitisha kwa vitendo kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta hii kwa lengo la kumkomboa mwananchi kiuchumi na kuliletea Taifa maendeleo endelevu. Serikali imewekeza kwa kutoa mikopo ya boti za kisasa kwa wakazi wa mikoa ya pwani hususani Mkoa wa Mtwara. Mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali pia ilitenga shilingi bilioni 9.5 kwa ajili ya kutoa boti 100 za kisasa na boti saidizi 76 kwa wananchi wa mwambao ili kuwezesha wavuvi wadogo wadogo ikiwemo Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwezeshaji wa Vijana na Wanawake *BBT* - Uvuvi: kupitia programu ya jenga kesho iliyo bora (*BBT*-UVUVI) Serikali imetoa hundi ya shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya kuwapatia mitaji vijana waliohitimu mafunzo ya ukuzaji viumbe maji na uvuvi kibiashara. Wananchi wa Mkoa wa Mtwara tayari wanatumia rasilimali zinazotokana na bahari ingawa uvuvi wa kwenda maji marefu unafanywa zaidi na wanaume na zaidi ya 70% ya shughuli za uchakataji na uuzaji wa mazao ya baharini zinasimamiwa na wanawake ikiwemo kufuga majongoo, zao la mwani, usindikaji unahusisha uongezaji thamani wa samaki, dagaa, ngisi na pweza, *prawns* ili kuwafanya wadumu kwa muda mrefu kabla ya kufika sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali, bado kuna changamoto katika sekta hii ya uvuvi kama ifuatavyo:-

(1) Uhaba wa mitambo ya kisasa ya kuchakata mazao hayo;

(2) Changamoto ya masoko na Dijitali;

(3) Mila potofu zinazo kandamiza wanawake kuhusu kumiliki mali;

(4) Uhaba wa vinu vya barafu;

(5) Teknolojia duni ya kukausha;

(6) Hakuna viwanda vikubwa vya kukausha na kusindika bidhaa;

(7) Gharama kubwa za Nishati ya umeme;

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali mambo yafuatayo kuboresha zana, miundombinu na teknolojia juu ya ukaushaji wa bidhaa na kutoa mafunzo ya kuongeza thamani ya bidhaa hizo; Kuwezesha vifaranga vya samaki na kamba ili kuongeza uzalishaji; Kujenga na kuongeza vizimba vya kufugia samaki na kamba; Kudhibiti uvuvi haramu; na Uhifadhi wa mazingira

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo Mkoani Mtwara, kihistoria ni mkoa unaotegemea kilimo cha korosho na shughuli za uvuvi, hali inayofanya mwamko wa sekta ya mifugo hususani n'gombe, mbuzi na kondoo kuwa chini ikilinganishwa na Mikoa ya Kanda ya Kaskazini au Kanda ya Ziwa.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kuleta mageuzi makubwa katika sekta za mifugo na uvuvi. Ninawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na watumishi wote wa sekta ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Mifugo ninashauri yafuatayo:

(i) Serikali iendelee kuvutia wawekezaji katika ufugaji wa mifugo wa kimkakati. Ninapongeza Serikali kwa kuingia mikataba na wawekezaji wanne wa kosafu bora za mifugo kwa nia ya ufugaji wa kitaifa wa kimkakati. Ninashauri Serikali iendelee kuvutia wawekezaji wakubwa wa kimkakati katika eneo hili ambao utaleta mageuzi makubwa katika kuongeza uzalishaji na tija wa mazao ya mifugo.

(ii) Uwekezaji katika vitalu vya *NARCO* uwe wa kisasa. Serikali iendelee kusimamia ili kuona uwekezaji katika vitalu vya *NARCO* unakuwa wa tija zaidi kwa kukodisha vitalu kwa wawekezaji wenye uwezo, watakaofuga kisasa.

(iii) Uhaba wa chanjo ya *FMD* katika Wilaya ya Muleba. Wilaya ya Muleba imekuwa na milipuko ya mara kwa mara ya ugonjwa wa miguu na mdomo ya mifugo kwa wanyama wenye kwato. Chanjo hiyo inapatikana katika sekta binafsi ambayo ni ghali katika sekta binafsi (Sh. 3,000 mpaka 3,500 kwa chupa). Tunaomba kuletewa chanjo ya *FMD* ya ruzuku.

(iv) Ukosefu wa dawa za kuogeshea mifugo katika Wilaya ya Muleba. Halmashauri ya Muleba imejitahidi kujenga na kukarabati majosho, lakini Wilaya ya Muleba ina ukosefu wa dawa za kuogeshea mifugo hasa za ruzuku.

(v) Uchache wa wataalamu wa mifugo katika Wilaya ya Muleba na pikipiki. Wilaya ya Muleba ina kata 43 na ina wataalamu wa mifugo 21. Tunaomba kuongezewa wataalamu wa mifugo. Halmashauri imepewa pikipiki 11 tu, tunaomba pikipiki nyingine kama Serikali ilivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi:-

(i) Raia wa kigeni kuingia katika visiwa na kununua dagaa na samaki badala kununua katika masoko. Serikali ifuatilie suala hili kwa kushirikisha vyombo vya dola ikiwemo Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Uvamizi huu umekuwa ukitokea katika Ziwa Victoria upande wa Wilaya ya Muleba hasa Visiwa vya Goziba, Kereba na Bumbire. Hii inarudisha nyuma jitihada za Serikali za kujenga uchumi wa wananchi wazawa.

(ii) Uvamizi wa wavuvi katika Ziwa Victoria unaofanywa na raia wa kigeni. Serikali ifuatilie uvamizi huu ikiwezekana

kuunda kikosi kazi cha kufuatilia matukio kama haya pamoja na uvuvi haramu.

(iii) Ununuzi wa boti za doria kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM inavyoelekeza. Tunaomba Serikali inunue boti tatu za doria kwa ajili ya Visiwa vya Goziba, Kereba na Bumbire.

(iv) Ukamilishaji wa soko la samaki na dagaa katika mwalo wa Kyamkwiwi, Kata ya Izigo, Muleba ambao umefikia 26%. Serikali ikamilishe soko hili ambalo limechukua muda mrefu kukalimika.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa aliyoyafanya katika sekta ya mifugo na uvuvi na hasa kwenye utoaji wa chanjo ya mifugo, lakini pia kwenye eneo la uvuvi hasa kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia uzinduzi wa meli kubwa ya uvuvi katika bahari kuu tarehe 25/4/2026 yenye uwezo wa kuvua zaidi ya tani 48 kwa safari moja. Tumeshuhudia pia Miradi ya Vizimba vya Samaki katika Ziwa Victoria ambavyo vimetoa fursa ya ajira kwa baadhi ya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ninatoka ukanda wa ziwa mchango wangu nitaulekeza kwenye Ziwa Victoria ili wilaya zinazozungukwa na Ziwa Victoria na hasa Wilaya ya Busega ambayo iko katika Mkoa wa Simiyu ziendane na wakati kuhusu uchumi wa bluu. Ninashauri tuanzishe *pilot project* katika Wilaya ya Busega ambayo itakuwa maalum kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hii ziwa letu liwekewe mipaka ya kisheria na kistratejia, ili kuwe na umbali maalum kuanzia nchi kavu kwenda ndani ya maji (kilomita tano mpaka ishirini) kadri itakavyoonekana inafaa kitaalamu) ambapo itakuwa ni marufuku kwa uvuvi wa kawaida wa nyavu. Kanda hii ijulikane kama “kanda tulivu ya mazalia”

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hapa ni kutengeneza "benki ya samaki" ambapo ndani ya eneo hili lililotengwa haitaruhusiwa kufanyika shughuli zozote za uvuvi ili kuondoa usumbufu kwa mazalia ya samaki. Tukifanikiwa kufanya hivi tutatengeneza mazalia ya uhakika ya samaki kwani samaki watapata mazingira tulivu ya kuzaliana kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia kuwa, Wizara ije na mpango madhubuti ya kuzalisha vifaranga kisayansi na kisha kuvirudisha ziwani ili viendelee kuzaliana na kwa kuwa eneo hili litakuwa tulivu, ninaamini kabisa kuwa vitaendelea kuzaliana kwa wingi. Hapa isiwe kwa Busega tu bali maeneo yote yanayozungukwa na Ziwa Victoria ili kukabiliana na upungufu wa samaki kwenye ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo hili litafanikiwa na kuwa na samaki wa kutosha kwenye ziwa, ninashauri Wizara ije na mpango wa utalii wa uvuvi *(fishing tourism)* kama chanzo cha mapato kwa Wilaya ya Busega na kwa Serikali pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ikiwezekana kuwe na boti ndogo ndogo maalum kwa ajili ya *fishing tourism* na kwa kuwa Busega iko karibu pia na Mbuga ya Serengeti, tutangaze utalii huu ambapo watalii wataruhusiwa kukodi boti hizi na kupewa ndoano ili waingie ziwani na kuvua samaki *in a traditional way* na kila samaki atakayevuliwa na mtalii apimwe na kulipiwa ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo umuhimu wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Simiyu na ule wa Serengeti unapoingia, kwani kutafungua utalii kwa Kanda ya Ziwa na kukuza uchumi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uvuvi haramu kwenye maeneo mengi ndani ya Ziwa Victoria na Serikali imechukua hatua kadhaa ikiwemo kuwakamata wavuvi haramu na kuharibu zana hizo. Niombe tusiishie hapo tu bali pia tuwachukulie hatua wafanyabiashara wanaouza nyavu hizi na mamlaka ambazo zimeruhusu zana hizi kuingizwa nchini. suala la uwajibikaji hapa ni muhimu sana maana tunatoa adhabu kwa mtumiaji na kumwacha muuzaji akiendelea kuuza zana hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Bunge lako Tukufu wa kuchangia katika Wizara hii. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu, ni Wizara tegemezi katika uchumi wa nchi na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kmpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hasan kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa umakini mkubwa na kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. Ninamwomba Mungu ampe afya njema na maisha marefu yenye manufaa naye. Aidha, ampe wepesi wa kazi zake.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya na kuniwezesha kushiriki mkutano huu. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta nzima ya mifugo na uvuvi, tumeshuhudia uboreshaji mkubwa kwenye sekta hizi, mikopo mbalimbali ya vitendea kazi imetolewa kwa wavuvi. Haya yote yanafanyika kuhakikisha sekta hizi zinaendelea kuchangia pato la Serikali na kukuza uchumi wa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msimamo wa Bajeti 2026/2027; Wizara imepata shilingi trilioni 1.1 kutoka 820,000,000,000 mwaka jana, ongezeko la 34%. Lengo kuu ni kuongeza mchango wa mifugo na uvuvi kwenye pato la Taifa kutoka asilimia 7.2 hadi 10% ifikapo 2027. Vipaumbele ni: kuzuia magonjwa, kuboresha mifugo asilia, kuongeza uzalishaji wa samaki na kuunganisha wafugaji na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kibaha Vijijini hii ni fursa kwa sababu jimbo lina kaya 22,000 zinazofuga ng'ombe, mbuzi, kuku

na uvuvi mdogo mdogo kwenye Mto Ruvu na bwawa la Mlandizi. Aidha, nimeona mambo manne mazuri kwenye hotuba hii yanayogusa Jimbo langu la Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; Chanjo na Udhibiti wa Magonjwa Bajeti imetenga shilingi 120,000,000,000 kwa chanjo ya mifugo nchi nzima. Lengo ni kufikia 80% ya ng'ombe na mbuzi. Kibaha Vijijini kwa sasa chanjo inafikia 41% tu, hivyo magonjwa ya mdomo na kwato, *CBPP* na *Newcastle* yanaua mifugo 2,300 kwa mwaka. Fedha hizi zikifika, jimbo linaweza kufanya kampeni ya chanjo bure kila robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Uzalishaji wa Maziwa na Nyama. Wizara imeeleza italeta ng'ombe 15,000 wa maziwa wa mbegu bora na kutoa ruzuku ya 50% kwa wafugaji. Kibaha Vijijini kina kituo cha maziwa Mlandizi chenye uwezo wa lita 10,000 kwa siku, lakini kinakusanya lita 2,100 tu kwa sababu mifugo ni ya asili na yenye mavuno madogo. Mfugaji akipata ng'ombe wa Friesian na lishe bora, mavuno yanaweza kupanda kutoka lita tatu hadi 15 kwa siku na kuwanufaisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Ufugaji wa Kuku wa Mayai, shilingi 85,000,000,000 zimetengwa kuendeleza kuku wa nyama na mayai. Lengo ni kupunguza uagizaji wa mayai kutoka nje. Kibaha Vijijini kina vikundi 34 vya vijana vinavyofuga kuku, lakini vinakosa vifaranga, chakula na masoko. Mradi huu ukiingia, kila kikundi kinaweza kupata vifaranga 1,000 na chakula kwa miezi mitatu bila riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; Uvuvi wa Ndani na Bwawa; Wizara imetenga shilingi 60,000,000,000 kwa mabwawa 200 ya samaki na mafunzo kwa wavuvi wadogo. Kibaha Vijijini ina Bwawa la Mlandizi na Mto Ruvu ambavyo havitumiki vizuri. Wavuvi 420 wa hapa bado wanatumia nyavu haramu na kupata kilo 2-3 kwa siku. Mradi huu ukiingia, uzalishaji unaweza kupanda hadi kilo 12 kwa siku kwa mvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu ninaomba kuelezea mapungufu matatu yanayoweza kuisababishia Kibaha Vijijini isinufaike:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; Ugawaji wa Fedha Hauzingatii Vijijini. Hotuba haielezi wazi ni kiasi gani kitakwenda kila mkoa. Kila mara fedha nyingi hukwama mikoani na wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; Hakuna Masoko ya Uhakika. Wizara inazungumzia uzalishaji lakini haizungumzii masoko. Kibaha Vijijini inazalisha maziwa lita 2,100 kwa siku, lakini 60% yanamwagika kwa kukosa barabara na friji. Bila kuunganisha na *SGR* Mlandizi na Barabara ya Mlandizi, uzalishaji zaidi utasababisha hasara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Huduma za Mifugo bado ni Hafifu. Jimbo lina Madaktari wa Mifugo wanne tu kati ya 18 wanaohitajika. Hotuba imetenga ajira 2,400 za wataalam wa mifugo nchi nzima, lakini hakuna uhakika Kibaha Vijijini itapata hata 12. Bila wataalam, chanjo na matibabu hayatafika vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kueleza nini kifanyike Kibaha Vijijini 2026/2027 ili kuondoa kasoro au changamoto zote nilizozielezea hapo awali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza; tudai sehemu ya ng'ombe 15,000 na kuku 500,000. Maombi yetu ya mara moja kwa Wizara kupata ng'ombe 300 wa maziwa na vifaranga 50,000 kwa vijana na akina mama. Hii itaongeza kipato cha kaya 1,200 moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili; kuanzishwe Vituo viwili vya Kukusanya Maziwa. Wizara itenge fedha kujenga friji ndogo na vituo Mlandizi na Ruvu. Hii itazuia upotevu wa maziwa na kupandisha bei kutoka Sh. 800 hadi Sh. 1,400 kwa lita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu;kufufua Bwawa la Mlandizi. Wizara itenge bilioni 1.2 kutoka kwenye bajeti yake ya mabwawa 200 kujenga vizimba 40 vya samaki na mafunzo kwa wavuvi 200. Bwawa likifufuka, kila mvuvi ataingiza Sh. 150,000 kwa siku badala ya Sh. 25,000 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya nne; Uhitaji wa Madaktari 12 wa Mifugo, Wizara itumie fursa ya ajira 2,400 za Wizara. Sisi

kama Jimbo tupeleke orodha ya wahitimu 18 wa mifugo waliopo na Serikali iwalipe posho ya mazingira magumu Sh. 250,000 kama ilivyo kwa afya ili wasaidie sekta ya mifugo Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuhitimisha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya 2026/2027 imetoa dira nzuri ya kuongeza uzalishaji wa mifugo na uvuvi. Kwa Kibaha Vijijini, fursa iko kwenye maziwa, kuku na uvuvi wa mabwawa. Changamoto ni kuhakikisha fedha na wataalam wanafika kijijini na masoko yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia fursa hii vizuri, kipato cha mfugaji wa Kibaha Vijijini kinaweza kuongezeka kwa 60% ndani ya miaka mitatu na jimbo liache kuwa la kupitisha mizigo tu liwe la kuzalisha na wananchi kunufaika, ninakubaliana na hotuba hii na mipango ya Wizara, lakini kwa masharti ya kuingiza Kibaha Vijijini kwenye mpango wa ng'ombe wa maziwa, vifaranga na Bwawa la Mlandizi mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa ninamwita Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa utayari mkubwa ambao amekuwa akiuonesha, hususan katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na ustawi mkubwa sana wa watu kupitia sekta ya mifugo na uvuvi; kwa kweli Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri. Ndiyo maana unaweza kuona katika kipindi kifupi alichokaa madarakani, kuna mabadiliko makubwa sana kwenye sekta hii kupitia katika bajeti, utendaji kazi wake, lakini vilevile matokeo makubwa ambayo tumeyashuhudia ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeyatangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, mkubwa wetu, *comrade* Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru. Ninafikiri wote hapa Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, ni mtu muadilifu ambaye anaifanya hii kazi kwa uzalendo mkubwa sana. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri; yeye pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara. Kwa kweli *commitment* inaonekana kwenye hii sekta na tutaona matokeo makubwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo ameisoma Waziri leo unaona kabisa imekusudia malengo makubwa ya kumsaidia mvuvi pamoja na mtu wa mifugo (mfugaji amepata nafuu kubwa). Vilevile, watu wa uvuvi wamepata nafuu kubwa. Nitaonyesha kama eneo moja, hapa unaona katika Serikali imefanya maboresho makubwa ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kwenye vifaa na zana za uvuvi ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha huo umetolewa katika baadhi ya zana za uvuvi na malighafi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, utaona katika eneo la nyavu na nyuzi za kutengenezea nyavu, Serikali imeondoa msamaha wa kodi katika eneo hilo; *engine* za kupachika kwenye maboti, Serikali imeondoa kodi ya *VAT* katika eneo hilo; maboya, ndoano, vifungashio, boti *(fibre boats)* ambazo zimekuwa zikitumika na wavuvi, Serikali imeondoa kodi ya zuio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mitambo ya ubaridi, mitambo ya kuzalisha barafu, magari yenye ubaridi kwa ajili ya kubeba samaki na mazao ya samaki, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* ili kumsadia mkulima. Hayo ndiyo tunayoyasema kwamba unaona nia njema ya Mheshimiwa Rais kumsaidia mvuvi kuhakikisha kwamba tunaleta ustawi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali vilevile imepunguza gharama za leseni na tozo katika maeneo mbalimbali na nyingine zimejumuishwa ili kumpunguzia tu kero mvuvi katika eneo lake. Sasa hapo unaona kabisa ni nia njema ambayo Serikali

imekusudia kusaidia Sekta ya Uvuvi, lakini vilevile na kwenda kusaidia sekta ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kwamba, kwa sasa hivi utaona kabisa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa maana ya Serikali imeruhusu matumizi ya leseni moja ya uvuvi katika eneo moja la maji tofauti na yalivyokuwa awali ambapo unakuta kila Halmashauri ilikuwa inatoa leseni yake. Sasa hivi ukishakuwa na leseni moja ya uvuvi katika eneo la maji utatumia hiyo hiyo leseni hata kama utakwenda katika eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo yote ni kuhakikisha kwamba Serikali inamsaidia mvuvi katika kuhakikisha kwamba tunaboresha ustawi wa maisha yake. Kwa hiyo, bado Serikali itaendelea kuhamasisha uvuvi endelevu na uhifadhi wa mazingira na kuendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika moja ya jitihada kubwa ambazo Serikali imekuwa ikifanya ni kuhamasisha watu vilevile kujiunga na hii elimu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa ya kuhakikisha kwamba uvuvi wa vizimba *(fish caging)* unaendelea na unafanyika ili kuhakikisha kwamba inapofika nyakati Serikali inasema jamani tunafunga Ziwa, lengo letu ni kuacha Ziwa lipumue ili baada ya msimu ule kupita samaki wamekuwa wamezaliana maana yake sasa watakaonufaika ni wavuvi wenyewe. Sasa haya yote ni Serikali imekuwa ikiyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Mheshimiwa Dkt. Bashiru wamekuwa wakiyasimamia kwa vitendo. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Bashiru, Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuipitisha bajeti yake, lakini vilevile kuhakikisha kwamba yale yote aliyoyazungumza tunamsaidia na tunayasukuma ili yaweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri ni mtu makini, ana uwezo, ana nia njema dhidi ya Taifa letu na hatuna shaka kwamba haya yote aliyoyazungumza yako ndani ya uwezo wake na ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, ninakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mtoa Hoja, Waziri wa Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwa na afya njema na kuwa tayari kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia tangu asubuhi ambapo tumepata wachangiaji 30; ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Kamati yetu na ninaomba kuahidi kwamba hoja zote 11 za Kamati kama zilivyoonekana katika michango ya Wabunge tutazizingatia. Mimi sina mengi zaidi ya ufafanuzi mfupi tu wa jumla na ninaahidi kwamba hoja zote za Wabunge na za Kamati tutazifafanua zote kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ya jumla inahusu dhana ya ujamaa ambayo imejitokeza humu ndani. Ujamaa ni imani na mimi ujamaa wangu na wenzangu siyo wa cheo ni wa imani. Misingi ya ujamaa ni kuhakikisha kwamba watu wote mnaishi pamoja kwa kushirikiana, lakini pia mnachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Rais aliomba kura kwa kauli mbiu ya Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. Sitaki kuingiza mjadala kuhusu ujamaa upi na ujamaa wa aina gani kama nilivyosema tukubalie tu kwamba ujamaa ni imani. Ahsanteni sana kwa wale ambao wameanzisha mjadala huu kwa sababu msingi wake ni Katiba ya Nchi na ni Katiba ya Chama Cha Mapinduzi. Kwa sababu hiyo, ninaomba nigusie mambo machache yaliyojitokeza katika mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Uvuvi. Waheshimiwa Wabunge wengi wameshauri kwamba tunahitaji chombo madhubuti kitakachosaidia kusimamia rasilimali za uvuvi na kuhakikisha kwamba uvuvi unaofanyika unazingatia sheria. Jambo hili tumeshalifikisha mahali ambapo lipo katika hatua za maamuzi na tuna hakika kabisa chombo hiki kitatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi haramu; uvuvi unaoendelea bila kufuata sheria lazima tuudhibiti na hatutachoka. Ninadhani Wabunge wote ambao wanaishi katika maeneo ya maziwa wanatoa ushuhuda ambao unaonyesha kabisa kwamba kazi kubwa inatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kuhusu Bandari ya Uvuvi ya Kilwa na Bandari itakayojengwa Bagamoyo. Ninawapongeza Wabunge wote ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa kutambua kazi kubwa anayoifanya. Hata kupongeza na kutambua nafasi ya Mheshimiwa Rais siyo jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukuzaji wa viumbe maji; limetajwa hapa na Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara na mimi nakubaliana na wewe kabisa kwamba hatuwezi tukafanya uvuvi wa vizimba kiholela. Ninadhani ndicho alichokuwa anakizungumza. Lazima tuzingatie taratibu na taratibu zipo na tusipokuwa makini kila mmoja akawa anaweka kizimba mahali fulani tutachafua maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wageni ambao wamewekeza katika ufugaji wa vizimba; lazima tuzingatie maslahi ya wavuvi wadogo na wafugaji wadogo ikiwemo kuhakikisha kwamba wanawekeza mitaji mikubwa katika teknolojia na viwanda vya chakula, kwa sababu tatizo kubwa tulilonalo katika eneo hili siyo maarifa ya watu, siyo utayari wa watu, siyo nguvu kazi ya watu isipokuwa tunalo tatizo la upatikanaji wa chakula cha samaki na upatikanaji wa vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli baada ya kutatua matatizo hayo, wafugaji kwa vizimba wa kawaida wadogo

wadogo wanaweza wakatoa mchango mkubwa bila kuhangaika kuleta wafugaji ambao wanaweza wakawa na mitaji inayofanana na Watanzania ambao wanashughulika na ufugaji wa samaki kwa vizimba. Kwa hiyo, ninadhani hayo malalamiko ambayo yapo tutayafanyia kazi na tutazingatia taratibu za ufugaji zinazozingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe watu wasiweke vizimba kwenye maji bila kufuata utaratibu. Ni muhimu sana tuzingatie utaratibu na utaratibu huo upo. Ninakiri kwamba bado tuna tatizo la chakula cha samaki na tuna viwanda vichache (tuna viwanda viwili tu peke yake sasa hivi). Tunawahimiza wawekezaji waweze kuongeza viwanda vingi vya samaki kwa ajili ya chakula cha samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto zilizotajwa kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima. Hapa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara alizozifanya na matamko na ufafanuzi alioufanya. Hata leo asubuhi kajibu swali la aina hiyo hiyo, lakini niwakumbushe Hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ndiyo ilitumika kufungua Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametuelekeza tuwe wasikivu kwa wananchi. Tusikie shida zao na tuwajibike kwao na kwa kauli yake amesema wasiposikilizwa wananchi na tusipowajibika kwa wananchi, basi tuwe tayari yeye kutubadilisha. Pia, nimeshasema Bungeni hapa na ninarudia sipo tayari kuwa sehemu ya watu ambao Mheshimiwa Rais atawabadilikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limejitokeza katika Hotuba na katika mijadala linahusu masuala ya chanjo na utambuzi wa mifugo. Katika mambo ambayo Mheshimiwa Rais atakumbukwa kwa maarifa yake, kwa utashi wake wa kisiasa, kwa ubunifu wake katika Sekta ya Mifugo, ni suala la chanjo na utambuzi wa mifugo. Hili ni jambo kubwa sana katika historia ya uongozi wa Taifa letu na hapa niwapongeze wafugaji kwa kuelimishana na kuwa tayari kushiriki katika zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kufafanua ni kwamba zoezi hili ni la miaka mitano kule ambako hatujafika wasidhani tumemaliza au tumewaacha. Kama Wabunge wameangalia bajeti tuliyoitenga, tumetenga pesa kwa mwaka unaofuata na hii kampeni imezinduliwa mwaka jana, lakini mapokeo yamekuwa makubwa kuliko tulivyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye eneo la utambuzi wa mifugo, mapokeo yamekuwa mazuri kuliko ilivyozoeleka huko nyuma. Kwa hiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais ninawashukuru sana wafugaji wa Tanzania kwa kupokea hiyo kampeni kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanikiwa ndani ya miaka mitano tutatatua matatizo makubwa mengi sana na hasa upatikanaji wa masoko nje ya nchi, lakini pia kupunguza gharama za ufugaji kwa wafugaji. Kwa hiyo, hili ni jambo kubwa katika sekta ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililosemwa ni la kufunga Ziwa kwa watu wa Tanganyika. Ninadhani hao nikikaa bila kulifafanua hili hatutaelewana. Ninawashukuru sana kwamba wanafuatilia na wameleta hoja za wananchi hapa na kama nilivyosema Mheshimiwa Rais ametuagiza Mawaziri wote tusikilize wananchi. Sasa ninasema hapa mbele yenu kwamba tuko katika hatua ya kufanya tathmini na hatutafunga Ziwa bila kuzingatia maoni ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe kabisa kwamba pamoja na Wizara yetu ya kisekta ya kushughulikia jambo hili, lakini Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ndiyo kinara wa masuala ya mazingira. Kwa hiyo, Wizara yangu na Ofisi ya Makamu wa Rais tunafanya tathmini baada ya jaribio la miaka mitatu kukamilika mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uamuzi wowote tutakaoufanya utazingatia tathmini tutakayoifanya na kwa kalenda ilibidi tufunge kuanzia kesho. Kwa sababu kwa utaratibu kwa miaka mitatu iliyopita tulikuwa tunafunga kila tarehe 15 mwezi Mei hadi tarehe 15 mwezi Agosti. Kwa hiyo, niwaombe

Wabunge wa Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa tusiondoke Bungeni bila kukutana na kushauriana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haimaanishi kabisa kwamba utaratibu wa kufunga hautakuwepo. Kwanza ni wa kisayansi, lakini pili ni makubaliano ya sisi nchi nne tunaotumia Ziwa pamoja. Tulichokubaliana ni kwamba lazima tufanye tathmini kwanza ya matokeo ya miaka mitatu ya majaribio tuliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; makubaliano mapya tutakayoyafanya yazingatie maoni ya wananchi na mahitaji ya nchi pamoja na makubaliano ya sisi watumiaji wa Ziwa hilo. Kwa hiyo, Wabunge wawaondoe wasiwasi wavuvi wa Tanganyika kwamba tunawasikiliza na hatutafanya uamuzi wowote bila kuzingatia maoni yao ambayo yamewasilishwa vizuri hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kusikia kabisa kwamba pamoja na kufunga au kutofunga maziwa yetu hayana samaki. Kwa hiyo maziwa yameshajifunga yenyewe hivyo, kazi yangu mimi ya kujibu suala la kufunga na kutofunga kwa kweli ni rahisi kwa sababu tumeshayafunga wenyewe kwa kuvua kiharamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema sehemu nyingine na ninasema hapa mbele yako; mimi siyo Waziri wa Maji, Waziri wa Maji ni Mheshimiwa Aweso. Mimi ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, sitakubali maji ambayo yanatakiwa yawe na samaki yasiwe na samaki. Maana yake ni sawa na kukataa kazi na mimi kazi hii ninaipenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wale ambao wanaendesha uvuvi usiozingatia sheria hakuna funika kombe mwanaharamu apite, tutapambana bega kwa bega na mimi nina mbinu nyingi kwa sababu ni shabiki wa Yanga. Kufunga magoli na kuyashangilia hilo si tatizo na hapa hakuna masihara. Tunao utashi wa kisiasa na maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Rais ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaenda sambamba na wageni kuingia ndani kiholela na kuanza kuhatarisha usalama katika maeneo yetu ya uzalishaji. Tayari tumeanza mazungumzo kupitia kwa *Chief Whip* na sekta zote zinazohusika kuhakikisha kwamba maziwa yetu yote yanakuwa salama, mipaka yetu yote inakuwa salama, wafugaji na wavuvi wote na wakulima na Watanzania wote wanafanya shughuli zao kwa usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda siyo mrefu wataanza kuona mabadiliko. Ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge tupewe ushirikiano wa kutosha. Tuleteeni taarifa sahihi tuchukue hatua inavyotakiwa. Hili nilitaka nilifafanue kusudi tuweze kuelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo ya ufugaji mimi sina tatizo kukutana nao, lakini ninachotaka kusisitiza; sitaki tuwe Wabunge wa wafugaji kwa kujiandaa kutengeneza uhasama na wakulima au tuwe Wabunge wa kuwakilisha wakulima kwa kutengeneza uhasama dhidi ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero kwa kuitaja Kampeni ya Tutunzane. Hii ni kampeni ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais, ushahidi upo Mheshimiwa Rais ametuelekeza, sisi ni Taifa moja lazima tuishi kwa kupendana na kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa ya wafugaji wawili au watatu wanaorusha mishale yasiwe makosa ya wafugaji wote. Tuwasake na tuwapeleke mbele ya mkono wa sheria. Kwa hiyo, ninawaomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshasema mara nyingi, tunashindana kutumia ardhi ambayo haiongezeki, lakini sisi tunaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maekezo ya Ilani ni kupima ardhi ya wafugaji, baada ya kuipima kuirasimisha, kuilinda kisheria na kuweka huduma ambazo zinahitajika kusudi wafugaji waweze kutumia ardhi bila kupambana au kugombana na wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kuna Mbunge mmoja hapa amesema, sasa hivi ufugaji na uvuvi hauna tena kanda au maeneo. Kwa ufugaji wa samaki sasa hivi unaweza ukafuga mpaka nyumbani kwako kwa teknolojia iliyopo, vivyo hivyo hata kwa mifugo. Kama tunakubaliana kwamba nchi hii ni ya kijamaa, lakini nchi hii kiuchumi ni ya kilimo na kilimo maana yake ni kilimo cha mazao, ni ufugaji, ni uvuvi, ni misitu, ni pamoja na nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna dira yetu inavyosema, mabadiliko yoyote ya kiuchumi roho yake kubwa itakuwa ni Sekta ya Kilimo na huo ndiyo ukweli. Viwanda vingi vitatokana na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na kwa maana hiyo ajira nyingi zitatokana na sekta hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunao wajibu kama viongozi na kama Watanzania kushirikiana kugawana rasilimali zilizopo, kuhakikisha wote tunatumia kukuza uzalishaji. Matatizo makubwa tuliyonayo katika mifugo kama walivyosema ni malisho, ni huduma za afya ya mifugo, ni miundombinu wezeshi ya maji, halafu ni mipango mizuri ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayawezi yakafanywa na Sekta ya Mifugo peke yake, ukisikiliza hotuba ya Waziri wa miundombinu ya barabara atagusa maeneo ya kukuza sekta hizo. Jana Wabunge wamesikia tulikuwa na Waziri wa Uchukuzi, hivyo viwanja vya ndege vinavyojengwa vinahitaji viwe na mifumo ya baridi kusudi nyama ziweze kupitia kwenye viwanja hivyo kusafirishwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Rais lazima sekta zote zishirikiane zifungamanishwe na Wizara tushirikiane na haya ndiyo makubaliano tuliyonayo. Tume ya Umwagiliaji itafanya kazi ya kuhakikisha kabisa kwamba inaweka miundombinu ya umwagiliaji kwa Sekta nzima ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mwenyekiti wa Kamati ya Maji na Mazingira. Wizara ya Maji kwa mpango kabambe wa Gridi ya Maji ya Taifa, malengo yake ni kuhakikisha kwamba gridi hiyo inakuwa inasaidia watumiaji wote wa maji. Kwa hiyo,

ninawahakikishia, badala ya kuanza kulaumiana na kulalamika, tuanze kushirikiana kwa sababu utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, miaka 25 ijayo itategemea tulivyokubaliana katika namna ya kujenga sekta hizo za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Dkt. Mollel, alitoa hoja yake hapa nami nimemwahidi kwamba nitakwenda kufanya ziara. Baada ya Bunge nitakwenda kufanya ziara katika maeneo ambayo yana changamoto zinazojulikana ambazo ni tete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo kwa upande wa mifugo nilipokwenda Ruvuma – Tunduru, baada ya kutumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuta kuna matatizo Ruvuma, kuna matatizo Mtwara, kuna matatizo Lindi, Pwani, Kilimanjaro na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninamwomba Mwenyezi Mungu anipe afya, nitafika huko tushauriane. Nitakwenda kwa utulivu zaidi kusudi tuweze kutatua matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, haya mambo tunayoyasema ni ya mpango wa miaka mitano ya ilani. Niko hapa kuwathibitishia Wabunge pamoja na Watanzania kwamba, mambo yote ambayo yameahidiwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuhusu Sekta za Mifugo na Uvuvi yote yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuruni sana na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI**:

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Baadaye Mheshimiwa.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI**:

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99- Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 *Administration and Human Resources Management Division*…………………Sh.7,522,729,289

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Fungu hili ndiyo Fungu lenye mshahara wa Waziri na tumepata jina moja la Mheshimiwa Fadhili Liwaka akiomba ufafanuzi. Mheshimiwa Fadhili Liwaka.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi nimeondoa baada ya ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Kifungu kilichotwaja hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Units*………Sh.1,918,028,862

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*………Sh. 2,236,983,675
Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*...........Sh. 612,014,900
Kifungu 1005 – *Information, Education and Communication Unit*……………………………………Sh.0
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*…………….Sh.2,178,211,820
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*…..........................Sh.578,093,900
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*……Sh.870,612,500
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit*…………………......Sh.793,842,800
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*…………………………Sh.718,154,700
Kifungu 1011 – *Environmental Management Unit*…....Sh.659,009,600
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*………Sh.998,777,400
Kifungu 1013 – *Government Communication Unit*……………………………….……Sh. 1,033,704,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*…………….........Sh.12,480,462,007
Kifungu 7003 – *Infrastructure Development Division*……………………………………Sh.6,800,964,255
Kifungu 7005 – *Research, Training and Extension Services Division*...............................Sh.26,134,686,558
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing Development Division*…....................Sh.9,562,126,030
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development Division*…Sh. 2,145,276,800
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*……Sh.13,616,392,244
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development Division*……………………………………Sh.7,419,348,660

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*...........Sh.145,584,408
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*…………….Sh.2,000,000,000

Kifungu 1011 – *Environmental Management Unit*........................Sh.0
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*..…Sh. 20,316,674,379
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*…..……………...Sh. 32,907,752,626
Kifungu 7003 – *Infrastructure Development Division*………..…………………...Sh.113,123,135,208
Kifungu 7005 – *Research, Training and Extension Services Division*..............................Sh.47,299,399,588
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing Development Division*……………….Sh.60,065,477,845
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development Division*...Sh. 5,412,997,590
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*………………...…………….Sh.31,448,092,356
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development Division*…………………………………Sh.22,380,591,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI**: Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kifungu cha 123(3)(a) na (b), ninaomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninatangaza rasmi kwamba Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Ninachukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, pamoja na watendaji wote Wizarani kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inatekelezwa, lakini pia kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa na tunawatakia kila la heri katika bajeti mpya ya mwaka 2026/2027.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa, Maafisa Uhamiaji wanaendelea kutoa huduma ya Hati za Kusafiria katika Viwanja vya Bunge na zoezi hilo litahitimishwa kesho tarehe 15 Mei, 2026. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge ambao hawajapata huduma ya Hati za Kusafiria wanaombwa kufika kesho kuanzia saa nne asubuhi, jengo la Utawala *Ground Floor,* Ukumbi Na. 9 ili kupata huduma hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tunakumbushwa pia kwa wale Wabunge ambao wanachangia kwa maandishi, basi zoezi hilo walifanye kupitia vishikwambi vyetu.

Mwongozo Mheshimiwa.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 79. Wakati tunaendelea na hotuba hii ambayo bajeti yake tumeipitisha sasa hivi, mchangiaji mmoja ambaye ni Mheshimiwa Jackson Kiswaga alichangia akisema kwamba, katika Wizara hii ina wahuni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zetu za Bunge zinazotuongoza na hasa ile ya 74(k) inakataza lugha inayodhalilisha mtu mmoja ama kundi la watu wengi. Kwa hiyo, ninaomba Mwongozo wako juu ya lugha iliyotumika, maana ninaona ni lugha isiyokubalika na Bunge kwa mujibu wa kanuni zetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa Mwongozo wako. Tumeupokea na tutapitia *Hansard* tutatoa Mwongozo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi katika Ukumbi huu wa Msekwa.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 15 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*